

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 18 Juni, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:-

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na Tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bajeti, Mheshimiwa Hawa Ghasia. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 438

Hitaji la Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya Mgungulu

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari ya kuwahudumia wagonjwa katika kituo cha Afya cha Magunguli –Mgololo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Menrald Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya Magungulu - Mgololo kilichopo kata ya Magungulu imekwishapatikana. Gari hili lilitolewa na Mheshimiwa Rais wakati anatoa msaada wa magari ya wagonjwa kwa halmashauri mbalimbali hapa nchini mnamo mwezi Machi, 2018 na taratibu za usajili zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kutambua uhitaji wa gari katika kituo hiki, gari hili limepelekwa kituoni moja kwa moja na kuanza kutumika huku taratibu za usajili wake zikiwa zinaendelea. Ni matumaini yetu kuwa gari hili, litasaidia kuleta wepesi kwa wananchi kufikia huduma za afya pale mahitaji yatakapo yanajitokeza.

SPIKA: Mheshimiwa Kigola swali la nyongeza nimekuona.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwa kumshukuru sana Makamu wa Rais

alipokuwa amekuja kwenye jimbo langu na mimi nilimwomba *Ambulance* siku ile na utekelezaji umefanyika nashukuru sana. Swali langu la kwanza kule jimboni kwangu nina vituo vya afya kama vitatu ambavyo viko vijijini sana hakuna magari kwa mfano pale Mninga na Mtwango ni vituo vikubwa sasa. Je, Serikali itanisaidia tena kuniletea (*Ambulance* katika hivyo vijiji viwili ambao wananchi wanapata shida sana?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, nina tatizo kubwa sana la watumishi wa Afya kwenye vituo vyangu vya afya na zahanati kwenye jimbo langu. Je, Wizara ya Afya ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba watumishi wa Afya tunaweza kuwapata?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya Serikali naomba nipokee shukrani ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Mbunge. Katika suala lake la kwanza, anaongelea vituo vya afya vingine viwili ambavyo viko mbali sana na vina uhitaji mkubwa wa magari ya *Ambulance*.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni azma ya Serikali pale ambapo gari zinapatikana tutazisambaza na hasa tutazingatia maeneo yenye uhitaji mkubwa sana. Sasa kama na eneo la kwake litakuwa miongoni mwa hayo maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa hakika sisi tutatekeleza hilo, lakini ni vizuri pia akatambua kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo hawakupata hata hiyo gari ambayo yeye amepata kwa hiyo kwa kadri gari zitakapopatika tutafuata uwiano unaotakiwa ili haki iweze kutendeka.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, anaongelea juu ya vituo vyake vya afya kutokuwa na watumishi wa kutosha, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge sasa hivi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeshatangaza

nafasi 6,180,000 na naamini pale ambapo watakuwa wameajiriwa na eneo la kwake litaweza kufikiriwa kupelekewa.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata la Desderius John Mipata Mbunge wa Nkasi Kusini.

Na.439

Barabara ya Namanyere- Ninde

MHE. DESDERIUS J. MIPATA aliuliza:-

Serikali imetumia zaidi ya shilingi milioni 350 kuimarisha barabara ya Namanyere – Ninde yenye urefu wa kilomita 67, lakini fedha hazikutosha kukamilisha barabara hiyo:-

Je, Serikali itatenga fedha zaidi kukamilisha barabara hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Namanyere- Ninde yenye urefu wa kilomita 67, kwa mara ya kwanza iliibuliwa na mradi wa *TASAF* Awamu ya I mwaka 2005/2006 kwa kulima barabara hiyo kwa kutumia nguvu kazi ya wananchi. Kwa kipindi chote hadi mwaka 2014/2015, barabara haikufunguka kwa kukosa miundombinu muhimu kama vile madaraja na makalvati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali ilitenga fedha jumla ya shilingi milioni 375.3 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ambapo fedha hizo zilitumika kwa kufyeka barabara na kuondoa miti katika barabara yote,

kuilima barabara kwa urefu wa kilomita 25 kwa kiwango cha udongo, kujenga Makalvati 15 pamoja na kujenga madaraja manne. Kati ya madaraja manne yaliyojengwa, mawili yapo katika Mito ya Lwafi na Ninde, hivyo matengenezo hayo yamewezesha barabara hiyo kufunguka kwa urefu wa kilomita 25 tu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na upatikanaji wa fedha, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kufanyia matengenezo barabara hiyo ambapo mwaka wa fedha 2015/2016, shilingi milioni 44.58 zilitengwa kwa ajili ya kufanyia matengenezo ya muda maalum kwa urefu wa kilomita 20. Aidha, mwaka wa fedha 2016/2017, kiasi cha shilingi milioni 20 zilitumika kuimarisha sehemu korofi zenye urefu wa mita 500.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuifungua barabara hii kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana ili kusaidia wananchi wanaotumia barabara hii katika suala zima la usafiri.

SPIKA: Mheshimiwa Mipata swali la nyongeza,

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kufuatia majibu ya Serikali tayari barabara hii imetumia zaidi ya milioni 439.8 katika jitihada ya kutaka kuifungua. hata hivyo, mwaka huu haijatengewa fedha na wanasema itaendelea kuitengea fedha kadri fedha itakavyozidi kupatikana. Je, Serikali haioni kwamba kwa kufanya hivi inachelewa na fedha ambazo tayari imesha-*invest* kwenye barabara hizi zitakosa thamani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kufuatia mvua nyingi zilizonyesha katika Mkoa wa Rukwa kuna barabara katika Jimbo la Nkasi Kusini zimefunga kabisa. Barabara hizo ni pamoja na Kisula - Malongo Junction - Katongolo-Namasi- Ninde - Kanakala na tayari *TARURA* imeleta taarifa ya orodha ya barabara hii. Je, ni lini fedha sasa zitatolewa kwa ajili ya kwenda kurudisha miundombinu ili iweze kutumika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Josephat Kandege majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza uniruhusu kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Mipata barabara hii amekuwa akiipigania kwa nguvu zake zote na ndiyo maana Serikali imesikia kilio chake na hicho kiasi cha pesa kikaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie kama ambavyo yeye mwenyewe amesema itakuwa si busara kwa Serikali kuweza pesa bila kupata matunda kwa sababu matunda yanayotarajiwa ni barabara kufunguka. Hata hivyo, naye atakubaliana nami kwamba barabara hii haikuwepo kabisa na kazi kubwa ambayo imekwishafanya kuhusiana na ujenzi wa madaraja pamoja na yale makalvati hakika pesa ikipatikana kipande ambacho kimebaki kitaweza kufunguliwa na wananchi waweze kupita kwenye hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, anaongelea baada ya mvua kunyesha kumekuwa na uharibifu katika barabara hizo ambazo amezitaja na bahati nzuri *TARURA* walishaleta makisio ya nini ambacho kinatakiwa kutumika. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pesa ambazo zilitengwa kwa ajili ya *emergence almost* zote zilishakwisha na theluthi mbili ya pesa hizo zilitumika katika kurudishia miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimhakikishie kwa sababu bajeti ilishapitishwa naamini muda siyo mrefu pesa ikianza kupatikana na eneo la kwake litaweza kufunguliwa hizo barabara.

SPIKA: Tuendeleo na Utumishi na Utawala Bora swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, kwa niaba yake! Mheshimiwa Selasini.

Na. 440

**Watumishi wa Umma kuzingatia Kanuni na Sheria za
Utumishi wa Umma**

MHE. . JOSEPH R.SELASINI - (K.n.y MHE. RUTH H. MOLLEL)
aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano inajinasibu kuzingati Utawala wa Sheria, Kanuni na taratibu katika Utumishi wa Umma. Hata hivyo, kuna ushahidi kuwa baadhi ya viongozi wanakiuka maadili na taratibu lakini wameachwa pasipo kuchukuliwa hatua zozote za kinidhamu:-

(a) Je, tunaweza kujenga uchumi imara bila Watumishi wa Umma kuzingatia Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Taifa linadumisha umoja ulioasisiwa na Baba wa Taifa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kusesitiza kuwa nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazojumuisha zile zinazosimamia Utumishi wa Umma. Endapo wapo watu wanaokiuka sheria, hao wanafanya hivyo kutokana na upungufu wao na kamwe haiwezi kutafsiriwa kuwa ni Sera ya Serikali ya Awamu ya Tano kwenda kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kinidhamu huchukuliwa pale inapothibitika pasipo shaka yoyote kuwa kosa limetendeka kwa makusudi. Pale ilipogundulika kuwa utendaji usiozingatia sheria unatokana na kutoelewa misingi

ya Sheria, Serikali imelazimika kutoa mafunzo maalum ili kuwajengea uwezo watendaji wake ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Umoja wa Tanzania ulioasisiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Shekhe Abeid Aman Karume unaendelezwa kwa njia mbalimbali, ikiwemo kuadhimisha siku maalum za viongozi hawa, ambapo maoni yao huakisiwa kupitia mikutano ya hadhara na makongamano mbalimbali kwa lengo la kuenzi malengo yao.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Selasini, nimekuona, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH R.SELASINI: Mheshimiwa Spika, katika awamu hii umezuka mtindo kwa baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwavua vyeo baadhi ya Walimu kutokana na sababu za shule zao kutofanya vizuri, kuwavua vyeo Madaktari na hata wengine kuwaondoa kazini. Sasa mtindo huu unavyoendelea tafsiri ya jamii inaonekana kwamba ni hatua ambazo ni mahususi zilizoagizwa na Serikali. Je, Serikali iko tayari kupitia maamuzi yote haya na kuwarejeshea hao Walimu au Madaktari haki yao kama ikithibitika kwamba walionewa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wako Walimu hasa ajira mpya na hawa wengi wako katika jimbo langu. Wanapoingia kazini hawapewi zile fedha *subsistence allowance* za kuwasaidia kabla hawajapata mishahara yao na nadhani hata maeneo mengine katika nchi yetu iko namna hiyo. Je, ni utaratibu gani ambao Wakurugenzi au Serikali inao wa kuhakikisha kwamba hao Walimu hawapati mateso wanapoanza kazi zao kwa mara ya kwanza?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) Mheshimiwa Kaptein Mstaafu Mkuchika.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, ametaka kujua je, kuwavua vyeo kunakoagizwa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Serikali iko tayari sasa kuwarudisha. Nilipojibu swali la msingi nilieleza kwamba nchi hii inaendesha kwa mujibu wa Sheria, taratibu na kanuni.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili ni kwamba yule aliyekuajiri wewe ndiye mwenye madaraka ya kukufukuza. Kwa hiyo, utaona kwamba mara nyingi wakigundua kwamba kuna makosa wanamsimamisha wakati wanasubiri yule mwenye madaraka ya ajira achukue hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge hili kama kuna mahali mtumishi amefukuzwa na Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya wakati yeye siye aliyemwajiri niletewe suala hilo nitalishughulikia mara moja, kwa sababu kwa taratibu zetu za kiutumishi yule aliyekuajiri ndiye anayekuaadhibi na ndiye anayekufuza. Nimeeleza hapa jamani sisi siyo malaika, nimeeleza kwamba wakati mwingine tunapowateua tunawapa mafunzo. Hao wanaozungumzwa tumeshawapa mafunzo, naamini nadhani hata Bunge hili kama mnafuatilia maji yametulia katika mtungi siyo kama tulivyoanza huko. *(Makoff)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Walimu hawapewi *subsistence allowance* kabla, moja nataka niseme, Wizara yangu ya Utumishi kazi yake ni kuajiri, nikishaajiri nakwambia wewe nenda Wizara ya Maji, Wizara ya Ushirika na kadhalika, sasa yule tajiri wako ndiye anayekushughulikia. Hata hivyo, siku za nyuma imetokea ilifanyika miaka ya nyuma namna hiyo, watu wakawa wanafanya ndivyo sivyo anakwenda anachukua hela anasema anakwenda kuripoti halafu haendei.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba kwa utaratibu tulionao sasa huingizwi wewe kwenye mfumo wa mishahara mpaka umefika, umeripoti, tuna uhakika kwamba

huyu mtu kafika. Huo utaratibu unatuwezesha kupunguza udanganyifu mkubwa katika masuala ya ajira.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mary.

Na. 441

Umuhimu wa Kuimarisha Chuo cha Ufundi Kibaha

MHE. MARY D. MURO aliuliza:-

Uanzishaji wa Vyuo vya Ufundi ulilenga kuwapatia elimu ya vitendo hasa vijana wetu, lakini Chuo cha Ufundi Kibaha kilicho chini ya Shirika la Elimu Kibaha hakina vifaa wala miundombinu ya kujifunzia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa pamoja na kufufua miundombinu katika chuo hicho?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa William Olenasha, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inasimamia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha kilichokuwa chini ya Shirika la Elimu Kibaha. Chuo hiki ni mojawapo ya vyuo 55 vilivyohamishiwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuanzia Mwaka wa Fedha 2016/2017. Vyuo hivi vina changamoto nyingi za uendeshaji ikiwemo; upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na

uchakavu wa majengo ya madarasa, karakana, mabweni, nyumba za watumishi na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya vyuo hivyo, Serikali imetoa Kandarasi kwa vyuo vitatu ambavyo ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Mbeya ili vifanye uchambuzi wa kina wa hall halisi ya miundombinu na vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika vyuo hivyo. Baada ya kukamilika kwa zoezi hili taratibu za kuvifanyia ukarabati zitaanza.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara pia inafanya zoezi la kubaini mahitaji ya watumishi katika vyuo vyote vya *FDC*. Zoezi hili linatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2018. Baada ya zoezi hili kukamilika, ujenzi, ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa vya kufundishia na kujifunzia utafanyika kulingana na mahitaji. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha ni mojawapo ya vyuo vilivyo katika mpango huu.

SPIKA: Mheshimiwa Mary Deo Muro, swali la nyongeza.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Amekiri kwamba kuna matatizo lakini swali langu la kwanza linasema, kama hivyo ndivyo, wanafunzi wamemaliza wakiwa hawana ufundi wowote, kwa sababu kile chuo kilikuwa cha madarasa kwa ajili ya vijana wetu na kilikuwa kinafundisha udereva hamna magari, karakana hamna, madarasa mabovu na wameondoka wakiwa hawana ujuzi wowote na *intake* yao imekwisha. Je, Serikali ina mpango gani kwa ajili ya vijana hao, baada ya kurekebisha upungufu huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa hakuna vifaa vya kufundishia miundombinu hakuna na bado *intake* hii wanachukua wanafunzi, nini kauli ya Serikali katika hilo?

SPIKA: Mheshimiwa Mary, hivi chuo chenyewe ni kipi ni kile *FDC* au chuo gani?

MHE. MARY D. MURO: *FDC* Kibaha.

SPIKA: Kile ambacho kilikuwa kinaitwa *FDC*?

MHE. MARY D. MURO: Ndiyo.

SPIKA: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba pamoja na upungufu uliopo katika Chuo cha *FDC* Kibaha, elimu iliyokuwa inatolewa inakidhi viwango stahiki vya ufundi ambao Chuo kile kimesajiliwa kwa ajili ya kutoa. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba wale vijana waliomaliza Serikali imejiridhisha kwamba wamekuwa wakipata mafunzo vinginevyo chuo kile kingeshafungwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba ni namna gani sasa tunarekebisha hiyo hali, nimeshamjibu kwenye jibu letu la msingi kwamba tayari tupo kazini, tunafanya tathmini ili kuweza kujua upungufu uliopo katika vyuo vyote 50 vya *FDC* ili sasa tuanze utaratibu wa kukarabati, na kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia na kufundishia ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba kuna nguvukazi ya kutosha ili elimu inayotolewa iweze kuwa bora kuliko sasa. Kwa hiyo, nimwambie tu asubiri tayari zoezi linaendelea.

SPIKA: Mheshimiwa Fatma Toufiq nimekuona na Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa nami kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Chuo cha Ufundi *VETA*, Dodoma kilijengwa muda mrefu na kilikidhi kwa wakati ule na sasa hivi kuna ongezeko kubwa sana la vijana na miundombinu bado ni ile ile; je, Serikali haioni kwamba umefikia wakati wa kuongeza majengo na miundombinu ili kiendane na hadhi ya Jiji?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu *VETA* Dodoma.

NAIBU WAZIRI ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali ina mpango wa kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vyote nchini, na sio Vyuo vya Ufundi tu. Kwa hiyo, tutaendelea kuangalia vyuo vile ambavyo vinahitaji matengenezo na ukarabati pamoja na kuongezewa Majengo, ili tuweze kufanya hivyo kadiri bajeti itakavyoturuhusu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie tu kwamba, hata Chuo cha Dodoma nacho ni moja kati ya vyuo tulivyonavyo na kwa vyovyote vile kulingana na upatikanaji wa fedha tutaangalia uwezekano wa kukipanua.

SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel, nilishakutaja.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Moja ya Malengo ya Umoja wa Mataifa ni kuhakikisha kwamba hakuna anayeachwa nyuma na katika vyuo vingi hasa vya Ufundi, havizingatii mahitaji ya kundi maalum la watu wenye ulemavu na hivyo wamekuwa wakiachwa nyuma. Ni nini sasa, jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba ili tunaendana sambamba na kauli hizo za Umoja wa Mataifa, watu wenye ulemavu hawaachwi nyuma?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Amina Mollel, kwa kweli amekuwa ni mtetezi mkubwa sana wa haki za watu wenye mahitaji maalum. Nimhakikishie tu kwamba, Wizara yangu imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba changamoto ambazo zilikuwepo huko nyuma za kutotoa msisitizo mkubwa kwenye mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu, kwa sasa tunahakikisha tunajaribu kutoa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Wizara ya Elimu ina Kitengo Maalum kinachohusika na elimu ya mahitaji

maalum. Vilevile kwa sasa tumetoa maelekezo kwamba katika ujenzi wowote ule utakaofanywa kwa fedha za Serikali ni lazima tuhakikishe kwamba mahitaji na mazingira ya watu wenye mahitaji maalum yanatiliwa maanani.

Mheshimiwa Spika, ukiacha hivyo, Serikali imewekeza sasa vilevile kwenye kutafuta Walimu na Wataalam wengine kwa ajili ya kuendeleza elimu ya watu wenye mahitaji maalum. Ndio maana tumefanya ukarabati mkubwa sana katika Chuo cha Patandi na tunaamini kwamba tunavyoendelea mbele, tutaendelea kuhakikisha kwamba kunakuwa na Walimu na wafanyakazi wengine ambao wana elimu ya kuweza kusaidia wanafunzi na watoto wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba Serikali inayafanyia kazi vizuri sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, twende swali linalofuatwa la Mbunge wa Bumbwini, linaulizwa na Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed kwa niaba yake Hamad Salim Maalim.

MBUNGE FULANI: Ndiyo huyu huyu.

SPIKA: Nishakuona Mheshimiwa Salim.

Na. 442

Kuweka Syllabus za Shule Mitandaoni

MHE. HAMAD SALIM MAALIM - (K.n.y. MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED) aliuliza:-

Kwa kuwa huu ni wakati wa Sayansi na Teknolojia na vijana wetu wamekuwa wakizitafuta *syllabus* za Masomo mbalimbali madukani bila mafanikio:-

Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kuziweka *syllabus* hizo mtandaoni?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhamed Amour Muhamed, Mbunge wa Bumbwini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inafanya kila jitihada kuhakikisha kuwa wadau wa elimu wanapata mahitaji yao ya Mitaala na Mihtasari kwa lengo la kufanikisha utoaji wa elimu nchini. Katika kuhakikisha hili, Wizara kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania, husambaza Mihtasari nchi nzima. Aidha, ili kukidhi mahitaji kwa wadau mbalimbali, Mihtasari imekuwa ikipatikana duka la TET na maduka ya vitabu nchini ambayo, wenye maduka ya vitabu huenda kununua kwenye duka la TET.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupita TET, imeshaanza kuweka mihtasari kwenye mtandao wa Taasisi ya Elimu Tanzania ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mihtasari hiyo. Baadhi ya mitaala na mihtasari ambayo tayari imewekwa kwenye mtandao wa Taasisi ya Elimu Tanzania ni Mitaala na Mihtasari ya Elimu ya awali, Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, aidha, lengo la Wizara kwa sasa ni kuweka Mitaala na Mihtasari ya Masomo yote kwenye mtandao ili iwafikie walengwa kwa urahisi na kwa wakati. Wadau wote wa elimu wanashauriwa kutembelea Mtandao wa Taasisi ya Elimu Tanzania (<http://www.tie.go.tz>) ili waweze kuona na kupakua Mitaala na Mihtasari husika.

SPIKA: Mheshimiwa Salim swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Wizara, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Wizara imekiri kwamba si mitaala na mihtasari yote iliyoko kwenye

mtandao. Je, lini Wizara itahakikisha kwamba mitaala na mihtasari yote hii inapatikana kwenye mtandao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mabadiliko ya mitaala na mihtasari yanayofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia huwa inachuka muda mrefu sana kutufikia kule Zanzibar na hiyo kupelekea wanafunzi wetu kuathirika sana wakati wanatumia mitaala na mihtasari ile mikongwe. Je, ni lini Wizara itahakikisha kwamba mitaala hii na mihtasari hii inafikia Zanzibar kwa wakati ili waweze kujitayarisha katika masomo yao? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kuhusu ni lini tutaweka mitaala na mihtasari yote kwenye tovuti, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba kama nilivyosema, kwenye jibu la msingi kwamba tumeshaanza na tayari baadhi ya mitaala na mihtasari inapatikana. Sasa kuhusu ile ambayo bado, nimhakikishie kwamba Serikali, itachukua hatua kuhakikisha kwamba tunaweka kwenye tovuti haraka na mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na changamoto iliyoko Zanzibar naomba nimhakikishie kwamba nimeipokea, tunaenda kuifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba nako mihtasari na mitaala iwe inapatikana kwa wakati.

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Ndalichako, una nyongeza yoyote hapo.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Labda tu nihakikishe kwamba utaratibu ambao uko kwa sasa hata mitaala inapofanyiwa mapitio kunakuwa na ushirikiano kati ya upande wa Tanzania Bara na upande wa Zanzibar na hata katika Bodi ya Taasisi ya Elimu pia kunakuwa na wawakilishi ambao wanatoka upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hivyo, inawezekana pengine changamoto ipo katika usambazaji inapokuwa imefika kwenye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri tumelipokea, tutahakikisha kwamba, kama kuna mahali popote kuna mkwamo, basi iweze kufika ,lakini ushirikiano ni mkubwa katika hatua zote tangu maandalizi.

SPIKA: Ahsante sana Profesa. Sasa tunaingia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Martha Mlata.

Na. 443

Kuongeza Matawi ya Vyuo Vinavyofundisha Sanaa ya Maigizo na Muziki

MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MHE. AISHAROSE N. MATEMBE) aliuliza:-

Sanaa ya Maigizo na muziki ni miongoni mwa Sekta zinazochangia asilimia kubwa ya vijana kujajiri lakini kuna Vyuo vichache nchini vinavyotoa elimu hiyo ya sanaa ya muziki na maigizo ambavyo ni Chuo cha Sanaa Bagamoyo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam huku masharti yake yakiwa ni changamoto kwa vijana wa mikoani:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha matawi ya Vyuo hivyo kwenye Kanda ama Mikoa ili kuongeza fursa zaidi kwa vijana?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Elimu ya Sanaa ya Maigizo na Muziki au kwa ujumla Sanaa, yanatolewa kwa ngazi ya Shahada na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kwa upande wa Serikali na Chuo Kikuu cha Tumaini Arusha kwa upande sekta binafsi. Aidha, mafunzo kwa ngazi ya Stashahada na Cheti kwa Vyuo vya Serikali hutolewa na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) yenye matawi takribani nchi nzima. Vipo vilevile vyuo binafsi ambavyo hutoa mafunzo ngazi ya Stashahada pamoja na Cheti.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa vijana na wadau wengine wanaotaka kubobea kwenye sanaa wajunge na vyuo hivi ambavyo vimetawanyika nchi nzima. Aidha, nawapongeza wadau wote walioanzisha vyuo hivyo ili kuunga mkono jitihada za Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Martha Mlata, swali la nyongeza.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pia nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Naibu Waziri na naipongeza Serikali kwa sababu imeendelea kuimarisha sana Sekta hii ya Sanaa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa sasa Serikali inatambua umuhimu wa vijana kujijiri kupitia sanaa; je, haioni sasa umefika wakati muafaka kuboresha vitengo vya Maafisa Utamaduni ambao kwa sasa hawana vitendea kazi. Ili waweze kuwapatia magari na fedha kwa ajili ya kuwafikia vijana hasa walioko vijijini na wenye vipaji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa vijana wengi sasa wamejitokeza kuonesha ufundi stadi wao katika sanaa mbalimbali, lakini kuna uharamia mkubwa sana katika mitandao, kuna fedha nyingi zimebaki kule. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati muafaka wa kurasimisha zile kompyuta ambazo zinatumiwa kuuza miziki ya Wasanii, ili Serikali yenyewe ipate mapato, lakini na Vijana waweze kupata mapato kupitia mitandao hiyo?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza kwa sababu amekuwa ni mpambanaji mkubwa sana ndani ya Bunge ya masuala yote ambayo yanahusu Sanaa pamoja na Wasanii.

Mheshimiwa Spika, sasa nikija katika swali lake ambalo ametaka kujua Serikali ina mpango gani katika kuboresha maslahi ya Maafisa Utamaduni Nchini. Nikiri kwamba sisi kama Serikali tunatambua kwamba, Maafisa Utamaduni nchini kote wanafanya kazi kwenye mazingira magumu. Hata hivyo, kwa sababu tunatambua pia kwamba sisi kama Wizara ya Habari, Maafisa Utamaduni wako kwenye Wizara ya Habari Kisera, lakini kiutendaji wanawajibika chini ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI, tutaendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba tunaboresha, mazingira ya Maafisa Utamaduni nchini. Kama haitoshi nimhakikishie kwamba kwa sasa hivi, Wizara ipo katika hatua za mwisho kabisa za kuhuisha na kuboresha ile Sera yetu ya Utamaduni ya mwaka 1997 ili basi iweze kuendena na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ameuliza kuhusiana na kurasimisha kompyuta ili kuweza kutunza haki za Wasanii. Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie kwamba, tunatambua kabisa kwamba kumekuwa na changamoto kubwa sana ya wizi wa kazi za sanaa. Sisi kama Serikali zipo jitihada mbalimbali ambazo tumezichukua katika kukabiliana na uharamia huo wa kazi za sanaa nchini. Si tu katika kurasimisha kompyuta, lakini kuna jitihada mbalimbali mojawapo ikiwa ni kutoa elimu kwa Wasanii wetu ili waweze

kujua ni namna gani ya kuweza kuhifadhi kazi zao, lakini vile vile waweze kusimamia haki zao, kwa sababu changamoto kubwa imekuwa ni wao wanaingia mikataba ambayo haizingatii maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo kama Wizara tumefanya, ni kuhakikisha kwamba, sasa hivi tumeunda Kamati ambayo inapitia Mikataba yote ya Wasanii. Ni hivi juzi tu tumeshuhudia Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe akilivalia njuga suala la Mzee Majuto kudhulumiwa haki yake na nimhakikishie kwamba kwa sasa hivi tumefika kwenye hatua nzuri. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba Kamati hiyo itakapokamilisha kupitia hiyo mikataba yote ya Wasanii nchini, Wasanii wataweza kunufaika na kazi zao.

SPIKA: Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kama haitoshi mwisho kabisa kwa sasa hivi, Wizara tuko katika kwenye mazungumzo na wenzetu wa Wizara ya Viwanda ili basi ile Idara ya *COSOTA* iweze kurudishwa kwenye Wizara ya Habari, Sanaa na Utamaduni.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, inatosh.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Ili basi matatizo yote ambayo yanawahusu Wasanii yaweze kushughulikiwa na Wizara Moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mjini Mheshimiwa Sima.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa changamoto kubwa inajitokeza kutokana na uhaba wa

hawa Maafisa Utamaduni kwenye halmashauri zetu. Sasa Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Maafisa Utamaduni ili kuweza kukidhi haja ya Sanaa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu mafupi kwenye swali hilo, kuna mpango wowote wa kuajiri Maafisa Utamaduni?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba, hapo nyuma kulikuwa kuna changamoto kubwa sana ya Maafisa Utamaduni kwenye halmashauri zetu, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, halmashauri nyingi zilishaandika barua ya kuomba vibali kutoka Utumishi vya kuweza kuajiri Maafisa Utamaduni. Mpaka sasa hivi karibu halmashauri nyingi zina Maafisa Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi sisi kama Wizara, tunaendelea na mchakato wa kuonesha kwamba tunaajiri Maafisa Utamaduni wapya, hususani katika Mikoa na Halmashauri ambazo ni mpya. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo hilo kwa kiasi kikubwa sana limeshashughulikiwa na Wizara yetu ya Habari, nadhani hata Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mashahidi.

SPIKA: Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga vijijini, uliza swali lako tafadhali.

Na. 444

Mradi wa Kusambaza Maji Dar es Salaam

MHE. MARTIN M. MSUHA aliuliza:-

Je, Serikali itakamilisha lini mradi wa kusambaza maji kwa wananchi waliopo pembezoni mwa bomba kuu litokalo Ruvu Juu hadi Dar es Salaam hususan wananchi wa Kata za Kwembe, Mbezi, Kibamba, Msigani na Saranga?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martin Alexander Msuha, Mbunge wa Mbinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imemwajiri mkandarasi Kampuni ya *Jain Irrigation Services* kutekeleza mradi wa usambazaji maji kwa wananchi waishio maeneo ya pembezoni mwa bomba kuu litokalo Ruvu Juu hadi Dar Salaam hususani wananchi wa Kata za Kwembe, Mbezi, Msigani na Saranga.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2018, utekelezaji wa mradi huo ulikuwa umekamilika kwa wastani wa asilimia 87. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kukamilisha ulazaji wa mabomba na kufanya majaribio (*Pressure test*). Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2018. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Msuha swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. MARTIN M. MSUHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pia nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nitakuwa na swali moja tu la nyongeza. Kata ya Litumbandyosi iliyopo Wilayani Mbinga inakabiliwa na uhaba mkubwa wa upatikanaji wa maji safi na maji salama. Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya visima virefu katika Kijiji cha Kingoli, Luhagara, Mabuni na Litumbandyosi?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Sijui kama vijiji hivyo Mheshimiwa Naibu Waziri anavifahamu, lakini majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru na nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri. Vile vile nilishukuru sana Bunge lako Tukufu limetuidhinishia bajeti na katika bajeti tuliyo idhinishiwa Mbinga tumeitengea Sh.1,773,000,000 katika kuhakikisha

tunatatua tatizo la maji. Nimwombe Mhandisi wa Maji wa Mbinga asilale atumie zile fedha katika kuhakikisha anatatua tatizo la maji kikiwemo Kijiji cha Kingole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

SPIKA: Swali la nyongeza kutoka Rukwa. Tuendeleo Mheshimiwa.

MHE. RHODA E. KUMCHELA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Nataka niulize swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Manispaa ya Mpanda imekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama na kutokana na ongezeko kwamba kwa sasa hivi ni Manispaa kumekuwa na changamoto hiyo na Idara ya Maji wamekuwa hawatoi taarifa kwamba ni lini watakata maji au ni lini maji yanaweza kuwa yanapatikana kwa wingi. Sasa nini tamko la Serikali kuhakikisha kwamba wakazi wa Manispaa ya Mpanda wanapata maji kwa wingi na yanawatosheleza wakazi hao?

SPIKA: Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji na Umwagiliaji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru na pia nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali nzuri. Kikubwa sisi kama Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha wananchi wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza. Nimepokea changamoto hiyo na namhakikishia Mheshimiwa Mbunge nitalifuatilia ili tuweze kuhakikisha watanzia wale wa Mpanda wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

SPIKA: Mheshimiwa Bulembo nilikuona na Mheshimiwa Shukuru Kawambwa utafuatia.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na swali la msingi lililoulizwa kuhusu Dar es Salaam naomba Wizara ya Maji ituambie kwa sababu baada ya Ruvu Chini na Ruvu Juu kukamilika sasa katika Jiji

la Dar es Salaam maji yanamwagika sana karibu asilimia 40. Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuondoa umwagikaji wa maji ili kuisaidia pesa ile ikarudi Serikali.

SPIKA: Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Aweso, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuhusu suala zima la upotevu wa maji. Serikali imekuwa ikiwekeza fedha nyingi sana katika kuhakikisha inatataua tatizo la maji. Hata hivyo, ipo hali ya kuona upotevu mkubwa wa maji barabarani ama mitaani na kuwa si hali nzuri sana kuona wananchi hawana maji lakini maji yanapotea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wangu aliagiza Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Maji na kufanya nao kikao na akawagiza kujenga na kutengeneza miundombinu ambayo rafiki ambayo itakayoweza kudhibiti upotevu wa maji mpaka kufikia kiwango kile cha kimataifa cha asilimia 20 ambacho kinakubalika. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na jitihada katika kujenga na kukarabati katika suala zima la kudhibiti upotevu wa maji.

SPIKA: Mheshimiwa Kawambwa. Swali la mwisho litakuwa la Mheshimiwa Mary Nagu.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na shukrani za wananchi wa Bagamoyo kwa Mheshimiwa Waziri kwa kutujengea tanki kubwa la lita milioni sita Bagamoyo Mjini. Naomba kuuliza swali moja kwamba ni lini sasa Wizara itaanza mradi wa kusambaza mtandao wa mabomba ya maji ili maji hayo sasa yaweze kuwafikia wananchi katika Mji wa Bagamoyo na Kata zote katika Jimbo la Bagamoyo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri na nia njema ya kuhakikisha wananchi wake wa Bagamoyo wanapata maji safi, salama ya yenye kuwatosheleza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa suala hili la maji ni la uhitaji mkubwa sana tutalifanya kwa haraka ili wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza.

SPIKA: Mwisho, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, tafadhali.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naipongeza na kuishukuru sana Serikali kwa kutoa fedha za kuweza kuimarisha upatikanaji wa maji Mji wa Kateshi ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Hanang na wenyewe viongozi wapo hapo *Gallery*, naomba Mheshimiwa Waziri atuhakikishie kwamba ifikapo mwezi wa tisa ambapo ni ukame na hamna maji Kateshi kama maji hayo yatapatikana na nitaishukuru zaidi Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Wale wageni wa kutoka Kateshi wamekaa upande gani. Hebu simameni, Oohoo! Karibuni sana. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Maji majibu kwa wananchi wa Kateshi ambao wamefuata jibu lao mpaka Bungeni hapa. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya na amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana katika suala zima la maji katika Mji wa Kateshi. Kubwa nimhakikishie utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha, Serikali imeshatafuta fedha na imeshapata. Kwa hiyo, nimwombe Mhandisi wa Maji afanye kila linalowezekana katika kuhakikisha wananchi hawa ndani ya mwezi wa Tisa wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Spika, lingine nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge nitafika Kateshi katika kuhakikisha tunaongeza msukumo ili wananchi wake waweze kupata maji safi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsate sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Waheshimiwa, tuendeleo na swali linalofuata la Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini.

Na. 445

Pesa Iliyotengwa kwa Ajili ya Bwawa la Mkomazi

MHE. MARY P. CHATANDA - (K.n.y MHE. STEPHEN H. NGONYANI) aliuliza:-

Serikali ilitenga shilingi bilioni 13 kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Mkomazi lakini baadaye Serikali ilihamishia fedha hizo mkoa mwingine:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha fedha hizo ili bwawa lililokusudiwa lijengwe?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimpe pole Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wake wa Korogwe Vijijini kwa msiba wa kufiwa na mke wake kipenzi. Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya marehemu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2003 na 2004 wananchi wa Kijiji cha Manga Mikocheni, Kata ya Mkomazi, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe walionesha hitaji la mradi

wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa zao la mpunga katika Bonde la Mkomazi. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa wakati huo kupitia Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro ilifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali ambapo walibaini kuwa jumla ya shilingi bilioni 13 zingehitajika kuendeleza bonde la Mkomazi ikiwemo ujenzi wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Spika, aidha, upembuzi huo, ulibainisha kuwa ujenzi wa bwawa hili ungesababisha Ziwa Manga lilipopo katika Kijiji cha Manga ambalo lina maji ya chumvi kuchanganya maji yake ya Bwawa la Mkomazi hivyo maji yote kuwa ya chumvi ambayo yangeathiri kilimo cha zao la mpunga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hii mwaka 2014/2015, Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro ilifanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kuepuka kuzamisha Ziwa Manga na kubaini kuwa jumla ya shilingi bilioni 1.5 zingehitajika kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia bajeti ya mwaka 2015/2016, ilitenga jumla ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Mkomazi. Hata hivyo, fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo hazikupatikana na hivyo kusababisha mradi huo kutotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa mradi huo na hasa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inatarajia kuliingiza bwawa hilo katika vipaumbele vya kutekeleza Mpango Kabambe wa Umwagiliaji wa Taifa ambao kwa sasa unafanyiwa mapitio kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*). Mapitio hayo yanatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2018. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mary Chatanda.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilikuwa bado haijaupa kipaumbele mradi huu na sasa wanasema walishaliweka katika vipaumbele vya kutekeleza mradi huu kama mradi kabambe wa umwagiliaji. Je, sasa Waziri atakuwa tayari kufuatana na Mbunge wa Jimbo ndugu yangu Stephen Ngonyani baada ya Bunge hili ili kwenda kuwaeleza wananchi wa Mkomazi kutokana na mradi huu kuwa unasuasua kwa muda mrefu?

La pili, kwa kuwa atakapokuwa anapita kwenda Mkomazi, kwa kuwa kauli mbiu ya Rais wetu mpendwa ni Hapa Kazi tu, je, atakuwa tayari kupita Korogwe Mjini kwenye mradi wa kwa Mgumi wa umwagiliaji ili aweze kwenda kuuona na hatimaye kuweza kuufanyia kazi kutokana na matatizo walionayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, ukitokea Pangani kupita Korogwe waweza.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, natambua kazi nzuri sana inayofanywa na Mheshimiwa Mbunge Hillary Ngonyani, Maji Marefu, kaka yangu, nataka nimhakikishie kwamba *striker* haogopi *back*. Kama Mbunge wa Jimbo la Pangani na Naibu Waziri wa Maji nipo tayari kwenda kuzungumza na wananchi wa Korogwe katika kuwahakikishia kwamba kilimo cha umwagiliaji kitafanyika katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, lingine nimhakikishie Mheshimiwa mama yangu Mary Chatanda tumekwisha kubaliana baada ya Bunge hili nitapita Kateshi, nitapitia Mkoa wa Tanga kufanya ziara yangu kuhakikisha wananchi wa Mkoa wangu wa Tanga wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Lubeleje, swali la nyongeza na Mheshimiwa mama Anne Kilango.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa kuna skimu za umwagiliaji ambazo zilijengwa sasa ni miaka 10 hazijafanyiwa ukarabati, katika Kijiji cha Chamkoroma, Mseta, Tumbugwe, Mlembule, Boli na Injovu. Hakuna hata mtaalam mmoja ambaye amepitia kuziona skimu zile. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda kukagua skimu za umwagiliaji katika maeneo haya?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Maji na Umwagiliaji. Swali hilo muhimu kabisa.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwa kutambua sasa hivi tunaelekea katika uchumi wa viwanda na uchumi wa viwanda unategemeana kabisa na kilimo cha umwagiliaji. Nipo tayari Mheshimiwa Mbunge kuongozana na yeye katika kuhakikisha tunakwenda kuziangalia skimu zile zake za umwagiliaji.

SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Kwa kuwa Kata ya Mkomazi ni jirani sana na Kata Ndungu na kwa kuwa pale kwenye Kata Ndungu kuna skimu kubwa sana ya umwagiliaji ambayo inasaidia kilimo kikubwa cha mpunga. Skimu ile sasa imeonekana kwamba imechoka sana na maisha ya wananchi wa Kata ya Ndungu, Kihurio mpaka Kalemawe yapo hatarini; je, Mheshimiwa Waziri atakapotoka Korogwe pale Mkomazi kwa sababu Ndungu ni jirani anatuambia nini, atakuja kuona skimu ile?

SPIKA: Majibu kuhusu skimu maarufu kabisa ya Ndungu. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena ukisoma Tenzi za Rohoni inasema unapotembea na kuzuru wengine naomba usinipite Mwokozi,

sitompita Mheshimiwa mama Anne Kilango katika kuhakikisha wananchi wake wanapata maji. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana. Hilo ndio jibu la siku kwa kweli zuri sana.

Waheshimiwa Wabunge tumalizie swali la mwisho kama mnavyoona la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako na kwa niaba yake litaulizwa na jirani yake Mbunge wa Njombe Mjini, Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo.

Na. 446

Ahadi ya Ujenzi wa Mradi wa Maji Mji wa Makambako

MHE. EDWARD F. MWALONGO - (K.n.y. MHE. DEO K. SANGA) aliuliza:-

Mji wa Makambako unakabiliwa na tatizo kubwa la maji kutokana na ongezeko la watu na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni aliahidi kuanza kwa ujenzi wa mradi wa maji na kazi ya usanifu wa mradi huo imeshafanyika:-

Je, ni lini sasa ujenzi wa mradi huo wa maji utaanza?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia awamu ya kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP I*) imekamisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Makambako. Kazi zitakazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa Bwawa Tagamenda, uchimbaji wa visima virefu vya Idofi na chemichemi ya Bwawani, ujenzi wa bomba kuu na mfumo

wa usambazaji wa maji na matanki makubwa ya kuhifadhi maji. Mradi huo unatarajiwa kunufaisha wananchi wapatao 155,253.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata fedha za kutekeleza mradi huo kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India wa Dola za Marekani milioni 500 zitakazotumika kutekeleza miradi ya maji katika Miji mbalimbali ukiwemo Mji wa Makambako. Tayari Serikali imesaini Mkataba wa Kifedha na Serikali ya India na ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2018/2019.

SPIKA: Mheshimiwa Mwalongo, swali la nyongeza.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza. Utaratibu wa Serikali wa kutekeleza miradi ya maji ni ule ambao unamtaka Mkandarasi atekeleze alete madai na aweze kulipwa. Lakini utaratibu huu umeonesha kwamba Wakandarasi wengi hawana uwezo matokeo yake miradi mingi inachelewa sana kutekelezwa na mingine inaharibika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha utaratibu wa utekelezaji wa miradi wa maji inayoanza kuanzia tarehe 1 mwezi wa 7 ukiwemo huu mradi wa maji wa Makambako?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mkopo nafuu kutoka Serikali ya India unahusu pia vilevile Mji wa Njombe ambao upembuzi yakinifu umefanyika kwa ajili ya kupata maji kutoka chanzo cha Mto Hagafilo na kusambaza katika Mji wa Njombe na sasa huu ni mwaka wa tatu, kila mwaka Serikali inatuambia kwamba mradi huu unaanza. Je, Serikali inatoa majibu gani ya uhakika sasa kuwahakikishia wananchi wa Mji wa Njombe kwamba mradi huu wa maji kutoka Mji wa Hagafilo unaanza kutelekezwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Wizara yetu ya Maji katika kuhakikisha Watanzania wanapata maji safi, salama na yenye kutosheleza, lakini imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo la Wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuona haja sasa Wahandisi wote wa maji kutoka Halmashauri waje kuweka katika Wizara yetu ya Maji ili tuwe na usimamizi wa ukaribu na majukumu ya pamoja katika kuhakikisha tunatua matatizo hayo. Kwa hiyo, mkakati wa Serikali ni kuanzisha sasa Wakala wa Maji Vijijini katika kuhakikisha Watanzania waliokupo vijijini wanafikiwa na asilimia 85 ya upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha, kama nilivyomhakikishia kwamba tumeshasaini mkataba ule wa kupata fedha, niwahakikishie wananchi wa Njombe kwamba watapata maji hayo safi, salama na yenye kuwatosheleza. Sisi kama viongozi wa Wizara tutasimamia kwa ukaribu ili wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza.

SPIKA: Mheshimiwa Mlinga nilikuona kule mwisho, uliza swali.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Jimbo langu la Ulanga Kijiji cha Gombe kuna mradi mmoja mradi wa kiinimacho. Mawaziri wote anapokuja Waziri maji yanajazwa kwenye tanki usiku kucha, akija Waziri asubuhi anakuta yanatoka. Kaja Waziri kafanyiwa hivyo hivyo, kaja Naibu Waziri kafanyiwa hivyo hivyo. Sasa Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kuhusiana na mradi huu kiini macho ambao unafanya wananchi wanashindwa kupata maji?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, nilifanya ziara katika Jimbo la Ulanga na tumefika katika eneo lile tumeona hali ya utekelezaji na moja ya majukumu nilichukua hatua ya kuhakikisha yule Mkandarasi anakamatwa kwa sababu ya kusuasua kwa utekelezaji wa mradi ule. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge nipo tayari kukutana naye leo baada ya saa saba tuangalie wapi walikofikia ili mwisho wa siku na sisi tuendeleo kuongeza nguvu wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Phillip Mulugo nilikuona, tafadhali.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, kwa kweli nashukuru sana kwa kuniona maana yake nikasema mbona ni mrefu kuliko wote lakini nimesimama mara 20. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nataka kumuuliza swali moja la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri. Nakumbuka mwezi Machi alikuja Songwe Wilaya mpya tulikuwa naye kwenye Kata ya Chang'ombe, Kijiji cha Chang'ombe na Mbuyuni na yeye mwenyewe aliona ufasadi wa maji katika mradi wa Chang'ombe uliokuwa unashikiliwa na Mkurugenzi Chunya na sasa ni Wilaya Mpya na aliniahidi kwamba atafuatilia kumrudisha yule Mkandarasi aje amalizie ule mradi wa maji Chang'ombe, lakini mpaka leo kimya. Nini kauli ya Serikali?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la mwisho, Mheshimiwa Aweso, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli nilishafika katika Halmashauri ya Songwe na tumeona changamoto hiyo na nilikwishatoa maagizo kwa Mhandisi wa Maji katika suala zima la kusimamia. Nimwombe Mhandisi wa Maji wa Songwe asimamie maagizo ambayo niliyompa na kama ameshindwa basi ajitathmini, kwa sababu sisi tunachotaka ni kazi na wananchi wale waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa, mtaona kwa uendeshaji wa kisayansi tumemaliza saa nne kamili.

Sasa tunaendelea kwenye matangazo, wageni wa kwa jukwaa la Spika ni wageni wawili wa Mheshimiwa Spika ambao ni Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania Mheshimiwa Jeroen Verheul, karibu sana Mheshimiwa Balozi kutoka Uholanzi. Karibu sana naona Uholanzi mwaka huu haipo kwenye *World Cup*. Pia Afisa Ubalози Neema Simon, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kibaigwa Ndugu Samson Mganga, karibu sana Samson. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 11 wa Mheshimiwa Martin Msuha ambaye ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Elson Msuha. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wawili (2) wa Mheshimiwa Hawa Ghasia ambao ni mtoto wake Ndugu Nasra Mhati na Mheshimiwa Ahmad Chigonda, Diwani wa Kata ya Ndumbwe, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara kutoka Mtwara Vijijini, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ambao ni Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Wapiga Kura wake kutoka Jimbo la Hanang, Mkoa wa Manyara. Karibuni sana Wageni wetu kutoka kule Hanang, mmeona Mbunge wenu anavyowajibika. *(Makofi)*

Wageni watatu (3) wa Mheshimiwa Rhoda Kumchela ambao ni wadogo zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wale pale. *(Makofi)*

Wageni watatu (3) wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambao ni Wajumbe wa Bodi ya KARAWASU kutoka Karatu Mkoani Arusha, karibuni sana ndugu zetu kutoka Karatu. *(Makofi)*

Wageni watano (5) wa Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Dada yake Ndugu Ashura Chikambo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 105 kutoka Chuo Kikuu cha *St. John's* cha hapa Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Yeriko Ngusi. Wageni kutoka *St. John's* karibuni sana wanafunzi kutoka *St. John's* majirani zetu kutoka hapa hapa Dodoma Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo moja; kama mlivyoshuhudia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 *(The Finance Bill 2018)* umeshasomwa kwa Mara ya Kwanza, sasa naelekeza Kamati ya Bajeti waanze mara moja kuufanyia kazi kwa mujibu wa kanuni na taratibu zetu.

Muswada huu kwa mujibu wa ratiba ya Mkutano huu utawasilishwa Bungeni Jumatano ya tarehe 27 Juni, 2018 kwa ajili ya hatua zinazofuata na umepangiwa siku mbili. Kwa hiyo, Kamati ya Bajeti muanze mara moja kuupitia pitia Muswada huu wa Fedha.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Ni wawili tu, watatu. Haya tuanze kama mlivyo. Tuanze hapo tunakwenda kwa Mheshimiwa pale Mary halafu tutamalizia kwa David.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa Kanuni ya 47. Nchi yetu inatumia zaidi ya bilioni 200 kugharamia elimu bure. Jana Serikali ilitangaza wanafunzi 70,000 tu watakaojiunga na kidato cha sita. Ikipendeza jambo hili liwe jambo la dharura kwa sababu waliofanya mitihani walikuwa 385,000 lakini waliopangiwa peke yake kidato cha tano ni 70,000 peke yake.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia watoto hawa wanaomaliza kidato cha nne ni watoto walioko chini ya miaka 16 na katika nchi yetu vyuo vya ufundi na vyuo vya

FDC umeona tulivyokuwa tunalumbana huku havipo. Jamii hii ya Watanzania wengi kiasi hicho wanaotoka kule vijijini ambao Serikali inatumia gharama nyingi kuwasomesha wanaishia kidato cha nne halafu wanarudi kijijini kwenye makundi, wanarudi katika kuvuta bangi na katika makundi mengine ambayo yanaathiri maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Bunge hili kama chombo cha wananchi na kama inavyosimamia Serikali Iijadili jambo hili kama jambo la dharura..

SPIKA: Mheshimiwa Kalanga mpaka sasa hivi sijaelewa hoja yako ni nini yaani sijaelewa. Naona unalalamika tu. Wamechaguliwa 70,000 ndiyo sasa kuna shida gani yaani kuna nini? Ulitaka wachaguliwe wangapi, yaani kuna nini ambacho kimefanyika kinyume ambacho unataka Bunge hili Iijadili.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, inavyoonekana Serikali ilivyotangaza waliofaulu walisema walifaulu zaidi ya 285,000 kati ya 385,000, lakini waliopangiwa peke yake ni 70,000, hao wengine ambao tunatangaziwa 285,000 walifaulu kwenda kidato cha tano wataenda wapi? Ni muhimu jambo hili likatolewa ufafanuzi kwamba waliostahili kupangiwa kidato cha tano ni wangapi na Serikali imewapangia wangapi? Ni kwa nini hao wengine wataenda wapi ambao walifaulu na wastahili kupangiwa lakini hawajapangiwa. *(Makofi)*

SPIKA: TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda, kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Julius Kalanga anafuatilia. Tumetoa maelezo ya kutosha tangu juzi na jana kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimsahihishe, waliochaguliwa kwenda kidato cha tano siyo 70,000 kama anavyosema hapa, ni 58,000. Wengine 16,000 hivi

watakwenda kwenye vyuo mbalimbali ambavyo wamechaguliwa, kwa hiyo. jumla yake ndiyo wanafika 70,000. Kwa hiyo, wale 21,000 ambao wamebaki tunatuma fedha kuanzia wiki ijayo na tumewaagiza kupitia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wakuu wa Mikoa wote wasimamie ujenzi wa haraka wa mabweni katika baadhi ya shule ambazo zipo zinaendelea za *high school* ili mpaka mwezi wa Nane mwishoni wote wawe wameshachukuliwa wamepata nafasi hiyo. (Makofi)

SPIKA: Unaona Bwana Kalanga sasa mjadala wa nini bwana, hakuna haja ya mjadala. Mheshimiwa Mary. Subiri kidogo Mheshimiwa Mary Deo Muro. Mheshimiwa Profesa majibu ya nyongeza tafadhali.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nitoe majibu ya nyongeza kama mtoa sera. Sera yetu ya Elimu kwa sasa elimu ya lazima ni ya elimu ya msingi. Elimu ya Sekondari kwenda kidato cha tano inategemea nafasi zilizopo za kwenda sekondari. Pia niseme kwamba wanaomaliza kidato cha nne haiwezekani wote waende kidato cha tano kwa sababu humo humo kunakuwa na wanaoenda kwenye uuguzi, kuna Bwana Mifugo, kuna Manesi, kwa hiyo kutokana na hayo pia kuna wanaoenda kusomea ualimu, kwa hiyo haiwezekani wote waende *high school*. Kwa hiyo, ni dhana potofu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niweke *record* vizuri kwamba hawa wanaofaulu miongoni mwao, kwa mfano, kusoma ualimu lazima uwe na sifa kama za yule ambaye anaenda kidato cha tano na cha sita. Kwa hiyo, haiwezekani wote wakaenda huko. Tunalalamika hapa tuna uhaba wa walimu tutawapata wapi kama wote wataenda kidato cha tano na cha sita? Kwa hiyo, kuna kozi za cheti na kuna kozi nyingine za *diploma* ambazo pia zinachukua miongoni mwa watu ambao wamefaulu kidato cha nne.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mary nilishakuita Mheshimiwa.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7), nikiomba mwongozo wako kwa sababu swali langu namba 441 halikujibiwa vizuri na halikujibiwa vizuri kwa sababu amejibu kwamba pamoja na kuwa hamna vifaa vya kufundishia lakini wanatoka wakiwa *qualified*.

Mheshimiwa Spika, sasa nimeshindwa kuelewa kama wanasoma *theory* na hawafanyi *practical* wanawezaje kuwa *qualified*. Unampeleka mtoto akajifunze gari, anafundishwa alama za barabarani hafundishwi kuendesha gari na vifaa vya gari vikiharibika, utasema amekuwa *qualified* vipi au kwa Shirika la Elimu pale kulikuwa na mabanda ya kuku ambayo walikuwa wanajifunza kwa kufuga na wakitoka wanatoka na ujuzi wa kufuga kuku. Sasa hivi hamna mabanda wala hamna miradi ile ikiendelea, wanatokaje wakiwa *qualified*?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

SPIKA: Ningeomba Mheshimiwa Mary mtafute muda tu mkae na Naibu Waziri halafu atakufafanulia vizuri. Swali lako ni la msingi sana, ndiyo maana nikauliza ni chuo gani kwa sababu *FDC* Kibaha ilikuwa ni moja ya vyuo vizuri sana vilipojengwa enzi zile, lakini najua baada ya miaka kinaweza kikawa kimepoteza poteza kidogo, kina mpauko fulani. Mheshimiwa Naibu Waziri nitaomba baadaye kwenye kikombe cha chai, basi uweze kumfafanulia Mheshimiwa Mbunge, usiporidhika utarudi kwangu tutaona utaratibu mwingine wa kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Silinde.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba mwongozo kupitia Kanuni yako ya 68(7) kuhusu kuvunjwa kwa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kidogo; sisi katika *order pape* ya leo jana tuliwasilisha Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango ili

isomwe leo katika Bunge lako Tukufu, lakini kwenye *order* yako *paper* imeondolewa na sababu za kuondolewa mpaka muda huu hatujapatiwa. Naomba nieleze kidogo mwenendo mzima wa hili jambo.

SPIKA: Soma kwanza 99(5).

MHE. DAVID E. SILINDE: 99(5) inasema kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara. Asubuhi ya siku ambayo Waziri amepangiwa kuwasilisha hoja ya Makadirio ya Wizara yake, Waziri, Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au Mjumbe yeyote atakayeteuliwa kwa niaba yake na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara husika wataweka mezani nakala ya taarifa zao kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli wa Bunge.

SPIKA: Sasa hiyo kanuni imevunjwaje?

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ndio nakuja. Kanuni iliyovunjwa ni Bunge kuondoa Taarifa ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Kwa hiyo, ninachotaka kueleza ni nini, siku ya Jumamosi majira ya saa 6.31 nilimpigia simu Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge, ndugu Nenelewa kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tutawasilisha Hotuba yetu siku ya Jumatatu. Akaniambia amefurahi sana Kambi ya Upinzani kuleta taarifa Bungeni, tunaomba hiyo taarifa ifike kwetu Jumapili. Nikamwambia sisi tutafikisha kesho Jumapili na akaeleza Jumapili kabla ya saa 10.

Mheshimiwa Spika, uliandika Dokezo lako ambalo kwa ajili ya ku-*support* hii Kanuni ya 95 kwa Wanadhimu Wabunge kwa maana Mheshimiwa Jenista tarehe 19 Aprili, 2017 pamoja na Mheshimiwa Tundu Lissu, hii umeiweka iko ofisini kwetu kwamba hizo taarifa za kambi ziletwe siku moja kabla.

Mheshimiwa Spika, sasa jana Jumapili saa 8.30 nimeleta Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani yenye kurasa 521 ili isomwe na Bunge lako Tukufu ndani ya Bunge, Watanzania waweze kuisikia na wajue nini ambacho maoni ya kwetu sisi Kambi ya Upinzani Bungeni. Nikampigia

Mkurugenzi wa *Hansard*, ndugu Hanifa, tumempigia simu akawa anauliza hiyo hotuba yenu ina kurasa ngapi, baada ya kuuliza kurasa ngapi tukamwambia tunaichapa tunakuletea tuko Bungeni humu humu ndani kwenye Ofisi ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo akawa hapokei simu, tumepiga mara zote hapokei simu, nikampigia Mkurugenzi tena wa Shughuli za Bunge,, nikampigia mara tano hakupokea simu. Nikamtumia *message* kwa ushahidi kwenye simu yangu ipo hapa, nikamtumia *message* tumeleta ile taarifa mbona hupokei simu? Akanijibu Mheshimiwa niko nje ya mji msibani, pelekeni Ofisi ya KB. Tumepeleka Ofisi ya KB wakasema hiyo hotuba haiwezi kupokelewa mpaka kesho asubuhi. Muitunze asubuhi ikifika muilete kwa Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Kagaigai.

Mheshimiwa Spika, asubuhi kwa sababu taarifa tunayo na *message* hizi ninazo, asubuhi hii taarifa imepelekwa kwa Katibu wa Bunge (KB), Ndugu Kagaigai, kapokea kasema hii taarifa yenu hatupokei na wala haitasomwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ikiwa hili Bunge ni letu sote na hii nchi ni yetu sote, wewe hapa tangu mwanzoni unakumbuka kulikuwa na shida moja kwamba wale watumishi wetu wa kuandika hotuba mliposhindwa kuwalipa kama Bunge, sisi Wabunge nafikiri umepata ile barua yako, tumejichanga tunakatwa posho zetu tumeita watu kwa ajili ya kusaidia kuandika hii hotuba ili Watanzania wasikie maoni yetu kama Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tumefanikisha, tumekatwa posho, tumeandika hotuba, tunaleta ndani ya Bunge, Bunge hamtaki, sasa hii tunashindwa kuelewa hivi tufanye nini kwenye hii nchi ndiyo tutaieleweka, kama endapo tumefanya kila namna kuleta hotuba Bungeni imekataliwa na Katibu wa Bunge, Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge anajua, Mkurugenzi wa *Hansard* anajua na tumefuata kanuni zote pamoja na huu mwongozo ulioutoa tarehe 19 Aprili, 2017. Tufanye nini ili muweze kutuelewa kwamba uzalendo siyo uko upande wenu

na asubuhi hii nikawa naangalia umeamka vibaya leo nini. Maana ilikuwa *weekend* ndefu, Idd Mosi, Idd pili, mambo mengi. Sasa unampelekea Katibu *document* asubuhi ya leo.

WABUNGE FULANI: Jana!

SPIKA: Amesema asubuhi ya leo ndiyo ameonana na Katibu wa Bunge. Sikiliza Katibu wa Bunge umeonana naye lini? Si umesema wewe mwenyewe umeonana naye leo asubuhi? Ulionana naye jana Katibu wa Bunge? Nisikilize mbona sisi tumekusikiliza. (*Kicheko*)

Wewe umepelekea leo asubuhi Katibu wa Bunge, wakati *order paper* imeshatoka tangu jana unategemea Katibu wa Bunge afanye nini? Kwa maana hiyo ndiyo utamu-*accuse* kwamba anaharibu Bunge kwa utaratibu huo? Katibu wa Bunge kazi yake ni kusimamia utaratibu. Sasa ni hivi ninyi jamani toka tumeanza Bunge hili la Bajeti mwezi wa Nne hamna hotuba yoyote mliyotoa kwa Wizara yoyote na sababu yake ni kwamba waliokuwa wanawaandikieni hawapo. (*Makofi*)

Sasa kumbe mmeshapata watu wengine wa kuwaandikia, tena hamuoni aibu kusema mnaandikiwa. Badala ya nyie Wabunge kukaa na kuandika hotuba zenu mnaita watu wanawaandikia halafu mnataka kuja kutusomea hapa Bungeni. Kweli kabisa jamani yaani... (*Makofi/Kicheko*)

Bunge lote limepita hili hakuna hotuba ya Upinzani kwa sababu hawapo wa kuwaandikieni, sasa mmechangachanga hela, umesema mwenyewe mmechanga hela, mmeshapata wa kuwaandikieni sasa mnapata ya kurasa 500. Kwa hiyo, hilo tuonane wakati mwingine tulijadili vizuri ilikuwaje; mngeweza hata kunipigia hiyo jana au juzi mlifanya hivyo? Nami napatikana muda wote na nipo hapa Dodoma. Hivyo, kwa sababu hili kwenye *Order Paper* halipo wala halina neno; mtachangia tu tuna siku saba za kuchangia kwa hiyo mambo yaliyopo humo nitawapa nafasi mtayasema kadri tunavyoenda. (*Makofi*)

Tunaendelea, Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI: Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga sheria itakayotoza au kubadilisha baadhi ya kodi, ushuru, tozo na ada mbalimbali, kufanya marekebisho kwenye sheria mbalimbali zinazohusu ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya umma (*A Bill for an Act to impose and alter certain taxes, duties, levies, fees and to amend certain written laws related to the Collection and Management of Public Revenues*).

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 (*The Finance Bill, 2018*)

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

na

Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Ahsante sana, baada ya kusikiliza Hotuba ya Bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Alhamisi iliyopita, sasa tunaendelea na utaratibu ule ambao niliueleza siku ile na tunaanza shughuli hiyo kwa kumwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa

Ghasia ili awasilishe maoni kamati hiyo ambayo Kamati hiyo pia wakina Mheshimiwa Silinde na wenzao wamo ndani ya Kamati hiyo, kwa hiyo maoni haya ni maoni yao wote, Mheshimiwa Hawa Ghasia tafadhali wasilisha taarifa yako. *(Makofi)*

MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 105(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo Januari 2016 naomba kutumia fursa hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bajeti imeendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wake wa Kikanuni wa kuishauri na kuisimamia Serikali pamoja na kusaidia Bunge kuchambua Bajeti ya Serikali kwa kujikita zaidi katika kuangalia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na kusimamia matumizi kwa kulinganisha na hali halisi ya ukuaji wa uchumi wa nchi. Aidha, taarifa hii itawezesha Waheshimiwa Wabunge...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaomba punguzeni sana sauti na ni vizuri mkamsikiliza Mwenyekiti wa Bajeti kwa sababu tuna uchangiaji utakaofuata kwa siku saba na kwa sehemu kubwa uchangiaji wetu uta-*base* na kuongozwa na wenzetu ambao wamekaa na kuchambua. Kwa hiyo, tusikilize kwa makini tafadhali, endelea Mheshimiwa. *(Makofi)*

MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa hii itawezesha Waheshimiwa Wabunge kujielekeza zaidi katika kuishauri na kuisimamia Serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango ili kushauriana kuhusu hoja mahsusi zilizowasilishwa na Kamati mbalimbali za Bunge kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kamati ilitoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kupitia Kamati ya Uongozi.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Kamati kuwa mashauriano haya kati ya Serikali na Bunge kupitia Kamati ya Bajeti yataendelea vema wakati wa mjadala wa Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 (*The Finance Act, 2018*) unaotegemewa kuanza kujadiliwa na Kamati pamoja na wadau mapema wiki hii. Kamati ya Bunge ya Bajeti itatoa taarifa yake kuhusu Muswada huo mara baada ya majadiliano hayo kumalizika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali kuhusiana na mikakati ya kutekeleza bajeti ya Serikali kwa ufanisi na kuimarisha uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu tayari limeshapokea taarifa kuhusu hali na mwenendo wa uchumi kwa mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 kama ilivyowasilishwa tarehe 14 Juni, 2018 na Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango. Taarifa hiyo imebainisha kuwa madhumuni makubwa ya Mpango wa Maendeleo ni kuongeza kasi ya maendeleo ili ifikapo mwaka 2025 nchi iwe imetoka katika kundi la nchi maskini duniani na kuingia katika kundi la nchi zenye kipato cha kati (*middle income country*).

Mheshimiwa Spika, lengo kuu ni kuhakikisha kuwa nchi inajenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa azma hiyo, Kamati ina maoni kuwa kauli mbiu ya ujenzi wa uchumi wa viwanda inapaswa kuzingatia misingi imara na uwezo wa ushindani utakaoiwezesha nchi kukabiliana na changamoto za maendeleo pamoja na kuweka mazingira wezeshi katika utoaji huduma, masoko, biashara, teknolojia na upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, takwimu kuhusu ukuaji wa uchumi kama zilivyoainishwa kwenye Taarifa ya Hali Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 (Ukurasa wa kwanza hadi wa tisa) unaonesha kuwa sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu hazijafanya vizuri na wastani wa mchango wake katika Pato la Taifa ulikuwa ni chini ya 4%. Pamoja na kuwa sekta hizi zinabeba na kugusa maisha ya watu wasiopungua asilimia 66.6 ya Watanzania wote, Serikali imeshindwa kufungamanisha ukuaji wa uchumi na ukuaji wa sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa shughuli zinazofanywa katika sekta hizi zinafanyika kwa tija na zinawaletoa wananchi manufaa na faida iliyo wazi na endelevu ili kupunguza umaskini kwa haraka na uhakika.

Mheshimiwa Spika, pamoja ya kuwa pato la wastani la kila mtu limekuwa na kufikia Sh.2,275,601 kwa mwaka huu, bado kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa ajira nchini hasa kwa vijana na hivyo kuendelea kuongeza mzigo wa utegemezi kwenye utekelezaji wa masuala muhimu ya kijamii. Ajira zinazotolewa na Serikali pamoja na sekta binafsi hazitoshelezi kabisa kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira nchini linaendana pia na viwango vya umaskini. Kama ambavyo wananchi wengi maskini wamekuwa wakikimbilia mijini, ambako hali ya umaskini iko chini kuliko vijijini. Kamati inaona ipo haja kwa Serikali ikishirikiana na sekta binafsi kuona kwa namna gani ukuaji wa uchumi utasaidia kutatua changamoto ya mahitaji ya ajira na kupunguza umaskini wa kipato nchini.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa mfumuko wa bei umepungua na umeendelea kuwa tarakimu moja na kufikia wastani wa asilimia 5.3 kwa mwaka 2017. Utulivu huu unatokana na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula nchini, utulivu wa bei ya nishati hasa mafuta pamoja na uimarishaji wa sera za fedha na kibajeti. Mafanikio hayo ya kupungua kwa mfumuko wa bei yamepatikana kwa kiasi kikubwa wakulima kupata hasara kwa kuuza mazao yao kwa bei ya chini kutokana na agizo la Serikali kuzuia uuzwaji wa mazao nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Desemba, 2017, Dola ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Sh.2,228.86 ikilinganishwa na wastani wa Sh.2,177.07 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Kamati inaona kwamba kasi ndogo ya kuimarika kwa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Kimarekani kunaathiri urari wa biashara hususan katika mauzo ya biashara nje.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara ya Fedha na Mipango inaonesha kuwa, mwenendo wa mikopo na viwango vya riba katika huduma mbalimbali za benki na taasisi za fedha vimeendelea kutegemea nguvu ya soko na hali ya ukwasi unaotokana na sera za fedha na kibajeti kama ambavyo takwimu zilivyoainishwa kwenye Taarifa ya Hali wa Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2017 (ukurasa wa 14 -15).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa mwenendo wa ongezeko la riba zinazotolewa na benki za kibiashara zinaathiri mwenendo wa biashara nchini, hivyo inaitaka Serikali kusimamia ipasavyo sera za fedha ili kudhibiti ongezeko la riba za mikopo ya mwaka mmoja na riba za amana.

Mheshimiwa Spika, ukirejea ukurasa wa 92 wa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017, utaona kuwa kwa ujumla uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje umekuwa ukiongezeka kuliko uuzaji wa bidhaa nje. Urari wa biashara unaonesha kuwa nakisi ina mwenendo wa

kuongezeka badala ya kupungua. Hali hii inachangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kupungua kwa shughuli za uwekezaji na uhamisho wa mitaji. Kamati inasisitiza Serikali kusimamia ipasavyo sera za fedha na kibajeti ili kuimarisha uchumi kupitia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2018 inaonesha kuwa, Tanzania ina wastani wa ongezeko la watu la asilimia 3.1 kwa mwaka. Katika kipindi cha miaka mitano (2013-2018) idadi ya watu imeongezeka kwa kiwango cha watu milioni 7.6 na hivyo kufikia idadi ya watu inayokadiriwa kuwa milioni 54.2. Hii inamaanisha kuwa idadi ya nguvu kazi (*economic active population*) inaongezeka sambamba na idadi ya watu tegemezi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba rasilimali watu inayoongezeka ikaelekezwa kwenye shughuli za uzalishaji ili kupunguza idadi ya watu tegemezi pamoja na kuongeza kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga shilingi trilioni 11.999 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo, sawa na asilimia 38 ya bajeti yote ya Serikali. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 8.969 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi trilioni 3.029 ni fedha za nje. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 kiasi cha shilingi trilioni 5.123 zilikuwa zimetolewa hii ikiwa ni sawa na asilimia 42.7 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha zilizotolewa, kiasi cha shilingi trilioni 4.347 ni fedha za ndani (sawa na asilimia 48) na shilingi bilioni 775.8 ni fedha za nje (sawa na asilimia 26).

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa utolewaji wa fedha za maendeleo ambao ni chini ya nusu ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa unaonesha ni kwa namna gani Serikali imeshindwa kuendana na malengo yake ya kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilipanga kutekeleza miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa hapo chini:-

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa reli ya kati; utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 10 kwa kipande cha Dar es Salaam-Morogoro. Aidha, kwa kipande cha Morogoro-Makutupora hatua za awali zimekamilika. Kamati inashauri Serikali kuharakisha taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya sehemu za Makutupora –Tabora.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuzalisha umeme wa maji Rufiji; Kamati inaunga mkono juhudi za Serikali kwa kuanza kutekeleza mradi huu muhimu ambao utasaidia kupunguza tatizo la umeme nchini kwa kuzalisha *megawatt* 2,100 kwa pamoja. Hata hivyo, Kamati inapata wasiwasi kutokana na kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi huu kutokana na utoaji hafifu wa fedha za mradi. Hii inajidhihirisha katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo mradi huu ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni 224, lakini hadi kufikia mwezi Machi ni shilingi bilioni 3.2 tu ndiyo zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, shamba la miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi, kwa ujumla utekelezaji wa mradi huu unaohusisha Shamba la Mkulazi I (ekari 28,000) na Shamba la Mbigiri – Mkulazi II (ekari 1,200) upo katika hatua nzuri za utekelezaji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mradi huu muhimu kwani utakapokamilika utasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa sukari nchini na kuondoa changamoto ya upatikanaji wa sukari nchini pamoja na kuondoa changamoto ya kodi ya sukari ya viwandani ambayo imekuwepo nchini

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mitambo ya kusindika gesi ya kimiminika, (*LNG*) huko Lindi. Mradi huu utatekelezwa kwa ubia kati ya Shirika la Taifa la Petrol (*TPDC*) na Kampuni za *BG/Shell, Statoil, Orphir, Pavilion na ExxonMobile*. Pamoja na umuhimu wake mkubwa, mradi huu umechukua muda mrefu sana pasipo utekelezaji wake kuanza.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Serikali bado haijalipa fidia wananchi watakaopisha mradi huu hadi hivi sasa. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kukamilisha majadiliano na wawekezaji kuhusu mkakati wa utekelezaji wa mradi huu pamoja na kulipa fidia kwa wananchi Likong’o Mkoani Lindi ili kupisha utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, bado maeneo mengi maalum ya kiuchumi yaliyotengwa kwa ajili ya Uwekezaji (*Special Economic Zones*) hayajaendelezwa. Maeneo hayo ni pamoja na Bagamoyo, Mtwara, kituo cha biashara Kurasini, Kigoma na Ruvuma kwa kuyataja baadhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuendeleza maeneo ambayo tayari imekamilisha ulipaji wafidia kwa kuyawekea miundombinu na kukamilisha ulipaji wa fidia kwa maeneo yale ambayo hayajalipiwa fidia ili kupunguza mzigo wa riba na kuwavutia wawekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na chuma cha Liganga huko Njombe. Taarifa za Serikali zinaeleza kwamba hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kukamilika kwa mfumo wa umiliki wa mitambo ambao utakuwa ni *Build, Own, Operate* badala ya mfumo wa *Build, Own, Operate and Transfer* uliokuwa umependekezwa na Serikali awali.

Mheshimiwa Spika, Majadiliano ya mauziano (*Power Purchase Agreement*) yamekamilika kwa mwekezaji kutumia umeme atakaozalisha. Pamoja na kufikiwa kwa hatua hizo, Kamati inaitaka Serikali kukamilisha haraka ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi pamoja na kukamilisha mchakato wa tangazo la Serikali – *GN* kuhusu vivutio vya uwekezaji vilivyokubaliwa/kubalika ili kuruhusu mwekezaji kuanza ujenzi wa kiwanda cha chuma haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu ili kufufua Kiwanda cha kutengeneza Matairi, Arusha (*General Tyre*). Mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 500. Hata hivyo, mpaka sasa kiwanda hiki bado hakijafufuliwa na kuanza kufanya kazi. Kamati inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya barabara zenye kufungua fursa za kiuchumi. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa ujenzi wa barabara nchini umekuwa na gharama kubwa kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya Wakandarasi wa ujenzi wa barabara hizo, hivyo kusababisha ongezeko la riba kutokana na ucheleweshaji wa malipo. Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya gharama za ujenzi pamoja na kuhakikisha ujenzi huo unakamilika katika muda uliopangwa ili kupunguza kuongezeka kwa gharama kutokana na riba.

Mheshimiwa Spika, kati ya nchi 13 za kipato cha chini, Tanzania ni nchi ya pili baada ya Ethiopia kwa ukuaji wa uchumi wa asilimia 7.1. Jambo la msingi la kujjuliza ni kwa namna gani ukuaji huu wa uchumi unafungamanishwa na maisha ya watu? Ili suala hili liweze kufanikiwa ni lazima Serikali iwekeze kwenye sekta zinazoajiri na kunufaisha wananchi moja kwa moja kama vile maji, elimu, afya na Sekta ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutoa elimu ya msingi bila ada na kuongeza upatikanaji wa vitabu shuleni, bado Sekta ya Elimu inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa miundombinu ya vyumba vya madarasa, nyumba za Walimu pamoja na mabweni.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa afya, bado kuna upungufu mkubwa wa miundombinu ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya na Rufaa kwa baadhi ya Mikoa. Sambamba na hilo, upo upungufu mkubwa wa Watumishi hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Sekta ya Maji inakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa majisafi na salama. Changamoto hii kwa kiasi kikubwa inasababishwa na kutopatikana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji hasa vijijini. Kwa mfano, kiasi cha shilingi bilioni 673.2 zimetengwa na kiasi cha shilingi bilioni 347 tu ndizo ambazo zimetolewa katika bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018; itakumbukwa kuwa siku ya Alhamisi, tarehe 14 Juni, 2018, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha hotuba yake ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati ya Bajeti ilipitia na kufanya tathmini katika maeneo mbalimbali hasa yale yaliyohusu masuala ya kikodi na dhumuni kubwa ni kutoa sura halisi na mwelekeo wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa fedha 2017/2018 na hivyo kuweza kuishauria Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati ya Bajeti iliangalia mwenendo wa mapato ya Serikali. Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato, bado kuna tatizo la ukwepaji wa kodi, ugumu wa kutoza kodi wafanyabiashara walioko katika sekta isiyo rasmi, mazingira yasiyo rafiki ya ulipaji kodi, mlolongo mrefu wa kodi pamoja na utitiri wa kodi, tozo na ada kwa huduma zinazotolewa na mamlaka za udhibiti (*Regulatory Bodies*), matumizi hafifu ya *EFDs*, udhaifu katika usimamizi wa uvunaji wa rasilimali na mchango mdogo na utegemezi wa Mashirika ya Umma katika bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia upya mifumo ya ukusanyaji kodi, viwango vya kodi, ada na

tozo, usimamizi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na Sera za Kodi zisizo rafiki kwa walipa kodi pamoja na kuzingatia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ongezeko la usajili wa walipa kodi siyo kigezo sahihi cha kuongezeka mapato ya kodi bali mifumo ya ulipaji kodi lazima iandaliwe vema. Pia lazima wadau wote wa kodi wahusike katika kulipa kodi na pia sheria zinazosimamia masuala ya fedha na kodi ziheshimiwe kwa pande zote mbili, yaani Serikali na wafanyabiashara. Vile vile kutafuta ufumbuzi wa udhaifu wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ambayo mchango wake katika bajeti ya Serikali umekuwa siyo wa kuridhisha. Pia kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iingie kwenye mfumo rasmi wa kodi ili kusaidia kuongeza mapato; na vile vile kuzijengea uwezo Halmashauri wa kugundua, kujenga na kuendeleza vyanzo vya mapato badala ya Serikali Kuu kuendelea kuvichukua na kuvihamishia Serikali Kuu vyanzo vinavyokusanyika kirahisi na kuwaachia vyanzo vyenye kero katika ukusanyaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa matumizi ya Serikali kwa mwaka 2017/2018, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 19.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 11.99 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mwenendo unaonesha hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 Serikali imetoa kiasi cha shilingi trilioni 21.68 sawa na asilimia 68.4 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 16.56 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 84 ya lengo la mwaka na shilingi trilioni 5.12 kwa ajili ya maendeleo sawa na asilimia 43 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa matumizi ya kawaida na maendeleo yalikuwa sawa na asilimia 63 ya makadirio ya bajeti ya shilingi trilioni 31.7. Hali hii inaonesha kuwa ni dhahiri kiasi cha shilingi trilioni 10 ambacho ni sawa na asilimia 37 ya bajeti hakiwezi kutolewa ndani ya miezi miwili (Mei na Juni, 2018) ambacho kimebaki. Kamati imebaini kuwa kati ya shilingi trilioni 5.12 zilizotolewa kwa ajili ya

maendeleo, shilingi trilioni 1.72 zilitolewa ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na bandari, shilingi bilioni 581.2 zimetolewa kugharamia mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu; na shilingi bilioni 382 zimetolewa kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa umeme. Kiasi kilichobaki cha shilingi trilioni 2.43 kati ya shilingi trilioni 5.12 zilizotolewa kimegawanywa katika mafungu 44 yaliyobaki yakiwemo ya Sekta za Afya, Elimu ya Msingi na Sekondari, Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huu wa utoaji wa fedha za maendeleo, Kamati inaona kuwa miradi ya reli na umeme ni muhimu kwa Taifa na hivyo inaishauri Serikali kutafuta mikopo nafuu kutoka vyanzo vingine ili kugharamia miradi hiyo. Hatua hii itasaidia kutoa unafuu wa makusanyo ya ndani ili yatumike kugharamia miradi ya maendeleo inayohusisha Sekta za Afya, Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia liliangalia Deni la Serikali na pia ilifanya uchambuzi wa Mifuko mbalimbali. Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa baadhi ya Mifuko iliyoanzishwa kisheria kwa malengo maalum ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, fedha za Mifuko hiyo zimewekewa uzio wa kisheria na hazitakiwi kuwekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa mantiki hiyo, ni vema Bunge lako Tukufu likapata taswira ya utekelezaji wa Mifuko hii ili liweze kushauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Barabara ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tozo ya Mafuta, Sura ya 220 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2006. Aidha, sheria hiyo imebainisha kwamba Mfuko huu utapata mapato yake kutoka kwenye vyanzo vya ushuru wa magari ya kigeni mpakani, tozo ya mafuta ya petroli, dizeli pamoja na faini ya magari yanayozidisha uzito.

Mheshimiwa Spika, aidha, takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mfuko wa Barabara uliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 917.55, lakini hadi kufikia

mwezi Aprili, 2018, jumla ya shilingi bilioni 628.6 sawa na asilimia 68 zilikuwa zimekusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hata hivyo, kati ya kiasi hicho ni shilingi bilioni 604.5 tu ndiyo zilikuwa zimepelekwa katika Bodi ya Barabara na hivyo kuonesha hadi kufikia mwezi Aprili, kiasi cha shilingi bilioni 24 milioni 148.6 bado kilikuwa hakijawasilishwa katika Mfuko wa Barabara. Kamati inaona kuwa ni vyema Bunge lako Tukufu likapatiwa pia taarifa ya makusanyo na utolewaji wa fedha hizo katika miezi ya Mei na Juni, kwa mwaka 2018 ili Mfuko huo uweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati iliingalia Mfuko wa REA ambapo takwimu zinaonesha katika Bajeti ya mwaka 2017/2018, Mfuko ulikuwa umeidhinishwa kiasi cha shilingi bilioni 499.1. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi, kiasi ambacho kilikuwa kimekusanywa ni shilingi bilioni 446.9. Taarifa ya Wizara ya Fedha iliyowasilishwa mbele ya Kamati inaonesha kuwa, kiasi ambacho kilikuwa kimepelekwa ni shilingi bilioni 251.3 fedha ambazo zinatokana na tozo ya mafuta tu. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 165.07 zilizoahidiwa na Washirika wa Maendeleo zilikuwa hakijawasilishwa katika Mfuko Mkuu wa REA.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Maji ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 129.56 na hadi kufikia mwezi Machi, 2017/2018, fedha zilizokuwa zimekusanywa zilikuwa ni shilingi bilioni 117.457 na kiasi cha shilingi bilioni 117.092 kilikuwa kimetolewa. Hata hivyo, tofauti ya kiasi cha shilingi milioni 362 kilikuwa hakijawasilishwa. Aidha, Kamati ilibaini kwamba kulikuwa na *certificates* nyingi za Wakandarasi zenye thamani ya kiasi cha shilingi bilioni 91 ambazo hazijalipwa na Wizara ya Fedha na Mipango zikisubiri uhakiki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za maji nchini, Kamati imebaini kwamba utoaji wa fedha kupeleka kwenye Sekta ya Maji umekuwa ukishuka kwa miaka miwili ukitoa mwaka 2017/2018 na katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 na 2017/2018, sawa na Jedwali la Na.1 hapo chini.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika Mfuko wa Reli ulikuwa na tatizo hilo hilo. Pia kulikuwa na Mfuko wa Uendelezaji Tasnia ya Korosho. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya mabadiliko ya kisheria ambapo liliongeza kifungu cha 17A (1) ambacho kilibainisha jinsi ya utozwaji wa ushuru wa mauzo ya korosho nje ya nchi utakaofanyika na kifungu cha 17A (2) kinaeleza mgawanyo wa fedha zitokanazo na chanzo hicho ambapo asilimia 65 inatakiwa irudishwe Bodi ya Korosho na asilimia 35 inatakiwa kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Kamati imebaini kuwa pamoja na uwepo wa sheria hii, Serikali imeshindwa kupeleka kwenye Bodi ya Korosho kiasi cha Sh.201,281,263,622.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 91.1 ni fedha za mwaka 2015/2016 na shilingi bilioni 110.13 ni fedha za mwaka 2016/2017. Licha ya kwamba Serikali imepeleka kiasi cha shilingi bilioni 10 tu, bado Mfuko huu unaidai Serikali kiasi cha shilingi bilioni 81 katika msimu wa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ya Serikali imeathiri zao hili kwa kiasi kikubwa katika upatikanaji wa pembejeo, viuatilifu, ujenzi wa maghala na kuendeleza utafiti wa zao hilo katika Kituo cha Utafiti wa zao la Korosho cha Naliendele kilichopo Mkoani Mtwara pamoja na kuathiri tasnia ya korosho katika msimu wa mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti pia ilipitia sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019, ambapo iliangalia Sera ya Mapato, Sera ya Matumizi na Deni la Taifa na ugatuaji wa madaraka. Pia Kamati ilitoa maoni katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148; miongoni mwa masuala yaliyoshauriwa na Kamati katika kipindi cha nyuma ni kuhusu kurejesha Mamlaka ya Waziri wa Fedha na Mipango ya kusamehe kodi kwenye mikataba ya misaada au mikopo ya miradi

inayosainiwa baina ya Serikali na Taasisi za Fedha au Benki ambapo Serikali ni mwakilishi.

Mheshimiwa Spika, katika hili, Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali kwa kutoa misamaha hiyo, lakini pia inapendekeza kwamba misamaha hii iende pia katika shule na hospitali binafsi na miradi yote ya kijamii ili kutoa unafuu wa utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetoa ushauri katika hatua ya Serikali kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike (*sanitary pads*), kwamba badala yake Serikali itoze asilimia sifuri ya ongezeko la thamani, hatua ambayo itawasaidia wenye viwanda hivyo kuweza kurudishiwa gharama ambazo wamezitumia katika kuzalisha bidhaa hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yote ya kikodi tutatoa ushauri wake wakati tutakapokuwa tunatoa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa jumla. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali imedhamiria kuanzisha mfumo wa stempu za kodi za kielektroniki ili kudhibiti udanganyifu wa wazalishaji wa bidhaa zinazotowza ushuru kwa bidhaa. Kampuni ya *SCIPA* kutoka Uswisi ndiyo iliyoshinda zabuni hiyo hapa nchini na ina mkataba wa miaka mitatu na Serikali kwa Mfumo wa *Self Financing*. Mfumo huu unamtaka mwekezaji kurudisha gharama zake za uwekezaji kwa kutoa stempu za kielektroniki kwa kila bidhaa inayozalishwa. Kiasi cha fedha kinachotarajiwa kuwekezwa na *SCIPA* ni Dola za Kimarekani 21,000.53 sawa na shilingi bilioni 48.47.

Mheshimiwa Spika, Kamati haina pingamizi na uanzishwaji wa mfumo huu. Jambo la msingi ambalo linahitaji lifanyiwe kazi kwa umakini ni kujiridhisha na gharama za mfumo huu ambazo zitabebwa na watumiaji wa bidhaa pamoja na mapato yatakayopatikana na mwekezaji kutokana na stempu hizi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu ambazo tumezipata za ujazo wa soda, bia na sigara, tunaona kwamba gharama ambazo mwekezaji atazitumia zitaweza kurejeshwa ndani ya mwaka mmoja wakati mkataba unaonesha utakuwa ni wa miaka mitatu. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara ya Fedha ijiridhishe katika suala hilo na ikiwezekana Serikali iwekeze yenyewe ili pesa zitakazopatikana kutokana na suala hili, ziwe ni mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhakiki na ulipaji wa madeni ya Watumishi, Wazabuni na Wakandarasi nchini; Serikali imekuwa ikitumia Kifungu cha (10) cha Sheria ya Bajeti Namba. 11 ya mwaka 2015 pamoja na Kifungu cha tano (5) cha Sheria ya Fedha za Umma kwa mwaka 2001 na marekebisho yake kuhomalisha usimamizi wa fedha za mifuko pamoja na uhakiki wa madeni na ulipaji wake.

Mheshimiwa Spika, ieleweke wazi kwamba Kamati haipingi zoezi la uhakiki na ulipaji wa madeni. Hata hivyo, Kamati inatambua kuwa Katiba imemtaja Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na majukumu yake mengine kuwa ni kukagua ripoti na fedha za Serikali. Aidha, Serikali kupitia kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani imekuwa na utaratibu wa kuweka Wakaguzi wa ndani kwa ajili ya kufanya jukumu hilo la uhakiki.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa uhakiki unaofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango unaleta mkanganyiko katika mgawanyo wa majukumu, kuongeza gharama za Serikali hasa katika kuongeza ongezeko la riba kwenye miradi ya maendeleo pamoja na kuchelewa malipo ya matumizi halali yaliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa mafungu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mathalani kwa upande wa madeni ya ulipaji wa *bill* ya Umeme kutoka *TANESCO* kwenda Jeshi la Polisi au Maji kutoka *DAWASCO* kwenda Magereza nayo yanahakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa mantiki hii, Kamati inajuliza: Je, Wizara ya Fedha na Mipango ikifanya

makosa wakati wa uhakiki na ulipaji, itakaguliwa na nani? Au je, Wizara ya Fedha na Mipango imekuwa haiamini majukumu ya Taasisi nyingine za Serikali? Kwa kuzingatia haya, Kamati inatoa ushauri katika maeneo matatu ambayo yanaweza kupatikana katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeainishiwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya (145) na Ibara ya (146) na imeainisha majukumu yake. Vyombo vya Serikali za Mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa ujumla. Sambamba na hili, sheria mbalimbali zimeainisha muundo wa Serikali za Mitaa pamoja na namna Halmashauri zitakavyopata mapato yake kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaiomba Serikali iheshimu suala la ugatuuji wa madaraka kwenda katika Mamlaka ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuiachia vyanzo vyake vya mapato.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, Kamati ya Bajeti imekuwa ikiishauri Serikali kufanya mabadiliko katika *(The Road and Fuel Tolls Act, Cap 220)* ili kuongeza kiasi cha Sh.50/= kwenye tozo ya mafuta ya dizeli na petroli yanayoingizwa nchini. Kamati imefikia hatua hii baada ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maji na kuona kwamba kuna hitaji la kuongeza Sh.50/= kama fedha ya ziada kwenye chanzo hiki ili kukidhi utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa hiki ni chanzo cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii iingie yote kwenye *Hansard* kama ambavyo imewasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT Refunds*) na asilimia 15 ya amana ya sukari ya viwandani; Serikali imekuwa hairejeshi marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) na amana ya asilimia

15 inayotolewa na viwanda vya sukari. Mfano, kampuni za madini zinaidai Serikali marejesho ya VAT yenye thamani ya shilingi bilioni 600 na wazalishaji wa Sukari wanaidai Serikali jumla ya Shilingi bilioni 35.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilianzisha akaunti ya *Escrow* kwa ajili ya kuhifadhi asilimia 15 ya muamana ambayo iliwekwa kiutawala wala siyo kupitia Sheria ya Bunge kwa lengo la kuzuia matumizi mabaya ya sukari ya viwandani. Hadi mwezi Machi, 2018, akaunti hiyo ilikuwa na Shilingi bilioni 18.2 ambazo bado hazijarejeshwa pamoja na uhakiki wa matumizi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji huu umekuwa na athari kubwa sana kwa Sekta binafsi kwa sababu kimsingi ni mtaji wa matumizi (*operating capital*) ambayo imefungiwa katika akaunti za Serikali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali:-

(i) Kurejeshwa fedha hizo kwa wadau husika ili ziweze kutumika katika biashara zao;

(ii) Kuruhusu kampuni zijirejeshea fedha hizo kupitia Kodi ambazo walipaswa kuilipa Serikali; au

(iii) Serikali itafute utaratibu mwingine wa kudhibiti uingizaji wa sukari ya viwandani ili kuachana na utaratibu huu wa sasa ambao unaathiri uwekezaji wa viwanda vya madawa, vinywaji baridi vyakula kama pipi na *biscuits*, kwa sababu utaratibu huu inaonekana Serikali imeshindwa kuutekeleza yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu asilimia 15 kutoka katika Mashirika ya Umma; Bunge lako lilifanya mabadiliko katika Sheria ya Madaraka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura 370, Kifungu cha 8(1)(f) na kuongeza gawio kutoka asilimia 10 hadi 15 ya pato ghafi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilipanga kukusanya shilingi bilioni 216.957. Hadi mwezi Machi, Serikali ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 309.986, sawa na asilimia 143 ya lengo. Kuvuka kwa lengo kumechangiwa

kwa kiasi kikubwa na gawio kutoka Benki Kuu ambayo ilitoa shilingi bilioni 300, sawa na asilimia 96.7 ya makusanyo yote ya mashirika 26.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaashiria kwamba mashirika 25 yaliyobakia yalichangia wastani wa kiasi cha shilingi milioni 399.455, kila moja. Aidha, Kamati imebaini kuna baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma zinachangia asilimia 15 ilhali wanaidai Serikali fedha nyingi kuliko ambazo zinaichangia, mfano, *DAWASA* imechangia shilingi bilioni 2.9 wakati huo huo inaidai Serikali bilioni 1.9 ambayo zinafanyiwa uhakiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati, inaishauri Serikali kulipa madeni inayodaiwa na Taasisi husika badala ya kuchukua asilimia 15 ya pato ghafi ili kutoa unafuu wa utekelezaji wa majukumu kwa Taasisi husika; kuangalia upya utaratibu wa *retention* kwenye mashirika ambayo yanategemea ruzuku ya Serikali kujiendesha; na kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ili kuruhusu makampuni na taasisi za Serikali zinazotoa asilimia 15 kuruhusiwa kuondoa kiwango hicho (*allowable deduction*) wakati wa kukokotoa kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati iliangalia Soko la Mitaji na Dhamana kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, ambapo ushauri wake tumeonesha katika taarifa yetu na pia tuliangalia utekelezaji wa miradi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo pia tumetolea ufafanuzi.

Mheshimkiwa Spika, kutokana na ugunduzi wa kiwango kikubwa cha gesi, Serikali imekuwa ikipata kodi na tozo na ada mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kuleta maendeleo nchini kwa kusimamia matumizi bora ya mapato ya gesi. Hatua hii imesaidia kuanzisha Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi ili uweze kusaidia kugharamia bajeti ya Serikali kwa upande wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Hotuba ya Bajeti ya Serikali haijaeleza mkakati wowote uliopo katika kuhakikisha

inapata mapato yatokanayo na shughuli za utafutaji na uwekezaji wa mafuta na gesi nchini. Pia taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2017/2018 imeshindwa kuchambua hali ya maendeleo ya Sekta ya Mafuta na Gesi.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa shughuli za utafutaji na uwekezaji wa mafuta na gesi zimekuwa zikipungua siku hadi siku. Tunaiomba Serikali kuangalia ni sababu ipi ambayo inasababisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi kushuka nchini kila siku?

Mheshimiwa Spika, tunaiomba pia Serikali kuangalia utaratibu wa kubakiza baadhi ya mapato ya maeneo mahususi hasa katika Balozi zetu zilizopo nje na upande wa Zimamoto. Utaratibu uliopo sasa wa kuzitaka Balozi zetu kukusanya pesa na kuleta nchini halafu baadaye tuwapelekee, tumekuwa tukipoteza mapato mengi sana kwa sababu wanakusanya kwa pesa labda dola za Canada, wanabadilisha kwenda pesa za Kichina, halafu unapeleka kwenye dola ya Kimarekani, unabadilisha kwenda shilingi ya Kitanzania na baadaye unabadilisha kwa utaratibu huo huo kuwarudishia tena. Sasa kumekuwa na pesa ambazo zinapotea kutokana na suala la ubadilishaji ambao tunaita *exchange loss*.

Mheshimiwa spika, kwa hiyo, tunaomba Serikali iuangelie utaratibu huu ili ikiwezekana Balozi zetu zirejeshe kile kiasi ambacho wanakusanya zaidi, lakini kile kinachoendana na bajeti yao wabakiziwe.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mapendekezo na maoni ya Kamati yetu. Pia napenda kumshukuru kwa namna ya kipekee Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati Vijijini, Makamu Mwenyekiti, kwa ushirikiano anaonipatia. Pia, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati wote ambao kwa kweli wamefanya kazi usiku na mchana na bila kuangalia hata Iddi hii, walikuwa bado wanaifanyia uchambuzi taarifa hii. Naomba majina yao yote yaingie kwenye *Hansard*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na Katibu Mkuu pamoja na Naibu Makatibu Wakuu na Wataalam wote kwa ushirikiano ambao wametupatia kama Kamati na pia kwa kupokea ushauri ambao tumekuwa tukiwashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa namna ya kipekee nirudie tena kukushukuru wewe binafsi na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Naibu Spika; na Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge pamoja na Watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Pia kwa namna ya pekee, naishukuru Sekretarieti yetu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kuhakikisha kwamba taarifa hii inafika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho na siyo kwa umuhimu niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtwara Vijijini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa vipindi vitatu mfululizo. Napenda niwahakikishie kwamba sitawaangusha na nitaendelea kuwajengea heshima na kushirikiana nao katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu la Mtwara Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ambayo imechambua hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Kwa kweli mmefanya kazi wakati wa Sikukuu na hata wakati wa *weekend* mlikuwa mnakutana na mmefanya kazi kubwa kutupatia ripoti hii yenye kurasa 60.

Nawapongezeni sana Kamati ya bajeti na hii itakuwa mwongozo kwa wachangiaji mlio wengi kuona Kamati ilipochambua imesema nini. Kwa kweli hiki ndicho tunachokitaka Bungeni, kwamba kinasomwa kitu ambacho Wabunge wenyewe wamekaa wakachambua wao wenyewe, wakaandika wakaleta. *(Makofi)*

Tofauti na wenzetu wanaolalamika kwamba wameandikiwa huko, halafu wanakuja na vitu lundo kumbe wameandikiwa. Ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakakaa wenyewe wakaandika maoni yao wenyewe. Hata mnapochangia humu, changieni maoni yenu wenyewe badala ya kuletewa na watu ambao hawapo hapa, hawaelewi kinachoendelea, wala hawajamsikia Waziri wa Fedha akiongea. Taratibu tutafika tu. (*Makofi*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2017, MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2018/19, TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/18 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 105 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo Januari 2016 naomba kutumia fursa hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/19 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bajeti imeendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wake wa Kikanuni wa kuishauri na kuisimamia Serikali pamoja na kusaidia Bunge kuchambua Bajeti ya Serikali kwa kujikita zaidi katika kuangalia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na kusimamia matumizi kwa kulinganisha na hali halisi ya ukuaji wa uchumi wa nchi. Aidha, taarifa hii itawezesha Waheshimiwa Wabunge kujielekeza zaidi katika kuishauri na kuisimamia Serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na wataalamu wa Wizara ya Fedha na Mipango ili kushauriana kuhusu hoja mahsusi zilizowasilishwa na Kamati mbalimbali za Bunge kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18 pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/19. Kamati ilitoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kupitia Kamati ya Uongozi.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Kamati kuwa mashauriano haya kati ya Serikali na Bunge kupitia Kamati ya Bajeti yatandelea vema wakati wa mjadala wa Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 (The Finance Act, 2018) unaotegemewa kuanza kujadiliwa na Kamati pamoja na wadau mapema wiki hii. Kamati ya Bunge ya Bajeti itatoa taarifa yake kuhusu Muswada huo mara baada ya majadiliano hayo kumalizika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali kuhusiana na mikakati ya kutekeleza bajeti ya Serikali kwa ufanisi na kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

SEHEMU YA PILI

2.0. UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI KUHUSU MWENENDO WA UCHUMI KWA MWAKA WA FEDHA 2017

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu tayari limeshapokea taarifa kuhusu hali na mwenendo wa uchumi kwa mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19 kama ilivyowasilishwa tarehe 14 Juni, 2018 na Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango. Taarifa hiyo imebainisha kuwa madhumuni makubwa ya Mpango wa Maendeleo ni kuongeza kasi ya maendeleo ili ifikapo mwaka 2025 nchi iwe imetoka katika kundi la nchi maskini duniani na kuingia katika kundi la nchi zenye kipato cha kati (middle income country). Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa *'Nchi inajenga Uchumi wa Viwanda ili kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo watu'* kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa azma hiyo, Kamati ina maoni kuwa kauli mbiu ya ujenzi wa uchumi wa viwanda inapaswa kuzingatia misingi imara na uwezo wa ushindani utakaoiwezesha nchi kukabiliana na changamoto za maendeleo pamoja na kuweka mazingira wezeshi katika utoaji huduma, masoko, biashara na teknolojia na upatikanaji wa ajira.

2.1. Ukuaji wa Uchumi na Kuondoa Umasikini

Mheshimiwa Spika, takwimu kuhusu ukuaji wa uchumi kama zilivyoanishwa kwenye Taarifa ya Hali Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 (Uk. 1-9) unaonesha kuwa Sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu hazijafanya vizuri na wastani wa mchango wake katika Pato la Taifa ulikuwa ni chini ya 4%. Pamoja na kuwa sekta hizi zinabeba na kugusa maisha ya watu wasiopungua asilimia 66.6 ya watanzania wote, Serikali imeshindwa kufungamanisha ukuaji wa uchumi na ukuaji wa sekta hizi. Kamati inashauri kuwa ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa shughuli zinazofanywa katika sekta hizi zinafanyika kwa tija na zinawaletea Wananchi manufaa na faida iliyo wazi na endelevu ili kupunguza umasikini kwa haraka na uhakika.

2.2. Upatikanaji wa ajira

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Pato la Wastani la kila mtu limekuwa na kufikia shilingi 2,275,601 kwa mwaka huu, bado kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa ajira nchini hasa kwa vijana na hivyo kuendelea kuongeza mzigo wa utegemezi kwenye utekelezaji wa masuala muhimu ya kijamii. Ajira zinazotolewa na Serikali pamoja na Sekta ya Binafsi hazitoshelezi kabisa kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la ajira nchini. Tatizo la ajira nchini linaendana pia na viwango vya umaskini, kama ambavyo wananchi wengi maskini wamekuwa wakikimbilia mijini, ambako hali ya umaskini iko chini kuliko vijijini. Kamati inaona ipo haja kwa Serikali ikishirikiana na Sekta Binafsi kuona kwa namna gani ukuaji wa uchumi utasaidia kutatua changamoto ya mahitaji ya ajira na kupunguza umaskini wa kipato nchini.

2.3. Mwenendo wa Mfumuko wa Bei na Thamani ya Shilingi

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa mfumuko wa bei umepungua na umeendelea kuwa tarakimu moja na kufikia wastani wa asilimia 5.3 kwa mwaka 2017. Utulivu huu unatokana na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula nchini, utulivu wa bei ya nishati hasa mafuta pamoja na uimarishaji wa sera za fedha na bajeti. Mafanikio hayo ya kupungua kwa mfumuko wa bei (core inflation) yamepatikana kwa wakulima kupata hasara ya kuza mazao yao kwa bei ya chini kutokana na agizo la Serikali kuzuia uuzwaji wa mazao nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Desemba 2017, Dola moja ya Kimarekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,228.86 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,177.07 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Kamati inaona kwamba kasi ndogo ya kuimarika kwa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Kimarekani kunaathiri urari wa biashara hususan katika mauzo ya bidhaa nje.

2.4. Sekta ya Fedha: Mwenendo wa mikopo na viwango vya riba

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara ya Fedha na Mipango inaonesha kuwa, mwenendo wa mikopo na viwango vya riba katika huduma mbalimbali za Benki na Taasisi za Fedha vimeendelea kutegemea nguvu ya soko na hali ya ukwasi unaotokana na sera za fedha na kibajeti kama ambavyo takwimu zilivyoainishwa kwenye Taarifa ya Hali wa Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 (uk.14-15). Kamati inaona kuwa mwenendo wa ongezeko la riba zinazotolewa na Benki za Biashara zinaathiri mwenendo wa biashara nchini hivyo inaitaka Serikali kusimamia ipasavyo sera za fedha ili kudhibiti ongezeko la riba za mikopo ya mwaka mmoja na riba za amana.

2.5. Uuzaji, uagizaji wa bidhaa na huduma nje:

Mheshimiwa Spika, ukirejea ukurasa wa 92 wa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017, utaona kuwa kwa

ujumla uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje umekuwa ukiongezeka kuliko uuzaji wa bidhaa nje. Urari wa biashara unaonesha kuwa nakisi ina mwenendo wa kuongezeka badala ya kupungua. Hali hii inachangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kupungua kwa shughuli za uwekezaji na uhamisho wa mitaji. Kamati inasisitiza Serikali kusimamia ipasavyo sera za fedha na kibajeti ili kuimarisha uchumi kupitia sekta hii.

2.6. Ongezeko la idadi ya watu

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2018 inaonesha kuwa, Tanzania ina wastani wa ongezeko la watu la asilimia 3.1 kwa mwaka. Katika kipindi cha miaka mitano (2013-2018) idadi ya watu imeongezeka kwa kiwango cha watu milioni 7.6 na hivyo kufikia idadi ya watu inayokadiriwa kuwa milioni 54.2. Hii inamaanisha kuwa idadi ya nguvu kazi (economic active population) inaongezeka sambamba na idadi ya watu tegemezi (non-working population). Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba rasilimali watu inayoongezeka ikaelekezwa kwenye shughuli za uzalishaji ili kupunguza idadi ya watu tegemezi pamoja na kuongeza kipato kwa wananchi.

SEHEMU YA TATU

3.0. UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

3.1. Utangulizi

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, Serikali ilitenga **shilingi trilioni 11.999** kwa ajili ya bajeti ya maendeleo, sawa na asilimia 38 ya bajeti yote ya Serikali. Kati ya fedha hizo, **shilingi trilioni 8.969** zilikuwa ni fedha za ndani na **shilingi trilioni 3.029** ni fedha za nje. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 kiasi cha shilingi **Trilioni 5.123** zilikuwa zimetolewa hii ikiwa ni sawa na asilimia 42.7 ya Bajeti ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizotolewa, kiasi cha

shilingi **trilioni 4.347** ni fedha za ndani (sawa na asilimia 48) na **shilingi bilioni 775.8** ni fedha za nje (sawa na asilimia 26).

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa utolewaji wa fedha za maendeleo ambao ni chini ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa unaonesha ni kwa namna gani Serikali imeshindwa kuendana na malengo yake ya kuhakiksha miradi ya maendeleo inatekelezwa kama ilivyo pangwa.

3.2. Mwenendo wa Utekelezaji wa Miradi ya maendeleo Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2017/18 Serikali ilipanga kutekeleza miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini:-

i. **Ujenzi wa Reli ya Kati.**

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 10 kwa kipande cha Dar es Salaam-Morogoro(uk.23). Aidha, kwa kipande cha Morogoro-Makutupora hatua za awali zimekamiliika. Kamati inashauri Serikali kuharakisha taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya sehemu za Makutupora – Tabora.

ii. **Mradi wa kuzalisha Umeme wa Maji Rufiji (Rufiji Hydro Power Project).**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono juhudi za Serikali kwa kuanza kutekeleza mradi huu muhimu ambao utasaidia kupunguza tatizo la umeme nchini kwa kuzalisha MW 2,100 kwa pamoja. Hata hivyo kamati inapata wasiwasi kutokana na kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi huu kutokana na utoaji hafifu wa fedha za mradi. Hii inajidhihirisha katika mwaka wa fedha 2017/18 ambapo Mradi huu ulitengewa kiasi cha Shilingi bilioni 224, lakini hadi kufikia mwezi Machi ni shilingi bilioni 3.2 tu ndiyo zilikuwa zimetolewa.

iii. **Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi.**

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla utekelezaji wa mradi huu unaohusisha Shamba la Mkulazi I (ekari 28,000) na Shamba la Mbigiri – Mkulazi II (ekari 1,200) upo katika hatua nzuri za

utekelezaji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mradi huu muhimu kwani utakapokamilika utasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa sukari nchini na kuondoa changamoto kubwa ya upatikanaji wa sukari nchini pamoja na kuondoa changamoto ya kikodi ya sukari ya viwandani ambayo imekuwepo nchini.

iv. **Ujenzi wa mitambo ya kusindika Gesi ya kimiminika, Lindi (LNG)**

Mheshimiwa Spika, Mradi huu utatekelezwa kwa ubia kati ya Shirika la Taifa la Petrol (TPDC) na Kampuni za BG/Shell, Statoil, Orphir, Pavilion na ExxonMobil. Pamoja na umuhimu wake mkubwa, mradi huu umechukuwa muda mrefu sana pasipo utekelezaji wake kuanza. Kamati imebaini kuwa Serikali bado haijalipa fidia wananchi watakaopisha mradi huo hadi hivi sasa. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kukamilisha majadiliano na wawekezaji kuhusu mkataba wa utekelezaji wa mradi huu pamoja na kulipa fidia kwa wananchi kijiji cha Likong'o Mkoani Lindi ili kupisha utekelezaji wa mradi huu.

v. **Maeneo Maalum ya Kiuchumi.**

Mheshimiwa Spika, bado maeneo mengi maalum ya Kiuchumi yaliyotengwa kwa ajili ya Uwekezaji (Special Economic Zones) hayajaendelezwa. Maeneo hayo ni pamoja na Bagamoyo, Mtwara, kituo cha biashara Kurasini, Kigoma na Ruvuma kwa kuyataja baadhi. Kamati inashauri Serikali kuendeleza maeneo ambayo tayari imekamilisha ulipaji wafidia kwa kuyawekea miundombinu na kukamilisha ulipaji wa fidia ili kupunguza mzigo wa riba na kuwavutia wawekezaji.

vi. **Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga – Njombe.**

Mheshimiwa Spika, taarifa za Serikali zinaeleza kwamba hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kukamilika kwa mfumo wa umiliki wa mitambo ambao utakuwa ni Build, Own, Operate badala ya mfumo wa Build, Own, Operate and Transfer uliokuwa umependekezwa na

Serikali awali. Majadiliano ya mauziano (*Power Purchase Agreement*) yamekamiliwa kwa mwekezaji kutumia umeme atakaozalisha (250 MW) na kutumia yeye mwenyewe. Pamoja na kufikiwa kwa hatua hizo, Kamati inaitaka Serikali kukamilisha haraka ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi pamoja na kukamilisha mchakato wa tangazo la Serikali – GN kuhusu vivutio vya uwekezaji vilivyokubaliwa/kubalika ili kuruhusu mwekezaji kuanza ujenzi wa kiwanda cha chuma haraka iwezekanavyo.

vii. **Kiwanda cha Kutengeneza Matairi Arusha (General Tyre)**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu ili kufufua kiwanda hicho. mwaka 2017/2018 Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi milioni 500. Hata hivyo, mpaka sasa Kiwanda hiki bado hakijafufuliwa na kuanza kufanya kazi. Kamati inataka Serikali ilieleze Bunge lako hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu.

viii. **Miundombinu ya Barabara**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya barabara zenye kufungua fursa za kiuchumi. Hata hivyo Kamati imebaini kuwa ujenzi wa barabara nchini umekuwa na gharama kubwa kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi waujenzi wa barabara hizo, hivyo kusababisha ongezeko la riba kutokana na ucheleweshaji wa malipo. Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya gharama za ujenzi pamoja na kuhakiksha ujenzi huo unakamilika katika muda uliopangwa ili kupunguza kuongezeka kwa gharama kutokana na riba.

ix. **Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu**

Mheshimiwa Spika, kati ya nchi 13 za kipato cha chini Tanzania ni nchi ya pili baada ya Ethiopia kwa ukuaji wa uchumi wa asilimia 7.1. Jambo la msingi la kujiuliza ni kwa namna gani ukuaji huu wa uchumi unafungamanishwa na

maisha ya watu. Ili suala hili liweze kufanikiwa ni lazima Serikali iwekeze kwenye sekta zinazoajiri na kunufaisha wananchi moja kwa moja kama vile maji, elimu, afya na sekta ya kilimo. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kutoa elimu ya msingi bila ada na kuongeza upatikanaji wa vitabu mashuleni bado sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa miundombinu ya vyumba vya madarasa, nyumba za walimu pamoja na mabweni. Aidha, kwa upande wa afya bado kuna upungufu mkubwa wa miundo mbinu ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya na Rufaa kwa baadhi ya mikoa. Sambamba na hilo upo upungufu mkubwa wa watumishi katika maeneo mengi hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, sekta ya maji inakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa maji safi na salama. Changamoto hii kwa kiasi kikubwa inasababishwa na kutopatikana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji hasa vijijini. Kwa mfano kiasi cha shilingi bilioni 673.2 zimetengwa na kiais cha shilingi bilioni 347 zimetolewa.

SEHEMU YA NNE

4.0. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/18.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa siku ya Alhamisi tarehe 14 Juni 2018, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha hotuba yake ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/19. Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipitia na kufanya tathmini katika maeneo mbalimbali hasa yale yaliyohusu masuala ya kikodi na dhumuni kubwa ni kutoa sura halisi na mwelekeo wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2017/18, na hivyo kuweza kuishauria Serikali ipasavyo.

4.1. Mwenendo wa Mapato ya Serikali

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2018, makusanyo ya ndani ukijumlisha na halmashauri yalifikia kiasi cha shilingi **trilioni 14.84** sawa na asilimia 74.3 ya lengo la mwaka. Mapato

yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), yalifikia kiasi cha shilingi **trilioni 12.61**, sawa na asilimia 73.74 ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 17.106** kwa mwaka. Aidha, makusanyo ya maduhuli yalikuwa ni shilingi **trilioni 1.79** sawa na **asilimia 82** ya lengo la mwaka, na makusanyo ya halmashauri yalikuwa shilingi **bilioni 437.6** sawa na **asilimia 64** ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa misaada na mikopo kutoka nje yenye masharti nafuu haukuwa wa kuridhisha ukilinganisha na lengo iliyojiwekea Serikali. Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia Aprili 2018, misaada na mikopo ya kibajeti iliyopokelewa ni **shilingi trilioni 1.865** sawa na **asilimia 47** ya makadirio ya mwaka; Misaada ya kibajeti (GBS) ilipokelewa kiasi cha **shilingi bilioni 70.2** sawa na **asilimia 7** ya makadirio ya mwaka (bilioni 941.2); Mikopo na misaada ya miradi ya maendeleo ilipokelewa kiasi cha **shilingi trilioni 1.612** sawa na **asilimia 65** ya makadirio ya mwaka na Misaada na Mikopo ya Kisekta ya kiasi cha shilingi **bilioni 182.94** sawa na **asilimia 33** ya lengo la mwaka (bilioni 556). Kwa upande wa mikopo ya kibiashara ya ndani, Serikali ilipanga kukopa jumla ya **shilingi trilioni 6.168** kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva (Rollover). Hadi kufikia Mwezi Aprili 2018, Serikali ilikopa jumla ya **shilingi trilioni 4.957** hii ikiwa sawa na **asilimia 80** ya lengo la Mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Mikopo ya Kibiashara kutoka Nje, hadi kufikia Mwezi Aprili 2018 Serikali imeweza kukopa kiasi cha **shilingi bilioni 224.1** hii ikiwa sawa na **asilimia 14** ya makadirio ya iliyoopanga kukopa ya kiasi cha **shilingi bilioni 1,595** ya lengo la mwaka. Mchanganuo kuhusu mwenendo wa ukusanyaji wa mapato umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1** hapa chini.

4.2. Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu mwenendo wa ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuongeza juhudi za

ukusanyaji wa mapato, bado kuna tatizo la ukwepaji wa kodi, ugumu wa kutoza kodi wafanyabiashara walioko katika sekta isiyo rasmi, mazingira yasiyo rafiki ya ulipaji kodi, mlolongo mrefu wa kodi pamoja na utitiri wa kodi, tozo na ada kwa huduma zinazotolewa na mamlaka za udhibiti (*regulatory bodies*), matumizi hafifu ya EFDs, udhaifu katika usimamizi wa uvunaji wa rasilimali na mchango mdogo na utegemezi wa mashirika ya umma katika bajeti ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali kupitia upya mifumo ya ukusanyaji kodi, viwango vya kodi, ada na tozo, usimamizi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na sera za kodi zisizo rafiki kwa mipa kodi pamoja na kuzingatia yafuatayo:-

i) Kwamba, Ongezeko la usajili wa walipa kodi sio kigezo sahihi cha kuongezeka mapato ya kodi bali mifumo ya ulipaji kodi lazima iandaliwe vema;

ii) Lazima wadau wote wa kodi wahusike katika kulipa kodi na pia sheria zinazosimamia masuala ya fedha na kodi ziheshimiwe kwa pande zote mbili yaani Serikali na Wafanyabiashara;

iii) kutafuta ufumbuzi wa udhaifu wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ambayo mchango wake katika bajeti umekuwa sio wa kuridhisha;

iv) Kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iingie kwenye mfumo rasmi wa kodi ili kusaidia kuongeza mapato;

v) Kuzijengea uwezo halmashauri wa kugundua, kujenga na kuendeleza vyanzo vya mapato na badala ya Serikali kuu kuendelea kuvichukua na kuvihamishia Serikali kuu vyanzo vinavyokusanyika kirahisi na kuwaachia vyanzo vyenye kero katika ukusanyaji.

4.3. Mwenendo wa Matumizi ya Serikali

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2017/18 Serikali ilipanga kutumia jumla ya **shilingi trilioni 19.7** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 11.99** kwa ajili ya matumizi ya

maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mwenendo unaonesha hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 Serikali imetoa kiasi cha shilingi **trilioni 21.68** sawa na asilimia 68.4 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 16.56 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 84 ya lengo la mwaka na **shilingi trilioni 5.12** kwa ajili ya maendeleo sawa na asilimia 43 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa matumizi ya kawaida na maendeleo yalikuwa sawa na **asilimia 63** ya makadirio ya bajeti ya shilingi **trilioni 31.71**. Hali hii inaonesha kuwa, ni dhahiri kiasi cha shilingi trilioni 10.03 ambacho ni sawa na **asilimia 37** ya bajeti hakiwezi kutolewa ndani ya miezi miwili (Mei na Juni, 2018). Kamati imebaini kuwa kati ya **shilingi trilioni 5.12** zilizotolewa kwa ajili ya maendeleo, **shilingi trilioni 1.722** zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na bandari, shilingi **bilioni 581.2** zimetolewa kugharamia mikopo ya elimu ya juu na shilingi bilioni 382.0 zimetolewa kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa umeme. Kiasi kilichobaki cha **shilingi trilioni 2.43** kati ya **shilingi trilioni 5.12** zilizotolewa kimegawanywa katika Mafungu 44 yaliyobaki yakiwemo ya sekta za afya, elimu ya msingi na sekondari, maji, kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huu wa utoaji wa fedha za maendeleo Kamati inaona kuwa kwa kuwa miradi ya reli na umeme ni muhimu kwa Taifa inashauri Serikali kutafuta mikopo nafuu kutoka vyanzo vingine ili kugharamia miradi hiyo. Hatua hii itasaidia kutoa unafuu kwa makusanyo ya ndani ili yatumike kugharamia miradi ya maendeleo inayohusisha sekta za afya, maji, kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Vilevile Serikali iangalie uwezekano wa kutumia njia ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya kimkakati. Hatua hii itasaidia kutoa ahueni kwa mapato ya ndani kuelekezwa katika miradi ya sekta ya afya, maji, kilimo, mifugo na uvuvi ambayo haivutii sekta binafsi pia inagusa wananchi walio wengi.

Jedwali Namba 1: Mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa kipindi cha hadi kufikia Aprili 2018.

Na	BAJETI YA SERIKALI	BAJETI YA MWAKA 2017/18	KIASI KIUCHOKUSANYWA HADI KUFIKIA MWEZI APRILI, 2018	ASILIMIA
	MAPATO			
1	Mapato ya Ndani-Serikali Kuu	19,289,695	14,400,928	75%
	• Mapato ya Kodi (TRA)	17,106,336	12,611,019	74%
	• Mapato Yasiyo ya Kodi	2,183,359	1,789,910	82%
2	Mapato ya Halimashauri	687,306	437,607	64%
3	Mikopo/Misaada kutoka Nje	3,971,103	1,865,760	47%
	• Mikopo/Misaada ya Masharti Natuu -GBS	941,258	70,202	7%
	• Misaada na Mikopo ya Miradi	2,473,770	1,612,614	65%
	• Misaada na Mikopo ya Kiseka	556,075	182,944	33%
4	Mikopo ya Ndani na Nje yenye Masharti ya Kibiashara	7,763,882	5,181,981	67%
	• Mikopo ya masharti ya Kibiashara ya nje	1,594,985	224,000	14%
	• Mikopo ya asilimia 11:5 ya GDP (ndani)	1,220,668	832,336	68%
	• Mikopo – Rollover	4,948,229	4,125,645	83%
	MATUMIZI	31,711,986	21,681,729	68%
5	Matumizi ya Kawaida	19,712,394	16,558,566	84%
	o/w (i) Denlia Taita	9,461,433	8,415,741	
	• Malipo ya Riba Ndani	1,025,546	1,099,576	
	• Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover)	4,948,229	4,125,645	
	• Malipo ya Mtaji Denlia Nje	1,182,651	1,117,904	
	• Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hiradhi ya Jamii	1,195,882	1,544,096	95%
	• Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu	435,633		
	(ii) Mishahara	7,205,768	5,631,458	78%
	(iii) Matumizi Mengineyo (OC)	3,045,193	2,511,367	82%
	• Matumizi yana yolingwa (protected expenditure)	1,965,245		
	• Matumizi ya Halimshauri (Own Source)	274,922	194,676	73%
	• Matumizi Mengine ya kuendesha ofisi	785,025		
6	Matumizi ya Maendeleo	11,999,592	5,123,163	43%
	• Fedha za Ndani	8,969,747	4,347,382	48%
	• o/w Matumizi ya Halimashauri	412,384	133,349	32%
	• Fedha za Nje	3,029,845	755,781	26%
	JUMLA YOTE	31,711,986	21,681,729	68%

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango, 2018.

4.4. Deni la Serikali

Mheshimiwa Spika, Deni la Serikali limeendelea kukua kila mwaka kutokana na kuwepo kwa nakisi kwenye bajeti ya Serikali inayoilazimu Serikali kukopa fedha ndani na nje ya nchi ili kuziba pengo hili. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2018, Deni la Serikali lilikuwa **shilingi trilioni 49.65** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 13.4** ikilinganishwa na ashilingi **trilioni 43.79** kwa kipindi cha Aprili, 2017. Kati ya fedha hizi, deni la nje ni **shilingi trilioni 35.60** na la ndani ni **shilingi trilioni 14.05**. Kwa mujibu wa Serikali, sababu kubwa ya kukua kwa Deni hili lilitokana na mikopo ya zamani na inayoendelea yenye masharti nafuu au kibiashara na malimbikizo ya riba ya deni la nje hasa kwa nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Deni la Serikali bado ni himilivu kwa vigezo vyote Taarifa ya CAG, imebainisha kuwa deni la ndani linaongezeka kutokana na Serikali kushindwa kufikia malengo ya ukopeshwaji katika soko la nje hivyo kulazimika kukopa katika soko la ndani pia kuongezeka kwa ubadilishwaji wa hati za ukwasi (*liquidity papers*) kugharamia matumizi ya Serikali. Hii imetokana na makusanyo ya mapato kuendelea kutokidhi matumizi ya Serikali. Takwimu zimeonesha kuwa kuongezeka kwa Deni la Serikali kwa takribani **shilingi trilioni 7** kwa kipindi cha mwaka mmoja kuna chochea ukuaji hafifu wa uchumi. Kwa mwenendo huu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufanya jitihada za kukopa kutoka vyanzo vya nje kwa kuwa kuendelea kukopa kutoka vyanzo vya ndani kunadhoofisha ukuaji wa uchumi hususani kwenye sekta binafsi kwani inashindwa kushindana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti bado inaishauri Serikali kuipatia Bunge mwenendo wa ulipaji wa Deni la Taifa katika kila mikopo ili kuwa na uhakika na kiasi cha fedha kinachotolewa (*fund disbursement*) kulipia deni hili kilingane na kiasi cha fedha kilicholipwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha suala la sovereign credit kwani limechukua muda mrefu licha ya Serikali kukamilisha taratibu zote za kupata kampuni zinazohusika na suala hilo.

SEHEMU YA TANO

5.0. UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MIFUKO MBALIMBALI ILIYOANZISHWA KISHERIA

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa baadhi ya Mifuko iliyoanzishwa kisheria kwa malengo maalum ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, fedha za Mifuko hiyo zimewekewa uzio wa kisheria (ring-fenced) na hazitakiwi kuwekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa mantiki hiyo, ni vema Bunge lako tukufu likapata taswira ya utekelezaji wa Mifuko hii ili liweze kushauri Serikali ipasavyo:-

5.1. Mifuko iliyoanzishwa kisheria kwa ajili ya kutekeleza Miradi Muhsusi ya Maendeleo.

a) Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Barabara ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Barabara na Tozo ya Mafuta (Sura ya 220) iliyofanyiwa mapitio mwaka 2006. Aidha, sheria hiyo imebainisha kwamba Mfuko huo utapata mapato yake kutoka kwenye vyanzo vya ushuru wa magari ya kigeni mpakani, tozo ya mafuta ya petrol, dizeli pamoja na faini ya magari yanayozidisha uzito. Aidha Takwimu zinaonesha kuwa, katika mwaka wa fedha 2017/18, Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) uliidhinishwa jumla ya **Shilingi 917,548,000,000.00** lakini hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 jumla ya **Shilingi 628,637,947,495.59** sawa na **asilimia 68.5** zilikuwa zimekusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hata hivyo kati ya kiasi hicho ni **Shilingi 604,489,346,576.00** tu ndiyo zilikuwa zimepelekwa katika Bodi ya Barabara. Ukirejea Jedwali Na.3 inaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 kiasi cha **Shilingi 24,148,600,919.59** bado hazijawasilishwa katika Bodi ya Barabara. Kamati inaona kuwa ni vema Bunge lako likapatiwa pia taarifa ya makusanyo na utolewaji wa fedha hizo katika miezi ya Mei na Juni, 2018 ili mfuko huo uweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

b) Mfuko wa Umeme Vijijini (*Rural Electrification Fund*)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Umeme Vijijini ulianzishwa kwa lengo la kuchochea usambazaji wa Nishati ya Umeme Vijijini. Vyanzo vya mapato ya Mfuko yametokana na na tozo ya mafuta (Fuel levy), tozo ya umeme pamoja na fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo . Aidha, takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2017/18, mfuko wa REA uliidhinishwa jumla ya **Shilingi 499,090,000,000.00** hata hivyo hadi kufikia mwezi Machi, 2018, kiasi kilichokuwa kimekusanywa kutoka katika vyanzo vyote vya mapato ni kilikuwa **Shilingi 446,911,870,747.00**.

Taarifa ya Wizara ya Fedha na Mipango iliyowasilishwa mbele ya Kamati inaonesha kuwa, kiasi kilichopelekwa na kupokelewa kwenye Mfuko kilikuwa **Shilingi 251,311,259,008.00** ambazo zinatokana na tozo ya mafuta tu. Aidha kiasi cha **Shilingi 165,074,341,017.00** zilizoahidiwa na Washirika wa maendeleo zilikuwa hazijawasilishwa katika Mfuko wa REA (**Rejea Jedwali Na. 1**).

c) Mfuko wa Maendeleo ya Maji

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa maendeleo ya Maji ulianzishwa kwa lengo la kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji inayowakabili Watanzania hasa waishio Vijijini. Aidha, vyanzo vya mapato ya mfuko huu ni Tozo ya Shilingi 50 kutoka kwenye mafuta ya taa, petrol na dizeli. Takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka wa Fedha 2017/18, Mfuko huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 129,563,939,266.00**. Hadi kufikia mwezi Machi 2017/18 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 117,457,000,000** na kiasi cha **Shilingi 117,092,000,000.00** kilitolewa. Hata hivyo, tofauti ya kiasi cha **Shilingi 362,000,000** hakijawasilishwa katika Mfuko wa Maji.

Aidha, Kamati ilibaini kwamba kulikuwa na *Certificate* nyingi za wakandarasi zenye thamani ya kiasi cha **Shilingi 91,000,000,000** ambazo hazijalipwa na Wizara ya Fedha na Mipango zikisubiri uhakiki (**Rejea Jedwali Na. 1**). Pamoja na changamoto za maji nchini, Kamati imebaini kwamba utoaji

wa fedha kupeleka kwenye Sekta ya maji umekuwa ukishuka kwa miaka miwili ukitoa mwaka mmoja wa 2017/18 katika kipindi cha kati ya mwaka 2015/16 na 2017/18 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali la Na. 1** hapo chini. Kamati inamaoni kuwa juhudi za Bunge katika kusimamia Serikali kuhakikisha huduma ya maji inapelekwa vijijini haijafanikiwa ipasavyo.

d) Mfuko wa Maendeleo ya Reli (Railway Development Levy)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Reli ulianzishwa kwa Lengo la kuendeleza na kukarabati miundombinu ya Reli nchini. Chanzo kikuu cha mapato cha mfuko huu ni **asilimia 1.5** ya *Cost Insurance and Freight (CIF)* ya mizigo yote inayoingia nchini kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Takwimu zinaonesha katika mwaka wa fedha 2017/18, Mfuko huu uliidhinishwa kiasi cha jumla ya **Shilingi 504,995,400,000.00**. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi **273,899,280,093**. Aidha, hakuna fedha zozote zilizopelekwa kwenye Mfuko huu.

Aidha, Kamati imebaini kwamba Mfuko wa Reli unadaiwa malimbikizo ya madeni mbalimbali yaliyofikia kiasi cha shilingi **21,994,254,017.63**. Hata hivyo, pamoja na mashauriano na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu ulipaji wa madeni haya, mpaka sasa Kamati ya Bajeti haijapata Taarifa yoyote ya malipo ya madeni ya Wakandarasi waliofanya upembuzi yakinifu wa reli ya Dar es salaam-Tanga-Arusha na Arusha – Musoma, Tabora-Kaliua-Mpanda na Tabora-Uvinza-Kigoma. Hatua hii imeathiri kwa kiasi kikubwa ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya Reli kati ya Tabora–Kaliua-Mpanda na Tabora-Uvinza–Kigoma.

e) Mfuko wa Uendelezaji wa Tasnia ya Korosho

Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya mabadiliko katika Sheria ya Tasnia ya Korosho (*The Cashewnut Industry Act, (Cap.203)*) kwa kuongeza kifungu cha 17A (1) ambacho kinabainisha jinsi utozwaji wa ushuru wa

mauzo ya korosho nje ya nchi utakavyofanyika na 17A (2) kinaeleza mgawanyo wa fedha zitokanazo na chanzo hicho ambapo **asilimia 65** inatakiwa irudishwe Bodi ya Korosho na **asilimia 35** inatakiwa kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Kamati imebaini kuwa pamoja na uwepo wa sheria hii, Serikali imeshindwa kupeleka kwenye Bodi ya Korosho kiasi cha **Shilingi 201,281,363,622.33**.

Aidha, kati ya fedha hizo **Shilingi 91,150,303,392.92**, ni fedha za mwaka **2015/16** na **shilingi 110,131,060,229.49** ni fedha za mwaka 2016/17. Licha kwamba Serikali imepeleka kiasi cha **Shilingi 10,000,000,000.00** tu bado mfuko huu unaidai Serikali kiasi cha Shilingi **81,150,303,392.92** katika msimu wa mwaka 2016/17.

Hatua hii ya Serikali imeathiri zao hili kwa kiasi kikubwa katika upatikanaji wa pembejeo, viuatilifu, ujenzi wa maghala na kuendeleza utafiti wa zao hilo katika kituo cha utafiti wa zao la korosho cha Naliendele kilichopo Mtwara pamoja na kuathiri tasnia ya korosho katika msimu wa kilimo wa mwaka 2018/19.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa mifuko hii, inaonesha kwamba zipo changamoto mbalimbali zinazosababisha kutopelekwa kwa fedha zote mathalani:- **Moja**; Kukiukwa kwa sheria zinazoelekeza matumizi maalum ya fedha za mifuko hii; **Mbili**, Maafisa masuhuli wa mifuko kutokuwa na mamlaka ya kufanya maamuzi ya matumizi ya fedha za Mifuko hiyo mpaka wapewe idhini kutoka Mlipaji Mkuu wa Serikali; **Tatu**, Wizara ya Fedha na Mipango kuanzisha utaratibu wa kubadili matumizi ya fedha zilizotengwa kisheria kwa ajili matumizi maalum, **Nne**, Kiasi cha fedha kinachopelekwa kwenye mifuko husika kutoendana na makusanyo halisi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unaonesha kwa kiasi gani utaratibu huu unavyopunguza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali ya kimkakati.

Jedwali Na.2 Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Miradi ya Maendeleo ya Maji kuanzia Mwaka 2006/7-2017/18

Na	Mwaka	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kiwango Kilichotolewa	% ya Bajeti iliyotolewa
1.	2006/07	166,591,106.150	78,156,420,091	47
2.	2007/08	236,821,758,000	127,310,916,403	54
3.	2008/09	195,820,768,919	213,722,299,922	109
4.	2009/10	293,491,141,828	183,932,564,388	63
5.	2010/11	230,317,297,415	199,580,417,730	87
6.	2011/12	476,777,694,007	127,088,493,263	27
7.	2012/13	465,576,338,442	303,257,000,000	65
8.	2013/14	553,243,200,000	354,220,000,000	64
9.	2014/15	485,269,410,000	249,317,755,999	51
10.	2015/16	485,269,410,000	178,417,970,937	37
11.	2016/17	915,193,937,771	230,997,934,671	25
12.	2017/18	623,606,748,000	347,500,000,000	56

Chanzo:Wizara ya Maji na Umwagiliaji

Jedwali. 3 Mwenendo wa Makusanyo na Utolewaji wa Fedha kwa Mifuko hadi Mwezi Aprili 2018 (Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango)

Na	Jina la Mfuko	Bajeti	Kiasi kilicho kusanywa hadi Aprili	Kiasi kilichotolewa	Kiasi kilichokusanywa na hakijatolewa
1.	Mfuko wa Barabara.	917,548,000,000.00	628,637,947,495.59	604,489,346,576.00	24,148,600,919.59
2.	Mfuko wa Umeme Vijijini	499,090,000,000.00	446,911,870,747.00	251,311,259,008.00	165,074,341,017.00
3.	Mfuko wa Maendeleo ya Maji	129,563,939,266.00	117,092,000,000.00	117,092,000,000.00	362,000,000
4.	Mfuko wa Maendeleo ya Reli	504,995,400,000.00	273,899,280,093	0	0
5.	Mfuko wa Uendelezaji wa zao la Korosho	201,281,363,622.33	110,131,060,229.49	10,000,000,000	100,131,060,229.49

SEHEMU YA SITA

6.0. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango inaonesha Serikali itachukua hatua mbalimbali kwa madhumuni ya kujiongezea mapato ya kodi. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza viwango vya kodi, tozo na ada mbalimbali. Aidha, Serikali inapendekeza kuchukua hatua mbalimbali za kupunguza na kufuta kodi pamoja na kusamehe riba na faini za kodi ili **kujenga na kuimarisha uchumi wa viwanda utakao chochea ajira na ustawi endelevu wa jamii na hivyo kuiongezea Serikali mapato**. Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kupitua na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18 pamoja na ulinganisho wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/19.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi huu ili kupata hali halisi ya mwelekeo wa Bajeti ya Serikali pamoja na utekelezaji wa malengo ya Bajeti yaliyowekwa. Uchambuzi huu unatoa hali halisi ya utekelezaji wa sera za kodi kwenye maeneo husika hasa maeneo yanayohusu Mapato ya Ndani (Mapato ya Kodi na yasiyo na kodi), Mapato ya Halmashauri, Misaada na Mikopo ya kibiashara ya ndani na kutoka nje. Kumekuwepo na ongezeko au punguzo katika baadhi ya maeneo ya mapato na matumizi kwa asilimia kadhaa kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa Sura ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 na Mwaka 2018/19 (Bilioni)


Na	MAPATO	2016/17	2017/18	2018/19	TOFAUTI	UHALSIA	ASILIMIA
		C1	C2	C3	C3-C2		
1	Mipato ya Ndani-Serikali Kuu	17,798,118	19,289,695	20,158,989	869,294	Ongezeko	4.5%
	• Mipato ya Kodi (IRA)	15,105,100	17,106,336	18,000,219	893,883	Ongezeko	5%
	• Mipato ya Vasio ya Kodi	2,693,018	2,183,359	2,158,770	-24,589	Punguzo	11%
2	Mipato ya Halmashauri	665,415	687,306	735,589	48,283	Ongezeko	7%
3	Mikopo/Misaada kutoka Nje	3,600,807	3,971,103	2,676,645	-1,294,458	Punguzo	32.5%
	• Mikopo/Misaada ya Masharti/Matuu-GBS	483,002	941,258	545,765	-395,493	Punguzo	42%
	• Misaada na Mikopo ya Miradi	2,745,659	2,473,770	2,005,016	-430,211	Punguzo	19%
	• Misaada na Mikopo ya Kiekea	372,147	556,075	125,864	-430,211	Punguzo	77%
4	Mikopo ya Ndani na Nje yenye Masharti ya Kibiashara	7,475,264	7,763,882	8,904,727	1,140,845	Ongezeko	15%
	• Mikopo ya masharti ya Kibiashara ya nje	2,100,895	1,594,985	3,111,058	1,516,073	Ongezeko	95%
	• Mikopo ya asilimia 1.5 ya GDP (ndani)	1,597,157	1,220,668	1,193,669	-26,999	Punguzo	2%
	• Mikopo - Rollover	3,777,112	4,948,229	4,600,000	-348,229	Punguzo	7%
	MATUMIZI	C1	C2	C3	C3-C2		
5	Matumizi ya kawaida	17,719,100	19,712,394	20,468,676	756,282	Ongezeko	4%
	o/w (I) Deni la taifa	8,000,000	9,461,433	10,004,480	543,047	Ongezeko	6%
	• Malipo ya Riba Ndani	1,092,162	1,025,546	1,413,631	388,085	Ongezeko	39%
	• Malipo ya Miji Ndani (Rollover)	3,777,112	4,948,229	4,600,000	-348,229	Punguzo	7%
	• Malipo ya Riba na Miji Nje	1,586,640	1,182,651	2,359,320	1,176,669	Ongezeko	99%
	• Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii	1,141,144	1,195,882	1,195,866	-16	Punguzo	0%
	• Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu	402,942	435,633	435,663	0	Hakuna	0%
	(ii) Mishaara	6,600,000	7,205,768	7,369,731	163,963	Ongezeko	2%
	(iii) Matumizi Mengineyo (O/C)	3,119,100	3,045,193	3,094,465	49,272	Ongezeko	1.6%
	• Matumizi yanayolindwa (protected expenditure)	2,492,934	1,985,245	1,902,325	-82,920	Punguzo	4%
	• Matumizi ya Halmashauri (Own Source)	266,166	274,922	389,862	114,940	Ongezeko	42%
	• Matumizi Mengine ya kuendesha ofisi	360,000	785,025	802,279	17,254	Ongezeko	2%
6	Matumizi ya Maendeleo	11,920,503	11,999,592	12,001,273	7,681	Ongezeko	0.06%
	• Fedha za Ndani	8,702,697	8,969,747	9,876,393	906,646	Ongezeko	10%
	• o/w Matumizi ya Halmashauri	399,249	412,384	345,727	-66,657	Punguzo	16%
	• Fedha za Nje	3,117,805	3,029,845	2,130,880	-898,965	Punguzo	30%
	JUMLA YOYE	29,539,603	31,711,986	32,475,950	763,964	Ongezeko	2.4%

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti kwa mwaka 2018/19 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka 2017/18; inaonesha kuwa kutakuwepo na ongezeko la kiasi cha **shilingi bilioni 763.964 (sawa na asilimia 2.4)** ya jumla ya bajeti yote. Pamoja na ongezeko hili bado kutakuwa na nakisi ya bajeti ya **asilimia 3.2 ya Pato la Taifa** (sawa na shilingi trilioni 3.3) Aidha, Mapato ya ndani yataongezeka kwa **asilimia 4.5 (ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 869.294)**; mapato ya mamlaka za Serikali za Mitaa yataongezeka kwa **asilimia 7 (ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 48.283)**; Misaada na mikopo toka nje itapungua kwa **asilimia 32.5 (yatapungua kwa kiasi cha shilingi trilioni 1.29)**; mikopo ya ndani yenye masharti ya kibiashara itaongezeka kwa **asilimia 15 (ongezeko la kiasi cha shilingi trilioni 1.14)**; matumizi ya kawaida yataongezeka kwa **asilimia 4 (ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 756.282)** na matumizi ya maendeleo yataongezeka kwa kiasi kidogo cha **asilimia 0.06 (ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 7.6)**.

Kielelezo Na. 1: ulinganisho wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2016/17, 2017/18 na 2018/19

Kielelezo Na. 1: ulinganisho wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2016/17, 2017/18 na 2018/19

Kielelezo Na. 1: ulinganisho wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2016/17, 2017/18 na 2018/19



Chanzo: Wizara ya Fedha

6.1. Sera za Mapato

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Bajeti kwa mwaka 2018/19, imeainisha hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na Serikali katika kuboresha ukusanyaji wa mapato yatakayofikia jumla ya kiasi cha shilingi trilioni 32.475. Kwa upande wa mapato ya ndani Serikali inalenga kukusanya kiasi cha trilioni 20.158; kati ya fedha hizo, Mapato ya kodi (TRA) ni shilingi trilioni 18.00 (sawa na ongezeko la asilimia 5); Mapato yasiyo ya kodi shilingi trilioni 2.158 (sawa na punguzo la asilimia 11) na Mapato ya Halmashauri shilingi bilioni 735.589 (sawa na ongezeko la asilimia 7) .

Mheshimiwa Spika, mwenendo unaonesha kuwa Serikali itategemea zaidi kupata mapato kutoka vyanzo vya ndani vya kodi. Takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka ujao wa fedha Serikali imeshindwa kubuni mkakati wa kuwezesha kuongeza mapato yasiyo ya kikodi ambayo yamepungua kwa asilimia 11 (punguzo la bilioni 24.58).

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa angalizo kuwa, ipo haja ya kuhakikisha kuwa ongezeko hili la mapato halifikiwi kwa kuanzisha kodi mpya au kuongeza viwango vya kodi bali kwa kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato toka katika vyanzo vilivyopo pamoja na kuweka mfumo thabiti wa usimamizi na ufuatiliaji wa ulipaji kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inategemea kupata kiasi cha **shilingi trilioni 2.67** kutoka kwenye misaada na mikopo ya kutoka nje. Kiasi hiki ni sawa pungufu ya **asilimia 32.5** ukilinganisha na Bajeti ya Serikali mwaka wa fedha 2017/18 (trilioni 3.9). Ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka 2017/18 utaona kuwa katika Sura ya Bajeti kwa mwaka 2018/19, Misaada ya kibajeti (GBS) imepungua kwa asilimia 42 (pungufu ya bilioni 395.49), Misaada na Mikopo ya miradi ya maendeleo imepungua kwa asilimia 19 (pungufu ya **shilingi bilioni 468.75**) na misaada na mikopo ya kisékta imepungua kwa asilimia 77 (pungufu ya **shilingi bilioni 430.02**).

Aidha, kwa upande wa mikopo ya masharti ya kibiashara kutoka nje, Serikali imepanga kukopa kiasi cha **shilingi trilioni 3.11** sawa na ongezeko la **asilimia 95** ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2017/18

Mheshimiwa Spika, Kamati inajuliza kuwa upungufu huu mkubwa wa mikopo na misaada kutoka nje unatokana na nini? Je ni Serikali kujizatiti kimapato? au ni kwa sababu Serikali halkidhi vigezo na masharti ya kupata misaada na mikopo ya masharti nafuu. Kama hivyo ndivyo, juhudi gani zinafanywa ili kufikia viwango na vigezo hivyo vya mikopo na misaada kwa ajili ya mwaka 2018/19.


Mheshimiwa Spika, ingawa juhudi mbalimbali zimeoneshwa na Serikali katika kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2017/18, hata hivyo hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 Serikali imeweza kupata kiasi cha **shilingi bilioni 224.1 tu** hii ikiwa sawa na **asilimia 14** ya makadirio ya mikopo iliyopanga kukopa ya kiasi cha **shilingi bilioni 1,595** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika mwaka 2018/19 Serikali inategemea kukopa tena kiasi cha **shilingi trilioni 2.13** kutoka kwenye masoko ya fedha ya kimataifa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ya kimkakati. Hata hivyo, Kamati imeshindwa kubaini kutoka kwenye Hotuba ya Bajeti ya Serikali kiasi hicho cha **shilingi trilioni 2.13** zimepangwa kutekeleza miradi ipi mahsusi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inategemea kupata mapato yake kupitia soko la fedha la ndani kwa utaratibu wa kuuza dhamana za muda mfupi na hatifungani za Serikali pamoja na mikopo ya masharti ya kibiashara. Kwa ujumla Mikopo ya ndani inategemea kuwa kiasi cha **shilingi trilioni 5.793** hii ikiwa ni punguzo la **asilimia 6** ikilinganishwa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18.

Kamati inaona kwamba punguzo la mikopo ya ndani inatokana na ukweli kwamba kwa sasa sekta za fedha hazifanyi vizuri katika kuchochea ukuaji wa uchumi, hivyo kuendelea kukopa ndani kutaendelea kuathiri uwezo wa

mabenki kukopesha sekta binafsi pamoja na kudumaza ukuaji wa sekta za fedha nchini. Kamati inamaoni kuwa hatua ya Serikali kukopa nje kiasi cha **shilingi trilioni 3.1** ili kuweza kugharamia bajeti yake ni hatua njema. Hata hivyo Kamati inatoa angalizo kuwa masharti ya mikopo hiyo yazingatiwe uhimilivu wa Deni la Serikali na fedha za mikopo hiyo ilekezwe kwenye miradi ya maendeleo ambayo itachochea ukuaji wa uchumi.

Kielelezo Na 2: ulinganisho wa mapato ya serikali kwa mwaka 2016/17, 2017/18 na 2018/19



Chanzo: Wizara ya Fedha

6.2. Sera za Matumizi

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2018/19 Serikali imepanga kutumia kiasi cha shilingi trilioni 32. 47 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizi kiasi cha shilingi trilioni 20.46 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (sawa na asilimia 63 ya bajeti yote) na shilingi trilioni 12.0 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo (sawa na asilimia 37). Aidha, takwimu zinaonesha kuwa matumizi ya kawaida yanazidi mapato yote ya ndani (ya kodi ya yasiyo ya kodi) kwa kiasi cha **shilingi bilioni 309.687** (sawa na asilimia 1) ya bajeti yote. Hii maana yake ni kwamba mapato yote ya ndani kwa kiasi kikubwa zitatoshwa kugharamia matumizi ya kawaida peke yake. Kutokana na hali hii ni vema Serikali ikasimamia vizuri mapato ili kuhakikisha malengo ya matumizi ya kawaida yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwezo huu wa ya kugharamia matumizi ya kawaida, Deni la Serikali (**shilingi trilioni 10**) bado linachukua kiasi cha asilimia 30 ya bajeti yote ya Serikali na asilimia 49 ya matumizi ya kawaida. Aidha, mishahara (**shilingi trilioni 7.3**) inachukua **asilimia 36** ya matumizi ya kawaida na matumizi mengineyo (OC) (**shilingi trilioni 3.09**) yanachukua **asilimia 15** ya matumizi ya kawaida. Changamoto iliyopo ni kuwa maeneo mawili tu (Deni la Taifa na Mishahara) yamechukua kiasi cha **trillion 17.3**, sawa na **asilimia 53** ya bajeti yote.


Mheshimiwa Spika, Maeneo mengine yote yanagawana **asilimia 47** iliyobakia (**shilingi trilioni 15.1**). Huu sio uwiano mzuri hata kidogo kwa utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Kamati inaona kuwa ingawa Deni la Serikali haliepukiki, deni hilo ni mzigo mkubwa katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kuwa linaathiri upatikanaji wa fedha za OC kwa mafungu mbalimbali. Jitihada kubwa zinahitajika ili kuhakikisha ulipaji huu mkubwa wa Deni la Taifa unapungua.

Mheshimiwa Spika, hivyo jitihada zaidi zinahitajika katika kutafuta vyanzo vipya vya mapato na kuweza kugharamia mafungu mengine ipasavyo. Aidha, kwa kuwa shughuli nyingi za maendeleo zinafanyika katika Mikoa na Serikali za Mitaa na ndiko waliko wananchi wengi walio masikini, kuna haja ya kuhakikisha kuwa Serikali za Mitaa zinapatiwa fedha za kutosha na zinajengewa uwezo ikiwemo kuachiwa baadhi ya vyanzo vya mapato hasa kodi ya majengo (*property tax*) ili ziweze kutekeleza majukumu yake inavyotarajiwa na hivyo kwenda sawia na dhana ya *Decentralization by Devolution* (D by D).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imetenga kiasi cha **shilingi trilioni 12** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo sawa na asilimia 37 ya bajeti. Kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi trilioni 9.86** ni fedha za ndani (ongezeko la asilimia 10 ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka 2017/18) na **shilingi trilioni 2.13** ni fedha za nje (imepungua kwa asilimia 30 ukilinganisha na Bajeti ya mwaka 2017/18). Kwa ujumla ikilinganishwa na Mwaka wa fedha 2017/18, fedha za maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha zimeongezeka kwa takribani shilingi bilioni 7.68 (sawa na asilimia 0.06). Inatia Moyo kuwa shughuli za maendeleo zitagharamiwa kwa kiasi kikubwa na fedha za ndani. Hata hivyo changamoto iliyopo ni kwa namna gani fedha hizo zitapatikana ikiwa kiasi kikubwa cha mapato ya ndani kinakwenda kugharamia ulipaji wa Deni la Taifa na Mishahara.


Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hii, ni vema Serikali ikazingatia hali halisi ya upatikanaji wa uhakika wa fedha za ndani pamoja na za nje katika kuchagua miradi ipi ianze nayo katika utekelezaji. Katika mwaka 2018/19, Serikali inakusudia kutekeleza miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye Sura ya Nne ya Kitabu cha Mpango na Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19.

Kielelezo Na 3: Mchanganuo wa Mgawanyo wa Bajeti Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17, 2017/2018 na 2018/19 (bilioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha

Kielelezo na 4: Ulinganisho wa Matumizi wa Bajeti ya serikali kwa mwaka 2016/17, 2017/2018 na 2018/19 (bilioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha

SEHEMU YA SABA

7.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2018/19

7.1. Hatua za Kodi zinazopendekezwa na Serikali

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya mabadiliko ya kodi na tozo mbalimbali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, yatakuwa ni sehemu ya pili ya mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali ambayo yatafanyika wakati wa majadiliano ya Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 (*The Finance Bill, 2018*). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti mbalimbali na Sheria za Fedha zilizopita. Hata hivyo bado kuna maeneo mengine ambayo Serikali haijaweza kuyafanyia kazi, Kamati inaitaka Serikali kuona umuhimu wa kufanyia kazi mapema mapendekezo hayo.

Aidha, kuhusu marekebisho ya kodi, ada na tozo mbalimbali yanayopendekezwa kwa mwaka 2018/19, Kamati inatoa maoni katika baadhi ya maeneo hayo kama ifuatavyo:-

7.1.1 Sheria ya Kodi la Ongezeko la Thamani Sura 148

Mheshimiwa miongoni mwa masuala yaliyoshauriwa na Kamati katika kipindi cha nyuma ni kuhusu kurejesha Mamlaka ya Waziri wa Fedha na Mipango ya kusamehe kodi kwenye mikataba ya misaada au mikopo ya miradi inayosainiwa baina ya Serikali na Taasisi za fedha au benki ambayo ni mwakilishi wa Serikali nyingine. Sambamba na hilo, Kamati ilishauri Waziri wa Fedha na Mipango arejeshewe Mamlaka ya kusamehe kodi kwa miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa mikopo ya kibiashara. Kamati inapongeza Serikali kwa kukubali ushauri huo wa Kamati kwani hatua hii itasaidia kurahisisha utekelezaji wa miradi ya Serikali, kutoa unafuu kwa wakopeshaji wa miradi ya Serikali na hivyo kuwezesha utekelezaji wa miradi ya Serikali kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizo, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa Mamlaka hayo ya Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuhusisha pia misaada na mikopo ya masharti nafuu ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa au miradi ya maendeleo ya Kijamii.

Mheshimiwa Spika, Hatua ya Serikali kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike (Sanitary pads) HS Code 9619.00.10 ili kuwezesha kupatikana kwa bidhaa hii muhimu kwa bei nafuu haitakuwa na manufaa kwenye mabadiliko ya bei. Kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike kunawafanya wazalishaji wa ndani kushindwa kurejeshewa kodi hiyo waliolipia katika malighafi walizotumia (input tax claims).

Mheshimiwa Spika, msamahu huu utawanufaisha zaidi wazalishaji wan je wanaoleta bidhaa hiyo nchini kuliko wazalishaji wa ndani. Kamati inashauri Serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Ongezeko la Thamana (VAT), SURA 148 kifungu cha (6) ili kutoa fursa ya wazalishaji wa ndani kurejeshewa Kodi ya Ongezeko la Thamani watakazokuwa wamelipa wakati wa ununuzi wa malighafi (input tax claims).

7.1.2 Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa mabadiliko yanayofanywa kwenye sheria hii, kwani ni jambo jema kumpa mamlaka Waziri wa fedha kuweza kutoa msamaha wa kodi kwenye miradi ya Serikali inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ya masharti ya kibiashara (*non-consessional loans*) hii itarahisisha upatikanaji wa mikopo na utekelezaji wa miradi ya Serikali.

7.1.3 Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutojielekeza zaidi kwenye kuona eneo la ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa zisizo za petroli kama ni eneo la pekee katika kupata mapato.

Katika eneo hili Serikali inalenga kuazisha ushuru wa bidhaa wa shilingi 200 kwa lita kwenye mvinyo uliotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda (kama ndizi, rozela/ choya, nyanya, nk) yanayozalishwa nchini tofauti na zabibu kwa kiwango kinachozidi asilimia 75. Kamati ina wasiwasi na idadi ya viwanda vinavyotengeza bidhaa hiyo hapa nchini na hivyo kuwa na shaka ya uwezekano wa kuvuia viwanda hivyo iwapo ushuru huu utaanza kutozwa kwa viwanda hivyo wakati havijafikia uwezo wa kujlendeshwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na pendekezo la kutobadilisha viwango vya kodi kulingana na Mfumuko wa bei kwa bidhaa zisizo za petroli kama kifungu cha 124 (2) kinavyotaka. Hata hivyo, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

i) Serikali kupandisha ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyoagizwa kutoka nje kutoka shilingi 3481 kwa lita hadi shilingi 3981 kwa lita sawa na ongezeko la shilingi 500 kwa lita;

ii) Serikali kupandishwa ushuru wa bidhaa ya maji ya matunda (juisi) iliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwa hapa nchini (*imported juice*) kutoka shilingi 221 kwa lita hadi shilingi 271 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 50 kwa lita

Mheshimiwa Spika, lengo la mapendekezo haya ni kutoa unafuu wa bei kwa vinywaji vikali na juisi zinazozalishwa ndani ya nchi na hivyo kulinda viwanda vya ndani.

7.1.4 Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria hii, Serikali inapendekeza kumpa Mamlaka Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kuzitaka Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya fedha wanazokusanya kutoka kwenye vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuwezesha vikundi vya wanawake na vijana. Kamati inatoa angalizo juu ya mgawanyo wa fedha hizo kuzingatia uwiano wa 4:4:2 yaani wanawake: vijana: walemavu. Hata

hivyo, Kamati inatambua uwepo wa halmashauri ambazo hazina uwezo wa kukusanya mapato kiasi cha kuwawezesha kutenga fedha hizo (asilimia 10) ya mapato hayo.

Kwa mantiki hii Kamati inashauri utengaji wa fedha hizo uzingatie kongano (clusters) za halmashauri kulingana na mapato wanayopata mathalani halmashauri za jiji na Manispaa zitenge asilimia 10, na halmashauri za miji na wilaya zisizo na uwezo zipewe ruzuku ya maendeleo ya asilimia 10 kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Lengo la mapendekezo haya linazingatia ukweli kwamba Serikali kuu imechukua baadhi ya vyanzo vikuu vya mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mabadiliko ambayo Serikali inapendekeza kuyafanya kwenye ushuru wa mazao, Kamati inapendekeza kuwa mabadiliko hayo yafanyike pia kwenye ushuru wa huduma inayotozwa kwa kiwango cha asilimia 0.03 ya mauzo ya bidhaa na huduma yazingatie madaraja ya leseni badala ya kiwango hicho kutozwa kwa huduma na biashara zote katika kiwango sawa.

7.1.5 Sheria za Serikali za Mitaa, SURA 290, Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348 na Sheria ya Benki Kuu, SURA 197.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya mabadiliko yanayoletwa kupitia Sheria hizi ni kuanzisha akaunti Jumuiifu ya Hazina (*Treasury Single Account*) ambayo itatumika kupokea na kufanya matumizi ya fedha zote za Serikali kupitia makubaliano ya Nchi Wananchama wa Afrika Mashariki kama yalivyoielezwa kupitia Hotuba ya Bajeti.

Kamati haikubaliani kabisa na suala hili kwa sababu huu ni utaratibu wa ndani wa nchi husika wa jinsi ya kukusanya na kutumia rasilimali fedha. Mathalani, mifuko iliyoanzishwa kisheria kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo mfano Mfuko wa Umeme Vijijini, Mfuko wa Reli, Mfuko wa Maji. Mfuko wa Barabara na Mifuko ya kuendeleza Mazao mbalimbali kama vile Pamba, Korosho, Kahawa,

Katani, Tumbaku, Chai na Pareto ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. Endapo Bunge litaridhia mabadiliko haya yataathiri kwa kiasi kikubwa katika sekta hii

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa makubaliano hayo yaliyofikiwa yanalazimu kuzifanyia marekebisho Sheria zilizotajwa hivyo Bunge lako lisifungwe kukubaliana na utekelezaji wa maamuzi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu kufanya hivyo kutaathiri utekelezaji wa miradi husika.

7.1.6 Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa tatu sasa Kamati inaishauri Serikali kuhusu kulishirikisha Bunge lako wakati wa kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki kabla ya kuyawasilisha kwenye Baraza la Mawaziri wa Kisekta, Uwekezaji na Fedha. Hata hivyo Serikali imekuwa haizingatii ushauri huo hali iliyolazimu Kamati kupitia kwa kina Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *The Treaty for the Establishment of the East African Community* na *The East African Customs Union Protocol* ili kujiridhisha iwapo kuna katazo la kufanya hivyo. Kamati imebaini kuwa kila nchi ina utaratibu wake wa ndani wa kupeleka mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria kwenye Jumuiya kwa msingi huo Serikali inaweza kushirikisha Bunge kuhusu mapendekezo hayo kupitia Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo sasa wa kupitisha mapendekezo hayo moja kwa moja kwenye Baraza la Mawaziri wa Kisekta la EAC hautoi fursa kwa Bunge lako kuweza kubadilisha mapendekezo yaliyo ridhiwa na nchi wanachama. Aidha, Kamati imebaini kwamba baadhi ya mapendekezo yanalenga katika kunufaisha na kuendeleza sekta binafsi za nchi jirani na hivyo, kuathiri sekta binafsi ya nchi nyingine ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya marekebisho ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki yamegusa Sekta moja tu ya

vifungashio na sio sekta nyingine kama vile nguo, ngozi, vyakula na nafaka. Licha ya kuwa kikao cha 18 cha Wakuu wa Nchi pamoja na mambo mengine kilipokea Taarifa ya Baraza la Mawaziri kuhusu kuziwezesha Sekta za nguo, ngozi vyakula vya nafaka pamoja na Vifungashio vya vyakula vya lishe kukua, suala hilo halijazingatiwa. Kamati pia imebaini kuwa nchi nyingine wanachama wamechukua hatua kubwa ya kutoa vivutio katika sekta ya nguo wakati Tanzania haijaweza kutekeleza uamuzi huo. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatekeleza uamuzi wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa EAC ili kuiokoa Sekta ya nguo na ngozi nchini.

7.1.7 Sheria zinazosimamia Bodi ya Mazao

Mheshimiwa Spika, Bodi za mazao zilianzishwa kwa lengo la kuendeleza mazao mbalimbali nchini, Bodi hizo hukusanya ada na tozo kutoka kwa wakulima wa zao husika ili kuweza kuziendesha na kuendeleza zao husika. Aidha, katika kitabu cha hali ya uchumi kinaonesha kuwa kuna mazao ambayo uzalishaji umeongezeka na baadhi umepungua. Mfano mazao ambayo uzalishaji wake umeongezeka ni Korosho asilimia 100.4, Karafuu asilimia 38.4, Katani asilimia 49 na Chai asilimia 9.5. Mazao ambayo uzalishaji wake umeshuka ni Tumbaku asilimia - 37.4, Pamba asilimia -23 na Kahawa asilimia -14.1. Pendekezo la Serikali la ushuru unaokusanywa katika Bodi hizo kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali itakuwa ni **msumari wa mwisho kwenye Jeneza** (*The Last Nail in the Coffin*) la mazao haya ya biashara. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuziachia bodi zote za mazao fedha zinazokusanywa kutoka kwa wakulima kwa ajili ya uendelezaji wake na si vinginevyo.

7.1.8 Marekebisho ya Ada na Tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kufanya marekebisho katika ada na tozo mbalimbali zenye lengo la kutoa unafuu wa kodi ya ardhi. Pamoja na nia hiyo njema ya Serikali kusamehe kodi ya ardhi kwa taasisi za umma pekee Kamati inashauri pia Serikali kuangalia uwezekano wa kusamehe

kodi hiyo katika shule binafsi pamoja na hospitali binafsi kwa kuwa kimsingi zinashirikiana na Serikali katika kutoa huduma kwa jamii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mabadiliko yanayopendekezwa na Serikali kwenye suala la uzalishaji wa chumvi, uzalishaji huo ulikuwa unatozwa kodi kama mgodi mwingine wowote mathalani mgodi wa dhahabu. Kamati inakubaliana na mapendekezo yote ya Serikali ya kuondoa ada na tozo katika uzalishaji wa chumvi. Hata hivyo, Kamati haikubaliani na pendekezo la kuondoa ushuru wa huduma kwa mazao ya chumvi unaozwa na Halmashauri kwa kuwa chanzo hiki ni muhimu kwa ajili ya mapato ya Halmashauri zinazotegemea zao hili kama chanzo kikuu cha mapato yao ya ndani mfano, Halmashauri ya wilaya ya Uvinza - Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kuna changamoto za tozo na ada mbalimbali kwenye Mamlaka za Udhubiti ambazo zimekuwa kikwazo kwa ukuaji wa Sekta Binafsi katika uzalishaji wa bidhaa za ndani dhidi ya ushindani wa bidhaa za nje. Mfano utozaji wa huduma za zimamoto kwenye shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuleta mabadiliko ya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Mamlaka za Udhubiti ili kuondoa vikwazo hivyo kwa sekta binafsi na hivyo na kupata unafuu wa gharama za uzalishaji na hatimaye kuongeza ushindani katika biashara.

7.2 MAONI NA USHAURI WA JUMLA

7.2.1 Stempu za Kieletroniki (*Electronic Tax Stamp-ETS*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19 Serikali imedhamiria kuanzisha Mfumo wa Stempu za Kodi za Kieletroniki ili kudhibiti udanganyifu wa wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa.

Kampuni ya *SCIPA* kutoka Uswiss ndiyo iliyoshinda zabuni hiyo hapa nchini na ina mkataba wa miaka mitano na Serikali

kwa mfumo wa *Self Financing*. Mfumo huo unamtaka mwekezaji kurudisha gharama zake za uwekezaji kwa kutoza stampu ya kieletroniki kwa kila bidhaa itakayozalishwa. Kiasi cha fedha kinachotarajiwa kuwekezwa na SCIPA ni **Dola za Marekeni 21,533,827** sawa na **Shilingi 48,472,644,577**.

Mheshimiwa Spika, Kamati haina pingamizi na uanzishwaji wa mfumo huu, jambo la msingi ambalo linahitaji lifanyike kwa umakini ni kujiridhisha na gharama za mfumo huo ambazo zitabebwa na watumiaji wa bidhaa pamoja na mapato atakayoyapata mwekezaji kutokana na stempu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa hatua ya Serikali kutoongeza ushuru wa bidhaa zisizo za petroli itakuwa haina maana kama gharama ya stempu itabaki kama ilivyopangwa na Serikali. Hatua hii itasababisha kuongezeka kwa bei kwenye vinywaji kama maji, soda, bia na juisi ambazo sasa hazitowzi stempu.

Aidha, tathmini ya Kamati inaonesha kuwa pale Serikali itakapokuwa inaongeza ushuru wa bidhaa kwa asilimia ya mfumuko wa bei kama Sheria ya Ushuru wa Bidhaa inavyotaka, kiwango cha stempu kitakuwa kinaongezwa juu yake kulingana na Mkataba kwa miaka mitano (**Rejea Jedwali Na. 5 na 6**) linaonesha jinsi bei itakavyoongezeka kwa vinywaji baridi.

Jewali Na. 5 Jinsi ETS itakavyoongeza Gharama kwa Mwananchi

Bidhaa	Ujazo kwa Mililita	Kodi ya Ushuru wa Bidhaa	Bei ya Stempu za Sasa	Bei ya Stempu za Kielektroniki	Ghamara atakayolipa mwananchi (Stempu+Ushuru)
Maji	300mls	18	0	13.5	31.5
	500mls	29	0	13.5	42.5
	1000mls	58	0	13.5	71.5
Soda	250mls	15	0	13.5	28.5
	300mls	18	0	13.5	31.5
	350mls	22	0	13.5	35.5
	500mls	31	0	13.5	34.5
Bia	500mls	225	0	22.73	247.73
	330mls	157	0	22.73	179.73
	1000mls	2,349	0	22.73	2,371.73
Konyagi na pombe kali za nje	1000mls	3,481	8.20	29.57	3510.57

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi ili kubaini kiwango cha fedha ambacho kampuni ya SCIPA itakipata katika Mkataba huo kwa Mwaka mmoja. Uchambuzi huo umehusisha takwimu za bidhaa tatu za maji, soda na sigara bila spiriti kwa kuangalia viwango vya uzalishaji wa bidhaa hizo kwa mwaka. Uzalishaji huo unaonesha Kama ifuatavyo:- kiwango kinachozalishwa nchini kwa mwaka; Maji ni **lita za ujazo 268,702,209** Soda ni **lita za Ujazo 732,315,008** Bia ni **lita za ujazo 409,274,746** na Sigara ni Pakiti **429,310,400**.

Mheshimiwa Spika, ukikadiri kwamba stempu itatozwa kwa idadi (unit) na sio kwa ujazo (lita), hivyo chupa moja ya bia ml 500 itatozwa **Shilingi 22.73**; Soda 500 mls itatozwa **Shilingi 13.5**, Spirit 1000 mls itatozwa **Shilingi 29.57**. Hivyo, ukijumlisha na ushuru wa bidhaa kwa kila bidhaa iliyoainishwa hapo juu inaonekana kuwa gharama itakwenda kwa mlaji wa mwisho. Kwa mantiki hii, ukokotoaji unaonesha kwa mwaka mmoja *SCIPA* atakusanya jumla ya **Shilingi 66,690,313,798.84** bila ya kuhusisha takwimu za bidhaa ya spiriti. Aidha, Kiasi hiki ni kikubwa kuliko alichowekeza katika kipindi cha mwaka mmoja tu wa mkataba.

Jedwali Na. 6 Mapato itakayopata Kampuni ya SCIPA katika Mwaka

Mmoja bila kuhusisha ukokotoaji wa bidhaa ya spirits

Na	Bidha	Uzalishaji Lita/ Pact za ujazo kwa Mwaka	Kiwango cha bei ya Stempu kinachotozwa kwa Lita/ Pakiti	Mapato ya SCIPA
1.	Maji	268,702,209	58	15,584,728,122.00
2.	Sigara	429,310,400	29.57	12,694,708,528.00
3.	Soda	732,315,008	27	19,772,505,216.00
4.	Bia	409,274,746	45.54	18,638,371,932.84
5	Jumla ya Mapato atakayopata SCIPA kwa mwaka mmoja			66,690,313,798.84

Chanzo: Wzara ya Fedha na Mpango. (Hapa tumechukulia kila bidhaa ni ujazo wa Lita Moja

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikifuatilia hatua mbalimbali za Serikali zenye lengo la kukusanya mapato yake yenyewe na sio kutumia mawakala kukusanya mapato. Mfano; kuhamisha fedha zake kutoka Benki Binafsi kupeleka Benki kuu, mfumo wa manunuzi ya Luku kutoka Kampuni ya Max Malipo na Mitandao ya simu kwenda GePGS (*Government Eletronic Payment Gateway System*), ukusanyaji wa mapato katika mabasi ya mwendo kasi na matumizi ya mashine za EFD.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa Serikali kuamua kumpa *SCIPA* Mkataba wa miaka mitano wa kuhakiki uzalishaji kupitia stempu za kielektroniki ilhali uhakiki huu ungeweza kufanywa na Serikali yenyewe. Hata hivyo, Kamati imeona kuwa kiwango cha mapato kinachotarajiwa kukusanywa katika kipindi cha mwaka mmoja (**Shilingi 66,690,313,798.84**) kwa bidhaa nne zilizo ainishwa hapo juu ni kikubwa kuliko kiwango cha uwekezaji cha **Shilingi 48,472,644,577** ambacho kimewekezwa na Kampuni ya *SCIPA*. Baada ya Kamati kufanya uchambuzi huo inaishauri Serikali yafuatayo:-

i. Serikali iwekeze yenyewe mfumo huu wenye mtaji wa kiasi cha **Shilingi 48,472,644,577** ili kiasi cha fedha kitakachopatikana iwe ni sehemu ya mapato ya Serikali badala ya mapato yatokanayo na stempu kuchukuliwa na Kampuni binafsi kama ilivyofanya kwenye Mfumo wa TANCIS;

ii. Serikali ianze kutumia mfumo huu kwenye vinywaji vikali ambavyo mara kwa mara mbele ya Kamati Serikali imekuwa ikithibitisha kuna udanganyifu mkubwa; na

iii. Ni bora Serikali kuongeza ushuru wa bidhaa kwa asilimia 5 ya mfumuko wa bei kama ilivyokuwa ikifanya hapo awali kuliko inavyopendekeza sasa kutumia mfumo wa stempu kwa bidhaa hizo kwa kuwa gharama za stempu ni kubwa kuliko ushuru wa bidhaa wa asilimia 5. Mathalani ukichukua bidhaa ya soda (250 ml) inatozwa ushuru wa bidhaa kiasi cha shilingi 15 na wa stempu utatozwa kiasi cha shilingi 13.5. Hivyo, gharama ya jumla (gharama ya ushuru

wa bidhaa na wa stempu) itakuwa kiasi cha 28.5 na hivyo itaongeza gharama kwa uzalishaji na kwa mlaji.

7.2.3 Uhakiki na ulipaji wa Madeni ya Watumishi, Wazabuni na Wakandarasi Nchini

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitumia Kifungu cha 10 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pamoja kifungu cha 5 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 na marekebisho yake kuhalalisha usimamizi wa fedha za mifuko pamoja na uhakiki wa madeni na ulipaji wake. leleweke wazi kwamba Kamati haipingi zoezi la uhakiki na ulipaji wa madeni, hata hivyo Kamati inatambua kuwa, Katiba imemtaja Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pamoja na majukumu mengine ni kukagua ripoti za Fedha za Serikali. Aidha, Serikali kupitia kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani imekuwa na utaratibu wa kuweka wakaguzi wa ndani kwa ajili ya kufanya jukumu hilo la 'uhakiki'

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa uhakiki unaofanywa na Wizara ya Fedha na mipango unaleta mkanganyiko katika mgawanyo wa majukumu, kuongeza gharama kwa Serikali hasa katika ongezeko la riba kwenye miradi ya maendeleo pamoja na kuchelewesha malipo ya matumizi halali yaliyoidhinishwa na Bunge kwa mafungu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mathalani kwa upande wa madeni ya ulipaji wa bili ya Umeme kutoka *TANESCO* kwenda Jeshi la Polisi au Maji kutoka *Dawasco* kwenda Magereza nayo yanahakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa mantiki hii, Kamati inajuliza je Wizara ya Fedha na Mipango ikifanya makosa wakati wa uhakiki na ulipaji itakaguliwa na nani? au je Wizara ya Fedha na Mipango imekua haiamni majukumu ya taasisi nyingine za Serikali? Kwa kuzingatia haya, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

i. Kutumia wakaguzi wa ndani kuhakiki madeni kabla hayajapelekwa Wizara ya fedha na mipango ambapo hivi sasa yanafanyiwa uhakiki tena na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi iliyo chini ya mifuko;

ii. Serikali kusitisha mara moja utaratibu wa kuitumia Benki Kuu ya Tanzania kusimamia ufunguaji wa Barua za Muamana (*Letters of Credit*) kwenye Mabenki ya Biashara kwasababu kwa kufanya hivyo inondoa uhuru wa Benki Kuu kuyasimamia mabenki hayo;

iii. Serikali kuondoa utaratibu wowote ambao unakwamisha utekelezaji wa miradi iliyoko chini ya mifuko kwa ufanisi.

iv. Kuboresha na kuihuisha mifumo ya ulipaji kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali

7.2.4. Mamlaka za Serikali za Mitaa na Ugatuzi wa Madaraka (*Decentralization by Devolution*)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 145 na Ibara ya 146 inaanisha majukumu yake. Vyombo vya Serikali za Mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa ujumla.

Sambamba na hili sheria mbalimbali zimeanisha muundo wa Serikali za Mitaa pamoja namna halmashauri zitakavyopata mapato yake kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi kwa niaba ya Serikali. Serikali katika miaka tofauti imekuwa ikichukua hatua ambazo zinaondoa dhana nzima ya ugatuzi wa madaraka hivyo kuondoa uhuru wa kupanga na kutekeleza miradi ya Maendeleo katika Serikali za Mitaa. Mfano; kufuta ada na tozo mbalimbali za Serikali za Mitaa, kunyag'anya ukusanyaji na utumiaji wa vyanzo kama mabango na kodi za majengo na kuwaondoa baadhi maafisa kuwajibika kwa Wakurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imefanya tathmini na kuona kuwa kwa hali hii sasa halmashauri nyingi nchini zina hali mbaya ya kifedha kutokana na Serikali Kuu kuchukua madaraka ya usimamizi wa fedha na ukusanyaji wa mapato. Hatua hizi zimekuwa na athari kubwa sana kibajeti

kwasababu hivi sasa Halmashauri zinaishi kwa msaada wa Serikali kuu na sio zijitegemee kimapato. Mfano; Halmashauri nyingi hivi sasa zimeshindwa hata kugharamia mikutano halali ya madiwani kwa kukosa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti inashauri Serikali kuheshimu maboresho ya Tamko la kisera ililolitoa mwaka 1998 kuhusu ugatuuji wa madaraka (*Policy Paper on Local Government Reform Programme on Decentralization by Devolution- D by D*) kama njia muafaka ya kufikisha na kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuinua utoaji wa huduma kwa wananchi.

7.2.5. Pendekezo la Bunge la kuhusu ongezeko la shilingi 50 kwenye mafuta ya petrol na dizeli kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, Kamati ya Bajeti imekuwa ikiishauri Serikali kufanya mabadiliko katika (*The Road and Fuel Tolls Act, CAP 220*) ili kuongeza kiasi cha **shilingi 50** kwenye tozo za mafuta ya dizeli na petrol yanayoingizwa nchini. Kamati imefikia hatua hii baada ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maji na kuona kuna hitaji la kuongeza **shilingi 50** kama fedha ya ziada kwenye chanzo hiki ili kukidhi utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa chanzo hiki ni cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, mathalani katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ilitenga jumla ya **shilingi 623,606,748,000** kwa ajili ya miradi ya maji ambapo kati ya fedha hizo mfuko wa maji uliidhinishiwa **shilingi 129,563,939,266**. Takwimu zinaonesha kuwa, hadi kufikia mwezi Machi, 2018 mfuko huo ulikuwa umekusanya na kutumia jumla ya **shilingi 117,092,000,000** kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maji vijijini ikiwa ni asilimia 90 ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja ya kuwa Hotuba ya Bajeti hajijaeleza chochote kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji, Kamati inaitaka Serikali kujumuisha sheria ya *The Road and Fuel Tolls Act, CAP 220* katika muswada wa sheria ya fedha

ya mwaka 2018 ili kuongeza shilingi 50 kwa ajili ya miradi ya maji vijijini. Aidha, sababu ambayo Serikali imekuwa ikiitoa mara kwa mara kuhusu chanzo hiki kuwa itaongeza mfumuko wa bei sio sahihi kwa kuwa bei za mafuta katika soko la dunia zina mwenendo wa kushuka hadi kufikia wastani wa Dola za Kimarekani 73 kwa pipa. Ni msimamo wa Kamati kuwa suala hili litekelezwe kwani ni chanzo cha uhakika ambacho Serikali inaweza kujiletea mapato na hivyo kutimiza azma yake ya kumtua Mama ndoo.

7.2.6. Hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika mwaka wa fedha 2016/17.

Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa taarifa ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kubaini maeneo ambayo Serikali ama inashindwa kukusanya mapato yake kikamilifu kutokana na sababu za kiutawala au kusababisha upotevu wa mapato kutokana na usimamizi mbovu. Mfano Mamlaka ya Mapato haikukusanya kodi yenye thamani ya **Shilingi 1,558,116,225,302.76** iliyotokana na mapingamizi ya kodi ambayo yalikuwa yameshughulikiwa na kukamilishwa, na kodi ya **Shilingi 269,612,850,131.28** haikukusanywa kwa mapingamizi yaliyokataliwa na Kamishna kwa sababu mapingamizi hayo hayakukidhi vigezo vya kisheria.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa mujibu wa taarifa hiyo, kuna kiasi cha **Shilingi 262,293,791,682** ya madeni ya kodi ambayo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) haija yakusanya kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kamati inashangazwa na mwenendo wa Serikali kuendelea kuchukua vyanzo vya mapato vilivyobuniwa na Serikali za Mitaa wakati ina vyanzo vyake vingi ambavyo imeshindwa kukusanya. Kamati inashuri Serikali kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na taarifa ya CAG kwenye eneo hili pamoja na kuhakikisha inasimamia ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo hivyo.

7.2.7. Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato kwa Serikali za Mitaa;

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ilipanga kukusanya jumla ya **shilingi 687,306,661,000** hata

hivyo, hadi kufikia mwezi Machi Serikali ilikuwa imeweza kukusanya **Shilingi 397,215,242,947** sawa na **asilimia 57.8** ya lengo. Kamati imebaini kati ya fedha zote zilizokusanywa Mkoa wa Dar es salaam ni **Shilingi 105,877,402,428** sawa na asilimia 26.6 ya mapato yote yaliyokusanywa na Serikali za Mitaa. Aidha, kamati imebaini katika mwaka wa fedha 2018/19 Mkoa wa Dar es salaam umetengewa jumla ya Shilingi **280,695,752,500** katika Bajeti ya Maendeleo na umepata miradi ya Kimkakati sita ya kuongezea Mapato yenye thamani ya **Shilingi 15,000,000,000**. Kamati, haipingi wala haina tatizo lolote na uwekezaji wa Serikali katika jiji la Dar es salaam suala la msingi ni Serikali ione jinsi ambavyo imeweze katika jiji hilo na mapato yaliyopatikana. Hivyo basi, ni muhimu Serikali iwekeze kwa kiwango kikubwa katika Mikoa mingine ili nayo ichangie kwa kiasi kikubwa kwenye mapato ya Serikali kama ilivyo kwa Mkoa wa Dar es salaam.

7.2.8. Marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT Refunds) na asilimia 15 ya amana ya sukari ya viwandani (15% imposition on Industrial sugar)

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa hairejeshi marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na amana ya asilimia 15 inayotolewa na viwanda vya sukari. Mfano, kampuni za madini zinaidai Serikali marejesho ya VAT yenye thamani ya zaidi **600,000,000,000** na wazalishaji wa Sukari wanaidai Serikali **Shilingi 35,000,000,000**. Aidha, mwaka 2017/18 Serikali ilianzisha akaunti ya escrow kwa ajili ya kuhifadhi **asilimia 15** ya muamana ambayo iliwekwa kiutawala na wala sio kupitia Sheria ya Bunge kwa lengo la kuzuia matumizi mabaya ya Sukari ya viwandani. Hadi Mwezi Machi, 2018 akaunti hiyo ilikuwa na **Shilingi 18,200,000,000** ambazo bado hazijarejeshwa pamoja na uhakiki wa matumizi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji huo umekuwa na athari kubwa sana kwa Sekta Binafsi kwasababu kimsingi ni mtaji wa matumizi "*Operating Capital*" ambayo imefungiwa katika akaunti za Serikali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali

(i) Kurejesha fedha hizo kwa wadau husika ili ziweze kutumika katika biashara zao;

(ii) kuruhusu makampuni kujirejeshea fedha hizo kupitia Kodi ambazo walipaswa kuilipa Serikali;

(iii) Serikali itafute utaratibu mwingine wa kudhibiti uingizaji wa sukari ya viwandani ili kuachana na utaratibu wa sasa ambao unaathiri uwekezaji wa viwanda vya madawa, vinywaji baridi na vyakula kama pipi na biscuits

7.2.8. Mchango wa asilimia 15 kutoka katika Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako lilifanya Mabadiliko katika Sheria ya Madaraka na Majukumu ya Msajili wa Hazina Sura ya 370 kifungu cha 8 (1) (f) na kuongeza gawio kutoka asilimia 10 hadi 15 ya pato ghafi. Katika mwaka wa Fedha 2017/18 Serilaki ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 216,957,463,783** hadi mwezi Machi, 2018 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 309,986,394,685** sawa na asilimia 143 ya lengo. Kuvuka kwa lengo kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na gawio kutoka Benki Kuu ambayo ilitoa **Shilingi 300,000,000,000** sawa na **asilimia 96.7** ya makusanyo yote ya Mashirika 26.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaashiria kwamba mashirika 25 yaliyobakia yalichangia wastani wa kiasi cha **Shilingi 399,455,787.4** kila moja. Aidha, Kamati imebaini kuna baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma zinachangia asilimia 15 ilihali yanaidai Serikali fedha nyingi kuliko ambazo zinachangia. Mfano, DAWASA imechangia jumla ya **Shilingi 2,906,331,937** wakati huo huo inaidai Serikali **Shilingi 1,900,000,000** ambazo zinafanyiwa uhakiki. Kamati, inaishauri Serikali yafuatayo:-

(i) Kulipa madeni wanayodaiwa na Taasisi husika kabla ya kuchukua asilimia 15 ya pato ghafi ili kutoa unafuu wa utekelezaji wa majukumu kwa taasisi husika;

(ii) Kuangalia upya utaratibu wa *retention* kwenye mashirika ambayo yanategemea ruzuku ya Serikali kujiendesha;

(iii) Kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 ili kuruhusu makampuni na taasisi za Serikali zinazotoa asilimia 15 kuruhusiwa kuondoa kiwango hicho (allowable deduction) wakati wa kukokotoa kodi ya mapato.

7.2.9. Soko la Mtaji na Dhamana kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, masoko ya mtaji na dhamana ni sehemu ya mfumo wa masoko katika sekta ya fedha yanayowezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya muda mrefu kugharamia shughuli za maendeleo ya muda mrefu yaani zaidi ya Mwaka mmoja. Kamati inatambua kuwa Serikali inaweza kutoa hati fungani (treasury/government bonds) kwa malengo maalumu kama vile kwenye ujenzi wa miradi mikubwa au ujenzi wa barabara (infrastructure bonds) au hati fungani inayolenga kupata fedha za maendeleo kutoka katika makundi maalumu kama vile watanzania waishio nchi za nje (Diaspora Bond). Hatua ya kutoa hati fungani itasaidia Serikali kupunguza kutumia fedha nyingi za ndani kwenye miradi mikubwa na hivyo kuweza kuelekeza fedha hizo kwenye miradi mingine midogo inayohusu jamii moja kwa moja hasa kama ile ya afya, maji na elimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi za Serikali kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Serikali za mitaa zinaanza kufikiriwa kutoa hati fungani za Serikali za Mitaa kwa ajili ya fedha za maendeleo katika mamlaka husika. Pamoja ya kuwa Serikali imeanza kutekeleza suala hili kama majaribio (pilot project) kwa kutoa mafunzo kwa majiji ya Mwanza, Arusha, Tanga na Manispaa ya Moshi,

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyanzo vikuu vingi vya mapato kwa halmashauri vimechukuliwa na Serikali Kuu, Kamati ya Bajeti inashauri kuwa, ili kuwezesha utoaji wa hati fungani hizo, Mamlaka za Serikali za Miji na Wilaya zinatakiwa kuboresha utunzaji wa hesabu na uthibiti wa mapato yake ili kuweza kuwafanya wawekezaji katika hati fungani kuwa na imani na masoko hayo. Aidha kuna umuhimu wa

kuwajengea uwezo watendaji wa Mamlaka hizo kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ili kuwa na wataalamu wa kutosha wenye ujuzi katika masuala ya masoko ya mitaji na dhamana.

7.2.10. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa hivi karibuni Serikali imeandaa mkakati maalum kwa madhumuni ya kuziwezesha Halmashauri kujitegemea kimapato. Mkakati huu umeelezwa kama pia mwongozo wa uandaaji mipango na bajeti 2018/19-2020/21. Katika kutekeleza Mkakati huu Mamlaka za Mitaa zinatakiwa kuhakikisha zinatamia kwa ukamilifu fursa za kimapato zilizopo katika maeneo yao na hivyo kuongeza uwezo wa kujitegemea kimapato. Kamati ya Bajeti inapongeza hatua hii ya Serikali kuweza kuleta mkakati huo hata hivyo, ili uweze kutekelezeka kikamifu Serikali inatakiwa kukamilisha haya yafuatayo:-

i) Kufanyia mapitio upya Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289 pamoja na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kuziwezesha halmashauri kukusanya tena kodi ya majengo na nyingine badala ya TRA kwa kuwa ilivyosasa, Serikali imekuwa ikisuasua kurejesha fedha hizo kwenye Halmashauri husika na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake.

ii) Serikali imekuwa ikileta mipango mbadala kati kati ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa tofauti na ile iliyoainishwa kwenye mpango wa maendeleo, hatua hii inaleta mkanganyiko wa utekelezaji wa bajeti za halmashauri ambazo kimsingi hapo awali Serikali ilikuwa imeishakubaliana na Serikali Kuu kupitia ukomo wa bajeti zao.

iii) Serikali ihakikishe inaweka utulivu (stability) kwenye Sera zake za fedha na kibajeti kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti ili kuruhusu watendaji wa Mamlaka za Serikali za

Mitaa kufanya kazi zao na kuwa na uhakika na vyanzo vyao walivyobuni kupitia kodi, tozo na ushuru kwa lengo la kujitosheleza kutoa huduma muhimu pamoja na uendeshaji wa shughuli za Mamlaka husika.

iv) Serikali inatakiwa kuweka vigezo rahisi vinavyoweza kutekelezeka kulingana na mazingira na mahitaji ya halmashauri husika ili kuziwezesha kufaidika na utaratibu huu.

7.2.11. Utafutaji wa Mafuta na Gesi Nchini

Mheshimkiwa Spika, kutokana na ugunduzi wa kiwango kikubwa cha gesi (futi za ujazo trilioni 55.08), Serikali imekuwa ikipata kodi, tozo na ada mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kuleta maendeleo ya nchi kwa kusimamia matumizi bora ya mapato ya gesi. Hatua hii imesaidia kuanzisha Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi (*Oil and Gas Fund*) ili uweze kusaidia kugharamia bajeti ya Serikali kwa upande wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Hotuba ya Bajeti ya Serikali haijaeleza mkakati wowote uliopo katika kuhakikisha inapata mapato yatokanayo na shughuli za utafutaji na uwekezaji wa Mafuta na Gesi Nchini, pia taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 imeshindwa kuchambua hali ya maendeleo ya sekta ya Mafuta na Gesi.

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonesha shughuli za utafutaji na uwekezaji wa Mafuta na Gesi zimekuwa zikipungua siku hadi siku na hivyo kushindwa kukidhi matarajio ya Serikali katika sekta hii kuweza kuchangia bajeti ya Serikali. Hivi Karibuni tumeshuhudia kampuni kubwa ya Kimarekani ya [Exxon Mobil](#) ikionesha nia ya kuuza visima vyake vya gesi nchini licha ya kuwa ilianza mchakato wa kuwekeza kwa njia ya kuchangia mtaji katika mradi wa LNG Likong'o -Lindi.


Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya tafiti na kuona nini hasa kimechangia kupungua kwa shughuli za utafutaji Mafuta na Gesi na nini kifanyike kwa haraka

kurekebisha kasoro hiyo na hivyo kuendelea kupata mapato kutoka katika sekta ya gesi. Aidha, Sura ya Bajeti inatakiwa ionyeshe kiasi cha mapato yaliyopatikana kwenye shuguli za utafutaji na uwekezaji wa Mafuta na Gesi.

7.2.12. Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Sekta Mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imepitia na kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali katika sekta mbalimbali hasa zile zinazosaidia maendeleo ya kijamii na kiuchumi kama vile miundombinu, elimu, mahakama, nishati, afya, maji na nyinginezo. Kwa kipindi cha miaka minne (2013/14-2017/18) Bajeti ya Serikali imekuwa ikiongezeka kwa upande wa miundombinu na Elimu wakati kwa upande wa sekta nyingine imekuwa ikibadilika mara kwa mara hasa kwa upande wa maji ambayo imepungua kama kielelezo hapo chini kinavyoonesha. Kamati inapongeza na kutambua juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kundeleza miradi ya sekta ya miundombimu kama vile ujenzi wa Reli (Standard gauge), ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege, upatikanaji wa nishati ya umeme (*stigglers gorge*), ununuzi wa ndege pamoja na usimamizi wa uchimbaji madini. Aidha, kwa upande wa sekta ya elimu Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kusimamia utolewaji wa elimu ya msingi na Sekondari bure.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizi kubwa za Serikali, Kamati inashauri Serikali kuelekeza nguvu pia kwenye kutenga fedha za kutosha pamoja na usimamizi wa maendeleo ya sekta nyingine hasa ya afya na maji ambazo kimsingi bajeti zake zimekuwa hazitoshi kutekeleza mahitaji ya kijamii. Mfano katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hadi kufikia mwezi Machi 2018, Sekta ya Afya (Fungu 52) imepata asilimia 36 ya fedha za ndani na asilimia 2 ya fedha za nje; na kwa upande wa sekta ya Maji (fungu 49) imepata asilimia 35 ya fedha za ndani na asilimia 9 ya fedha za nje.



Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi imeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa cha takribani asilimia 30.1 katika Pato la Taifa hasa katika upande wa Mazao (asilimia 17.0) mifugo (asilimia 6.9) misitu (asilimia 4.0) na uvuvi (asilimia 2.2). Aidha, kwa pamoja sekta hizi kuajiri kiasi cha asilimia 66.6 ya wataanzania, bado kiasi cha bajeti kinachotengwa kwenye sekta hizi ni kidogo na changamoto zake hazijaweza kutatuliwa. Mathalani katika mwaka huu wa fedha sekta ya kilimo imetengewa **asilimia 0.4**, Mifugo imetengewa **asilimia 0.1**, Uvuvi imetengewa **asilimia 0.06**, maji imetengewa **asilimia 2.2** na Afya imetengewa **asilimia 2.7** ya Bajeti yote ya Serikali. Kama sekta hizi zingepewa kipaumbele cha kutosha katika Bajeti ya Serikali basi kingeweza kuchangia kiasi cha takribani asilimia 60 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Bajeti uk 39-40 imetaja maeneo ya kipaumbele ikiwemo na sekta ya kilimo. Hata hivyo hotuba hii haijieleza kwa kiasi gani fedha zimetengwa katika

kutekeleza maeneo ya msingi yaliyoainishwa kama miundombinu ya umwagiliaji, maghala na masoko, utafiti, kuimarisha upatikanaji wa pembejeo pamoja na kuendeleza sekta ya uvuvi na mifugo. Kamati inaona ni muhimu Serikali ikaonesha kiasi cha fedha zitakazoelekezwa katika maeneo haya na mikakati ya kuteleza vipaumbele hivyo.

Mheshimiwa Spika, ukirejea uk wa 82-83 wa Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2017 utaona kuwa kwa mwaka 2017, bado sekta ya kilimo haifanyi vizuri kwa upande wa mauzo ya bidhaa asilia kwenda nje kama vile mazao ya kahawa (-17.5), Pamba (-23.2), Tumbaku (-37.4). Hata hivyo, zao la korosho limeendelea kufanya vizuri kwa mwaka 2017 ukilinganisha na mwaka 2016 kwa kiwango cha asilimia 100.2. Kamati inashauri kuwa ni vizuri Serikali ikatafiti na kuona nini kinafanyika katika zao la korosho na kuweza kukifanyia kazi katika mazao mengine ili yaongeze upatikanaji wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua iliyochukua Serikali ya kupunguza kiwango cha kodi ya Mapato ya Makampuni (corporate income tax) kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 20 kwa kipindi cha miaka Mitano ili kuvutia uwekezaji wa viwanda vipya vya madawa ya binadamu na ngozi. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa bado kuna umuhimu wa Serikali kuchukua hatua ya kufuta *export levy* kwenye ngozi (*wet blue*) inayouzwa nje pamoja na kupiga marufuku uuzaji wa ngozi ghafi nje. Hatua hii itasaidia kukuza uzalishaji wa viwanda vya ngozi vilivyopo (takribani 7 tu) na hivyo kusaidia kuongeza uzalishaji wa ngozi, kuongeza ajira, pamoja na makusanyo ya kodi (*indirect tax*). Kamati inashauri Serikali kupanua wigo wa punguzo hili la kodi ili lihusishe pia viwanda vilivyopo vya madawa ya binadamu na ngozi kwa lengo la kuzilea

Mheshimiwa Spika, aidha Hotuba ya Bajeti ya Serikali haijaweza kuanisha mikakati yoyote ya kusaidia kukua kwa sekta ya uvuvi ili iweze kusaidia upatikanaji wa mapato. Ukirejea Uk. 33 wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, mipango iliyoainishwa kwenye sekta ya uvuvi haijaweza kuoanishwa

vizuri na Bajeti iliyosomwa kama sehemu muhimu wa kipaumbele cha Serikali katika upatikanaji wa mapato.

7.2.14. Utaratibu wa Kubakiza baadhi ya mapato kwa maeneo mahususi

Mheshimiwa spika, katika mwaka wa fedha 2015/16 Serikali iliondoa utaratibu wa *retention* kwa Wizara, Idara na Taasisi zake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Kuondolewa kwa utaratibu huu kumesababisha athari katika baadhi ya maeneo kama vile Ofisi za Balozi na jeshi la Zimamoto. Mfano Serikali imekuwa ikipoteza mapato kwa balozi zetu kwa sababu mapato yanayokusanywa na Ofisi za Balozi kabla ya kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali inalazimu kuyabadilisha kwenda kwenye *global exchange currency* baadae kubadilishwa kwenda kwenye Shilingi ya Kitanzania. Vilevile, Serikali inapofanya mgao wa matumizi kwa Balozi inalazimika kupitia utaratibu huo wa kubadili Shilingi kwenda kwenye sarafu ya nchi ambayo Tanzania ina ubalozi. Utaratibu huu unasababisha hasara kubwa kwa Serikali (*Exchange loss*) kutokana na kubadili fedha kutoka sarafu moja kwenda nyingine. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kurudisha utaratibu wa retention kwa baadhi ya maeneo hasa ya ubalozi.

7.2.15. Sekta ya Utalii

Mheshimiwa Spika, licha ya utalii kuchangia zaidi ya asilimia 17.5 kwenye Pato la Taifa pamoja na kuchangia asilimia 25 ya mapato ya fedha za kigeni, Hotuba ya Bajeti ya Serikali haijaweza kuanisha hatua zozote zitakazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha utalii unakuwa na kuendelezwa na hivyo kuongeza mapato ya Serikali kupitia maliasili zilizopo. Kamati inashauri Serikali kuangalia hatua mbalimbali za kuwekeza na kuboresha miundombinu katika maeneo mapya ya utalii kama vile maeneo ya kusini na nyanda juu kusini pamoja na kuhamasisha na kutangaza utalii wa ndani, utalii wa fukwe na mambo kale. Aidha, Serikali ingalie namana ya kupunguza na kuondoa mlolongo wa kodi, tozo na ada mbalimbali zinazodumaza maendeleo ya sekta hii.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba kabla ya kuanza kutoza VAT kwenye huduma za kitalii, sekta hii ilikuwa ikikua kwa asilimia 12 tofauti na ukuaji wa asilimia 3 wa sasa baada ya VAT kuanzakutozwa.

7.2.16. Uboreshaji wa Mazingira ya Uwekezaji kwa Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mipango mbalimbali nchini ya kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Uwekezaji Nchini. Mfano Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Ufanyaji Biashara Nchini (*The Road Map for Improving Investment and Doing Business in Tanzania*), Matokeo Makubwa Sasa (*Big Result Now*) na sasa hivi tuna *Blue Print* ya kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini. Kamati inatambua kuwa kuandaliwa kwa *BluePrint* hiyo, itasaidia sana kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara kwa sekta binafsi. Kwa mantiki hii, Kamati inaishauri Serikali taarifa hiyo iwekwe wazi na ijadiliwe na Bunge pamoja na wadau mbalimbali ili kuiboresha kulingana na mahitaji ya wadau kabla ya kuanza matumizi yake.

7.2.17. Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa Serikali haiwezi kutekeleza miradi yote ya maendeleo kwa fedha zake tu bila kutambua umuhimu wa kushirikisha Sekta Binafsi katika kutekeleza baadhi ya Miradi ya Maendeleo. Kamati inaishauri Serikali iendelee kuweka mazingira rafiki ili iweze kuvutia sekta binafsi kuwekeza nchini ili kuhakikisha kuwa miradi muhimu ya kimkakati inatekelezwa haraka matahalani Mradi wa ujenzi wa reli ya Mtwara – Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga na Mradi wa ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma

SEHEMU YA NANE

8.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati

Vijijini na Makamu Mwenyekiti, kwa ushirikiano anaonipatia. Pia, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kuchambua na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
5. Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
6. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibajuka, Mb
7. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
8. Mhe. Dalaly Peter Kafumu, Mb
9. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
10. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
12. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
13. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb
14. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
15. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
16. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
17. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
18. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
19. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
20. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
21. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
22. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mhe. Dkt Philip Mpango (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuwa

tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri kutoka kwa Wajumbe wa Kamati wakati wote wa mjadala wa makadirio haya.

Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na wadau wa Sekta Binafsi kwa ushirikiano waliutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika na Ndugu Stephen Kagaigai - Katibu wa Bunge pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Ndugu Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala na Maombi Kakozi kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

Juni, 2018

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye uchangiaji. Mchangiaji wetu wa kwanza, tumpe heshima hiyo Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, kutoka upande wa CUF. Karibu Mheshimiwa Rukia. (*Makofi*)

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nakushukuru kwa kunipa heshima iliyo kubwa, nakuhaidi kwamba nitaienzi. Baada ya kusema hayo, naipongeza Serikali kwa kusikiliza kilio chetu Waheshimiwa Wabunge Wanawake (PWPG) pamoja na akinababa ambao walitunga mkono kwa kuondoa VAT kwenye taulo za kike. Sasa watoto wetu watasoma vizuri na utoro shuleni utapungua. Tunaishukuru sana Serikali katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naanza na kuchangia kwa kusema kwenye pato la Taifa. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri amesema kama pato la Taifa limeongezeka kwa asilimia 7.2 kwa mwaka 2018 kutoka asilimia 7.1 mwaka 2017. Pia katika kitabu hicho hicho kasema kama mapato ya ndani yamekua, yamefikia asilimia 15.8 katika mwaka 2018/2019 kutoka asilimia 15.3 kutoka mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa pato la Taifa, pia ni kuongezeka kwa fedha kwa wananchi wetu na wao wakawa nazo mfukoni. Hali ya wananchi wetu ni ngumu sana, maisha yamekuwa magumu kupita maelezo. Sasa tukisema kama pato linaongezeka, lakini maisha ya Watanzania yanazidi kuwa magumu, bado naona pato halijaongezeka na hali bado ni ngumu. Kwa hiyo, Serikali ifikirie namna gani ya kuwatoa watu wetu katika umaskini huu uliokithiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake, sijui kama ni kwa mwono wangu mdogo lakini kachangia zaidi, yaani kaelezea zaidi namna ya kuongeza mapato kwa kodi, lakini hakuna mahali nilipopaona ambapo kaonesha namna gani tutafanya biashara ili watu wetu waweze kupata ajira na kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya nchi, maisha ni magumu. Ushahidi wa haya, tuliangalieni Jiji la Dar es Salam lilivyo. Watu wengi wameanza kuhama, kuna baadhi ya matajiri wamefunga milango ya maduka, hawauzi; kodi na tozo zimekuwa ni nyingi. Zamani ilikuwa ukitaka mlango Kariakoo

mpaka umwondoe mtu kwa kumpa pesa, yaani kilemba zaidi ya shilingi milioni 10 au 20, anaondoka anakuachia wewe mlango ufanye biashara. Leo ukienda Kariakoo milango ni bure zaidi ya ile kodi utakayolipa, unachukua wala hakuna mtu wa kumwondoa. Hii yote ni kutokana na ugumu wa maisha na biashara haziendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zamani wafanyabiashara walikuwa wanakwenda Zanzibar kuchukua biashara kuleta Bara. Leo hakuna anayekwenda, kodi zimekuwa kubwa, gubu na kero la *TRA* imekuwa kubwa, wafanyabiashara wanashindwa, wamefunga mikono, wengine wanarudi vijijini, wengine wanahama.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya matajiri sasa hivi wanauza majumba yao, wanafunga biashara Tanzania wanakwenda nchi za Arabuni wanapewa *resident permit* na wanapewa na nyumba wanaishi huko. Sasa hali ikiendelea hivi, maisha yatazidi kuwa magumu kwa sababu hawa wananchi wadogo wa kipato cha chini wanashindwa kupata ajira. Kwa hiyo, naishauri Serikali tutafute namna gani ya kuwasaidia watu wetu waondokane na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mpango, kasema katika ukurasa wake wa 32, kuwa kuna mikakati ya Serikali ya kuongeza mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na urasimishaji wa majengo na kupima viwanja. Sasa napenda niitanabaishe Serikali, katika kupima viwanja huku ikiwa wataona tutaongeza mapato, tunawaumiza wananchi wetu wa hali ya chini. Kwa sababu kuna watu wameishi katika Vijiji miaka pengine 20 au 30 wamezaliwa hapo, wameishi wamejenga nyumba zao za tope, Serikali inakwenda kupima inawaondoa halafu bila ya kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, haya nasema kwa ushahidi hapa Dodoma, Swaswa Ng'ambo kuna watu ambao wamekwenda kupimiwa pale wameambiwa wakahamie Mkalama. Matokeo yake hawalipwi na hivyo viwanja wanavyopewa Mkalama wanaambiwa walipe Sh.200,000.

Hivi jamani tujiulize Mama Lishe anapika chakula ile hela hata ya ugali wake na watoto wake hapati au anajitwika beseni la ndizi anapita akiuza, ikifika jioni hata hela ya kula hana. Serikali inamlazimisha atoe Sh.200,000/=, atazipatia wapi?

Mheshimiwa Spika, sasa napenda niulize Serikali, wale wananchi tunaowahamisha sasa Ng' ambo tunawalazimisha wakanunue viwanja Mkalama, kama mtu kashindwa ina maana nyumba yake itavunjwa na yeye hatalipwa na atakosa pa kukaa? Tunawatia watu wetu umaskini. Serikali lazima iangalie, tusiwafanye watu kuichukia Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli kutokana na mambo tunayoyafanya sisi viongozi. Naishauri Serikali watu hawa walipwe na huko wanakopewa viwanja wapewe bure, siyo waambiwe wanunue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nataka kuzungumzia kuhusu *BoT*. *BoT* wanasajili Benki ambazo hazina sifa. Kuna Benki zimefunguliwa kwa mfano, *FBNE*. Benki hii ilifilisiwa tokea mwezi Agosti, 2017. Sasa najjuliza, hivi *BoT* mlivyoisajili hii Benki hamkujua kama haina viwango? Haikidhi haja? Benki hii imefilisiwa, kuna watu wamefanya kazi miaka 40, kachukua pesa zake za *gratuity* kaziweka katika benki ile, matokeo yake Benki imekuja kufilisiwa anaambiwa mtu huyu atalipwa; maana yake imewekwa ufilisi chini ya Benki ya Amana. Wamelipwa shilingi milioni 1.5, wameanza kulipwa Novemba, 2017. Wameambiwa kama watalipwa tena ni baada ya kuuzwa mali za ile Benki. Hapo mwanzo walipoisajili Benki hawakujua kama haina vigezo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *BoT* waache kusajili Benki ambazo hazina viwango. Benki zilizoshindwa kufanya kazi zifungwe. Tusiwatie umaskini wananchi wetu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja hapa atuambie watu walioweka pesa zao *FBNE*, watu wale hawana makosa, ni maskini wa Mungu, sisi ndio tuliwahamasisha waweke fedha zao benki. Kwa hiyo, tuambiwe lini watalipwa pesa zao? Kama hatukuambiwa, tunashawishi watu, tunazuia shilingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mpango, hiyo mipango yake yote aipange, atuambie lini watu hawa watalipwa fedha zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka nijielekeze kwenye Zimamoto. inavyoonekana Serikali imeshindwa kusimamia vifaa vya umeme nchini; havina viwango, ni vibovu. Kila siku yanatokea maafa ya moto, ukiuliza unaambiwa ni *fault* ya umeme. Inakuaje hata nchini viingizwe vifaa ambavyo havina sifa? Vibovu! Tunawatia watu hasara, tunawatia umaskini. Maafa ya moto yamekuwa makubwa. Juzi Kariakoo imeungua nyumba siku tatu imeshindikana kuzimwa. Kwanza hatuna vifaa. Serikali iagize vifaa vya Zimamoto, halafu tuongeze magari ya Zimamoto. Katika Wilaya zetu hakuna Ofisi za Zimamoto.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwanza ihakikishe vifaa vya umeme vinavyoingia nchini viangaliwe, viwe vina viwango na pia tuhakikishe tunaagiza magari ya Zimamoto ambayo yatasaidia kuzima moto, tena tuagize na vifaa vya kisasa. Maafa ya moto yamezidi, kuna mashule yameungua, juzi Buguruni zimeungua nyumba zaidi ya nne, sijui tano; Kariakoo moto umeshindikana kuzimwa siku tatu; Zanzibar kila siku moto unatokea. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuhakikishie jambo hili analifanyia kazi ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka nijielekeze sasa kwenye huduma za afya. Mheshimiwa Waziri Mpango wanawake tunakufa bila ya kiasi. Tunakufa kutokana na Vituo vya Afya kutokuwa na Wodi ya Mama na Mtoto, hatuna Wodi ya Wazazi. Naomba Serikali ihakikishe kila Wilaya kuwe na hospitali ambayo itakuwa na Wodi ya Wazazi, chumba cha upasuaji pamoja na chumba cha mama na mtoto.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa, malizia.

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed. Kwa upande wa CCM atakayetuanzishia ni Mheshimiwa Janet Mbene, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta. Mheshimiwa Janet Mbene, tafadhali.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuipongeza sana Serikali kuanzia na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa hatua thabiti anazochukua za ujasiri na uthubutu wa hali ya juu katika kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi yetu sasa zinanufaisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri sana mbili zote ambazo zimetolewa ambazo kwa kweli zimeonesha jinsi gani Serikali imekuwa sikivu, imezingatia masuala muhimu ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyatoa mara kwa mara, lakini imejielekeza sasa katika suala zima la uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi sana kwa sababu nimeona jinsi ambavyo hii bajeti kwa kweli safari hii imefurahisha Umma mzima wa Watanzania. Kuna mambo machache tu ya kurekebisha ambayo yako chini ya uwezo wao na naamini kabisa watayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kuzungumzia suala zima la amana pamoja na mikopo kwenye benki zetu. Bado kuna hatua kubwa sana inahitajika kufanyika katika kuelimisha wananchi wa Tanzania matumizi ya benki kwa maana ya kuweka akiba na mikopo. Bado benki zetu zinafanya kazi kwa kiwango cha chini sana kwa maana ya kuwafikia wananchi wengi ambao wanahitaji huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna suala zima la huduma za kifedha kutumia mitandao. Hii ingekuwa ni fursa kubwa sana kwa benki sasa kujiunga katika huduma kama hizo kurahisisha kuwafikia wananchi kwa huduma za kifedha kwa maana ya amana pamoja na mikopo.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala hilo hilo la mikopo, kutokana na taarifa tulizopokea bado tuna tatizo kubwa la mikopo kwa sekta binafsi haliendi vizuri na hata kwa benki zenyewe. Hii imedhihirika kutokana na sababu kubwa za mikopo chechefu ambapo tumekuwa tukielezewa ambayo vilevile kwa upande mmoja inatokana kwanza, pengine na jinsi ambavyo benki yenyewe imekuwa ikitoa mikopo hiyo lakini kwa kiasi kikubwa inatokana na Serikali na Taasisi zake kushindwa kulipa Wakandarasi na watoa huduma wengi na hivyo kuwasababishia wao kushindwa kulipa mikopo yao benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili naomba sana Serikali ilifanyie kazi kwa sababu uchumi unategemea sana mzunguko wa fedha. Sasa kama kuna fedha iko mahali imetumika lakini hairudi, inasababisha wafanyabiashara, wazalishaji wadogo na hata hao wanaoambiwa wamefunga maduka au wamehamia wapi na wapi, inatokana na kuwa labda wameshindwa kumudu sasa kuendesha biashara bila kurudishiwa madeni ambayo wanadai Serikali. Napenda sana hilo lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna suala zima la uwekezaji kwenye miradi ya umma au miradi ya kimkakati. Kwa muda mrefu sana humu ndani tumekuwa tukizungumzia miradi ya kimkakati ambayo kwa msingi wake, hii ndiyo ingezindua au ingefufua au ingechangamsha sana viwanda vyetu. Miradi ya chuma, makaa ya mawe, magadi (*soda ash*); hii ni miradi ambayo inajenga msingi wa viwanda. Sasa bila hii kuanzishwa na kuendelezwa tutashindwa hata kuendeleza viwanda ambavyo tunavitegemea.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi wa Kilimanjaro *machine tools*, huu ulishindwa kuendelea kwa sababu huko nyuma ilibidi chuma kiagizwe kutoka nje, sasa tuna chuma nchini, kiendelezwe ili viwanda kama hivi sasa vianze kuchonga vipuri tunavyohitaji kwa ajili ya viwanda vyetu. Kwa hiyo, unaona moja kwa moja kuna muunganiko mzuri sana sasa hivi katika nchi yetu wa kiuchumi ambao utawezesha viwanda kukua kwa haraka sana. Tungependa

sasa kuona jinsi ambavyo hii miradi ya kimkakati inaanza kufanya kazi. Tumeisikia kwa muda mrefu, tunataka sasa ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna suala zima ambalo nataka kuipongeza sana Serikali, wamejikita katika kuhakikisha kuwa kilimo, maji na miundombinu ya uwekezaji wa kwenye nishati unapewa kipaumbele. Hii vilevile ni misingi mizuri kwa ajili ya viwanda. Sasa kwenye kilimo nataka kuishauri Serikali, tusifanye kazi kwa mazoea. Kilimo kinahitaji mapinduzi makubwa sana ili kiwe kweli kilimo kitakacholeta tija. Tunatakiwa kuwekeza asilimia 10 ya mapato yetu kwenye kilimo peke yake. Hiyo ndiyo itatuwezesha sasa kukuza kilimo katika yale mazao ya msingi ambayo tunajua yatatusaidia katika viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mifano ya nchi kama Vietnam. Vietnam mpaka mwaka 1990 walikuwa wanaagiza chakula nje. Sasa hivi katika nchi 10 au 20 zinazozalisha mazao ya kilimo kwa wingi, Vietnam na yenyewe imo ndani. Wameboresha kilimo chao na uzalishaji wao na ufugaji kwa ku-*modernize*, kwa kutumia teknolojia, kwa kutumia ubia na nchi zilizoendelea ili kuhakikisha kuwa wananchi wao wanazalisha kwa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kwa nini tusifanye hivyo? Sasa hivi tumeingia kwenye uhusiano wa Kidiplomasia na Israel. Israel wana teknolojia ya hali ya juu katika masuala haya ya maji, umwagiliaji na kilimo. Tunaweza tukaungana nao. Hii siyo ngumu sana, kwa sababu vijana wetu wakienda kule au wao wakija kwetu, moja kwa moja tunaweza tukajikuta tunakuza kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, tuna mazao tayari yanaonyesha tija kubwa sana. Kwa mfano, korosho, ufuta, mbaazi, nafaka za aina mbalimbali na dengu; sasa hivi tunahitaji kupeleka pia uzalishaji mkubwa kwenye kilimo cha mawese na alizeti. Yote haya ni mazao yanayotakiwa yapewe kipaumbele zaidi ya yale mazao ya kawaida ambayo tulikuwa tumezoea kuzalisha ya kahawa na mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuki-*diversify* namna hii tutakuta kilimo chetu kinachangia pato kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa hivi. Ni lazima sasa hivi tujipambanue na kilimo kama njia kubwa ya kuingia kwenye viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile biashara ni eneo ambalo tumekuwa tunakua vizuri, siyo Tanzania peke yake, lakini Afrika Mashariki, Afrika na hata dunia nzima. Tanzania tuko katika nafasi nzuri sana kwa sababu tuna maeneo makubwa ya mipakani. *Cross border trade* bado ni eneo zuri sana kwetu sisi Watanzania, lakini limegubikwa na mambo mengi ya urasimu ambayo yanafanya isiwe rahisi kwa biashara kuendeshwa kati ya mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo ya watu wa *customs*, tuna matatizo ya uwezo mdogo wa kusimamia masuala haya, tuna matatizo ya rushwa, tuna matatizo ya *bureaucracy*, yaani *licensing* na zile taratibu nzima za kufanya biashara kati ya nchi na nchi bado hazijawa nzuri hata katika Kanda ambazo tayari tuko katika umoja. Kwa mfano, *East Africa*, tujaribu sasa kuondoa zile *non-tariff barriers* ambazop ndiyo zinazoturudisha nyuma, tuanze kufanya biashara sisi wenyewe kwa wenyewe. Tuachane na mambo ya kukimbizana na nchi za nje ambao wanatuletea vikwazo vingi sana. Tuna fursa kubwa sana sisi Waafrika kwa Waafrika kufanya biashara pamoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Janet Mbene. Nilishamtaja Mheshimiwa Margaret Sitta, atatafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab. Mheshimiwa Mama Sitta, karibu.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na wakati huo huo nawashukuru wapiga kura wa Urambo wanaoendelea kunipa ushirikiano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na hasa Wizara inayohusika, Mawaziri wote na watendaji wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na hasa kwa bajeti hii ambayo inalenga kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia ukurasa wa 40 ambako kumetolewa maelezo wazi kabisa kwamba bajeti hii itaangalia suala la upatikanaji wa maji vijijini kama walivyopendekeza pia Kamati inayohusika, pia itazingatia suala ala afya. Hapa naomba niikumbushe Serikali kwa upande wa afya, pamoja na jitihada nzuri zinazofanywa na Serikali, bado tuna tatizo kubwa sana la uhaba wa wafanyakazi. Tunaomba suala la wafanyakazi lipewe kipaumbele; na pia uendelezaji wa ujenzi wa Vituo vya Afya ambavyo bado vinahitajika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu pia imeelezewa, lakini nielezee tu kwamba, kuna kifungu hiki kimoja katika ukurasa wa 40 ambacho nimekipenda sana, ila naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha afafanue. Kinasema: "*Aidha, mahitaji ya makundi maalum katika jamii yetu; wanawake, vijana, watoto, watu wenye ulemavu na wazee wataendelea kuangaliwa kipekee.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha, atueleze 'kipekee' maana yake ni nini? Je, wenzetu wenye ulemavu wa ngozi wategemee mafuta wanayotumia pengine yatapunguzwa bei? Je, wenzetu wasioona watapata pengine fimbo za kutembelea? Tunaomba aneo hili liwekwe wazi ili watu waendelea kuishi kwa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wabunge Wanawake na Wabunge Wanaume wanaotuunga mkono katika kutetea haki za wanawake na watoto wa kike, naipongeza sana Serikali kwa ukurasa wake wa 46 ambapo wametamka wazi kabisa kwamba wanaondoa kodi katika taalo za kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, hii ajenda ni ya wanawake wote chini ya Chama chetu au Umoja wetu unaoitwa *TWPG*. Tumekuwa tukilizungumzia suala hili kwa muda mrefu na nachukua nafasi hii pia kuishukuru Serikali, imekuwa ikikubali kuwaleta Wawakilishi wao katika vikao mbalimbali ambavyo tumekaa pamoja ili kuhakikisha kwamba hili leo walilolitamka linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wanawake wa Bungeni wote kuishukuru sana Serikali kwa ukurasa wake wa 46 ambao umekubali kupunguza kodi ya ongezeko la thamani. Nimefanya hesabu hapa, nimeona kwamba *VAT* asilimia 18 kwa taalo za kike zinazouzwa Sh.2,000/= zitakuwa zimepungua kwa Sh.360/= na kwa taalo za kike ambazo zitauzwa kwa Sh.3,500/= gharama itapungua kwa Sh.630/=.

Mheshimiwa Spika, tumechukua hili kwa uzito wake kwamba angalau Serikali imefikiria. Ndugu zangu akinamama na akinababa mnaotuunga mkono, tuipongeze Serikali kwa hatua hii. Kwa sababu kwa watoto wa kike wanaoshindwa kwenda shuleni kila mwezi kutokana na kukosekana kwa taalo za kike, wanapoteza siyo chini ya siku nne au tano. Kwa hiyo, kwa nusu muhula wanapunguza karibu wiki tatu wanashindwa kwenda shuleni na ukichukulia kwa muhula mzima wanashindwa kwenda shuleni kwa wiki sita na kwa miaka minne kuanzia *form one* mpaka *form four*, wanapoteza wiki 24 za kutokwenda shule.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia sana habari za utoro kwa watoto wa kike na kwa taarifa au utafiti uliofanywa na *UNESCO* umeonesha wazi kwamba katika watoro wa kike 10, mmoja anashindwa kwenda shule kutokana na ukosefu wa taalo za kike. Kwa hiyo, hii hatua ya Serikali tunaipongeza sana nikiamini kwamba pengine itachukua hatua zifuatazo ili huu msamaha huu wa kodi uwe na manufaa zaidi:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunaiomba Serikali iwashawishi wawekezaji wa viwanda wengi zaidi wawekeze katika eneo hili. Viwanda vikijengwa vingi, hizi taulo zitapatikana kwa wingi zitasaidia pia hata kushusha bei zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, tunaiomba Serikali sasa, katika malighafi zitakazotumika kutengeneza taulo za kike, VAT pia iondolewe, yaani wapate msamaha wa kodi ili malighafi zipatikane kwa bei nafuu ili wengi zaidi watengeneze taulo hizo. Tunaiomba Serikali, siyo iwaombe tu wafanyabiashara kupunguza bei, hapana; tunaomba hata ikiwezekana itoe bei elekezi ili angalau hizi taulo za kike zipatikane. Naamini, ndugu zangu kwamba hizi taulo za kike kupunguziwa kodi ni hatua ya kwanza. Tunaiomba kwa heshima Serikali tukitegemea kwamba iko siku itafikiria kutoa hizi taulo za kike bure kwa kadri ya uwezo wa bajeti utakavyowezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuja na uamuzi wa kuondoa riba katika mikopo inayotolewa kwa akinamama na vijana. Tunaomba hili suala liendelee, sheria itakapowekwa vizuri, basi kusiwe na riba yoyote katika mikopo.

Mheshimiwa Spika, itakuwa sikutenda haki kama sikukutaja wewe siku ya leo kwamba umekuwa mstari wa mbele kutuunga mkono akinamama tunapoangalia vipingamizi vya watoto wa kike kuhudhuria shule. Moja ilikuwa ni hili la taulo za kike ambalo Serikali imelifikiria, lakini la pili ni uhaba wa vyoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vyoo vingi karibu asilimia 52 vinavyotumiwa na watoto wa kike havina milango. Kwa hiyo, tunakupongeza wewe kwa kutuunga mkono kwa *fund raising* tunayoitegemea tarehe 22 Juni, 2018, ili tuchangie upatikanaji wa vyoo vya kike, tutoe vyoo vya mfano ili vyoo vitakapojengwa sasa viweze kumsitiri mtoto wa kike na wa kiume pamoja na walemavu. Tunakushukuru sana kwa kutuunga mkono kwa suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nililotaka kuzungumzia ni suala la kodi za mazao. Tumbaku ifikiwi pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakupongeza wewe kwa kutuunga mkono. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Sitta. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Urambo. Mheshimiwa Adadi Rajabu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kamala. Mheshimiwa Balozi.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo pamoja na Bajeti ya mwaka 2018/2019. Kwanza nampongeza sana Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha. Najua kazi kubwa wanayo, lakini kutuletea bajeti hii ni kitu kimoja ambacho wamefanya usiku na mchana na kwa kweli bajeti imeonekana na ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais hasa kwa kipindi hiki kifupi cha miaka miwili na nusu kuweza kuja na miradi mikubwa, ya kisasa na ya kileo ambapo kwa kweli miradi hii itakapomalizika, naamini kabisa kwamba uchumi wa nchi yetu utakuwa mkubwa sana. Miradi hii imeorodheshwa vizuri kabisa. Miradi kumi ambayo ameiorodhesha Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake cha mpango ambayo ukianza na reli, mambo ya ndege, mambo ya bomba la mafuta, umeme, Mkulazi na kadhalika, ni mizuri sana na imechukua matrilioni ya hela, lakini hii itakuwa ni historia ambayo Awamu ya Tano itaiweka katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni ya tatu ya Awamu ya Tano. Kwa kweli ukiiangalia bajeti hii ni nzuri sana na imelenga hasa kulinda viwanda vya ndani. Mheshimiwa Waziri ameeleza kwenye hotuba yake hapa, ameongeza kodi nyingi sana kwa bidhaa ambazo zinatoka nje kwa ajili ya kuingia

ndani. Kwa kweli tunampongeza sana kwa sababu kutoka page 48 - 52 ameorodhesha bidhaa zote hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri na hii ni hatua nzuri ambayo inaonekana kutoa mwanya sasa kwa wawekezaji kuweza kuweka viwanda hapa nchini, kuongeza ajira na kufanya mambo mengi ili ku-*discourage importation* kutoka nje. Suala hili la ku-*discourage importation* kutoka nje lilifanyika na nchi nyingi tu; India wanafanya sana, hawataki bidhaa kutoka nje au vitu kutoka nje na wanatumia vitu vyao vya ndani, *South Afrika* na nchi nyingine nyingi. Kwa hiyo, hii ni hatua na mwenendo mzuri sana ambao naamini kabisa utatupa faida sana kwenye hii nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nianze kuchangia pia kwenye mambo ya mfumo mpya wa kodi za *Electronic (Electronic Tax Stamp - ETS)*. Mpango huu ni mzuri sana na ni mpango ambao unatutoa kwenye *manual system* na unatupeleka kwenye *electronic*. Ni mpango ambao utaweza kujua ni bidhaa gani zinazalishwa na kupata takwimu sahihi ambazo zinatoka kwenye viwanda.

Mheshimiwa Spika, mpango huu pia wameuchukua kwenye nchi nyingi ambazo wamewahi kufanya. Wameuchukua kutoka Kenya, Morocco, Uturuki, Malaysia na Switzerland. Nchi zote hizo ambazo zimechukua mpango huu, wamekwenda kwenye mambo ya *sprits*; bia, vinywaji vikali na sigara. Sasa sisi mpango huu tumejumuisha vinywaji vikali, bia, sigara, maji na *soft drinks*. Kitu ambacho nina wasiwasi na Kamati ina wasiwasi ni kwamba huenda tukaweka *burden* kubwa sana kwa mnunujaji, mtumiaji wa vitu hivi.

Mheshimiwa Spika, naona kwamba mpango huu ni mzuri na unatakiwa uanze mara moja, lakini ni vizuri Wizara ikajitathmini kwamba itakapochukua vitu vyote hivi *in totality* hasa maji na *soft drinks*, huenda mzigo mkubwa ukaenda kwa mtumiaji. Ni vizuri iangalie kwa makini kwa sababu siyo ajabu kwa mpango huu vitu hivyo vikaongezeka bei, ingawa

kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba bei hazitaongezeka kwenye bidhaa hizo, lakini nina uhakika kwamba wataongeza bei hapa. Kwa hiyo, naomba aangalie vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, la pili, mpango huu, hiyo Kampuni ya *SCIPA* ambayo imepewa imeonekana kwamba itakuwa *self financing*, lakini sidhani kama itakuwa *self financing*. Hakuna biashara ambayo inafanyika bila kupata faida.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya tu kwamba vitabu vya hotuba yetu havijafika, lakini kuna mchanganuo ambao umetoa na unaonekana kwamba huenda kampuni hii ikapata faida kubwa sana. Wasiwasi uliopo ni kwamba, kampuni hii tumeipa miaka mitano. Kwa nini tuipe miaka mitano? Kwa nini tusipunguze? Tumeweka mkakati gani wa kuweza kuangalia kwamba tutafanya vipi kuweza ku-*train* watu wetu ili baada ya huo muda tuweze kuendelea wenyewe na huo mpango? Kwa hiyo, niliona tujaribu kuangalia hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine nataka tuangalie *system* hii ya Akaunti Jumuiifu ya Hazina (*Treasury Single Account*). Tumekwenda vizuri sana kwenye Mifuko. Mfuko wa Maji umekwenda vizuri sana na umesaidia sana, kwa sababu ulikuwa *ring fenced* kwamba huruhusiwi, umezuiwa na Hazina walikuwa wamefanya vizuri sana wanapopata fedha zile moja kwa moja wamezipeleka kwenye maji na umesaidia sana kuleta maendeleo ya maji na miradi mingi ya maji. Hii ni pamoja na *REA* na barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumekwenda tunataka tuanzishe hii *Treasury Single Account*, kwamba sasa hii Mifuko yote inaweza kufa. Itakapokufa, majukumu yote yanakuwa kwa Wizara. Sasa hii ni *issue* ambayo ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge tuiangalie. Kweli Wizara imejitayarisha kupokea hela zote na kuhakikisha inazigawa hela zote kwa wakati? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hapa ni muhimu sana kuangalia; Wizara imejitayarisha namna gani? Ni vizuri kama wanajitayarisha, wajitayarisha kwa *E-system* ili kuweza kutoa hizo fedha kwenye maendeleo. Kwa sababu kuna miradi mingi ambayo imeshaanza, imetiwa saini, lakini hakuna uhakika wa kwamba hii *system* itakapoanza wakati huu, hiyo miradi itaendelea namna gani?

Mheshimiwa Spika, hapa tunaona hela za maendeleo zimechelewa sana kupelekwa kwenye mikoa. Sasa tunakuja kwenye *E-system*, hii miradi ambayo tumeshasaini mikoani itakuwaje? Ni vizuri Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind-up* aweze kutoa ufafanuzi wa hili suala kwa sababu ni muhimu sana na nashauri kwamba tujitayarisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la *PPP*. Ni muhimu sana kitengo hiki kikaimarishwa kwa sababu miradi mingi na mikubwa, ni vizuri ikafanyika kwa njia hii. Naamini kabisa ile miradi ambayo *feasibility study* imeshafanyika, basi itangazwe. Itakapotangazwa, nina uhakika wawekezaji watatokea. Tumefanya hivyo kwenye hivi viwanda vya madawa na watu wengi wametokea. Sasa hii miradi mingine, kwa mfano *road toll*, barabara ya Ubungo - Dar es Salaam – Morogoro...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Malizia Mheshimiwa.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, kwa nini tusingie kwenye *road toll*? Ni kitu cha muhimu sana, naomba sana tuangalie. Au *feasibility study* ya reli ya Tanga, imeshamalizika, kwa nini wasiitangaze sasa wawekezaji watokee? Naamini kabisa kwamba tutakapochukua uamuzi huu, mambo haya yataweza kwenda kwa haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kuna suala moja ambalo sekta binafsi inalalamika sana kuhusu

malipo yao ya fedha za VAT. Wanadai shilingi bilioni 600, haya mambo ya wawekezaji kwenye mambo ya sukari. Naamini kabisa Serikali italiangalia kwamba umechukua hizi hela 15%, basi hakikisha unazirudisha kama ambavyo umeamini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mengine nitaandika, nakushukuru sana kwa muda huu. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab. Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Magereli, kwa upande wa CHADEMA.

MHE. DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuchangia bajeti muhimu iliyo mbele yetu; bajeti ya kujenga Tanzania ya Viwanda. Kwa kweli ukiiangalia bajeti, ukiisoma utaona kwamba sasa tumeanza kupaa kuelekea Tanzania ya Viwanda kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa kwenye bajeti, kila mtu anapotazama bajeti, mwingine atapendelea kuona ni fedha kiasi gani zimetengwa na zinaenda wapi? Kwa mchumi atapendelea kuangalia Sera za Kikodi zinasemaje na zinaweza kusaidia nchi namna gani? Hilo ndilo jambo kubwa sana kwenye bajeti. Ndiyo maana nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake kwa bajeti nzuri ambayo imewasilishwa na ukiisoma kwa kina na viambatisho vyake, ni bajeti nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda tu nitoe angalizo kidogo tu, hasa kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, awaambie watalaam wake kila jambo linalowasilishwa hapa Bungeni tunasoma kila nukta nakila koma; na mtu mwingine anaweza akasoma kitu kidogo akakitumia kuonesha kwamba bajeti haiko sawa, kumbe ni makosa tu kidogo labda ya Wasaidizi wameshindwa kuweka mambo sawa.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano tu, halafu naomba Mheshimiwa Waziri awaelekeze Watalaam wake na Wasaidizi wake wawe kila jambo linaloletwa ndani ya Bunge

hili wahakikishe liko sawa. Vinginevyo linaweza likawa jambo dogo halafu mtu akaanza kushughulika na hilo ikaonekana bajeti yote haina kitu, kumbe ni uzembe wa mtu mmoja kwenye dawati fulani. Huu ni mfano tu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukisoma kitabu cha Mipango kinaeleza vizuri tu kwamba akiba ya fedha za kigeni, tuna fedha za miezi mitano (5.4). Ukisoma kitabu kingine hiki cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2017, hawa wanatuonesha tuna fedha ya miezi sita. Sasa sita na 5.4 ni vitu viwili tofauti. Sasa makosa madogo madogo kama haya yakikutana na wenzetu wa upande wa pili kule, wanaweza wakashughulika nayo ikaonekana ni jambo kubwa kumbe ni uzembe kidogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bajeti ni nzuri na nisingependa kupoteza muda kwa vitu vidogo vidogo kama hivyo. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tujikite kwenye mambo ya msingi na namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wawambie Wasaidizi wao wawe wanaangalia vitu hivi visije vikatupotezea muda bila sababu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitazungumzia kuhusu *PPP (Public Private Partnership)*, naona ni jambo muhimu sana hili. Ni jambo muhimu sana kwa sababu ukiangalia changamoto tuliyonayo, kilio tulichonacho ni kwamba fedha za maendeleo haziendi kwa wingi kama tulivyotarajia, lakini ukiangalia na shughuli za maendeleo tulizonazo, mahitaji ya maendeleo tuliyonayo nayo ni makubwa; tunaingia kwenye Rufiji, tunahitaji fedha nyingi, *standard gauge* tunahitaji fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, miradi hii kama tungejipanga vizuri, tunaweza tukatafuta fedha kutokana na vyanzo vingine na kwa hiyo, tukatoa unafuu mkubwa sana kwenye bajeti kujikita kwenye shughuli nyingine za maendeleo na shughuli nyingine. Nadhani ni eneo la kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili tulifanye, tunayo Sheria ya *Public Private Partnership*. Sheria ile ukiisoma inatoa vivutio lakini haivutii sana wawekezaji kupenda kuingia kwenye *Public Private Partnership*. Katika Bunge hili tutakuwa tumefanya jambo kubwa kama sheria hiyo Mheshimiwa Waziri akiona inafaa, ikaletwa tukajaribu kuongeza vivutio vitakavyotusaidia kuhimiza watu kuingia kwenye *Public Private Partnership*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba tulifanye hili, kwa sababu tusipofanya hivyo, tutajikuta miaka mitano inaisha, Watanzania wanaendelea kulalamika kwamba hawaoni fedha kwenye mifuko, tutajikuta tunaendelea kuwa na miradi mikubwa, ambapo utekelezaji wake ni gharama. Kwa kweli mtu akiangalia kwenye mfuko kama fedha haioni, hata uelezee uchumi vipi Mheshimiwa Mpango itakuwia ngumu sana kueleza. Maana watu wanaangalia je, akipeleka mkono kwenye mifuko kuna kitu?

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kwa mara ya kwanza nilipogombea Ubunge katika hotuba ya kwanza nikaeleza sera za uchumi zilivyo, mfumuko wa bei na kadhalika. Baadaye kuna Mwalimu mmoja wa Shule ya Msingi moja pale, akaja akasema, kijana unaongea vizuri mambo ya uchumi haya, lakini mbona hatukuelewi? Unazungumza vizuri, mfumuko wa bei na kadhalika, lakini mbona hatuelewi Mheshimiwa?

Mheshimiwa Spika, Katibu wa Chama wa Wilaya yangu Mzee Kamaleki, akaniambia, Mheshimiwa Kamala, unajua kule ulikuwa unafundisha, sasa huku umerudi kwa watu. Sasa unachofundisha darasani na kwa watu, lazima viendane. Nikamwuliza, tunafanyaje? Akasema, wewe subiri nikuoneshe, angalia ninavyoomba kura, mimi Mheshimiwa Kamaleki Masikini Lufufu nisikilize vizuri, kwa *style* hii ukifanya kama ninavyofanya mimi, watu watakuelewa. Kwa hiyo, taratibu nikabadilika. Kwa hiyo, nikajua kuna kile kilicho kwenye vitabu, lakini kuna kile cha kutekeleza, ni vitu viwili tofauti kabisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango naomba aliangalie hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *PPP*, nitaenda haraka. Kuna mifano mingi tu. Kwa mfano, ukienda Johannesburg pale, utakuta mradi mkubwa wa Gautrain unaounganisha Johannesburg na Pretoria wa *train*, wamejenga kwa *PPP*. Ukienda Marekani unafahamu Mheshimiwa, unaenda mara nyingi kule, *New York* pale utakuta daraja linalounganisha Manhattan na Queens wamejenga kwa *PPP*. Naomba Mheshimiwa Mpango waliangalie. Hii *PPP*, tuletieni ile sheria tuongeze vivutio itatusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka nilipokuwa Balozi kule Brussels, nilimpigia simu Mheshimiwa Mpango tukazungumza na aliniambia kwamba alikuwa na miradi ya kielelezo, tukazungumza. Nikamwambia nilikuwa nimeandaa mkutano mkubwa kule, bahati mbaya hakuweza kuja. Sasa bahati nzuri sasa ni Waziri wa Fedha, hiyo miradi najua bado anayo na bahati nzuri nami niko hapa, hebu alete miradi yake hapa na Mheshimiwa Spika atalifanyia utaratibu nitarudi tena Brussels niuize sasa kama Mbunge. Haya yanawezekana; na ile miradi najua bado anayo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo miradi tukiifanyia kazi itatusaidia sana kupaa. Hatuhitaji kutumia shilingi, unahitaji tu utoe fedha kidogo, unipe *per diem* kidogo hapa, Mbunge anaenda *first class*, usisahau; haendi *economy*. Sasa Balozi huwezi kumweka *economy*. Tukienda hivyo, tutauza hii miradi na nchi itaenda. Ule mradi wa Mkulazi, tunazungumzia mambo ya Kitaifa. Pale Mkulazi kuna mashamba tu, kiwanda bado hawajaanza kujenga. Jana usiku nilikuwa nazungumza na Maafisa Magereza wako pale, wakasema Mheshimiwa pale Mkulazi bado hatujaanza kujenga, kuna *store* tu peke yake...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

SPIKA: Mheshimiwa Balozi, malizia tu.

MHE. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nimalizie kwa kuunga mkono kwa uamuzi wako

kuhusu malighafi, kuhusu *Crude Palm Oil*, ile kodi ya 25% na 35% hatua alizochukua Mheshimiwa Waziri ni sahihi na naomba asiyumbe. Kwenye bajeti amesema kwa mwaka mmoja; isiwe kwa mwaka mmoja, iwe kwa miaka yote. Kwa sababu tunataka kujenga Tanzania ya Viwanda. Yuko sahihi, aendelee kufanya hivyo hivyo, asiyumbe na wala asiogope, kwa sababu najua jambo hili lina changamoto nyingi, lakini asimame imara na sisi Waheshimiwa Wabunge tuko imara, tutasonga mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Kamala kwa hotuba yako nzuri. Ni kweli Mheshimiwa Balozi nilikuwa nakuwa naye mara moja moja pale Brussels mpaka kule Matongee kwa Wakongomani. Ahsante sana.

Mheshimiwa Lucy Magereli, akifuatiwa na Mheshimiwa Charles Kitwanga. Mheshimiwa Lucy; hayupo tena! Mheshimiwa Kitwanga tuendelee, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Salim Maalim.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii. Kwanza nianze tu kwa kusema, kwa kweli bajeti hii ni bajeti iliyotengenezwa, ikapikwa, ikawekwa, ikachujwa na ikatoka kuwa bajeti ya uchumi wa viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea naipongeza Serikali kwa kile inachofanya na Mheshimiwa Mpango pamoja na Naibu wake na wafanyakazi wote katika Wizara nawapongeza sana, bajeti yao ni nzuri kwa Taifa letu. Nianze kwa kutaja tabia za pesa. Tabia za pesa ziko hivi.

SPIKA: Mheshimiwa Kitwanga sekunde moja. Unajua Waheshimiwa Wabunge hawa huwa hatufahamiani humu ndani. Mheshimiwa Kitwanga ni *Senior Officer* aliyefanya kazi *Bank of Tanzania* kwa zaidi ya miaka 23. Kwa hiyo, anaposhuka hapa unamsikiliza kwa maana hiyo. Mheshimiwa Kitwanga endelea tu. (Kicheko/Makofi)

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa *complement* hiyo.

Mheshimiwa Spika, tabia ya pesa ziko mbili ya kwanza pesa huwa hazitoshi, pili pesa huwa haiishi utamu. Kwa hivyo, ndugu zangu wa mkono wangu huku wa kulia kila siku wanapokuwa wanalalamika kwamba tuna madeni ni kwa sababu pesa siku zote haitoshi na utamu hauishi. Nj jambo ambalo lazima tujivunie kwamba bajeti hii imelenga katika ule mpango wa 2025, tuwe uchumi wa kati vilevile tuwe na viwanda.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mapunguzo katika elimu hii ni katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na *resource* inayoitwa *human capital*. Hawa watu tutakaokuwa tunawahitaji kwenye viwanda vyetu wasiwe ma-*expert* tuwajenge kutoka hapa, kwa hivyo tunapopunguza katika daftari, tunapopunguza katika vifaa vya elimu tunataka tuwe na wataalam wa kwetu, Watanzania watakaoweza ku-*serve* katika viwanda vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tufanye nini cha ziada, kwanza tuache hizi biashara ndogondogo, naipongeza sana Serikali kwa kile ilichokifanya hasa kwa upande wa simu. Nakumbuka nilipokuwa Naibu Waziri wa Sayansi na Teknolojia mwaka 2011 nili- *suggest* kwamba tuweke mitambo *TCRA* itakayo- *monitor* matumizi ya simu ili tuweze kujua kila senti inayotumika je, inalipiwa kodi, tumechukua miaka mingi kidogo.

Mheshimiwa Spika, nikiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini mwaka 2013 nilipendekeza kufunga *flow meter* kwenye upakuaji wa mafuta, nikapendekeza vilevile tukawa tumeunda timu ya kuweza kusaidia tuwe na *single off-loading point*, najua ndani yetu humu ndani wako Wabunge wengine ambao wanafanya biashara za mafuta na wanaipinga sana hiyo *single point off-loading*, naomba hili tulitilie mkazo sana.

Mheshimiwa Spika, *flow meter* zifungwe na iwe ni sehemu ya *off-loading* kwenda kwa wale matenki ya watu

siyo pale wanapopokea, kwa sababu wanasema na wanadanganya kwamba kuna *evaporation*, kuna asilimia kubwa inatokea kwamba mafuta yanapotea, tuhakikishe kwamba tunachukua pesa zetu pale tunapowapelekea hawa wauzaji. Kwa hivyo, mafuta yatakapokuwa yanapakuliwa kutoka kwenye meli yaende sehemu moja, halafu kutoka kwenye sehemu hiyo sasa tunawapelekea hawa sijui *OILCOM*, *MOIL* sijui *PUMA* ndipo wapelekewe na tunapowapelekea tayari tumeshachukua pesa zetu. Nadhani hili litatusaidia sana kuweza kuongeza mapato katika Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niombe Serikali kwa ujumla *to work as a team*, naomba ndugu zangu wa viwanda na biashara, ndugu zangu wa ardhi na ndugu zangu wengine tuwe na ushirikiano. Mwekezaji anapokuja isichukue siku 40, miezi miwili mpaka anapata kibali cha kuanzisha kiwanda. Inashangaza pale ambapo mwekezaji anataka kutengeneza magari anaacha kuwekeza Tanzania anakwenda anawekeza Rwanda! Wakati ukitaka kupeleka vitendea kazi pamoja na *raw material*/Rwanda ita-*incur cost* nyingine kuvisafirisha kwenda kule.

Mheshimiwa Spika, nadhani tuliweke *incentive* sana kwenye madini, *incentive* hizo tuziweke kwenye viwanda. Halafu niwaambieni kitu kimoja madini *resources* kubwa iko ardhini kwetu, akishachimba akaitoa haiwezi kurudi, lakini *resources* kubwa kwenye viwanda ni *capital* yake atakayoileta na akishajenga kiwanda hawezi kukibeba akakitoe akaenda nacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo lazima tuwe na mipango na sera ambazo ni za kuvutia zaidi kwa sababu *after all* hatuko *stationary* lazima kuwe na mabadiliko, tukimrahisishia akaleta kiwanda hapa, pale ambapo tutaona kwamba upande wetu labda hatukuwa tumefanya vizuri sana, bado *we can negotiate, we are negotiating now* kwenye madini, lakini tutaendelea kuwa mtu akiwa ameleta kiwanda atakuwa ame-*employ* watu

wetu, atakuwa amelipa *tax*, hawa watu walikuwa *employed* na wenyewe watakuwa wamelipa *tax* kupitia kwenye *pay as you earn*.

Mheshimiwa Spika, tutumie uzoefu wa sehemu zingine kuweza kuona kwa nini sisi ukiangalia Kenya, ukiangalia Tanzania, Kenya bajeti yao ni 30 *billion USD*, Tanzania ni 14 *billion USD why?* Nasi tu wengi na vilevile ni nchi kubwa! Kwa hivyo ni lazima tuhakikishe tunaweka miundombinu inayopendeza au inayovutia ili tuweze kuwashinda wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *PPP* imezungumziwa sitaki kuirudia, kwa mfano tumezungumzia reli ya kutoka Mtwara kwenda Mbamba Bay sijui muda gani.

SPIKA: Malizia Mheshimiwa.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba, tuhakikishe kwamba hiyo reli inavutia, uzoefu aliosema Spika umenikutanisha na watu wengi sana. Pale ambapo tutahitaji kusaidiana maana yake Mtanzania lazima ui-*serve* nchi yako kutokea mahali popote. Mimi nina watu wa kutosha zile *contacts* zangu nikiwa *Bank of Tanzania* bado ninazo na naweza nikawapa watu wapo wengi tu wanaotaka kuwekeza hasa kwenye reli hiyo na maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Charles Kitwanga.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, lakini sijasema kitu kimoja tu, naunga mkono hoja asilimia 108. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana, umenigusa katika hoja moja ambayo hata mimi nitapenda siku moja Waziri wa Fedha atuambie, ni hoja ya wivu tu, kwamba kwa nini Kenya wawe na bajeti mara mbili ya bajeti yetu, yaani mara mbili kabisa

yaani kwa nini? Ni hoja ya wivu tu ahsante sana. Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Hamadi Salim Maalim. (*Kicheko*)

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pia nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Naomba nianze na Kitabu cha Mpango kama Mheshimiwa Waziri Mpango alivyoelezea, kwenye ukurasa wa tisa uchumi wa Taifa, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba Pato la Taifa limepanda kutoka asilimia 7.0 hadi asilimia 7.1 ambapo pato hili lilikuwa ni trilioni 47.173 mpaka trilioni 50.5.

Mheshimiwa Spika, pato la Taifa najua ndilo linalo-*determine* kile kima cha kila mtu kwa nchi ile, sasa tukija kwenye kima cha kila Mtanzania kutokana na pato hili la Taifa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kima cha kila Mtanzania kitakuwa ni Sh.2,275,000 kutoka Sh.2,086,000.

Mheshimiwa Spika, tukichukua Pato la Taifa ambalo ni trilioni 50.5 sijui tugawe kwa idadi ya watu wangapi tulionao mpaka tupate milioni 2,275,000; kwa kweli naona kwamba bajeti imetudanganya katika kiwango hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hivyo kitabu cha *CAG* ukurasa wa 63 amesema kwamba Pato la Taifa ni trilioni 106.8 lakini kitabu cha Waziri Mpango kinasema ni trilioni 50.5, sasa sijui tushike ipi iliyo na ukweli ya *CAG* au ya Waziri Mpango? Inawezekana pengine na Kamati ya Bajeti na wao wana kima chao sijui ni ngapi. Kwa hiyo naomba Waziri atueleze je, wametumia takwimu ipi ya *CAG* ya kitabu cha Mpango katika kutuelezea pato la kila Mtanzania la 2,275,000 kwa kila mtu. Hilo ni jambo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba niende kwenye mapato ya Taifa na matumizi. Bajeti ya 2018/2019, imekisia kwamba itakusanya trilioni 32.48, sasa tukija katika matumizi yaliyopangwa, tumepanga kwamba tutalipa madeni ya Serikali ambayo ni trillioni 10, sasa trilioni 10 hizi tukizilipa kwa mwaka tunakuta kila mwezi tukichukua *calculation* ya kila mwezi tunatakiwa tulipe bilioni 833.33, lakini baadaye

tunakuwa na mishahara ambayo tumepanga kwamba kwa mwaka tutatumia trilioni 7.409. Hii tukiigawa kwa mwezi tunapata kwamba kila mwezi tunatakiwa tutumie bilioni 617, ambazo tukujumuisha hizi za madeni tu na mishahara ni karibu trilioni 1.4 wakati makusanyo ya Taifa tunasema ni kati ya trilioni 1.2 mpaka 1.3, hatujaingiza matumizi mengine hatujaingiza miradi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, matumizi mengine Serikali imepanga kwamba itatumia trilioni 3.054 kwa mwaka ambapo kwa kila mwezi tunatakiwa tutumie bilioni 254. Miradi tumepanga kwamba tutatumia trilioni 12, hizi tumesema trilioni 2.13 ni mapato ya nje, tuyaweke mbali inamaana tuna trilioni 10 ambazo zinatokana na mapato ya ndani. Trilioni 10 hizi tukigawa kila mwezi tunapata bilioni 833.33. Sasa tukijumlisha yote tunakuta kwamba tukitoa zile bilioni mbili tuwe na makusanyo ya shilingi trilioni 2.529, hivi kweli Serikali tuna uwezo wa kukusanya mapato haya kwa kila mwezi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, watueleze Serikali wana mikakati gani wakati *trend* ya 2016/2017, imeonesha tumekusanya trilioni 21, *trend* ya 2017/2018 tumekusanya pia trilioni 21.89 je, kuna mikakati gani waliyoiandaa mpaka kuweka makisio makubwa kiasi hichi. Hii bajeti ni ya udanganyifu na wala haitekelezeki. Kwa hali hii inaonesha kwamba mkakati huu uliopangwa wa mapato na matumizi wote ni hewa, bajeti haitekelezeki. Hilo ni jambo la pili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, naomba niende kwenye kueleza kwamba bajeti yetu ni hewa, tunapanga makubwa makusanyo yetu lakini uwezo wa kukusanya ni mdogo. Mwaka 2016/2017 tulipanga makusanyo ya trilioni 29.54 tukakusanya trilioni 20 ambayo ni sawa na asilimia 70, asilimia 30 hazipo, kwa hivyo inaonesha kwamba hizi asilimia 30 tulijikusanyia tu kumbe ni hewa hazipo, sawa tulijipangia kumbe ni hewa hazipo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018 tukaongeza yaani ule mzigo mdogo tuliokuwa nao 2016/2017, tukauona

kwamba ni mdogo tukaongeza mwingine tukajikusanyia huku mgongoni kutoka 29 tukaja 31, hii 29 haikuteteleza jamani tunakuja 31. Nashauri bora tungerudi nyuma tukaangalia ule uwezo wetu, kwamba hatuna uwezo wa nakusanyo ya trilion 29 tuangalie *reference* kwamba *reference* inaonesha kwamba uwezo wa makusanyo yetu ni mdogo sana, kwa hivyo tuisogee mbele wakati pale tulipokisia mwanzo hatukupafika, nashauri kwamba tungerudi nyuma tukaweka makisio ya makusanyo ambayo tunaweza kuyatekeleza. Kwa hali hii inaonesha kwamba mipango tunayoipanga yote inakuwa ni mipango hewa, Serikali tupangieni mipango inayotekelezeka msitupangie mipango ya kisiasa, sawa jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie na kifungu cha nne ambapo ni suala zima la asilimia 10 ya vijana na wanawake. Naomba nimalize kwamba kwenye asilimia 10 hii ya vijana na wanawake mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, inaonesha kwamba takribani halmashauri nyingi zinakuja na bajeti yao kwamba 10 *percent* ya wanawake na vijana ni kwa mfano makusanyo ni bilioni 50, inawekwa *ten percent* kwamba ni pengine 25 *millions* lakini ukiangalia kilichotumiwa ni milioni 5,000,000! Sasa ukiuliza hiki chingine kiko wapi?

Mheshimiwa Spika, Kila Mkuu wa Mkoa anayekuja ukimuuliza hichi chingine kimepelekwa wapi, hakuna majibu. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba asilimia 10 hii ya vijana na wanawake itolewe katika hali inayostahiki kwa sababu katika kupitia kwetu kwenye Halmashauri tumekuta kwamba asilimia 10 hii inatumika vizuri sana kwa vijana na wanawake na inatuondolea lile tatizo la ajira. Nashauri kwamba Wizara husika waisimamie katika hali ya asilimia mia moja ili itekelezwe kama inavyopasa.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hamad.

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Spika, namalizia na ushauri mwingine kidogo.

SPIKA: Muda haupo upande wako, nashukuru.

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, siungi mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Hamad Salim Maalim nakushukuru sana. Mheshimiwa Julius Kalanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nitasemea maeneo machache na nianze na suala la viwanda. Hakuna mtu ambaye anapinga suala la ujenzi wa viwanda kwa sababu inatusaidia kukuza uchumi kama Taifa, lakini kuondokana na tatizo la umaskini kwa mwananchi mmoja mmoja. Hoja yetu hapa ambayo tunataka Waziri wa Fedha atuambie, hivi lengo la viwanda hivi tunavyojenga ni kwa ajili ya nani, tunajenga viwanda hivi ili tuwe na viwanda vingi katika Taifa hili au tunajenga viwanda ili tuwasaidie wananchi wetu kuondokana na umaskini katika Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo mara ya kwanza nchi hii kuwa na viwanda, lakini vimekufa si mara ya kwanza nchi hii kuwa na ndege lakini zimekwisha, kwa hiyo suala siyo kuwa na miradi mikubwa, suala ni kuwa na miradi mikubwa lakini endelevu (*sustainable development project*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpaka leo miaka mitatu tunaimba sera ya viwanda lakini hakuna *hand out guideline* ya nchi inayoeleza muktadha mzima wa viwanda vitakavyosimamiwa nchi hii. Hivi akiondoka Rais huyu akaja Rais mwingine hili suala la viwanda si limekufa? Kama tuna *millennium* ya 2025 kwa nini tusingekuwa na *program* ya Taifa kama Taifa ambapo kila mwananchi na kila sehemu anayo inayoonesha namna suala la viwanda vitakavyoendelezwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuendeleza viwanda kama hauna kodi stahiki ambazo zinasimamiwa kwa muda fulani ambao mwekezaji atawekeza, tunabadilisha kodi kila

mwaka tunafanya *trial and error* ile tunayosoma kwenye *biology* kwamba unatengeneza kaboksi halafu panya anaenda huku anakosa mlango, anaenda anakosa mlango, ndiyo maana kila mwaka wanarekebisha Sheria ya Kodi, kila mwaka wanakuja wanasamehe kodi hii, wanaanzisha kodi hii, kwa nini tusingekuwa na *program* ya nchi inayoonesha kwamba ni kodi gani tuache kwa sasa ili tu-*invite* wawekezaji halafu watu waweze kuwekeza, lakini wanafanya uwekezaji hawaja-*base* katika rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, hakuna mahali popote Wizara inazungumza habari ya ujenzi wa vyuo vya kati ili vijana wetu wanaomaliza *form four* waweze kupata ujuzi waende wakafanye kazi kwenye viwanda vyetu. Ndiyo maana watajenga viwanda lakini wataanza kuomba vibali vya kupata *expert* kutoka nje kuja kufanya kazi katika viwanda vya nchi yetu kwa sababu hatujawaandaa vijana kufanya kazi katika viwanda. Maana yake viwanda tutakuwa tunajenga kwa ajili ya watu wengine lakini siyo kwa ajili ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo nilikuwa nasema asubuhi nchi hii inazalisha zaidi ya vijana laki tatu wa kidato cha nne kila mwaka ambao hawaendelei na kidato cha tano. Waziri wa Elimu amenijibu kisiasa kwamba wataenda kwenye Vyuo vya Ualimu ambapo wanaenda lakini hawaajiri na wao sera ya elimu wanasema kuanzia miaka ijayo wanafuta kidato cha nne kuanzia sasa shule ya msingi zinafundishwa na watu wenye *Diploma*, hivi mtu aliyemaliza *form four* anaweza kusoma *Diploma* kwa kuunganisha au mpaka aende *Certificate*? Kwa hiyo ni muhimu tuwe na viwanda ambavyo tumeandaa vyuo vya kati na vya juu vinavyoandaa vijana wetu kwenda kufanya kazi katika viwanda tunavyovijenga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu rasilimiali kwa maana ya malighafi, hakuna muunganiko kati ya viwanda, kilimo chetu na mifugo yetu. Bajeti mbili zimepita tu hapa kwa mbinde, tena baada ya kwenda kukaa *party caucus* Bajeti ya Kilimo,

na bajeti ya Mifugo na Uvuvi, lakini walitupa matumaini na Kiti cha Spika kilitupa matumaini kwamba wakati wa Bajeti Kuu Serikali ita-*subsidize kule* ambavyo tulikuwa tumelalamikia katika kupeleka ruzuku na katika kusaidia uwekezaji katika sekta ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, nimesoma kitabu hiki hakuna, hakuna *amendment* yoyote ya kuiongezea bajeti Wizara hizo, hivi Waziri wa Kilimo atafanyaje kazi, Waziri wa Mifugo atafanyaje kazi kama hana fedha. Kwa hiyo ni muhimu kama kweli wangekuwa wanatujali na wanataka kuunganisha Sekta ya Mifugo, Kilimo na Viwanda wangeleta bajeti ambayo itasaidia kule wakulima wetu walime kisasa. Haiwezekani ukajenga kiwanda cha kutegemea kilimo cha msimu, kwamba unasubiri mvua inyeshe halafu mwenye kiwanda afunge kiwanda kwa sababu hamna mazao kwa ajili ya kuendesha kiwanda. Ni lazima tuwe na *sustainable projects* ambazo mwekezaji wa kilimo akiwekeza awe na uhakika wa kupata *raw material* mwaka mzima bila ya kutegemea mvua ambayo hatujui kama inanyesha au hainyeshi, miradi hiyo iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hu ni mwaka wa tatu Serikali iliahidi kuleta miradi ya kimkakati ambapo mpaka sasa tunavyoongea siyo Liganga siyo Mchuchuma siyo Engaruka siyo *General Tyre* hata mmoja hauja-*mature*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, agizo la Serikali tangu tunaanza Bunge hili ni kwamba tutakuwa na miradi hiyo ya kimkakati, Liganga na Mchuchuma tulikuwa tunasikia tukiwa nje ya Bunge tumekuwa ndani ya Bunge, mpaka leo hawajatekeleza. Miaka mitatu hii hata Watumishi wameshindwa kuwapandishia mishahara halafu wanasema wana-*control inflation* hawaja-*control inflation* imeji-*control* yenyewe kwa sababu *purchasing power* hakuna, wananchi hawana fedha, kwa hiyo kama hawana fedha huwezi kupima *inflation* kwa sababu hakuna mtu anayanunua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ituambie, kwa sababu uchumi wa nchi hii hauwezi kujengwa na kila mtu

kuwa mtaalam katika eneo lote. Tunataka kama tuna maono ya kuwa na viwanda, tuwape wataalam watuandalie programu ya kuwa na viwanda katika Taifa hili. Tuache hizi kauli za kisiasa za kutetea kitu ambacho hatuoni, tunatamani kama ni viwanda kila mtu aone, siyo wanatuletea vile viwanda 3,600 kwenye makaratasi, lakini mnatuambia tu, tupelekeni *site* hamna ujasiri huo, kwa nini? Kwa sababu wana-*politicize* miradi mingi badala ya kuangalia uhalisia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala siyo kuwa na viwanda vingi, suala ni kuwa na viwanda vinavyosaidia kubadilisha maisha ya wananchi. Hata kama tungekuwa na kiwanda kimoja, kinachobeba mazao yote ya wakulima wetu, hicho kiwanda ni bora, kuliko kuwa na viwanda 100 ambavyo vyote malighafi unaagiza kutoka nje. Kwa hiyo ni muhimu tuwe na lengo la Taifa kusaidia wananchi katika miradi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niseme jambo lingine, historia inaonesha Serikali zinapita, Serikali iliyopita ilikuwa inasema Kilimo Kwanza, imemaliza imeondoka, imekuja Serikali ya viwanda. Kilimo Kwanza hatujafanya na tungefanya Kilimo Kwanza viwanda vingejengwa *automatically* kwa sababu *raw material* zingepatikana vya kutosha na watu wangejenga. Mpaka leo hakuna mkakati wowote Serikali imewekeza katika kusaidia kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri mambo machache, ni muhimu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mpango kama anataka kusaidia Taifa hili, Serikali ilete mpango mkakati wa kusaidia sekta ya kilimo katika nchi hii ili iweze kuzalisha kwa tija. Kwa sababu mazao si mazao tu lazima mazao yawe na ubora unaostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, umefanya hii kazi kwenye *industry* ya utalii, ukiiangalia Arusha yote na Kaskazini ambavyo tuna utalii wa kutosha, lakini tunaaagiza nyama kutoka Kenya, tunaagiza *material* ya kwenye *hotel*, hata nyanya kutoka nje,

ni kwa sababu uzalishaji wetu hauna viwango. Kwa hiyo siyo kuzalisha nyanya tu, siyo kuzalisha matunda tu ni lazima tuzalishe katika ubora unaostahili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Julius Kalanga. Mheshimiwa Peter Serukamba atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nami nakushuru sana kwa kunipa nafasi niongee kwenye Bunge lako Tukufu, kwa kweli toka tumeanza nilikuwa sijachangia. Leo naomba nianze kwa kuipongeza Serikali, nimpongeze Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya, nimpongeze Waziri Mpango, nimpongeze Katibu Mkuu wa Fedha, Naibu Waziri, rafiki yangu Ndugu Kichere wa *TRA* na *task force* yote kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo nitaanza na *page 47* ambapo Mheshimiwa Waziri ameamua jambo kubwa na la kihistoria kupunguza *corporate tax* kwa ajili ya viwanda vya ngozi na viwanda vya madawa kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 20. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aende zaidi; kwa viwanda vya ngozi vilivyopo, vinavyokuja, na viwanda vya madawa afanye zero *corporate tax*. Akifanya zero *corporate tax* kitakachotokea Tanzania itakuwa *hub* ya biashara ya madawa. Viwanda vyote vya madawa vitakuja Tanzania kwa sababu itazalisha kwa wingi waende wakauze nchi zote zinazotuzunguka. Viwanda vya ngozi tutaweza kuwa *competitives* kwenyesoko la dunia, lakini tutapata ajira na *production* itaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzetu huko duniani tunashindana na Mheshimiwa Spika umesema kuhusu Kenya lazima twende kwa kasi zaidi. Kwenye suala la ngozi naomba tuondoe asilimia 10 ya *export levy* tukiondoa na tu-*ban* tuhakikishe hakuna kusafirisha tena ngozi ambayo ni *raw*. Uki-*ban raw* halafu ukatoa 10 *percent* na umeondoa *corporate*

tax ni *zero*, unayo hakika viwanda vyetu vya Tanzania vitazalisha ngozi na vitakwenda kushindana kwenye soko la dunia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hapo kwenye kiwanda nataka niongeze na Kiwanda cha Mbolea. Naombeni Mheshimiwa Waziri tuamue, tuondoe *corperate taxiwe zero rated* ili watu wote duniani waje wajenge viwanda vya mbolea. Wakijenga viwanda vya mbolea Tanzania kitakachotokea Tanzania ndiyo tuta *re-export* mbolea kwenye Afrika yote, leo mbolea yote inanunuliwa Morocco, *why?* Tanzania tuna Gesi, Tanzania tuna Bandari, tunayo sababu tuweke huo mkakati, nina hakika viwanda hivyo vikiwekwa tutapata ajira, *production* itaongezeka lakini na bei ya mbolea Tanzania itashuka na kwa sababu hiyo tutakipa thamani kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo leo nitachangia liko *page* ya 52. Mheshimiwa Waziri ame-*introduce electronic stamp*, namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Nampongeza na naomba nianze kwa kusema kwenye *taxkuna task evasion* na *tax avoidance*. *Tax evasion* ni kosa la kijinai, *tax avoidance* ni mtu anatumia sheria zako za kikodi anakwepa kodi na hilo wala siyo kosa la jinai. Tufanye nini ili kuzuia *tax avoidance*? Mambo mawili lazima yafanyike.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuweka sheria ambazo zitazuia watu wasiweze kukwepa kodi, pili ni kuweka *infrastructure* ambayo itazuia ama kuweka *system* watu wasiweze kukwepa kodi. Kwa kufanya hivi tutakuwa tumeenda mbali sana, Waziri wa Fedha ameliona na amelifanya, hongera sana ndugu yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wako watu watapinga huu mfumo, siyo kwa sababu nyingine yoyote. Mfumo huu unakwenda kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mfumo huu unakwenda kufanya *production count*, kila kitakachozalishwa kwenye kiwanda chochote, *TRA* wanaona. Jambo la pili kubwa

ambalo litatokea kwenye mfumo huu ni *revenue* itakua. Kila walio-*embrace* teknolojia hii ya *electronic stamp*, nchi 47 ninazozifahamu kodi ilipanda kwa asilimia 40 mpaka asilimia 65. Kwa hiyo, naamini mwaka kesho tutakapokutana hapa kodi itakuwa imepanda kwa kiasi kikubwa sana, lakini jambo kubwa ambalo litatusaidia ni bidhaa feki. Kwa wale ambao ni wanywaji kama mimi naomba waniambie ukienda kwenye *spirit* watu wetu wanakufa sana kwa vinywaji feki. Kwa sababu zile *stamp* za karatasi kila mtu anaweza akazitengeneza, lakini hapa ni *stamp* siyo za kutengeneza, kwa hiyo tutaondoa vitu feki na tukiondoa feki wenye viwanda watapata mapato zaidi kwa sababu mapato yao yalikuwa yanashuka kwa sababu ya vitu feki.

Mheshimiwa Spika, wako Watu wanasema tuna hand over *sovereignty*, *sovereignty* gani tuna *hand over*? hapa tunachofanya tunakwenda kuzuia ili Serikali ipate mapato makubwa. Naomba Serikali iendee itekeleze jambo hili na ikiwezekana ipeleke kwenye kila bidhaa, wametuibia inatoshwa umefika wakati tupate mapato makubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo PPP inayosemwa na kuna wenzetu wanaomba PPP lakini PPP zikija naomba hii muitambue hapa amekuja mtu ana fanya *self-investment* lakini sisi tutapata na yeye atapata, ndiyo maana ya PPP hawezi mtu kuja na *technology* halafu asipate, haiko dunia ya hivyo. Mtu huyu ameleta hela zake, ameleta *techology* yake, wewe ghafla unasema na mimi naweza nikafanya mbona hukufanya jana?

Mheshimiwa Spika, ninachoomba sana kwa Serikali jambo hili ni zuri litaongeza ajira. Kubwa zaidi huyu anayekuja kufanya ataajiri Watanzania above all atalipa *corporate tax*, kwa hiyo *revenue* itaongezeka *both side*. Kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri hili mlisimamie haraka ili liweze kuanza tuweze kupata mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, toka nimeingia Bungeni mwaka 2005 kila mwaka kwa wale tulikuwepo na Mheshimiwa Spika wewe

utasema. Kila mwaka tuliongeza *excise duty* ya bia, soda, maji pamoja na vinywaji vikali na sigara kila mwaka mpaka tukawa magazeti yanaandika bajeti ya sigara, bajeti ya pombe. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametanzua jambo hilo kwa mara ya kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano. Kwa kufanya hivyo maana yake ni nini? Maana yake *production* itaongezeka, maana yake matumizi yataongezeka, nilikuwa nawatania wenzangu kwa kutoongeza *excise duty* wale ambao tulikuwa tunakunywa bia mbili sasa tutakunywa tatu kwa sababu zitabakia kwenye bei zile zile tutaweza kutumia hizo bia zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kusema ni kuhusu mafuta ya kula, Waziri wa Fedha amechukua *very good measure* kupandisha kwenda asilimia 35 na asilimia 25. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha lipo jambo la kufanya. Jambo la kwanza lazima aje na *extensive master plan ya agriculture* ya michikichi pamoja na alizeti. Tusipofanya hivyo bei hizi zitapanda, Wabunge tutarudi hapa kupiga kelele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumeamua kufunga mkanda, tukitaka kuulegeza mkanda lazima sasa kilimo cha michikichi, kilimo cha alizeti tukipe bajeti. Kwa bahati mbaya sana ukisoma bajeti ya Wizara ya Kilimo hakuna hata senti tano moja inayokwenda kwenye michikichi. Kwa hivyo, inawezekana hii *measure* ni nzuri lakini ikawa *counterproductive*.

Mheshimiwa Spika, nami niseme ulikuwa unasema kwa nini Kenya wako mbali? Moja ya sababu ni Kenya wana-*embrace commercial farming*. Narudia tena mimi siyo muumini wa ujamaa, kama tunataka kilimo kitoke lazima tuanzishe *commercial farming*. Ukianzisha *commercial farming* utatoa ajira nyingi zaidi, *production* itaongezeka kwa sababu yule anayeleta fedha zake atatafuta Wagani wake, atatafuta mbolea na ataongeza *production*.

Mheshimiwa Spika, ukienda leo michikichi ya Kigoma yote imezeeka, haizalishi mawese tena, ili uweze kuokoa kilimo cha michikichi Kigoma lazima ugawe mbegu mpya. Tukigawa mbegu mpya ndani ya miaka miwili, mitatu tutaweza ku-*clear* hili *gap* na mafuta yataongeza.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la *transit trade*. ukisoma *record* za uchumi, sekta mbili zilizoleta fedha Tanzania ni bandari na tourism. Maana yake ni nini? Ili bandari ifanye vizuri zaidi lazima tu-*embrace transit trade*. Tuondoe vikwazo ili watu wengi watumie bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mafuta yanayokwenda *transit trade*, mafuta yakiwa yanakuja yakifika Dar es Salaam baada ya siku 30 hayajatoka tunawaambia waya-*localise*. Ukienda Beira ni siku 90, ukienda Durban siku 120, Walvis Bay siku 90, Mombasa siku 60 maana yake ni nini? Tanzania siyo sehemu ya kwenda kupitisha *product* hiyo. Tukiongeza siku zikawa 90 maana yake *destination* ni Dar es Salaam, tutaongeza ajira, tutapata *wharfage* tutapata *storage*. Tukipata *storage* maana yake bandari iende *fast*, bandari ijenge *storage capacity* ili tuweze kuweka mafuta hayo. *Storage capacity* tuliyonayo ilijengwa mwaka 1970, leo ni miaka 47 Taifa limebadilika sana. Ninaomba hilo tulifanye kwa haraka ili tuweze kufanikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine nataka kusema *PPP project*, nimesema kila nilipoingia kwenye Bunge hili, naombeni tubadilishe sheria, naombeni tufanye *PPP* itatusaidia *to easen budget*. Hili nalisema kwa sababu nataka leo wenzangu muangalie ukienda *page* ya 78 ya kitabu cha Waziri wa Fedha ameonesha mfumo wa bajeti ya mwaka wetu. Ukichukua *first charge* pesa ambazo lazima hata afanyeje Waziri lazima alipe ni trilioni karibu 27 hizi hana *choice* lazima alipe.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye *revenue* ukatoa mikopo fedha ambazo anaweza akakusanya na hapa maoteo yamepata kwa asilimia 100 ni trilioni 23. Sijaweka

OC, sijaweka hela za *Development*. Unafanyaje katika *situation* hii? *Situation* hii lazima uje na *PPP*, *PPP* lazima u-*embrace concession loan*. Kwa mfano, leo Mheshimiwa Rais Magufuli ame-*embark* kwenye kufanya mambo makubwa mawili ya kihistoria, moja kujenga Reli ya Kimataifa, mbili kujenga *Stiglers Gorge* jambo kubwa la kihistoria na kwa kweli naamini historia itamuandika Rais Magufuli kwa kufanya miradi hii mikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kwa haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, miradi hii tunaijenga kwa fedha za ndani, miradi hii tunaijenga kwa kukopa *commercial loans*, tukikopa *commercial loans* maana yake ni moja tu, ukikopa mkopo wa kibiashara unaanza kuulipa ndani ya miezi sita, wakati unaanza kuulipa hata miradi hii haijakwisha, miradi hii haijaleta fedha. Tumeweka *seven* trilioni mpaka Dodoma lakini mpaka leo tunalipa deni lakini reli haijafika Dodoma. Sasa ili tuweze kupata *concession loans* lazima tufanye yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba sana, mimi Rais Magufuli namuamini, Rais lazima aende, akutane, afanye mambo ya kidiplomasia. Akutane na Xi Jinping wa China, akutane na Angela Merkel wa German, akutane na Shinzo Abe wa Japan, akutane na Donald Trump wa US, akutane Vladimir Putin wa Urusi, akutane na Theresa May wa UK maana yake nini? Watu wawili wanakutana na mimi najua uwezo wa Rais Magufuli atakwenda na nchi *at heart* ata-*re-negotiate for the country* tutapata *concession loans*.

Mheshimiwa Spika, tukipata *concession loans* maana yake ni moja tu, maana yake tutapata fedha, tutajenga reli yetu, wakati huo hatulipi mpaka baada ya miaka 15 tuwe tunaanza kulipa deni. Maana yake ukienda kwenye *figure* za bajeti pale kwenye eneo la deni la Taifa la trilioni mbili litapungua, likipungua Waziri wa Fedha atapata fedha sasa ya kupeleka kwenye maendeleo ya vitu vingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya yote wenzetu wamefanya, hapa Ethiopia wamejenga reli juzi, tena ni reli inayoenda kwa umeme, wamekopa China *concession loan tena one percent*. Wakenya wamechukua *concession loan*, sisi ni nani? Naamini halijaelezwwa vizuri, naamini uwezo mkubwa alionao Rais Magufuli hili jambo akiamua litatokea kesho. Tutapata fedha za *concession loans*, tutafanya miradi mikubwa na maana yake bajeti yetu ya Serikali tutawarahisishia watu wa Wizara ya Fedha ku-*balance* bajeti.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo naomba leo nichangie ni suala la *Small Business Act*. Waziri wa Fedha naomba awape zawadi Watanzania, zawadi hiyo ya kuwapa Watanzania alete *Small Business Act*. Ni nini maana yake? Tuamue sasa kwenye *corporate tax* tuweke kitu kinaitwa *brackets* za kodi kwamba kwa mtu ambaye ana mtaji wa milioni 10 mpaka milioni 100 mtu huyu alipe kodi labda asilimia tano. Kwa mtu ambaye labda ni milioni 100 mpaka bilioni moja alipe asilimia kumi, maana yake ni nini? Tunawa-*include* watu wote kwenye uchumi. Tukiwa-*include* watu wote kwenye uchumi tutapata mapato mengi zaidi kuliko yalivyo sasa. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, mwisho nikuombe sana nimalizie la mwisho kwangu mimi ni la muhimu sana. Kwenye hoja hii ya viwanda nikuombe kuna *measure* kubwa wenzetu wa Kenya ambao ni washindani wetu wameweka. Wakenya wameondoa asilimia 30 ya bei ya umeme kwenye *manufacturing*. Maana yake ni ili viwanda vyao viweze kuwa *competitive*, tunajenga viwanda, lazima tuweke *competition* na sisi, tukiondoa hata tuondoe asilimia 40. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema wakati wanajenga kiwanda cha saruji kikubwa Ethiopia, Ethiopia alipewa punguzo la umeme la asilimia 60. Alipopewa punguzo hilo, bei ya saruji ilishuka kwa asilimia 70, *here* yamefanyika, *we are not inventing the wheel*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema nakushukuru sana, naomba niunge mkono hoja, Waziri wa Fedha namuunga mkono, bajeti yetu hii mwaka huu ni nzuri sana ni bajeti inayokwenda kujibu matatizo ya viwanda na matatizo ya kukuza biashara Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Leo sina hata wachangiaji wa CHADEMA hapa, leo mkae msikilize CCM wanavyoteremka. Tulikuwa tunasema kwamba bajeti ya Kenya ni mara mbili ya Tanzania, msivunjike moyo Waheshimiwa Wabunge, bajeti ya Tanzania ni mara mbili ya bajeti ya Uganda, kwa hiyo tunakwenda vizuri. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili kuweza kutoa mchango wangu kwenye hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na Naibu wake pia niwapongeze Watendaji walioko ofisini kwao, Katibu Mkuu pamoja na wote walioko ofisini kwa kufanya kazi kwa juhudi kubwa na hatimaye kutuletea bajeti ambayo ni nzuri kwa kweli na ni bajeti ambayo inaleta matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni nzuri kwa sababu moja imeweka vizuri kodi ambazo zilikuwa zinasumbua hasa wakati huu tunapotaka kujenga uchumi wa viwanda. Hakuna kodi iliyoongezeka kuzidi kiwango hata mahali ambapo kodi zimeongezeka na hasa wazalishaji wetu wa ndani, bajeti hii imewaangalia vizuri kwa kweli. Wasiwasi wangu tu ni huu utambulisho wa *electronic tax stamp*, sijaelewa sawasawa kama kweli haina matokeo ambayo ni hasi kwa mlaji na wazalishaji. Tutajifunza huko mbele,

tutaona pengine haitakuwa na matokeo haya. Lakini vinginevyo kama ina matokeo chanya basi tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia mapato yetu ya ndani. Mapato yetu ya ndani yanaendelea kuongezeka lakini ongezeko kubwa liko kwenye kodi. Mapato yasiyotokana na kodi bado ni madogo sana, bajeti iliyopita kutokana na hotuba hizi zilizosomwa hapa, mapato yasiyo ya kodi ilikuwa trilioni 1.7 na mwaka huu ambao bajeti yake tunajadili mapato yasiyotokana na kodi yanakadiriwa yatakuwa trilioni 2.16. Sasa kitakachokusanywa bado hatuelewi.

Mheshimiwa Spika, mapato haya siyo makubwa sana na mapato haya yanatakiwa kuwa makubwa kwa sababu ni lazima sasa yaweze ku-*supplement* mapato yanayotokana na kodi. Mapato yanayotokana na kodi bado ni madogo kwa sababu uchumi wetu unatawaliwa na sekta isiyo rasmi kubwa sana, kwa sababu sekta isiyo rasmi ni kubwa basi hatupati kodi ya kutosheleza huko. Sasa lazima tutafute namna ya kongeza mapato yasiyo ya kodi. Tunaweza kuyaongeza kwa namna mbili tu ambazo napendekeza hapa.

Mheshimiwa Spika, moja ni kufanya Ofisi ya *TR* isimamie vizuri makampuni na taasisi za Serikali ambazo zinazalisha. Kusema ukweli *TR* anatakiwa awezeshwe kiasi cha kutosha kabisa ili aweze kusimamia vizuri mahali ambapo Serikali ina *stake*, kwenye kampuni ambazo Serikali ina *stake*, *TR* asimamie vizuri kuhakikisha tunapata mapato ya kutosha kule. Pia taasisi zingine na ikiwezekana taasisi ambazo hazizalishi au ni mzigo kwa Serikali basi tuweze kuondokana nazo, kwa nini kuendelea kuzipa ruzuku, kuendelea kuzipa pesa wakati hazizalishi na haziongezi mapato yoyote kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la pili ambalo kama nchi tumeendelea kulizungumza kwa muda mrefu, suala la uvuvi kwenye Bahari Kuu. Inasemekana tunapoteza shilingi

trilioni moja kila mwaka kwa sababu ya kutoweka maanani uvuvi kutoka kwenye Bahari Kuu. Sasa Serikali imekuwa na maelezo tofauti kwamba wanafanya upembuzi yakinifu ili kutengeneza bandari ya uvuvi, lakini huu mwaka ni wa tatu niko kwenye Bunge lako bado upembuzi yakinifu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani umefika wakati kwamba sasa tuanze uvuvi wa Bahari Kuu ili utusaidie kutuongezea mapato yasiyo ya kodi. Vinginevyo tutaendelea kuimba wimbo wa namna hii, bado tutakuwa na mapato chini tutakuwa na mapato duni na hivyo tunapotaka kufika 2020 au 2025 tuwe na uchumi wa kati itatuchelewesha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la pili, suala la maji. Suala la tozo ya maji kwenye mafuta. Suala la maji ni muhimu sana kwenye nchi yetu kwa sababu mbili pia. Kwanza maji tunayataka sisi kama binadamu kwa matumizi yetu mbalimbali, lakini pia maji tunayataka kwa ajili ya kilimo chetu. Kilimo chetu kwa sababu ya kutegemea mvua kimekuwa kilimo cha chini, kimekuwa kilimo ambacho hatuna uhakika hata tukilima kama tunaweza kuvuna. Tukiweka nguvu kubwa kwenye maji tuna uhakika na kilimo na tuna uhakika wa kuwapatia watu wetu maji ambayo wanahangaika usiku na mchana mahali pengi.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka kijijini kabisa, kijiji changu tunachota maji kilomita saba kwenda, kilometa saba kurudi. Sasa suala la maji ni suala kubwa na ni suala muhimu sana kwenye nchi yetu. Tuliomba Serikali iongeze shilingi 50 kwenye maji. Serikali inasema haiwezi kuongeza kwa sababu itaongeza mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei unaoongezwa na mafuta ni wakati mafuta yamepanda bei huko tunakoyanunua, lakini kwa muda wa miaka miwili sasa na huu ni wa tatu nadhani, mafuta hayajaweza kupanda sana kwenye soko la dunia kiasi kwamba yakipanda, pengine tukiyanunua kwa gharama ya juu kule hapa tutajiletea *inflation* (mfumuko wa bei) *imported inflation*, lakini mafuta hayajapanda sana huko kwa wenzetu.

Mheshimiwa Spika, pia hapa kwetu...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ndaki.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nami kupata nafasi hii ya kuchangia kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kazi yetu kubwa ni kuishauri sana Serikali na kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza yale yote ambayo tunajaribu kuyaona kwa faida ya wananchi wetu. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la utekelezaji wa yale tunayoyaamua ndani ya Bunge, mwaka 2016/2017 na mwaka 2017/2018 nilitoa ushauri kwenye Bunge hili na nikawaambia ni vizuri sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha akajaribu kujikita sana kutoa ushauri pia kuhakikisha kwamba utekelezaji wa bajeti zetu zote ambazo tunazipitisha ndani ya Bunge zinatekelezwa kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kuamini, utekelezaji wa bajeti kwenye nchi hii sasa hivi imekuwa ni kitendawili. Hoja kubwa hapa ya kutengeneza bajeti hizi ni kwa ajili ya kuinua maisha ya Watanzania, lakini pia Serikali hii inasema kwamba inataka kwenda kwenye uchumi wa kati. Kwenda kwenye uchumi wa kati kunahitaji hatua, huwezi kutoka kwenye ufukara ukaenda kwenye uchumi wa kati, ni lazima uchumi wa kati uwe na hatua zake.

Mheshimiwa Spika, leo huwezi kuamini, Watanzania wanazidi kuwa fukara, wanazidi kurudi nyuma, leo tunakazana tu kwamba tunataka kwenda kwenye uchumi wa kati, kwa sababu tunachokifanya sasa hivi kwenye bajeti hizi tunafanya bajeti ya vitu na siyo kwa ajili ya wananchi wetu na hili ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili unaweza ukaliangalia katika bajeti zetu zote. Ukiangalia maeneo ambayo wananchi wengi maskini tunatakiwa tuwainue maeneo haya hayapelekewi fedha kabisa. Ukiangalia kwenye kilimo, mifugo pamoja na uvuvi, fedha haziendi kabisa. Ukiangalia kwenye kilimo mwaka 2016/2017, fedha iliyokuwa imetengwa ilitengwa bilioni 101 lakini kati ya bilioni 101 fedha iliyokwenda kuinua kilimo ni shilingi bilioni 3.3 peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018, ilitengwa bilioni 150 lakini fedha iliyokwenda kuinua kilimo imekwenda kupelekwa shilingi bilioni 27.2 peke yake. Sasa tunavyosema kwamba tunataka kuinua uchumi wa Tanzania ni lazima tuzungumzie kwa wananchi hawa ambao ni wavuvi, wafugaji pamoja na wakulima. Tusipoweza kuinua kilimo, tusipoweza kuwainua wavuvi pamoja na wafugaji, tunakoelekea tunatatwanga maji kwenye kinu, tutabaki hapa na tutaendelea kuishangaa Kenya na nchi zingine zinapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema jambo moja, ukiangalia kilimo pamoja na uwekezaji wa bilioni tatu kwa mwaka 2016/2017, lakini mchango wa kilimo kwenye Pato la Taifa ulichangia asilimia 29.2, pamoja na uwekezaji mdogo ambao ulifanyika. Kwa hiyo, kama kweli tutawekeza vizuri kwenye kilimo, hata tungewekeza labda hii fedha bilioni 150 ingetumika yote, inawezekana kilimo kingeweza kuchangia Pato la Taifa hata kwa asilimia 50 au 45. Kwa hiyo tungekuwa tayari tunasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, umeona wavuvi, leo wavuvi katika Taifa hili imekuwa ni janga, wanachomewa nyavu, wanaharibikiwa mambo yao, wanakamatwa, ziko sheria kandamizi ambazo zimetungwa na sasa hivi huwezi kuamini, wavuvi sasa katika Taifa hili hawaonekani kama ni watu muhimu katika kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017 kwenye uvuvi peke yake, shughuli za maendeleo, tulitenga shilingi

bilioni mbili ili fedha ziende kule lakini miaka miwili yote hakuna hata shilingi iliyopelekwa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye mifugo, tulitenga bilioni nne kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaimarisha mifugo yetu, pia na kuwawezesha wafugaji wetu lakini hakuna hata shilingi iliyopelekwa kwenye maeneo hayo. Leo tunakaa ndani ya Bunge tunasema tunatengeneza bajeti kwa sababu ya wananchi maskini, hao wananchi maskini tunaowasema ni watu gani?

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kununua ndege tano kwa wakati mmoja tafsiri yake ni kwamba tunakwenda kuinua uchumi wa watu asilimia tano tu, kwa sababu katika nchi hii watu wenye uwezo wa kupanda ndege ni asilimia tano peke yake. Tunatumia mamilioni ya fedha kupeleka kule tunawaacha Watanzania maskini ambao tulipaswa kuwainua ili waweze kujenga nchi na kuhakikisha kwamba uchumi unaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitaka kukuonesha hali halisi iliyopo, ukiangalia kwenye nchi yetu kila mwaka wanafunzi wanaohitimu elimu ya juu ni karibuni 800,000 kati ya watu 800,000 wanaopata ajira ambazo ni rasmi wanapata watu 40,000 peke yake. Kwa hiyo, kuna wananchi ambao ni wasomi 760,000 hawapati ajira kabisa na wanategemea ajira hii ambayo siyo ramsi, kilimo, ufugaji pamoja na uvuvi, lakini hakuna fedha inayokwenda kule.

Mheshimiwa Spika, hii tafsiri yake ni kwamba hatujajiandaa kuondoa umaskini wa Watanzania badala yake tunaendekeza maneno ndani ya Bunge hili. Hakuna mtu yeyote, wanayemdanganya, wamepewa madaraka makubwa na wananchi wa Tanzania, nia na madhumuni wakiwa na matumaini kwamba wangeweza kuwafikisha wanapohitaji. Leo Watanzania kila maeneo wanalia, tunataka tuseme, ni lazima wabadilike! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu pekee unayeweza kujenga nchi sasa hivi ni wewe kwa sababu Muhimili wako ndiyo

unaosimamia Serikali, Mhimili wako ndiyo unaoweza kutoa maagizo na kuhakikisha kwamba Serikali inafanya kazi vizuri, lakini kama na wewe utashindwa kuhakikisha kwamba unasimama kama kiongozi wa Mhimili na kuhakikisha kwamba unakemea bajeti hizi, kama kweli bajeti zinakuja tunatekeleza kwa asilimia 18, tunatekeleza kwa asilimia 20, tunatekeleza kwa asilimia sifuri, tutakuwa hatuwatendei haki Watanzania hawa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tutekeleze wajibu wetu wa kuisimamia Serikali kuhakikisha kwamba Serikali hii inatekeleza wajibu wake kama ambavyo tunapitisha bajeti humu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia sana barabara. Ukiangalia mtandao wa barabara katika nchi hii ni karibuni kilometa 86,472, kati ya kilometa hizi mtandao wa barabara ambao sasa hivi uko kwa lami karibuni ni asilimia 9.7 peke yake. Kwa hiyo, hata kwenye barabara pia bado tuko nyuma sana, tafsiri yake ni kwamba tuna safari ndefu ya kujenga uchumi wa nchi kwa sababu hatutakwenda kwenye viwanda kama hata barabara hatuna. Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba tunaonesha ni namna gani tunaweza tukajenga uchumi huu kwa vitendo na siyo kwa maigizo kama ambavyo yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunazungumzia pia madini. Tunasema, ooh! Sasa hivi tunataka tujikite kwenye madini, yatachangia Pato la Taifa, madini yanawezaje yakachangia Pato la Taifa kama uwekezaji unakuwa kidogo kiasi hiki! Ukienda kuangalia kwenye madini mwaka jana *STAMICO* tuliwatengea shilingi bilioni 20.9, fedha ambayo tuliwapelekea *STAMICO* tuliwapelekea bilioni 2.8 peke yake ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 10 tu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, tunawezaje tukahakikisha kwamba tunapata mapato mengi kwenye madini wakati hatuwekezi. Kwa hiyo, yako mambo mengi ambayo ni lazima pia tusimame tuangalie, kama Taifa ni namna gani tunaweza tukajenga Taifa hili kama inavyotakiwa.

SPIKA: Malizia Mheshimiwa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie la mwisho kabisa ni kampuni ya jotoardhi. Kampuni ya jotoardhi ukisoma kwenye ukurasa wa 24, ukiangalia Mheshimiwa Dkt. Mpango anasema, kati ya shilingi bilioni 409 zilipelekwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba umeme vijjini pamoja na jotoardhi. Hata hivyo, ukiangalia hapa mwaka jana fedha iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya joto ardhi ilikuwa bilioni 21, lakini fedha iliyopelekwa ilikuwa ni Sh.53,715,000/= ambayo ilikuwa ni sawasawa na asilimia 0.24 ndiyo iliyokwenda kwenye jotoardhi. Katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri anaonesha kwamba fedha nyingi ilipelekwa kitu ambacho hakikufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuisubiri miujiza, ni lazima tutekeleze bajeti zetu tunazozipanga ndani ya Bunge zikatekelezwe huko na watu wote wanamlaumu Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tunaomba abadilike na kama ameshindwa, atuachie nafasi ili tuweze kusogeza Taifa hili mbele.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mwakajoka, hujaunga mkono hoja. *(Kicheko)*

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, naikataa hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumeanza vizuri, tutaendelea tena jioni. Kama tulivyosema sasa ni wakati wa mjadala wa zile hotuba mbili ambazo Mheshimiwa Waziri alizitoa Alhamisi, ile hotuba ya Mipango na ile hotuba yenyewe ya Mapato na Matumizi kwa maana ya Makadirio ya 2018/2019. Kwa hiyo, wale wote ambao majina yenu yapo hapa mezani mjiandae, muwe na uhakika kwamba mtapata nafasi ya kuzungumza. Watakaowahi ndiyo tutakaoanza nao, tukikutaja jina hupo, basi tunasonga mbele, haturudi nyuma.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nitishe shughuli za Bunge hadi kumi na moja leo jioni. Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge siyo saa kumi jioni ni saa kumi na moja leo jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Vijijini, Mheshimiwa Antony Komu, karibu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii. Nianze kwa kusema hili suala la utekelezaji duni wa bajeti kwa kweli ni tatizo kubwa ambalo lisipopatiwa ufumbuzi itatuwia shida sana. Kwa sababu naona na najjuliza kweli kwamba ni kwa nini tunakaa kwenye hili Bunge na kupoteza muda mwingi namna hii na kufanya uchambuzi kama tunavyofanya na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mpango pale anakuja na yote haya aliyokuja nayo, lakini mwisho wa siku kunakuwepo na utekelezaji mpaka wa sifuri kwenye baadhi ya maeneo ambayo ni ya msingi sana kama ilivyorejewa hapa na watu mbalimbali kama kilimo na umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, sasa hii inaondoa maana ya Bunge hili, vilevile na nimekuwa nikisema mara kwa mara kuna tatizo la kutumia fedha vibaya. Kama unapeleka fedha zile zinazoitwa za matumizi ya kawaida na OC ambazo hakuna kazi inayokwenda kufanyika. Kwa sababu hizi fedha tunazotoa kama matumizi ya kawaida ni ili zikafanye mambo fulani fulani ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kama hili jambo halitarekebishwa kama Wabunge na chini yako tutakuwa sisi tunatumia fedha za wananchi ambao ni walipa kodi vibaya. Kwa hiyo

ningekuomba sana tuweze kuungana kwa pamoja kama Wabunge tuwaulize Serikali tatizo liko wapi, kwa nini wasije na bajeti ambayo ni ina uhalisi inayotekelezeka ili tukipitisha hapa tunajua kwamba tumefanya kitu ambacho kinakwenda. Wengine ni waathirika wakubwa wa huu utekelezaji duni wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, nina miradi kule kwenye Jimbo langu, miradi ya barabara 2016/2017, barabara moja ambayo inatoka Kiboroloni inakwenda Kikarara inapita kule Suduhi mpaka kule Kidia imetengewa fedha shilingi bilioni 2.5 haikuja hata shilingi. Mwaka 2017/2018 ikatengewa fedha shilingi milioni 810 haijaja hata shilingi. Safari hii nimeona tena Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi ameitengea shilingi bilioni moja na yenyewe sijui niseme itakuja tena sifuri au namna gani.

Mheshimiwa Spika, umesoma kule kwetu unajua kwamba barabara zetu kujengwa kwa kiwango cha lami si *luxury* ni suala la lazima. Kwa sababu ya hali halisi ya aina ya udongo wetu kule. Vivyo hivyo tuna mradi mmoja wa Telamande - Old Moshi toka mwaka 2012 unazungumzwa kwenye makabrasha yote haujaanza mpaka leo. Sasa katika hali ya namna hii naona ni fedheha kwa Serikali na hata kwa Bunge lako ambalo linakaa hapa na kutumia fedha nyingi kiasi hiki kupitisha vitu ambavyo kimsingi sijui niseme havipo au ni hewa au ni namna gani. Kwa hiyo ni vizuri tukawaomba Serikali wakija hapa watueleze ni kwa nini mambo yanakwenda hivi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni sekta binafsi. Sekta binafsi ni kichocheo kikubwa na ni *engine* mahali popote pa uchumi. Leo asubuhi uliuliza hapa ni kwa nini Kenya wako kama walivyo, ni kwa sababu wanaheshima na *commitment* kwa *private sector*. Sisi katika Taifa letu tunazungumza kila siku kitu kinachoitwa *PPP*, niulize leo ni mradi gani ambao unaendeshwa kwa huo utaratibu wa *PPP*, hakuna! Hata hivyo, tunashindwa kufanya mambo kwa sababu hatuwapi fursa watu wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji tumekuwa na ziara juzi hapa huko Nyanda za Juu Kusini, Njombe, tukakuta wawekezaji wanalalamika. Wakati wanapoagiza vitu kwa ajili ya kuwekeza hapa kuna unafuu wanaopewa wa kodi, lakini wanaambiwa na Serikali walipe *fully*, walipe kodi zote halafu wa-*claim*. Hizo pesa hazirudishwi na hata zikirudishwa zinarudishwa baada ya muda mrefu sana, jambo ambalolinaondoa imani kwa Serikali, linaondoa imani kwa wawekezaji na sekta binafsi. Sasa wenzetu huko duniani hawako hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna kiwanda cha Chai kule Njombe na nasikia Mheshimiwa Rais anakwenda huko, ni vizuri wanadai bilioni 8.2, hawajarudishiwa. Tanga wanadai bilioni 17 hawajarudishiwa, tulipita wakati fulani kule Mwaui tukakuta hivyo hivyo bilioni 12. Sasa katika hali ya namna hii tutakuwa hatujengi uchumi wetu na hatuwatendei haki watu wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine mzuri kuna Wakala wa Mbolea, walifanya kazi hapa wanadai zaidi ya bilioni 64, lakini kirahisi tu Serikali imesema hawadai baada ya uhakiki. Ukienda kuwauliza mpaka leo watu wanadaiwa na mabenzi na mbolea zilikwenda, lakini shauri ya *technicalities* tu unakuta kwamba wameambiwa hawadai. Sasa hali kama hii kwa kweli haiwezi ikatupeleka mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuwa na miradi mingi na ambayo kila siku tunaanza miradi mipya, wamezungumza watu hapa asubuhi. Tuna miradi kwa mfano, tukienda kwenye eneo la umeme, tuna uchumi ambao tulihubiriwa sana uchumi wa gesi. Hivi ni tatizo gani limeingia kwenye kile kitu tulichokuwa tunazungumza habari ya uchumi wa gesi.

Mheshimiwa Spika, nasikia mpaka leo tunafanya *utilization* ya 6.8 basi katika uchumi wa gesi na pesa zote ambazo tumewekeza. Sasa katika hali ya namna hiyo ni jambo ambalo linaacha maswali mengi. Pia kuna suala la

Mchuchuma na Liganga, kuna suala la bwawa la Kidunda yote haya yangetupa umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa kama watu hawa wangeamua wakashika mambo machache na wakayafanyia kazi kwa ukamilifu leo tusingekuwa tunaenda kuhangaika na vitu kama *Stiegler's Gorge*, ambayo mimi na naomba iinge kwenye *record* kwamba siungi mkono hilo suala la *Stiegler's Gorge* kwa sababu ni jambo ambalo linakwenda kuleta athari kubwa sana kwa uoto wetu wa asili na wanyama wanaoishi kule Selou na sioni ni kwa nini. Kwa sababu tungefanyia kazi vyanzo hivi vya umeme ambavyo tunavyo tungeweza tukafika mbali zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwamba chema chajiuzua kibaya chajitembeza, hivi kweli hizi sifa zote tunazoandika huku hatuwezi kuacha tu historia ikaja ikasema tuliyoyafanya na ambayo tumeshindwa kuyafanya?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Antony Komu. Sasa namwita Mheshimiwa Edward Mwalongo na atafuatiwa na Mheshimiwa Benardetha Mushashu.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa uwasilisho wa bajeti nzuri ambayo tunaiona inatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la *TRA*. Katika Mji wa Njombe iko Ofisi ya *TRA*. Tunaposema kwamba ulipaji kodi unatakiwa uwe rafiki nadhani ni pamoja na mazingira ya kulipia kodi. Katika Ofisi ya *TRA* Njombe mazingira ni mabaya sana, jengo lile lina vyumba sita, limechakaa, linavuja lakini lina watumishi wachache sana. Matokeo yake ni kwamba kunakuwa na msongamano mkubwa sana, watu wanakwenda kulipa kodi siku mbili mfululizo anakaa *TRA* kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Hii nayo inawavunja nguvu sana walipa kodi, niombe sana Serikali ilione hilo na itujengee jengo lingine lenye nafasi. Tuliambiwa kwamba kuna mpango wa kuhamisha *TRA* pale, lakini hatuoni kama kuna dalili ya kuhama leo wala kesho na makusanyo ya *TRA* Njombe ni zaidi ya bilioni 12 kwa mwaka. Kwa hiyo, haya ni makusanyo makubwa ukilinganisha na mikoa mingi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nikiacha suala la *TRA* niende kwenye suala la kilimo. Njombe ni wakulima na katika kilimo yako mambo ambayo ni msingi sana yakatekelezwa kwa wakati. Jambo la kwanza kabisa ni suala la miundombinu inayowahusu wakulima, wakulima wanahitaji miundombinu ya barabara ili waweze kusafirisha mazao kutoka katika mashamba kwenda katika masoko.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la pembejeo, pembejeo zimekuwa zikifika kwa kuchelewa sana kwa wakulima, hali ya barabara ni mbaya sana kwa wakulima. Niombe sana Serikali iangalie kwamba ni kwa namna gani sasa itaweza kuwawezesha wakulima wa mazao ya chakula na biashara waliopo katika Jimbo la Njombe Mjini ili kusudi waweze kufanya kazi yao vizuri, msimu wa mavuno waweze kusafirisha mazao vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna Kiwanda kipya cha Chai kimejengwa pale Rwangu, Njombe. Kiwanda kile kinahitaji chai nyingi sana na ile chai inalimwa maeneo mbalimbali sana ambayo hayana hata barabara. Kwa hiyo, ni jukumu sasa la Serikali kuona ni namna gani inawezesha kupeleka fedha za kutosha katika Jimbo la Njombe Mjini, kutengeneza barabara kwa ajili ya mashamba ya chai katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kilimo tunazungumzia na masoko, sasa hivi Njombe tumeanza kulima zao la parachichi na zao la parachichi linaiingizia fedha ya kigeni nchi. Sasa hivi tuna-*export* parachichi kwa wingi sana kutoka Njombe, lakini miundombinu yetu siyo rafiki. Kwa hiyo, inasababisha bei ya lile zao isiwe na

ushindani, kwa sababu anatokeza mtu mmoja na kwa kuwa miundombinu inayotakiwa ni ile yenye ubaridi. Niiombe sana Serikali ilione hilo.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu nikiambuka huko nyumba wakati uwanja wa Ndege wa Songwe unajengwa tuliambiwa uwanja huu unajengwa Kusini kwa lengo kwamba uweze kusaidia kusafirisha mazao ya matunda na maua kwenda masoko ya Ulaya. Uwanja umekamilika, mazao yanalimwa lakini mpaka leo yanasafirishwa kwa malori. Wafanyabiashara wanasema mazao ya Njombe hayapati bei nzuri kwenye soko la dunia kwa sababu gharama ya usafiri iko juu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanasafirisha kwa malori kutoka Njombe mpaka Dar es Salaam, hebu tuone sasa hivi tumetengeneza wale wanaitwa *white elephant* au ni nini. Kwa sababu uwanja ule uko tayari, mazao yako tayari lakini hatuoni dalili ya kuona kwamba sasa tunaanza kuutumia ule uwanja. Tunakwenda na miradi mingi mikubwa, kama tunashindwa hii miradi ambayo ipo ilishakamilika ikiwemo TAZARA hakuna hata dalili ya kusafirisha mizigo kutoka Nyanda za Juu Kusini kupeleka kwenye masoko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukajikuta tunafanya miradi mikubwa mingine lakini bado ikawa haifanyi kazi. Sasa hivi tunakwenda kuhamasisha kuna soko kubwa sana ya nje gere changa huko Ulaya na mahindi machanga yanahitajika yakiwa *fresh*, tunahitaji miundombinu ambayo itatusaidia kusafirisha haya mazao kwa ajili ya masoko ya huko Ulaya na haya mazao yanaleta fedha ya kigeni moja kwa moja. Naomba sana hilo jambo liweze kutiliwa maanani kwamba Uwanja wa Ndege Songwe na TAZARA - Makambako wawekewe miundombinu yenye ubaridi ili kusudi waweze kusafirisha haya mazao *fresh* kwa ajili ya masoko ya nje na wafanyabiashara hawa wapate unafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la maji. Katika Jimbo la Njombe suala la maji limekuwa gumu sana.

Nimeshangaa sana kuona kwamba inaonekana suluhisho la maji kwenye Mji wa Njombe na miji mingine ni kutungwa kwa sheria inayompa idhini Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa kodi. Jambo hili tumelizungumza miaka mitatu, miaka mitatu yote kwenye bajeti fedha inaoneshwa kwamba kuna miradi ya maji, kuna mkopo nafuu toka India. Kumbe tatizo ni sheria ilikuwa inagomba miaka mitatu!

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana nikiangalia jinsi Baraza la Mawaziri na Serikali yetu ilivyosheheni wasomi jambo kama hili linachukua miaka mitatu kupata ufumbuzi, je, huo utekelezaji utakuwaje sasa? Sasa tunapitisha hii ili kusudi Waziri apate hiyo idhini, niombe sasa watekelezaji watakapoanza kutekeleza hii miradi, ikiwemo mradi wa maji wa Njombe Mjini waone kwamba mradi huu wananchi wamekosa huduma kwa miaka mitatu. Kwa hiyo, waende na kasi ya kufidia hiyo miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la fedha za maendeleo. Fedha za maendeleo kwenye Halmashauri zetu haziletwi na sisi ambao vyanzo vyetu kama vile vyanzo vya kodi ya majengo vimechukuliwa inatumiza sana. Tumejenga zahanati, tunashindwa kuezeka, tumebaki na mapagale. Sasa nashindwa kuelewa kwamba ikiwa Serikali imechukua vyanzo vya mapato kama vya kodi ya majengo ikidai kwamba itafidia halafu haitufidii, tumejenga zahanati katika Kijiji cha Mamongolo, Kata ya Makoo; tumejenga zahanati Kifanyo, tumejenga zahanati Luponde, tumejenga zahanati Magoda tunashindwa kumalizia zahanati hizi kwa sababu tu hatuna fedha na Serikali fedha za maendeleo haituletei.

Mheshimiwa Spika, hebu niombe basi Serikali ione kwamba ili twende sawa kwa sisi ambao vyanzo vya mapato ambavyo ni haki yetu kabisa, vyanzo vya mapato vya kodi ya majengo vimechukuliwa, tupewe basi hizo pesa tuweze kumalizia hayo majengo. Kuna wakati wameita Wakurugenzi wa kila Halmashauri wamefika hapa

wamepewa maelekezo, wameandika na kila kitu lakini mpaka leo fedha haitoki. Niombe sana jambo hili lifanyiike ili kusaidia maendeleo ya maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la elimu. Ukiangalia kwenye kitabu cha Bajeti cha Mheshimiwa Waziri anasema nchi hii inawahitimu laki laki nane kila mwaka, lakini wanaopata bahati ya kuajiriwa ni wahitimu 40,000. Kwa hiyo, watu zaidi ya laki saba wanabaki bila ajira na watu hawa hawana ujuzi wowote zaidi ya kujua kusoma na kuandika. Kila wakati nasimama hapa naelezea kwamba hebu tusaidie nchi hii tuweke shule za ufundi katika shule za Kata ziwemo shule za ufundi.

Mheshimiwa Spika, watu wote hapa wang' ang' ana *VETA*, hatuna uwezo wa kujenga *Vocational Schools* leo zikatosheleza nchi hii, lakini njia rahisi ya kufanya tubadili baadhi ya shule za Kata ziwe shule za ufundi ili kusudi tuokoe kundi kubwa la vijana. Tutawasaidia vijana hawa watakuwa wamepata elimu ya ufundi ili waweze kujitegemea hivi hapa ugumu uko wapi au ni nani atamke? Naomba sana jambo hili lifanyiwe kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtazamo wa walio wengi wanaona kabisa kwamba kitu cha ufundi ni kitu kikubwa sana lazima kuwe na ma-*workshop* kuwe na mashine za ajabu ajabu, lakini nimekuwa nikieleza hapa mara zote kwamba jambo hili wala siyo kubwa kiasi hicho. Hebu twende turudi chini tuangalie tulifanyie kazi, tuweke mpango ambao utasaidia angalau kila Halmashauri iwe na fani angalau moja mbili katika shule zake za Kata kuzifanya kuwa za ufundi ili ziweze kufundisha vijana wapate maarifa na baadaye waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivyo, tatizo la kujajiri kwa vijana halitakaa lipate suluhisho, italeta shida sana kwa maana ya kwamba wanaomaliza elimu ya msingi na wanaomaliza elimu ya sekondari ni wengi sana. Kwa hiyo, elimu ya ufundi ndiyo ukombozi na elimu ya ufundi siyo inapatikana kwenye Vyuo vya Ufundi tu kwa maana ya *VETA*,

tunaweza kabisa kuzifanya shule zetu za sekondari zikawa sehemu ya mafunzo ya ufundi na ikawa imesaidia vijana wengi kupata hayo maarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mushashu utafuatiwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad.

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu. Naanza kwa kumpa pongezi Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote Wakuu kwa kuandaa bajeti nzuri. Kwa kweli, bajeti hii ni nzuri, nasema ni nzuri kwa sababu bajeti hii imewalenga watu wa kawaida na ukiangalia mipango iliyopo unaona kabisa kwamba, bajeti yetu hii inawalenga watu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia bajeti hii imelenga kupunguza matumizi na gharama za maisha, lakini imelenga kuhusianisha ukuaji wa uchumi pamoja na maendeleo ya mtu mmoja mmoja. Bajeti hii imelenga kuendeleza viwanda na wakishaendeleza viwanda ina maana kwamba, wakulima watatoa hizo malighafi, watapata mahali pa kuuza bidhaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema bajeti hii ni nzuri kwa sababu unakuta kwamba, inalinda viwanda vyetu vya ndani. Sasa hivi tunasema tuko katika *era* ya kukuza viwanda katika Tanzania kwa hiyo, lazima tuvilinde viwanda vyetu vya ndani, ndiyo maana nimefurahishwa niliupoona kwamba, katika bajeti hii wanaondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifungashio vya dawa za binadamu, kwa hiyo mtu wa kawaida atapata dawa kwa bei nafuu. Vilevile virutubisho vya vyakula vya mifugo, kama vyakula vya kuku vinaondolewa *VAT* kwa hiyo, vitazalishwa kwa bei nafuu, mkulima atafuga na kuweza kupata faida kwa sababu gharama za uzalishaji zitakuwa ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile bidhaa zinazozalishwa humu nchini kama *juice*, bia, maji, mvinyo, vinywaji baridi, ushuru haukupanda kwa hiyo, gharama za uzalishaji zitakuwa ndogo, *therefore* wataweza kuzalisha kwa faida. Mheshimiwa Mpango hongera sana pamoja na Naibu Waziri kwa kutuletea bajeti nzuri ambyo inalenga watu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia kwenye Ibara ya 43 kwenye bajeti hii ambayo inazungumzia vipaumbele, kipaumbele cha kwanza kilichozungumzwa ni kilimo, kilimo ndiyo sekta ambayo inajiri Watanzania walio wengi. Hongereni sana ni bajeti ya watu ni bajeti ambayo inawalenga Watanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, watoto wa kike wanashindwa kwenda shule kati ya siku mbili mpaka nne kila mwezi kwa sababu ya maumbile. Kwa kipindi kirefu sana Wabunge Wanawake mnatuona huwa tunakwenda pale Pius Msekwa kwenye Ukumbi tunafanya mikutano mbalimbali, baadaye tukawaomba na wanaume wakatuunga mkono, tunapanga mipango, tukaunda Kamati mbalimbali zikaenda kuongea na Serikali, hatimaye Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekubali ikalionga hili na kuondoa kodi ya VAT kwenye taalo za kike ili kusudi watoto wa kike waweze kuzipata kwa bei nafuu na wakishazipata kwa bei nafuu ina maana sasa hata wataweza kwenda shule kila siku kwa sababu wataweza kujisitiri, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupanga kuleta mabadiliko ya Sheria ya Serikali za Mitaa ambayo inasema sasa asilimia 10 zitengwe, kwa ajili ya asilimia tano kwa wanawake na vijana asilimia tano. Pamoja na kwamba, viongozi mbalimbali hasa Mawaziri walikuwa wanakaa hapa wanatuambia hizo asilimia zitengwe, lakini Halmashauri nyingi walikuwa wanakwepa, hawatengi asilimia 10, wakitenga ni asilimia mbili au tatu. Sasa sheria ikishakuja itawabana itabidi wazitenge hizo asilimia.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaambia mimi najishughulisha sana na vikundi vya vijana na vikundi vya wanawake kwa kweli, hizi hela zinasaidia. Hizi hela zikienda kwenye vikundi vya vijana wataweza kufanya shughuli zao, watakuwa wamejiajiri, akinamama watafanya biashara zao, watafanya ujasiriamali, wataweza kulisha hizo familia.

Mheshimiwa Spika, leo hii naleta kero kubwa ya wakulima wa Mkoa wa Kagera na kero yenyewe ni bei ndogo sana ya kahawa. Unakuta mtu analima kahawa, anautunza mbuni kwa miaka miwili mpaka minne katika miaka hiyo analima, anapalilia, anaweka mbolea, anaweka viua-wadudu, lakini anakuja kuuza kilo moja ya kahawa kwa Sh.1,000. Hii ni bei ndogo sana, pamoja na kwamba Serikali ilitangaza kati ya tozo zile 26 zilizokuwa kwenye mazao mbalimbali zilipunguzwa, lakini bei ya kahawa haikupanda.

Mheshimiwa Spika, hata leo hii msimu wa kahawa umefunguliwa, lakini bei bado ni ndogo. Ni ndogo kwa sababu, hadi leo mtu akiuza kahawa kilo moja unakuta kuna ushuru wa Halmashauri ya Mji Sh.84, kuna ushuru wa Chama cha Msingi Sh.200, kuna ushuru wa Chama Kikuu, kuna ushuru wa sijui uboreshaji, usafirishaji, ukaushaji shilingi Sh.330, kuna gharama za mikopo, yaani wao wanakopa, riba wanaiweka kwenye kila kilo ya kahawa inayouzwa Sh. 367 na gharama nyingine zinakuja mpaka Sh.1,600.

Mheshimiwa Spika, unakuta mtu labda kahawa kwenye *World Market* imeuzwa kwenye Sh.3,000, lakini Sh.1,600 zote zinakatwa, lakini na mwenyewe akienda kuuza anapewa malipo ya awali labda kama Sh.1,000/=, wanasema wakishauza kule watakuja kumpa malipo ya pili na malipo ya pili na yenyewe huwa hawapati.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kwenye kitabu kinachozungumzia hali ya uchumi hapa naona kwamba, uzalishaji wa kahawa umepungua kwa 20.7% wakati

uzalishaji wa korosho umepanda kwa 70.7%. Hakuna muujiza hapa, muujiza ni bei, bei ya kahawa ikipanda watu wenyewe watalima, watakata ile mibuni ya zamani, watalima mipya. Tunaomba vituo vya utafiti kama *TACRI* wapewe fedha watengeneze miche bora, wasambaze kwa wakulima walime kwa tija waweze kuuza mazao kwa bei zinazoeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeshangaa kwenye hiki kitabu cha hali ya uchumi wanazungumza kwamba, kwa mwaka 2017 kahawa ya robusta na arabika iliweza kuuzwa kati ya Sh.4,200 mpaka Sh.5,900 sasa inakuwaje mkulima anapata Sh.1,000 jamani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye jembe letu na ndiye tegemeo letu. Tunaona amefanya kazi nzuri sana kwenye mazao mengine kama korosho, tumbaku na pamba. Wote hapa Wabunge wanaotoka kwenye mikoa inayolima kahawa tunaomba na kwetu aje atusaidie, bei ya kahawa ipande ili kusudi watu wa kwetu waweze kuondokana na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana waliyoifanya kwa kujenga upya shule ya Ihungo na Nyakato *Secondary School* ukaifanyia ukarabati wa kina baada ya kuwa shule hizi zimeharibiwa sana kwa tetemeko. Sasa hivi shule zimekamilika lakini hakuna samani, kwa sababu baada ya tetemeko wanafunzi walisambazwa kwenye shule mbalimbali katika Mkoa. Sasa zile samani walihama nazo na katika hamisha hamisha samani zikaharibika.

Mheshimiwa Spika, watoto wanapaswa kuingia *form five* mwezi wa Julai/Agosti, lakini hakuna samani. Mkoa umeshaleta mahitaji ya samani katika Wizara zinazohusika, tunaomba samani zipelekwe ili kusudi hizi shule ziwe tayari kuwapokea, hata itapunguza ile *backload* niliyosikia asubuhi wanasema kwamba, watoto 20,000 wamekosa kwenda *form five* kwa sababu, hakuna miundombinu. Pale miundombinu ipo, kinachohitajika ni samani.

Mheshimiwa Spika, Madiwani ni watu wa muhimu sana. Madiwani ni viongozi wenzetu ambao ndiyo wako karibu na wananchi. Wale kila siku wanazunguka kwenye Kata, wanapanga mambo ya maendeleo, wanaibua miradi, wanachangia maendeleo, wao wanatoa huduma za jamii, wao magari yao na pikipiki zao ndiyo zinasomba...

SPIKA: Mheshimiwa malizia sasa.

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, tunaomba kwa sababu ya hali ya maisha, posho ya Madiwani ipandishwe au ikiwezekana walipwe mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema hii bajeti ni nzuri, inawalenga Watanzania walio wengi na hasa Watanzania wenye kipato cha kawaida.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwalimu Benardetha Mushashu. Kama nilivyokuwa nimesema hapo awali, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, baada ya hapo Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu atafuatia.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Serikali. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia leo hii kupata fursa ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa bajeti hii ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema Tanzania, hususan kupitia Wizara ya Fedha haijawahi kuja hapa na bajeti au maandishi kwenye bajeti tukalaumu, tukaiona labda kwamba ina upungufu, ni mbaya. Maandishi yanapokuja yanakuwa ni mazuri, yanalenga vizuri, lakini tatizo linakuja kwenye utekelezaji wa maandiko yetu, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, hata mwaka jana ilikuja hapa bajeti tukaisifu, tukaipigia sana makofi, tukairembaremba,

tukaizungumza vizuri, lakini tulipoenda kwenye utekelezaji sasa tukaacha yale ambayo tumeyazungumza hapa na badala yake tukaenda tukavamia mambo mengine tukayatekeleza bila hata utaratibu mzuri kufuatwa, bila hata kuangalia hasa nini tunakihitaji. Ndiyo maana hata kwenye bajeti za Wizara mwaka huu tumeona maneno mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengine wameita kwamba, bajeti zinakuwa ni bajeti za vitu badala ya bajeti ya watu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tumesema kwamba, bajeti yetu imezungumza uchumi umepanda kwa asilimia 7.2, lakini kelele za umaskini Tanzania zimezidi kwamba, Watanzania wameendelea kuwa maskini. Watanzania wameendelea kupiga kelele kwa utaratibu wa kodi ambazo zinawaumiza. Hili linawakwaza Watanzania na linawaweka katika kipindi kigumu na linaendelea kuwaweka katika mazingira magumu ya maisha.

Mheshimiwa Spika, tunataka kuona kwamba, tukiambiwa uchumi umepanda basi tunataka tuone kwamba, sasa umaskini kwa Watanzania uwe umepungua. Siyo kwamba, tunaambiwa hapa uchumi umepanda kwenye vitabu, lakini ukifika huko nje, ningemwomba, maskini Mheshimiwa Dkt. Mpango hana Jimbo, Jimbo lake lipo Ikulu, lakini kama ana Jimbo tungemtaka Mheshimiwa Mpango arudi Jimboni akawaangalie wananchi wa Jimbo lake wanasemaje? Hapo angekuja na jibu zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya au nzuri Jimbo lake yeye lipo jumba kubwa na jumba kubwa hata umaskini haupo, sasa hiki ni kitu ambacho kinamgharimu. Ningemwomba dada yangu pale amshauri vizuri kwa sababu yeye ana Jimbo pale Kondo, arudi Jimboni aende akaangalie *rate* ya umaskini, *rate* ya kelele za wapiga kura wake wanasemaje?

Mheshimiwa Spika, hili suala la kwamba, uchumi umekua, lazima sasa uchumi huu ulenge kwa wananchi,

usilenge moja kwa moja kwenye labda, tunahesabu uchumi umepanda kwa sababu, tumeweka mradi wa ujenzi wa reli, kwa sababu tumeweka mradi wa ujenzi wa *flyovers* kwa sababu, huo uchumi haujagusa moja kwa moja maisha ya wananchi wa Tanzania. Tunataka tuone kwamba, uchumi upanda, lakini umeenda kugusa moja kwa moja maslahi na maisha ya Watanzania yameboreka, afya na huduma za maji safi zimeboreka.

Mheshimiwa Spika, leo tunasema uchumi umepanda huduma za maji bajeti sifuri, huduma za kilimo ambacho kila mtu ananyanyuka hapa anasifu kilimo kwamba kilimo ndiyo kimegusa takribani asilimia kubwa ya Watanzania, kimegusa maslahi ya Watanzania walio wengi, lakini kilimo kinatengewa bajeti ya maendeleo sifuri. Uvuvi ambao umegusa pia wananchi wengi wa Tanzania, bajeti ya maendeleo ni sifuri. Kwa kweli, tutakuwa tunawadanganya...

(Hapa kipaza sauti kilizima ghafla)

MBUNGE FULANI: *Microphone zime-collapse.*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, zimeni hizo *microphones* zote ambazo mmeziwasha, ya kwake itafanya kazi. Mheshimiwa Hamad, njoo uongeleee hii *microphone* hapa, njoo hii hapa mbele hapa.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naomba nilizungumze ni suala la ujenzi wa viwanda. Hakuna Mtanzania yeyote ambaye anakataa dhamira ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, lakini uchumi wetu wa viwanda ulenge pia kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na maneno na yana ukweli kwa kiasi kikubwa sana kwamba, viwanda vinavyojengwa haviwalengi wananchi, viwanda vinavyojengwa havilengi kwenye Halmashauri na Wilaya ambazo zimejengwa. Leo hata kiwanda chenye thamani

ndogo tu kikijengwa Serikali inaenda inachukua maeneo yote ya viwanda, inachukua tozo zote katika viwanda, hivyo nitoe ushauri tu kwamba, viwanda vinavyojengwa baadhi ya tozo katika viwanda hivyo, baadhi ya mapato katika viwanda hivyo ziendelee kubaki au tozo hizo au fedha hizo ziendeleo kubaki kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, vile viwanda vingekuwa na mgawanyiko, kukawa na viwanda vyenye viwango fulani ambavyo pengine ni viwanda vikubwa vikaenda moja kwa moja Serikalini, lakini viwanda vidogovidogo na viwanda vya kati pengine tungefikiria pato lake tukaliacha kwenye Halmashauri husika, ili wananchi wa maeneo hayo waendeleo kufaidika na viwanda ambavyo vinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango, nafikiri kama sikosei ni ukurasa wa 16 amezungumza kwamba, Tanzania kwa mwaka inatoa wahitimu karibu laki nane, lakini akazungumza kwamba ajira Serikalini zinazowezekana tunatarajia kuajiri watu 40,000. Sasa angalia kwamba, leo tuna wahitimu laki nane, lakini Serikali ina uwezo wa kutoa ajira elfu arobaini tu, wapi na wapi? Watu elfu arobaini ni asilimia tano tu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha hivi hajioni kwamba, ana-*fail*? Kama Watanzania wanaohitimu ni laki nane, hawa wengine waende wapi au wafanye nini?

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya sasa Wizara ya Fedha na Serikali kwa jumla kukaa kutafakari hili. Mheshimiwa Mpango amekuja hapa na bajeti yake hii kwa mbwembwe sana, amekuja na mbwembwe nyingi, ving'ora na vitu vingine vingi. Katika bajeti ile Mheshimiwa Dkt. Mpango amekuja na maandiko mengi ya Biblia. *Amekuja na maandiko mengi ya Yesu kasema, Yesu kasema. Mheshimiwa Dkt. Mpango hivi na wewe unataka kuwa Yesu au...* *(Makofi/Kicheko)***[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

SPIKA: Mheshimiwa nadhani unakoenda sasa....

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, nataka kueleza kitu tu, sina maana kwamba, ni mazungumzo tu.

SPIKA: Ningependa ulifute tu hilo ili...

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, ahsante nimefuta.

Mheshimiwa Spika, labda Mheshimiwa Waziri anajiandaa na yeye kuwa msaidizi wa kuongoza. Mimi naamini kwa maandiko aliyokuja nayo tunapata matumaini kimsingi kwa sababu, yupo mmoja katika viongozi wakubwa tu alisema anajiandaa kuwa msaidizi wa kuongoza malaika mbinguni.

Mheshimiwa Spika, sasa labda Mheshimiwa Dkt. Mpango na yeye anajiandaa sasa kuwa msaidizi wake. Sasa tuone basi kama ni hivyo, kama unataka kwenda mbinguni na una ndoto ya kuwa msaidizi wa kuongoza malaika mbinguni, basi hayo aliyoyaandika yatekeleze, Yesu hakuwa bahili. Toa fedha kwenye taasisi zinazogusa watu, toa fedha kwenye taasisi ambazo, Wizara ambazo zinagusa maisha ya watu, asitoe fedha kwa sababu ya kutaka kuonekana kajenga reli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, reli ni nzuri inagusa maslahi ya watu, lakini inagusa maslahi ya watu wachache, kuna sekta hapa zinagusa maslahi ya watu wengi, toa fedha. Naamini akija ku-*wind up* utakuja na maneno mazuri zaidi kuliko yale ambayo...

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Naam! Anayeongea yuko wapi?

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Spika, niko huku.

SPIKA: Mheshimiwa nani?

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Taska Mbogo.

SPIKA: Ni nini, taarifa au nini?

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Spika, ni taarifa.

TAARIFA

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Spika, naomba mzungumzaji asitanie dini za watu. Afute maneno yake anayotumia ya Yesu na Malaika wa Mbinguni.

SPIKA: Mheshimiwa ndiyo maana nilikwambia huko unakoelekea unataka kutu... lakini bahati nzuri naona unaanza kutokatoka kwa hiyo, endelea kutoka tu upande huo. *(Kicheko)*

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, tumuombe Mheshimiwa Waziri kwamba, haya aliyoyaandika basi ayatekeleze na ayatekeleke kwa vitendo bila upendeleo, bila hiyana na bila ubahili wa kutoa fedha, hususan fedha katika taasisi ambazo zinagusa watu kama vile kilimo, maji, ili bajeti inayokuja aje hapa azungumze vizuri zaidi kuliko vile ambavyo amekuja hapa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la Katiba Mpya. Tanzania katika Serikali ya Awamu ya Nne ilileta mchakato wa Katiba. Katiba ambayo tulikuwa na matumaini ingekuwa ni suluhisho la matatizo ya Tanzania kwamba, mpaka Rais Kikwete anata...

SPIKA: Mheshimiwa Juma Kombo Hamad hiyo Katiba kwenye bajeti ya Mheshimiwa Dkt. Mpango iko ukurasa wa ngapi?

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, ungenisikiliza kwanza kwa sababu haya ni mawazo yangu na tunazungumzia masuala ya matumizi ya fedha za Serikali, fedha za umma, hatuna budi kuzungumzia na yaliyopita, kwamba Tanzania hii imetumia fedha nyingi.

SPIKA: Lakini ni bajeti ya 2018/2019, yaani huna kabisa ya kuchangia kwenye hii mpaka unafukua makaburi na nini.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, ninalo lingine, ujumbe umefika kwamba bado Watanzania wana kiu ya kuona Tanzania inapata Katiba mpya. Kwa hiyo hili litambulike wazi kwamba bado hatujasahau kwamba fedha za Watanzania zilitumika nyingi na mchakato huu uli-*cost* muda wa watu wengi na muda wa taasisi nyingi, lakini baadaye ukawekwa pembeni. Kwa hiyo haja bado ipo.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la Deni la Taifa. Kila Mtanzania amekuwa akipiga kelele kwamba deni la taifa linakua kwa kiasi kikubwa sana. Serikali zetu hizi zinakuwa na matatizo, kwamba mpaka jambo litokee ndipo waone kwamba hili suala hili ni la kweli. Watanzania wamekuwa wakipiga kelele wengi wachambuzi wa bajeti hii hata wamekuwa wakisema sana wataalam wamekuwa wakisema sana, kwamba ukuaji wa deni la Taifa ambao unaloendelea sasa hauko salama kwa Watanzania na ni wazi kwamba hautaiacha salama Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ningemwomba tu Mheshimiwa Waziri Mpango awe na tahadhari na hili ili hatimaye mzigo huu asije akaubeba pekee yake kwa sababu mwishowe; Waswahili kule kwetu wanasema vyako vyako vyako na wenzio vikikupata ni vyako pekeo. Mheshimiwa Mpango mzigo huu iko siku utakuja kuelemeza peke yako. Kuna *standard gauge* inataka kujengwa...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na siungi mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Nagu atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Akbar.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nzuri ya kuweza kuchangia bajeti ya Serikali itakayotekeleza mpango wa mwaka unaokuja, kwa sababu bila bajeti mpango ulioletwa mbele yetu utakuwa ni vigumu sana kutekelezwa. Naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutoa maelekezo kila wakati ya kuimarisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila bila kutambua kazi nzuri ya Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango; Naibu Waziri, Dkt. Kijaji; Katibu Mkuu, wataalam wote wa Wizara ya Fedha kwa kuchukua ushauri na kuufanyia kazi na wote umeoneshwa kwenye bajeti hii ilivyokuwa nzuri. Ahsanteni sana na Mungu awaongezee afya na nguvu ya kuweza kutekeleza hayo yote ambayo mmeyaweka kwenye bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kutekeleza yote ambayo yako kwenye bajeti kwa sababu kutekeleza hayo ndiyo yanayofanya maendeleo yawepo na matumizi ya fedha za Serikali ziende kwenye kuleta ustawi wa jamii. Ukiangalia mwaka uliopita, mwaka 2017/2018, utaona kwamba Wizara ilitengea kila sekta kiasi fulani cha fedha na mwenyewe Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba kwa miradi ya maendeleo ni asilimia 45 tu imetolewa katika fedha zilizotengwa. Kwa hivyo utekelezaji bila shaka utakuwa umeenda kwa asilimia hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia bajeti vile vile kwa matumizi ni asilimia 80 imetumika. Kwa kiasi hicho matumizi yameenda vizuri kwa sababu ukitaka kuonesha kwamba mpango uliowekwa ni mzuri unaweza tu ukapungua kwa

asilima 15 au ukawa zaidi kwa asilimia 15, ikiwa zaidi ya hivyo ni kwamba mipango yetu haitaenda kama tulivyoweka. Kwa hivyo, kwa sababu Mheshimiwa Waziri mwenyewe ametambua hili nina hakika kwa mwaka 2018/2019, mambo yatakuwa tofauti na nategemea kwamba miradi ya maendeleo imetengewa tayari itatolewa hela zaidi na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi utaenda kama ulivyotengemewa na nitashukuru sana kuona hilo linatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, tuangalie fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi zinalipwa kwa nani, kwa sababu kama ma-*contractor* wanaotoka nje na hela ni za bajeti ya Serikali tukiwalipa kama hatuna masharti ya hela hizo kubakia ndani ya mabanki yetu, ni kwamba hela hizo zitakwenda kujenga uchumi wa watu wengine. Kwa hivyo nategemea ma-*contractor* watakaopewa kazi watakuwa ni hawa wa ndani ambao wakipata hela, fedha zao zitabakia ndani ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo pengine hatutapata *contractor* wa ndani; kwa mfano kwenye reli hii ambayo inatengenezwa watakuwa wametoka nje, lakini Mheshimwa Waziri wa Fedha aweke masharti fedha hizo zikae kwenye mabanki yetu kwa muda ili nazo zichangie katika ujenzi wa uchumi wetu, kwa sababu Serikali mpaka sasa ndiyo *businessman* mkubwa. Kama kweli mipango yake haitapangiliwa vizuri kufikia uchumi wa viwanda na kipato cha kati itakuwa ngumu sana kama hatutakuwa waangalifu sana. Ndiyo maana nasema tuone nani anapewa miradi mbalimbali ili fedha zinazotolewa za Serikali zizunguke ndani ya nchi. Tuliongea juu ya *credit*...

SPIKA: Mheshimiwa mama Nagu dakika moja tu. Yaani Wabunge wa CCM ninyi mna shida gani, yaani nyie wenyewe hamwezi kusikia tu sauti ni kubwa kiasi ambacho inakera *everybody*? Hamsikilizi na nyie ndiyo Chama Tawala kwa hiyo, utakaposimama utasema yako, kumbe mwenzako amekwishaongea. Nataka kuzungumzia kidogo kwa nini hampunguzi sauti.

Pili naomba nitoe ushauri wa ujumla, mnaokwenda kwa Waziri Mkuu msikae zaidi ya dakika moja. Yaani pale unakwenda una – *secure appointment* tu basi. Kwa sababu Waziri Mkuu ni vizuri akasikia haya yanayosemwa humu ndani maana naona hamumpi nafasi kabisa ya kupumua. Mheshimiwa Mama Nagu endelea. (*Makofi*)

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuwaambia hivyo. Nilikuwa nasema tuwaangalie ma-*contractor* ambao tunawapa miradi yetu wawe ni wale ambao wataendelea kuangalia mzunguko wa fedha unabaki ndani ya nchi yetu na kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi ina nafasi kubwa sana ya kuchangia uchumi wa nchi yetu na Mheshimiwa Waziri amelisema hilo kwenye hotuba yake; nampongeza na namshukuru kwa kutambua sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hili Serikali imeweka mazingira wezeshi ya kisera, kisheria na naomba na ya kitaratibu iwekwe. Daima nimesema kuweni na *one stop centre* kwa ajili ya sekta binafsi kuwekeza kwa urahisi. Ukitaka kujua hiyo iko Rwanda. Rwanda kuna Rwanda *Development Center* ambapo *TBS* sijui *TFDA* na kila mtu yuko kwenye ofisi moja anapoenda mwekezaji hachukui siku moja inachukua hata masaa ameshapata leseni na kibali cha kuwekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hizo sheria na utaratibu pamoja na sera iweze kurahisisha uwekezaji wa sekta binafsi ambayo ni muhimu sana. Napongeza Serikali kwa hili lakini naomba ifanyike kwa matendo kuliko ilivyo kwenye hotuba. Jukumu la sekta binafsi ni kutumia mazingira haya ili kuwekeza; naomba mwone bajeti hii ni nzuri na hotuba ya Waziri ni nzuri na sekta binafsi iweze kuwekeza. Naomba sera na sheria ziwe zinatabirika (*predictability*) wawekezaji wanachotaka wajue wakiweza leo waliyoyaona leo yatakuwepo mwaka ujao na hasa ifikie miaka mitatu au zaidi ili wasiwe na wasiwasi, tuondoe wasiwasi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naipongeza Serikali, kwa mfano kuondoa VAT au kuondoa tozo na kodi mbalimbali kwenye pembejeo na kwenye zana za kilimo na Waziri mwenyewe kwenye hotuba yake amesema kilimo kimepewa kipaumbele; isiwe ni kwa kusema tu naomba tufanye kwa matendo, kama walivyoondoa tozo mbalimbali na kodi mbalimbali kwenye pembejeo na kwenye zana za kilimo zitasaidia sana wawekezaji kuwekeza kwenye kilimo. Hakuna *investment* inayohitaji fedha kama kilimo. Naomba watakapokuwa wamewekeza mazao yatakayopatikana yaweze kushindana na mazao katika nchi nyingine za *East Africa* au Afrika Mashariki na za *SADC*.

Mheshimiwa Spika, tulienda Iringa tukakuta wamezalisha chai nzuri na ina hadhi ya juu kweli kweli na ubora wa hali ya juu. Hata hivyo, ukienda sokoni Kenya inauza zaidi kuliko sisi kwa sababu ya vivutio vilivyowekwa. Naomba sana tunavyopeleka nje basi nasi tuangalie mazao yetu ya kilimo yanataka nini ili tuweze kushindana kwenye soko. Kwa hiyo, naomba sana Sera na Sheria ziwe na uhakika na ziwe zinatabirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kushukuru sana kuona kwamba malighafi zinazokwenda kwenye viwanda hazitozwi kitu chochote, kwa sababu kwenye bidhaa za mwisho tunaweza tukatoza kodi ili tuwe na viwanda ambavyo vitachakata mazao ya kilimo na malighafi nyingine ambazo zinapatikana Tanzania. Siyo hivyo tu, viwanda hivi vitafanya watu walime zaidi kwa uhakika wa soko na kwa hivyo Watanzania wengi watapata ajira kwenye kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na akinamama wenzangu kupongeza kuondoa tozo na kodi mbalimbali kwenye taulo za kike. Huko ni kudhamini uzazi kwa sababu chimbuko la uzazi ni hedhi. Kwa hivyo, taulo hizo zitakavyopunguzwa bei iende moja kwa moja kwa wanaotumia si kwa wale ambao watakuwa hapa katikati. Kwa hivyo, naomba Wizara ya Afya na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko; wataona kwamba taulo hizi zinawapa

manufaa wale watakaozitumia na siyo wale watakaotengeneza na wale ambao watauzu.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niungane na wenzangu, tunasema Tanzania inatakiwa kuwa nchi ya viwanda na yenye kipato cha kati. Nami nataka niwaambie katika viwanda kuna viwanda mama au viwanda vya msingi, kuna viwanda vya Kati kwa ukubwa lakini vile vile kuna viwanda ambavyo vitatengeneza bidhaa zitakazotumika kwa kuliwa au kwa matumizi mengine. Naomba tuone viwanda vya msingi vinapewa kipaumbele; na Mheshimiwa Waziri amesema atatoa kipaumbele kwenye mradi wa Linganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie, hakuna kitu ambacho hakitegemei chuma nchi hii. Huwezi kuwa na tairi bila chuma, huwezi kuwa na baiskeli bila chuma, huwezi kuwa na jembe bila chuma na tukiacha kuona umuhimu huo tutakuwa tunajenga uchumi wa wale wenye chuma kule nje na wa kwetu hauendelee kwa sababu tumeacha makusudi kutekeleza mradi wa Linganga na Mchuchuma.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, taarifa, niko huku.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Lakini tuisahau eneo ambalo liko Mchuchuma na Linganga...

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

T A A R I F A

SPIKA: Mheshimiwa Mwamoto mbona unafanya fujo bwana?

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, ndiyo napenda nimpongeze Mheshimiwa mchangiaji kwa sababu mchango wake ni wa Kibunge na ndiyo michango ambayo inatakiwa.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, ahsante, nimepokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Liganga na Mchuchuma iko maeneo ambayo hayajaendelea hata kidogo. Linganga na Mchuchuma zitakapotekelzwa watu watapata miradi na watapata kazi za kufanya. Mama ntilie watapika, vijana wataajiriwa na wakulima watalima kwa sababu watakaokuwa kule watakula. Kwa hiyo naomba sana, Mheshimiwa Waziri Bajeti ijayo au hapo katikati tutakapofanya *review* aseme Liganga imeanza kutekelezwa, tutamshukuru sana na tutamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *General Tire* tulifunga kwa sababu ilikuwa inasimamiwa na wawekezaji kutoka nje na walikuwa wanachukua hela zetu hatujui wanapeleka wapi na matairi yalikuwa hayatengenezwi. Serikali ikasimamisha, tukasema tutafute wawekezaji walipatikana, sasa tunajuliza hiki ni kitu gani kiko hapa katikati? Hakuna tairi zinazotoka Arusha; tungefurahi kuona tairi zinatoka ili na sisi uchumi wetu uwe rahisi.

Mheshimiwa Spika, viwanda si kazi rahisi, viwanda vinataka taknolojia, utaalum, ufanisi na tija, viwanda ni soko la rasilimali ambazo zinatokana na maeneo yetu kama mazao ya kilimo, madini na mengine kama misitu; kwa hivyo tutakavyoanzisha viwanda mjue kwamba rasilimali zinazotoka Tanzania zitakuwa zinapewa thamani kubwa humu nchini badala ya kwenda hivi hivi.

Mheshimiwa Spika, *tanzanite* ikitengenezwa mikufu, pete, ikitengenezwa mambo mengine ya vito itakuwa na thamani kubwa zaidi Tanzania kuliko kwenda Jaipur au Marekani na *South Africa*. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwenda kuweka kipaumbele kule Manyara ambako *tanzanite* inapatikana na kuweka ukuta ambao utahakikisha kwamba mnada utakapofanyika pale Wakenya watakuja pale badala ya Watanzania kupeleka *tanzanite* Kenya na badala ya Tanzania kupeleka *tanzanite South Africa*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naamini hii bajeti ilivyoandikwa ni nzuri sana. Hata hivyo, naomba sana mazao ya kilimo yasiwe na kodi mbalimbali jamani, yafike kwenye soko ili tuweze kushindana vizuri. Soko zuri na la uhakika ni viwanda vyetu; kama hakuna kodi viwanda hivyo vitatumia malighafi rahisi na bidhaa zitakazotokana na viwanda zitakuwa ni rahisi zitashindana na viwanda vya Kenya vya Malawi na *South Africa*.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo nakushukuru sana na naomba sana kwamba wananchi wa Hanang ni wakulima wa mbaazi iliyokosa soko; mahindi yakafunguwa mipaka watu wakawa maskini, lakini safari hii imefungua mipaka naomba tusaidiane kuona wakulima wanapata soko wa Kibaigwa, huko wa Hanang, Kiteto na maeneo yote hasa wale wa kusini wanaolima mahindi mengi sana na mahindi yana bei nzuri isipokuwa ni sera tu inakoshesha wananchi kupata bei nzuri; naomba sana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi Watanzania asilimia 80 wanalima, sera zikiwa nzuri na hasa za kodi zitasaidia sana wakulima kuwa na masoko na wataendelea kulima na kwa sababu wakilima bila masoko ni sawasawa na kutupa shilingi chooni na hilo halikubaliki. Nilikuwa...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa...

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, nimesahau kusemea Serikali kwa kufunga mipaka na kuona wananchi walivyodidimia, lakini watafurahi sana wakisoma hotuba hii na kuona kwamba inatekelezwa. Mungu awape afya, nakushukuru na nakupongeza Waziri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na Mungu akubariki. Naunga mkono kwa nguvu zote hotuba ya Waziri wetu wa Fedha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mary Nagu. Kama alivyosema Mheshimiwa Mwamoto basi wale wengine

tujifunze hivyo, kuchuka namna hiyo. Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango mkubwa katika Wizara hii, Wizara mama ambayo kwa kweli tunaitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii mimi nina wasiwasi kidogo. Wasiwasi wangu ni kwamba juzi Mheshimiwa Mpango ameonesha kwamba bajeti hii ametoa punguzo kwenye viwanda, maana yake amewasaidia wafanyabiashara wa ndani, lakini ameishia hapo hakwenda mbali zaidi, hii mimi imenitia wasiwasi sana. Kwa kuwa hakwenda mbali zaidi ina maana kwamba karibu asilimia 70 ya wananchi wa Tanzania ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tulitegemea kuwa hiyo asilimia 35 ambayo ameiongeza kwenye ushuru au kodi maana yake sasa angerudi tena kwa wakulima wa nchi hii ambao ni wakulima wa alizeti, korosho, mahindi na karanga ili ahakikishe kwamba anawawezesha hawa Watanzania ili tupate *raw material* ya kwenda viwandani; lakini hilo hakulifanya Mheshimiwa Mpango. Kwa sababu hiyo sasa kunakuwa na ugumu wa jinsi ya kupata *raw material* katika hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mpango atakapokuja atueleze, kwamba, je, kama amepunguza kwenye viwanda, akishapunguza au akishaongeza kodi kwenye *raw material* ambayo ni *imported* maana yake hivyo viwanda usipowezesha wananchi wa ndani vitakuwa *stagnant*, kwamba hakutakuwa na *raw materials* kutoka nje wala hakutakuwa na *raw materials* ambayo iko ndani. Itakuwa kama wanavyosema Wamakonde, kwamba, *uchiteme wala uchimumunye*, maana yake huwezi kusogea, utakuwa huna *raw materials* kutoka nje wala ya kutoka ndani.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini sasa kama huna *raw materials* kutoka nje wala huna *raw material* ya ndani maana yake ni hivi viwanda vyote vitasimama kwa wakati mmoja na watatengeneza shida ambayo ni kubwa sana. Kwa hiyo aangalie namna atakavyovifanya hivi viwanda. Leo tunasema hapa kwamba amewasaidia wafanyabiashara, lakini sidhani kama amewasaidia wafanyabiashara, atakuwa amewaweka njia panda kwa sababu *production* ya ndani ya *raw material* kwa ajili ya viwandani, hamna njia yoyote au hajaweka *process* ambayo tutahakikisha kwamba tunapata.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi kwa sababu mwaka jana wananchi walipolalamikia kuhusu upande wa kilimo alisema kwamba atasaidia wakulima, kwanza kwa kufanya *importation in bulk* kwa upande wa mbolea. Wale wananchi hawakusaidiwa, kwenye mambo ya *bulk importation*. Mwaka jana alichokifanya ni kupunguza ushuru, ule ushuru wa mazao kutoka asilimia tano hadi asilimia tatu. Alitengeneza nini baada ya pale? Maana yake ni kwamba walipopata nafuu ni wachuuzi, kwa sababu sheria inasema kwamba asilimia tano, maana yake kwamba ushuru utalipwa na mnunuzi, kwa hiyo unavyosema kwamba umepunguza hadi asilimia tatu unakuwa hukumsaidia mkulima na badala yake umemsaidia mnunuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo maana yake wakulima pale wakawa wamepigwa changa la macho ambalo hawakuliona, tukadhani kwamba, *ok* utafidia kwenye mambo ya *importation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu vile vile imetokea, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba *ok*, sasa tunataka ushuru wa mazao, kwa mfano huu wa korosho, maana Sheria ya Korosho tunayo, anasema kwamba asilimia 35 ya mazao ya korosho yatakwenda kwenye Mfuko Mkuu na asilimia 65 itarudi tena kwenye Bodi ili kuwezesha wale wakulima wa korosho waweze kuhakikisha kwamba wanapelekwa kwenye taasisi kwa mfano Naliendele.

Mheshimiwa Spika, wakifanya tafiti zile huu ugonjwa wa mnyauko, maana yake hautakuwepo. Sasa anavyong'ang'ania pesa zote bilioni mia mbili, akitegemea kwamba mwakani atapata kutoka wapi? Nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwamba ni vizuri zile fedha za korosho ambazo anazo katika mfuko wake ambazo haku-*release*; maana leo mfuko wa *sulphur* unauzwa Sh.65,000, kwa hiyo ile *production* ya mwaka jana ambayo alipata bilioni mia tatu sitini na tano asitarajie mwaka huu kwamba atapata kwa sababu hiyo *sulphur* haipo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri asitarajie kupata yai la dhahabu kwa kumchinja kuku mwenyewe badala ya kumwezesha yule kuku aendelee kutaga ili apate kidogo kidogo. Kwa hiyo natarajia kabisa mwaka huu inawezekana kabisa kwa namna yoyote asipate zile bilioni mia tatu sitini na tano; kwa hiyo, maana yake atatuweka katika hali ngumu sana Mheshimiwa Dkt. Mpango. Hebu afanye utaratibu kwa kuhakikisha kwamba hawa wakulima wanapata zile pembejeo za kilimo, ili mwakani aweze kupata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, lingine, namsifu sana Mheshimiwa Mpango, kwamba ni mkusanyaji mzuri wa mapato. Hata hivyo Mheshimiwa Dkt. Mpango, halipi madeni kwa ma-*supplier*wa ndani. Asipowalipa ma-*supplier*wa ndani maana yake hakuna mzunguko wa fedha wa humu ndani...

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Spika, mzunguko wa ndani usipokuwepo, maana yake umaskini utakuwepo kila mahali, utakuwepo Arusha...

SPIKA: Mheshimiwa Rashid...

MHE. AJALI R. AKBAR:...utakuwepo Singida, Utakuwepo Dodoma, utakuwepo kila mahali. Kwa hiyo nimwombe sana alipe ...

SPIKA Mheshimiwa Rashid kuna mtu anataka kutoa taarifa.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka kumpa taarifa mzungumzaji, anamwambia Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwamba *sulphur* mwaka huu tumeshachelewa, kwa hiyo anamwomba afanye mpango ije *sulphur* ili kuokoa jahazi. Nataka kumpa taarifa kwamba hilo jambo haliwezekani, mwaka huu tulishafeli, kwa sababu sasa hivi ukiagiza *sulphur* itakuja mwezi wa Kwanza au mwezi wa Pili ambapo msimu wa korosho utakuwa umekwisha. Kwa hiyo, mwaka huu tuseme tu kwamba kwa kuwa hela zetu za *export levy* wameshakula, basi mwaka huu tumeshaanguka. Nampa hiyo taarifa.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Spika, nashukuru hiyo taarifa nimeipokea na hiyo taarifa vile vile Mheshimiwa Dkt. Mpango naomba aipokee; kwamba ule mchezo alioufanya, sasa hivi unatupeleka mahali pabaya. Zile fedha ambazo mwaka huu alipata, bilioni mia tatu sitini na tano, mwaka huu alitarajia labda angepata bilioni mia saba hizo fedha hatazipata tena. Maana yake si ajabu, ule mnyauko uko kule na mikorosho inakauka na ni mikavu sana.

Mheshimiwa Spika, namwombe Mheshimiwa Dkt. Mpango, *in future*, ahakikishe kwamba hawa wakulima na hizi taasisi zake hizi, hasa Naliendele au zile ambazo ni za kilimo ahakikishe zile fedha zinaenda mapema ili *production* kwa wakulima iende kwa wakati na uzalishaji uende kwa wakati ili waweze kupata fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama akiendelea kung'ang'ania hizi fedha, akiwa nazo mfukoni atazitumia mwisho hata hizo kidogo hatazipata Mheshimiwa Mpango. Nimwombe sana, najua *TRA* kama nilivyomwambia kwamba ni kweli anakusanya vizuri na atumie mbinu ambazo kwa kweli ni shirikishi kwa wafanyabiashara, maana *TRA* wanajifanya kana kwamba ni polisi, wanawatisha wafanyabiashara mpaka wale wafanyabiashara wanaogopa.

Mheshimiwa Spika, namwambia Mheshimiwa Waziri wenzake tulikusanya ushuru wa mazao lakini tulikuwa tunawashirikisha hawa wafanyabiashara kiasi kwamba ukienda mtu anakulipa yeye mwenyewe; usiende pale kwa vitisho. Aangalie hii Taasisi yake ya *TRA* iwe shirikishi na ishirikiane na wafanyabiashara ili akusanye mapato vizuri, isiwe kwamba wakiwaona *TRA* wanakimbia wanafunga maduka; huo si utaratibu wa kukusanya fedha. Naomba *TRA* wawe rafiki kwa wafanyabiashara ili mapato ya nchi yetu yapate kuongezeka na yeye mwenyewe itakuwa rahisi katika utendaji wake wa kazi, vinginevyo atakuwa anapata ugumu kila siku.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwa hizi asilimia tano kuzipunguza mpaka asilimia tatu amezifanya halmashauri ziwe maskini. Leo halmashauri zinashindwa kulipia yale mahitaji muhimu. Anazitaka halmashauri leo zilipie bili ya maji, lakini *celling* yetu amepunguza ile kutoka asilimia tano hadi tatu, sasa hizo fedha zitatoka wapi ikiwa kila siku anatoa maagizo kwamba kuwe na miradi huko, fedha zinatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, kana kwamba hiyo haitoshi halmashauri haziendelea kwa sababu hata hizi *property tax* amewanyang'anya, maana yake fedha zote sasa hivi badala ya kuwa kwenye *Local Government* ziko kwenye *Central Government*. Hii inamaanisha kwamba tunarudisha utawala wa kiimla, wa kizamani, kwamba hakuna ushirikishwaji katika miradi kutoka kwenye *Local Government*, miradi yote inatoka Serikali Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mpango kwamba, arudishe utaratibu kama Mzee wetu Mwalimu Nyerere alivyokuwa amesema kwamba tunatoa madaraka mikoani, tunapeleka huko chini ili kuhakikisha wananchi wanashirikishwa katika mapato ili miradi hii iwe shirikishi, badala ya kila kitu kwenda Serikali Kuu; inakuwa ni ngumu kiutendaji; nimwombe sana awashirikishe wananchi katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo mchango wangu ni huo, ila nimwombe sana Mheshimiwa Mpango aache kung'ang'ania zile fedha za korosho, atoe *release* ili watu wapate kununua zile pembejeo muhimu za kimsingi za kilimo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Huyo ni Mheshimiwa Rashid Akbar, Mbunge wa Newala Vijijini. Aliposema ule msemu wa Wamakonde ule *uchiteme, uchimumunye*, nikaona Wamakonde wote wanapiga makofi humu ndani, nami nikakumbuka msemu mmoja ukimpenda Mmakonde basi upende na *ndonya* yake. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Pauline Gekul, tafadhali atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Masele.

MHE. PAULINE PHILIPO GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni yangu katika Bajeti ya Serikali iliyokuwa mbele yetu. Naomba nianze mchango wangu kwa kusoma Mwanzo 1:26. Mimi ni Mkristo naomba tu nisome. Inasema: "*Mungu akasema na tumfanye mtu kwa mfano wetu.*"

Mheshimiwa Spika, mzungumzaji aliyepita sasa hivi alikuwa anazungumzia suala la ushirikishwaji, kwamba halmashauri zetu zishirikishwe na Bajeti ya Serikali ishirikishe yote. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati ametuletea Bajeti yake Alhamisi iliyopita, kuna jambo ambalo si zuri sana masikioni mwa Watanzania. Jambo la kumtukua mtu mmoja kwamba amefanya, amefanya, amefanya, amefanya. Ameanza ukurasa wa tatu (3) akieleza Mheshimiwa Rais kafanya, kafanya mpaka kujenga ukuta wa Mererani kafanya.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni ya kwetu sote na nchi yetu inaongozwa kwa taratibu na sheria. Bunge inapitisha matumizi ya yeyote, mpaka ya Ikulu tunapitisha. Serikali pia inasimamia kile ambacho Bunge tumepitisha na Mahakama pia wanatusaidia. Kwa hiyo, mimi binafsi naona, hayo ni

mawazo yangu, kumtukuza sana Mheshimiwa Rais hatumsaidii. Tuongee ukweli kwamba Watanzania wanalipa kodi, kodi hizi zimetumika zimefanya haya na haya na haya na haya. Tuongee tu ukweli, kwamba Bunge limepitisha Bajeti hii; tena Mheshimiwa Spika juzi uliweka vizuri, ukasema kinacholetwa Bungeni ni mapendekezo, Wabunge sisi tuna-*amend*, tunarekebisha, tunaweka mawazo yetu, tuna-*own* pamoja kwa sababu Tanzania ni ya kwetu, kuna watu wanalipa kodi, kuna watu lazima wahudumiwe...

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. PAULINE P. GEKUL: ...lakini kusema kwamba Mheshimiwa Rais amefanya, amefanya; mimi...

T A A R I F A

SPIKA: Mheshimiwa Pauline pokea taarifa, Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa dada yangu Mheshimiwa Pauline kuwa lazima tumsifie Rais kwa sababu yeye akiamua visifanyike havitofanyika. Kwa mfano, wao wanavyochangishwa milioni 73 kila mwezi kwa ajili ya kujenga Chama na hakijengeki, kwa sababu ya Mwenyekiti kaamua. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais akiamua atajenga hata kama tukipitisha, akiamua kubomoa atabomoa. Ahsante. (*Kicheko*)

SPIKA: Kumbe mnachangishwa kila mwezi? Taarifa hiyo, unaipokea au?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, naomba niendeleo na hapa tunazungumza masuala ya msingi, ni bajeti ya wananchi iko mbele yetu. Kwa hiyo mambo mengine tupunguze tu utani.

Mheshimiwa Spika huu ni ushauri wangu, kwamba ni kweli Rais ameomba kura kwa Watanzania, lakini Rais hafanyi

kila kitu. Tusiwe waongo, na tusimtukuze Rais, tumshauri kwa upendo, tumweleze ukweli.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Mama Mary Nagu.

T A A R I F A

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kutoa taarifa kwa mwanangu, Pauline. Kwamba sheria ya kujenga ukuta wa Mererani ilipitishwa 2002, mpaka mwaka huu ulikuwa haujajengwa. Mheshimiwa Magufuli akatoa maelekezo ujengwe, ni nani amejenga kama si yeye jamani? Tumshukuru, na kwa sababu Mererani iko Manyara ambako Pauline anatoka tushukuru na tumwombe Mwenyezi Mungu afanye mengine makubwa. (*Makofi/Vigelegele*)

SPIKA: Umepokea taarifa Pauline.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, unajua ukimheshimu mtu muda mrefu sana unaweza ukachoka, ukamvunjia heshima. Huyu mama kuna siku nitachangia Jimbo lake lina matatizo mengi sana. Kuliko majimbo mengine yote, lakini huwa namheshimu sana.

Mheshimiwa Spika naomba niendeleo, kwa hiyo naendelea kumheshimu mama yangu. Suala la Rais kafanya, mara elimu bure, mara ukuta, mara hiki. Nchi hii kuna mihimili mitatu, kila mhimili una kazi yake; lakini pia hizi fedha sisi ndio tunaidhinisha. Hata hilo la ukuta wa Mererani ni Kamati zilizopita za Bunge walishauri. Kwa hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri tu Mheshimiwa Waziri, hatuna sababu ya kumtukuza Mheshimiwa Rais, alishachaguliwa ni vizuri unapoandika...

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Pauline, pokea taarifa hiyo nyingine.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa

Mwenyekiti, leo naomba nitumie kanuni ya taarifa nimwambie Mheshimiwa Gekul, pamoja na yale ya kiutaratibu yanayokatazwa kwenye Kanuni ya 64, lakini leo naomba nimpe taarifa kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 34(3); naomba nimsomee. Ibara hiyo inasema:-

34.-(3) Mamlaka yote ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano, na pia juu ya mambo mengine yote, yahasuyo Tanzania Bara yatakuwa mikononi mwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba tu Mheshimiwa Pauline Gekul kama anakerwa kwa Rais wetu kusifiwa na kupongezwa ajue haya pia ni mamlaka ya Kikatiba. Kwa hiyo avumilie tu, ajue haya ni mamlaka ya Kikatiba. Rais atasifiwa, Katiba inamtambua. Kwa hiyo Mheshimiwa Pauline Gekul akubaliane na hayo tu, vinginevyo hana *choise*. Huu ndio utaratibu wa Kikatiba, wa Kikanuni, wa Kisheria. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Pauline unajitakia haya mambo, muda wako unazidi kwenda. Ungetoka hapo ingekuwa salama zaidi. *(Kicheko)*

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba tu niendeleo, mimi nafikiri ushauri umefika kwamba hata Mheshimiwa Kikwete...

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Sijakuruhusu, endelea Mheshimiwa Pauline.

MHE. PAULINE P. GEKUL: ... kama kuna Rais alifanya mambo makubwa kwenye nchi hii ni Mheshimiwa Kikwete...

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Na watu waliopotea vile vile yanamhusu Mheshimiwa Rais. *(Kicheko)*

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, ni maamuzi yenu kuendelea kumtukuza lakini hata Mungu katika Mwanzo 1:26 alisema tumfanye mtu kwa mfano wetu. Alihitaji ushirikishwaji, si kutukuza tu mtu mpaka mnapitiliza, ni vizuri mka-*moderate*, huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukiongea sana kuhusu Bajeti *delivery* na *disbursement* ya fedha zenu kwa Wizara. Bajeti hii ambayo imetekelezwa ambayo sasa wanatueletea leo wametuonesha kuwa kuna baadhi ya Wizara wamewapa fedha kuliko Wizara nyingine zozote.

Mheshimiwa Spika, mfano, Wizara ya Habari, waliwapa bilioni nane kati ya nne; Tume ya Taifa ya Uchaguzi bilioni mbili kati ya sita; Wizara ya Mambo ya Ndani, bilioni kumi na moja kati ya nne; Ofisi ya Makamu wa Rais bilioni tano kati ya mbili; wakati Wizara ya Maji iliomba bilioni mia sita maji ambayo yanagusa maisha ya Watanzania; kila mmoja wetu, bilioni mia mbili mliwapa kati ya mia sita za *development*.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisema kwamba, ni vizuri wakaheshimu maamuzi ya Bunge pale tunapokuwa tumepitisha fedha hizi. Haiwezekani Wizara moja wakaipa zaidi ya asilimia 300 hata Mwaka wa Fedha haujakwisha wakati maeneo mengine hawapeleki fedha. Kwa hiyo ni vizuri, wakaangalia wao wenyewe. Hata Wizara yao juzi wakati wametuletea zaidi ya asilimia 63 wameipa, wametumia sawa, kwa sababu anayekaa na chungu cha ugali ndiye anayekata tonge kubwa, sawa; lakini maeneo mengine hawapeleki fedha na maeneo mengine wanapeleka zaidi ya asilimia 200. Hivi tunawaaminije wa? Kwa hiyo, nahitaji ufafanuzi juu ya hili, kwa nini wanatoa fedha kwa upendeleo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala zima la bajeti hewa, tunapoambiwa hii bajeti ni hewa, ni vizuri tu wakatuelewa. Kwa sababu kazi yetu leo ni kushauri, lakini Watanzania ipo siku wataamua kwamba ninyi mtakaa

pembeni na ninyi mtashauri na sisi tutaongoza. Kwa hiyo naomba nizungumze kuhusu bajeti hewa, ni vizuri kwa sababu kila mmoja ana muda wake wa kuchangia. Kila mmoja atashauri, tuna siku saba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Kamati ya Bajeti ambayo wamekaa nayo muda mrefu sana imeshauri, kwamba mpaka sasa wameweza ku-*perform* kwa trilioni 20, 10 nzima hawawezi ku-*delivery* kwa muda uliobaki. Ni kwa nini sasa wanatuletea Bajeti ile ile? Bajeti ya sasa hivi wameongeza bilioni mia tano, *on top of* bajeti ya mwaka jana. Ni kwa nini sasa wanaongeza bajeti wakati wanajua *performance* yao ni trilioni 20 kati ya hizo zaidi ya 31, 32, ambazo wanaziomba? Kama wao ni waungwana hawataki tuite kwamba bajeti yao ni hewa hata *performance* hii ambayo wamekaa na Kamati ya Bajeti japo na Hotuba yetu wameikataa hata haya hawayaoni?

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha, katika fedha ambazo tumezitenga za *Development* ni trilioni tano tu ndizo wameweza ku-*delivery* mpaka sasa; hivi wanategemea hii bajeti ambayo wanatuletea kati ya trilioni kumi na moja za maendeleo, tano tu ndizo wamepeleka mwezi mmoja ndio umebaki, hawawezi kufanya, ndiyo maana tunawaambia bajeti hii ni hewa. Ni vizuri wakakubali wakakaa chini wakaiandika upya, tufanye *according to* kile ambacho tunaweza kukusanya.

Mheshimiwa Spika, *TRA* wamekusanya mpaka sasa trilioni kumi na mbili, Halmashauri zetu wamekusanya bilioni mia nne kati ya mia sita; lakini wanatuletea wakati wanaona *performance* ya bajeti hii imefeli. Ndiyo maana tunasema uungwana ni vitendo, wakubali yaishe, kwamba tutumie kile ambacho tunaweza, maana hata mikopo ya wafadhili na zile *support* tunazopata kwa wahisani zime-*drop*, fedha haziji. Halafu wanatuletea bajeti ambayo hatuwezi kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba tu nizungumzie masuala ya msingi sasa kwenye halmashauri zetu. Mheshimiwa Waziri tulizungumza sana kuhusu

halmashauri kuzi-*cripple*. Wamefanya halmashauri zetu zimeshindwa kufanya kazi; mzungumzaji aliyepita ameongea vizuri. Walivyopitisha bajeti ya mwaka jana kodi ya ardhi, ushuru wa machinjio na hivi vingine wakaona kwamba wafute na vingine Serikali Kuu ikusanye.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya kawaida fedha haziji kwenye halmashauri zetu; *OC* haziji na kama zinakuja zinakuja kidogo sana. Wakati huo huo hata ile mikopo ambayo halmashauri ilikuwa inapata riba pia wameondoa riba mimi sina tatizo. Kama nia ni njema pia wangekumbuka hata wazee kwenye mikopo ya asilimia 10; lakini kodi ya majengo, kodi ya mabango, mpaka sasa hawasemi kwamba turudishe kwenye halmashauri zetu. Wanachoendelea kufanya wanaendelea ku-*cripple* halmashauri zetu wanaondoa mpaka na watumishi; halmashauri hizi wameziwa.

Mheshimiwa Spika, tuliwashauri mwaka jana hawakusikia, mwaka huu wameendelea na *business as usual* maana yake ni nini? Itafikia hatua nchi hii kila kitu kita-*paralyse* kwa sababu halmashauri hizi zilianzishwa kwa mujibu wa sheria. Wanatakiwa waziachie halmashauri zetu vyanzo vyao vya mapato.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri pia bajeti yetu ika-*reflect* maisha ya Watanzania. Leo tunavyoongea hii bajeti wanayoleta hapa na vigelegele hapa watumishi hawajawagusa, hakuna *increment* ya *salaries* kwa watumishi ... (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge wanavyosema hii bajeti inayotekelezwa ni bajeti hewa, kuna posho mtu anadai hapa, si mmelipwa mwaka mzima ninyi kwa bajeti hiyo hiyo iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Masele tafadhali.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hizi hotuba mbili za Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hotuba zote hizi zilizoletwa mbele yetu ni hotuba nzuri ambazo sisi kama wawakilishi wa wananchi tunao wajibu wa kuziunga mkono na kuhakikisha kwamba zinafanyiwa kazi ili Watanzania waweze kupata manufaa ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mipango katika hotuba yake ya Uchumi wa Taifa katika mwaka wa fedha 2018/2019 ukurasa wa 28 mpaka 33 ameeleza miradi ya kielelezo. Miradi hii mingine tayari imeshaanza kutekelezwa ikiwemo ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*. Jambo hili ni jambo la muhimu kwa ajili ya ujenzi wa Tanzania ya Viwanda. Viwanda vitakavyokuwa vinazalisha mali au vitendea kazi mbalimbali vitakavyokuwa vinazalishwa kwenye viwanda ambavyo tunavitarajia vitahitaji kusafirishwa na sehemu ya muhimu ya kuweza kusafirisha vitu hivi ni reli.

Mheshimiwa Spika, Tanzania yetu ni Tanzania ambayo ina Watanzania wengi ambao ni wakulima na tunahitaji malighafi za viwandani ambazo zilizo nyingi zinatokana na kilimo. Kwa maana hiyo, ushauri wangu ni kuishauri Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba sekta hii ya kilimo nayo inapewa kipaumbele, hasa kuhakikisha kwamba mbolea inapatikana kwa wingi na kwa bei ambayo ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ihakikishe kwamba viwanda vya mbolea vinajengwa hapa nchini kwa kasi kubwa. Kama ambavyo tumeona kiwanda kikubwa cha *DANGOTE* kimesaidia sana upatikanaji wa *cement* na kwa maana hiyo ujenzi wa nyumba na shughuli mbalimbali za ujenzi zimekuwa zikienda vizuri kwa sababu saruji inapatikana kwa bei ambayo ni rahisi kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, niombe tu Serikali iendelee kuhakikisha kwamba viwanda vya mbolea

ambavyo tulikushudia vijengwe kutokana na kupatikana kwa gesi hapa Tanzania basi navyo vijengwe na vianze uzalishaji ili kusudi wananchi wetu waweze kuzalisha mazao ya biashara na chakula ili Tanzania ambayo tunaitarajia iwe Tanzania ya viwanda basi iwe na Watanzania ambao wanapata chakula na wanapata malighafi ambazo zinaweza zikafanyiwa kazi katika viwanda ambavyo vinazalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningeshauri Serikali yangu ni kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vya zana za kivita; katika Mkoa wa Morogoro tunavyo vya Mzinga na Nyumbu. Niseme kabisa wazi kwamba Tanzania ya viwanda haiwezekani bila kuwa na Tanzania ambayo imeimarika kiulinzi. Kwa maana hiyo, niombe Serikali ihakikishe kwamba Mashirika yetu ya Nyumbu na Mzinga yanapewa pesa ya kutosha na kwa wakati ili kusudi basi majeshi yetu yaweze kuwa na zana za uhakika pindi hali ya hewa itakapokuwa imebadilika basi tuweze kukabiliana nayo. Ijulikane wazi kwamba katika mataifa yote ambayo yamefanikiwa kiuchumi pia yapo imara kiulinzi. Naishauri tu Serikali ihakikishe kwamba upande huu na wenyewe unafanyiwa kazi na unaeleweka.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kuja na mpango mwingine kabambe wa uzalishaji wa umeme. Najua kabisa kwamba sekta ya umeme ndiyo sekta mama ambayo inaweza kutusaidia kuhakikisha kwamba Tanzania yetu inakwenda haraka katika suala zima la ujengaji wa viwanda. Kwa hiyo, naunga mkono asilimia 100 ujenzi wa bwawa la uzalishaji wa umeme la *Stiegler's Gorge* Serikali iendeleo nalo na tuhakikishe kwamba tunakwenda kwa haraka sana ili tuhakikishe kwamba hizo *megawatt* 2,100 zinaingizwa katika *Grid* ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nalo linatakiwa kwa kweli Serikali ilipe kipaumbele ni suala zima la viwanda vya chuma Liganga na Mchuchuma kule. Tumekuwa tukizungumza jambo hili kwa muda mrefu sana na kwamba kwa wale ambao wamekuwa wakiangalia

vyombo vya habari wamekuwa wakiona ni jinsi gani ambavyo Watanzania wanapata shida sana ya upatikanaji wa vyuma. Matokeo yake sasa wanaingia hata kwenda kuharibu miundombinu ya barabara, wanaenda wanaokota vyuma vya kwenye barabara hata kwenye reli kwa ajili ya kuuza kama vyuma chakavu. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba upatikanaji wa vyuma hapa nchini inaonekana ni mdogo na kwa hiyo kama *supply* inakuwa ni ndogo, matokeo yake sasa watu wanaamua kuchukua sasa *scraper* na vitu vingine ambavyo wakati mwingine ni vya maana kama alama za barabarani na zenyewe zinachukuliwa na kwenda kuuzwa kama vyuma chakavu ili kusudi viwanda vya vyuma viweze kufanya kazi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Tanzania ya viwanda bila kuwa na upatikanaji wa chuma kule Liganga na Mchuchuma kwa kweli tutakuwa bado ndoto yetu haitafikiwa kwa wepesi. Nije sasa katika suala zima la...
(*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Malizia Mheshimiwa Masele.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nashukuru niseme kwamba kwanza naipongeza Serikali tena kwa kuja na mpango wake wa kujenga Makao Makuu ya nchi yetu na kuifanya Dodoma kuwa Mji Mkuu na Mji ambao kwa kweli sasa hivi umepewa hadhi ya kuwa Jiji, niseme tu Serikali iendelee kutoa pesa kwa ajili ya ujenzi wa mji huu ili uendelee kuwa mji wa kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Masele. Mheshimiwa Musa Ntimizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Monko na Mheshimiwa Chacha Marwa Ryoba ajiandae. Mheshimiwa Ntimizi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, hayupo.

SPIKA: Ameingia mitini eeh. Mheshimiwa Joseph Monko.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii katika Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niipongeze Serikali kwa ujumla, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote kwa bajeti hizi mbili ambazo wametuletea ambazo zina akisi taswira ya maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla. Nawapongeza sana kwa sababu bajeti hizi zimegusa maeneo mengi ambayo yamewagusa wananchi wetu katika sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kwa kupitia ukurasa wa 14 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri ambapo alikuwa ameongelea sana changamoto ambazo zilitukumba hasa katika utekelezaji wa bajeti iliyopita. Changamoto hizo amezitaja hapo, mojawapo ikiwa ni ajira. Tatizo hili la ajira Waheshimiwa Wabunge wengi waliotangulia wameshalizungumza kwamba tunao wahitimu laki nane lakini wanaopata ajira Serikalini ni elfu arobaini tu. Natambua sana kwamba Serikali ndiye mwajiri mkubwa na pamoja na kwamba ni mwajiri mkubwa hawezi akaajiri wahitimu wote ambao wanakuwa wamehitimu katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Spika, tunazo sekta nyingi ambazo zingeweza zikawachukua wanafunzi hawa kwa taaluma hizo ambazo wameshazipata. Moja ya sekta ambazo mimi naiona ni sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo ambayo kwa bahati mbaya sana pia imetengewa bajeti ndogo sana katika bajeti ya mwaka 2018/2019 ambayo ni sawa na 0.4 ya bajeti nzima ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ndiyo inayoajiri wananchi wengi sana, zaidi ya asilimia 65. Ni sekta ambayo

inagusa wananchi wengi hasa wa vijijini, sawa na kule kwenye Jimbo langu ambako nilipotoka mimi. Hata hivyo utaona kwamba uwekezaji katika sekta ya kilimo umekuwa ni mdogo sana. Matokeo yake tumekuwa na tatizo la ajira, matokeo yake tumekuwa na umaskini mkubwa na mpaka sasa kwa mujibu wa takwimu za Mheshimiwa Waziri hapa tunao maskini wa zaidi ya asilimia 26.4. Tatizo hili ni kubwa, wananchi wengi bado wanaishi chini ya dola moja.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo linatufanya tuanze kuangalia katika kuwekeza katika sekta ya kilimo ambayo inaweza kabisa ikawagusa wananchi wengi na ikawaondoa wananchi wengi katika dimbwi la umaskini tulionao. Kwa hiyo, ningeishauri sana Serikali ijaribu kuangalia namna ya kuwekeza katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano, katika Jimbo langu la Singida Kaskazini sisi ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya mahindi, mtama, vitunguu na alizeti. Tunacho kiwanda kikubwa sana cha alizeti Afrika Mashariki ambacho kiko pale Mount Meru; hakina malighafi za kutosha na wananchi wengi wanashindwa kuhamasika kulima kwa sababu wanategemea zaidi tu kilimo cha mvua. Hakuna kilimo cha umwagiliaji ambacho kinaendelea. Ziko skimu za umwagiliaji ambazo hazijafanya kazi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nitatolea mfano skimu moja ya umwagiliaji iliyopo katika Kata ya Msange ambayo tangu mwaka 2009 ilishafanyiwa upembuzi, wananchi walishalipwa katika maeneo yaliyozunguka katika lile bwawa, ni skimu ambayo inatarajiwa kuwa na hekari elfu tatu na kuhudumia wananchi zaidi ya elfu kumi.

Mheshimiwa Spika, skimu hii ya umwagiliaji ilianza kutengewa fedha, ilionekana inahitaji fedha zaidi ya bilioni 1.3 tangu bajeti ya 2009/2010. Hadi ninavyoongea hivi sasa skimu hiyo haijafanyiwa chochote hatujapata fedha na wananchi wameendelea kubaki na mpaka sasa tulianzisha

tu skimu ndogo ya ekari 25 ya umwagiliaji wa matone ambayo kwa kweli haijaweza kutoa tija kwa wananchi wa Kata ya Msange Maghojoa na Mwasauya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali ni kuweka uwekezaji mkubwa katika sekta ya kilimo ambayo inaweza kuwagusa wananchi walio wengi. Tukiwekeza katika kilimo tutakuwa tumewekeza katika kuongeza ajira kwa vijana wetu. Tutakuwa vile vile tumeongeza Pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunaongea ukuaji wa uchumi wa asilimia saba, sekta ya kilimo yenyewe inakuwa kwa asilimia 3.7. Ukuaji huu ni mdogo mno na ndiyo maana hali ya umaskini inashindwa kuondoka na wananchi wetu wanazidi kuwa maskini kila siku na hata ukiangalia huduma ambazo wanaendelea kuzipata kule vijijini tunashindwa kwa sababu mapato yetu ni madogo na Serikali haina uwezo wa kuhudumia miradi mingi ya maendeleo. Kwa hiyo, nataka niombe sana Serikali kuwekeza sana katika hilo.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 61 mpaka 62 ya kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wameweka tozo. Toza ushuru wa forodha wa asilimia 25 badala ya sifuri (0) na 10 katika mafuta ghafi ya kula mfano wa alizeti, mawese, soya, mizeituni na kadhalika. Hili ni jambo zuri na lengo hapa ni kujaribu kulinda viwanda vyetu vya ndani. Hata hivyo, tunajiuliza, tozo hizo kwa bidhaa zinazolingia kutoka nje ambazo tumeweka zinawezaje sasa kuwa-*encourage* wananchi wetu wakaweza kuongeza kipato na kuongeza uzalishaji? Tutakuwa na viwanda vikubwa kama ambavyo tulivyo navyo *installed capacity* sasa ni kubwa, lakini malighafi zilizopo ni ndogo. Hadi sasa kwa mfano alizeti tunazalisha kati ya tani laki mbili na nusu mpaka tani laki tatu; lakini kiwanda cha *Mount Meru* pale Singida kinahitaji zaidi ya tani milioni mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, sasa tunahitaji kuwekeza katika mbegu bora zinazotoa mafuta mengi, tunahitaji kuwekeza katika kuwapa wananchi mbegu zilizo bora ili waweze

kuongeza tija katika uzalishaji huo. Tukifanya hivyo tutakuwa tumefika mbali na wananchi wetu tutakuwa tumewasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, liko jambo lingine ambalo linaambatana na hilo, hasa kwenye upande wa chakula cha mifugo, mfano kuku, ng'ombe na mifugo mingine ambacho kinatokana na mashudu ya alizeti, mashudu ya pamba, Soya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha *zero VAT* katika chakula cha mifugo. Hilo ni jambo jema na lengo lake lilikuwa ni katika kuweza kuwasaidia wafugaji. Hata hivyo, tunalo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Monko, malizia.

MHE. JUSTIN J. MONKO: ...tunalo tatizo kwamba zipo malighafi za chakula cha mifugo. Kwa mfano, mashudu ya alizeti, mashudu ya pamba bado yanatozwa *VAT* kwa sababu msamaha ulitolewa ulikuwa peke yake kwenye *HS code* ya 23.09 ambao haugusi mashudu haya ambayo yanazungumzwa. Sasa hivi tunavyoongea mashudu haya yanakwenda Kenya yanatengenezwa chakula cha kuku kwa sababu kunakuwa na *zero VAT* unapo-*export*, halafu chakula hicho kinarudi tena Tanzania na sisi ndio tunakuja kununua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wawekezaji wengi wanaona bora kuwekeza Kenya wakachukua malighafi Tanzania na hatimaye kurudisha chakula hicho Tanzania na sisi tunashindwa kulinda viwanda vyetu, tunakosa ajira na tunakosa mapato. Kwa hiyo niombe sana Serikali iweze kuondoa *VAT* katika mazao haya ambayo ni *input* kubwa kwa asilimia 80 katika utengenezaji wa chakula cha mifugo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Marwa Ryoba atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Hongoli.

MHE. CHACHA R. MARWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nami nisome Mithali 29:1-2, halafu nitaendelea, inasema: *“Aonywae mara nyingi akishupaza shingo atavunjika ghafla wala hapati dawa. Wenye haki wakiwa na amri watu hufurahi, bali muovu atawalapo watu huugua.”* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hali ni mbaya. Ukienda mtaani hamna hela, mimi sijui kwenye majimbo yenu, lakini mimi kwa Serengeti hela hakuna, wamepeleka wapi hela? Mheshimiwa Dkt. Mpango amepeleka wapi hela? Yaani hela hamna, hivi nini kimetokea? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri, wala mimi siwezi kumlaumu Rais Magufuli, wala siwezi kuilaumu CCM; maana angalia kwenye kilimo; ukisoma ukurasa wa 15 ile namba tatu inasema sekta ya kilimo inayojumuisha mazao, mifugo na uvuvi ambayo inaajiri asilimia 66 ya Watanzania inachangia asilimia 30 ya pato la Taifa. Inaendelea kukua kwa kasi ndogo ya wastani wa 3%, nani kasababisha ikue kwa asilimia ndogo?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mpango ameandika yeye, aliyesababisha kasi ya ukuaji wa kilimo ikue kwa 3% ni nani? Ni yeye kwa sababu gani? Njoo kwenye bajeti, kwenye kilimo mwaka 2016/2017, walitengewa bilioni 100.5 wakapewa bilioni mbili, asilimia mbili aliyesababisha sekta ya kilimo isikue ni nani, ni yeye ambaye hakupeleka fedha. Mwaka 2017/2018, ilitengewa bilioni 150, akapeleka bilioni 16, sawa na asilimia 11, nani kua sekta ya kilimo, ni yeye. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye Mifugo mwaka 2016/2017, ilitengewa bilioni nne, akapeleka 150 milioni yaani ni sawa na *Landcruiser* moja, sawa na 3%, nani kua hii sekta ni yeye. Mwaka 2017/2018, mwaka huu wa fedha tulionao tulitenga sisi Bunge bilioni nne, amepeleka shilingi ngapi, sifuri. Nani

kaua sekta ya kilimo na uvuvi na mifugo ambayo inaajiri 66% ya Watanzania? Ni yeye Mheshimiwa Dkt. Mpango na huyo Mheshimiwa ambaye wamekaa naye hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusitafute mchawi kwamba kwa nini hela haiko mtaani, hela haiko mtaani kwa sababu hatujawekeza kwenye kilimo, mifugo na uvuvi. Kama tunataka hela iwe mtaani tupeleke pesa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo wanasema viwanda; kama kuna viwanda ambavyo tungewekeza vikaisaidia nchi cha kwanza ni Kiwanda cha Mbolea. Hebu aniambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuna viwanda vingapi vya mbolea? Kila leo tuna-*import* mbolea kwa ajili ya nchi yetu, tunatumia pesa nyingi za kigeni kwenda kununua mbolea nje, pesa ambazo zingefanya mambo mengine. Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, kwa nini Tanzania tusijenge kiwanda cha mbolea? Nini tunashindwa? Yaani kama kweli kiwanda tu cha mbolea cha kuwasaidia wakulima wetu tunashindwa sasa tunaongelea viwanda, viwanda gani? Maana kama kuna kiwanda cha kujenga ni cha mbolea.

Mheshimiwa Spika, maana tukisema tuna viwanda, viwanda gani? Kama mbolea hakuna una-*import* kila kitu unategemea nini? Kwa hiyo, haya mambo yanauma sana, hebu tusaidie wakulima wa Tanzania. Tuache mambo ya vyama, mimi ni CHADEMA lakini ninachoangalia hapa Utanzania wetu kwanza. Kule mtaani hamna hela, Mheshimiwa Jenista kuna hela kule? Hamna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu niambieni.

SPIKA: Mheshimiwa Warioba wanasema huenda wewe ndio huna hela, halafu unafikiri na wenzako wote hawana. *(Kicheko)*

MHE. CHACHA R. MARWA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mazao ya biashara; hivi katika mazao ya biashara ya nchi hii ni mangapi, tumbaku iko wapi? Serengeti tulikuwa

tunalima tumbaku, pale Serengeti tumbaku ilikuwa inaleta bilioni kumi na sita mpaka bilioni ishirini. Wananchi unakuta bilioni kumi na sita ikimwagika kwenye ile wilaya, wilaya inachangamka. Sasa hivi *Alliance One* kampuni pekee iliyokuwa inafanya biashara ya tumbaku imeondoka. Unategemea hela itakuwepo, mzunguko wa hela utakuwepo, hakuna.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

T A A R I F A

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Ryoba ipokee toka Tabora Mjini.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, anataja zao la tumbaku kama ni zao ambalo sasa halipo, napenda nimpe taarifa kwamba hata uzalishaji wa msimu uliopita ilikuwepo tumbaku ya ziada mpaka ikakosa wanunuzi na Serikali ikafanya mpango kununua ile tumbaku ya ziada. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba tumbaku haipo. *(Makofi)*

MHE. CHACHA R. MARWA: Yuko sawa, si kwamba Watanzania wanashindwa kuzalisha tumbaku, wamezalisha nyingi imekosa soko, yuko sawa. Watanzania wamezalisha nyingi imekosa soko, nani alaumiwe? Wamevuruga wenyewe makampuni ya kununua. Watanzania wako tayari kulima tumbaku, kule Serengeti wamehama na maeneo mengine Songea huko walikuwa wanalima tumbaku, maeneo mengine wamevuruga. Nenda pamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu namshukuru sana. Hebu tumpigie makofi Waziri Mkuu kafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

T A A R I F A

SPIKA: Mheshimiwa Ryoba unaingia kwenye mazao ambayo huyajui sana sasa taarifa zinakuwa nyingi, Mheshimiwa mpe taarifa.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Naomba tu kumpa taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) mzungumzaji kwamba tumbaku kwa Namtumbo; maana Songea nadhani alikuwa na maana ya Namtumbo; mwaka huu tuna tani 1,500 wakati mwaka jana tulikuwa na tani 250 tu. Kwa hiyo tumbaku inapanda na kupanda kwake ni kwa sababu ya upatikanaji wa soko.

MHE. CHACHA R. MARWA: Mheshimiwa Spika, Serengeti wanalima tumbaku. Duniani yako makampuni manne yanayonunua tumbaku na Tanzania yako manne. Kwa hiyo, nadhani sijui anaongea nini, Watanzania hawajashindwa kuzalisha tumbaku, wanazalisha kwa wingi hata Serengeti ipo mpaka leo, imeshindwa kununuliwa.

Mheshimiwa Spika, pamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi nzuri, ndiyo maana nikasema tumpigie makofi amefufua zao la pamba, tatizo soko. Mpaka leo ninavyoongea Serengeti hakieleweki, wananchi wamekaa na pamba yao hawajui nini cha kufanya. Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie hawa wataalam wa Wakuu wa Mikoa sijui watu gani wanawadanganya. Ukienda kwa wananchi, mimi Mbunge wao napigiwa simu na si mimi peke yangu, Wabunge wengi wanaotoka kanda ya ziwa wanasumbuliwa na wananchi wao kuhusu ununuzi wa pamba, ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, alizeti; mimi nimshukuru Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango huyu, wamepandisha ile kodi ya ku-*import* mafuta safi ili tuzalishe alizeti kwa wingi tuwe na viwanda vyetu. Hata hivyo, Mheshimiwa Dkt Mpango nikitaka kujenga kiwanda cha kuchakata alizeti kodi kwenye zile mashine ninazo-*import* si aondoe.

Mheshimiwa Spika, mimi siyo Mwanauchumi lakini ili u-*import* kuna VAT 18%. Sijui kuna *import duty*, sijui kuna nini, si waondoe. Kama kweli wanataka tujenge uchumi wa viwanda waondoe kodi kwenye mashine ambazo tuna-*import* kwa ajili ya viwanda, kama Ghana walivyofanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna *issue* ya *corporate tax* sijui na nini, naomba nihame hapo niongelee mambo ya wakandarasi. Wakandarasi sasa hivi wa Kitanzania wana hali ngumu, sijawahi kuona. Wakandarasi wana hali ngumu, ndiyo hiyo naomba kwenye wale wanaofanya mambo ya ujenzi, vifaa hivi vya ujenzi wanavyo-*import*, wapunguze kodi. Tutengeneze wazawa ambao watafanya miradi yetu wenyewe. Tunao vijana wazuri wenye makampuni lakini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Malizia Mheshimiwa.

MHE. CHACHA R. MARWA: Mheshimiwa Spika, sijui niseme nini hali ni mbaya kweli kweli, naomba tuwasaidie Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nakupenda sana, nikwambie na ukisimama vizuri hawa jamaa watanyooka hapa, nchi itaenda vizuri, simama, mimi nakuunga mkono. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joram Hongoli atafuatiwa na Mheshimiwa Ramo Makani.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo kwenye Wizara ya Mipango na Fedha kwa maana ya bajeti nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa namna anavyofanya kazi, nimpongeze pia Naibu Waziri namna wanavyofanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba Watanzania mipango ya fedha na mipango mingine inaenda vizuri; niwapongeze wanakwenda vizuri. Nimwombe Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema ili wasikate tamaa wasirudi nyuma, waweze kwenda mbele na kutusaidia kuhakikisha kwamba

rasilimali za nchi hii zinawekwa vizuri na hatimaye zinagawanywa vizuri kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nianze kusema kwamba wananchi Watanzania walio wengi wamejiajiri kwenye shughuli za kilimo, takribani asilimia 65.5 wanajihusisha na kilimo. Kwa hiyo tafsiri yake ni kwamba uchumi pengine wa nchi ya Tanzania unategemea sana kilimo. Kwa hiyo ni lazima tujikite tuhakikishe kwamba tunaboresha sekta ya kilimo ili tuweze kupata pato la Taifa na liweze kukua kutokana na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kilimo haziwezi kukua kama hatujaweka miundombinu mizuri wezeshi; na moja ya miundombinu wezeshi mizuri ambayo inaweza ikasababisha kilimo kiweze kukua na hatimaye pato la Taifa liweze kukua ni barabara. Sote tunatambua kwamba kilimo kinafanyika maeneo ya vijijini na huko ndiko wakulima wetu waliko, wanazalisha kwa kiasi kikubwa, lakini changamoto kubwa imekuwa ni barabara. Imekuwa hawawezi kufikisha mazao kwa wakati, mazao hayawezi kufikia soko kwa wakati na hata yakifika yanakuwa tayari yameshapoteza ule ubora wake.

Mheshimiwa Spika, juzi wiki iliyopita tulikuwa kwenye mkoa wetu, Mkoa wa Njombe na Kamati ya Kilimo. Kamati ilijionea yenyewe namna jinsi wakulima wetu wanavyopoteza fedha nyingi, rasilimali nyingi kutokana na changamoto kubwa sana ya barabara. Njombe tunazalisha mazao mengi; tunazalisha chai, tunazalisha matunda, tunazalisha mbao, tunazalisha kila aina ya mazao ambayo yanazalishwa hapa nchini, lakini changamoto kubwa ukiangalia mazao yote kwa ujumla wake kwa hali ya hewa ya Njombe ni hali ya mvua. Kwa hiyo yamekuwa yakiathiriwa sana na barabara zetu ambazo si nzuri sana, kwamba hazipitiki wakati wa kifuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme juu ya zao mojawapo zao la Parachichi. Zao la parachichi katika nchi hii linalozalishwa Njombe ni la tofauti sana. Ni wakati ambapo Njombe peke

yake inazalisha hili zao, maeneo mengine duniani kunakuwa hakuna uzalishaji wa parachichi. Sote tunajua matumizi makubwa ya parachichi katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ikiwemo mafuta, mafuta ya nywele, dawa mbalimbali, lakini ukiangalia miundombinu ambako hili zao linazalishwa ni mibovu sana.

Mheshimiwa Spika, niombe kwenye upande hasa wa barabara, tukiangalia barabara zetu hasa kwa mfano, kwenye jimbo langu Jimbo la Lupembe, barabara ya kutoka Kibena kwenda Lupembe mpaka Madeke ambako huko kuna uzalishaji mkubwa sana wa parachichi, barabara hii imekuwa haipitiki wakati wa kifuku.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili tumepitisha bajeti mara kadhaa, tumepitisha bajeti ya mwaka 2016/2017, tumepitisha tumeweka fedha. Tumepitisha bajeti ya mwaka 2017/2018 na hata mwaka huu 2018/2019, tumeweka fedha pale. Fedha hizi zimekuwa hazitoki, kwa hiyo kimsingi tunapoteza fedha nyingi kwa kuacha yale mazao yaliyopo kule vijijini yasiweze kutoka kwenda kwenye lami, kwenda kwenye soko kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango lakini pia niombe kwa Serikali yetu kwa ujumla, niombe kwenye bajeti hii ya mwaka huu tujitahidi basi barabara ya Lupembe kwa maana ya Kibena – Lupembe- Madeke na kuunganisha kwenda Morogoro iweze kupewa fedha ianze kujengwa kwa kiwango cha lami ili mazao haya niliyotaja kama chai na parachichi yaweze kusafirishwa kirahisi zaidi na yaweze kufikia soko.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa tukizalisha kwa wingi, tukiweka barabara zikawa zinapitika kipindi chote cha mwaka mazao kama chai, parachichi kama nilivyosema, mbao na nguzo za umeme zitaweza kupitishwa kwenye barabara hii na hatimaye tutaokoa fedha nyingi sana ambazo tumekuwa tukipoteza wakati wa mvua kutokana na ukosefu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Mpango kwa kushirikiana na Serikali nzima na Wizara zote tuhakikishe hii barabara inatengenezwa kwa kiwango cha lami na barabara nyingine zilizopo katika Mkoa wa Njombe ambako kama nilivyosema kuna uzalishaji mkubwa sana wa parachichi ambazo zinazalishwa Njombe tu.

Mheshimiwa Spika, katika dunia nzima kuna msimu ambako Njombe tu zinapatikana na wafanyabiashara wote duniani wanakuja kununua parachichi Njombe ili ziweze kwenda kwenye masoko hayo na tuweze kupata mabilioni ya fedha mengi na hatimaye kukuza pato la Taifa, tuhakikishe kwamba barabara hizi zinatengenezwa kwa kiwango ili ziweze kutumika wakati wa kifuku.

Mheshimiwa Spika, pia niseme jambo moja juu ya risiti za *EFD* hasa kwa wazalishaji wa mazao ya misitu hasa mbao. Kumekuwa kuna tatizo Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa wakulima wangu wa Lupembe wanaozalisha mbao. Zinapokwenda sokoni njiani wanakutana na kikwazo kwamba ni lazima aliyeuza hiyo miti, aliyezalisha hiyo mbao lazima awe ana risiti ya *EFD*. Sasa mkulima ameuza miti yake ameuza heka mbili, heka tatu, heka tano tu unamwambia awe na risiti ya *EFD* na anauza pengine kwa miaka 15 mara moja tu; sasa hii mashine ya *EFD* atapata wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe Wizara ya Fedha wajaribu kuliangalia jambo hili hasa la *EFD* mashine kwenye mbao zinazotokana na wakulima wa misitu, hasa wakulima wa misitu ya mbao. Kwa hiyo niombe tuliangalie vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia nataka niseme kidogo juu ya jambo moja la vifungashio. Tulipita na Kamati ya Kilimo na Uvuvi, kuna maeneo ambako tayari kuna wafanyabiashara wananunua mazao haya, kama nilivyosema matunda na mazao mengine kama njegere na mazao mengine. Wanatumia vifungashio kutoka Kenya na pale nje wanaandika *Made in Kenya*. Kwa hiyo, inaonekana kwamba zao lile au njegere hizo au parachichi hizo

zimezalishwa Kenya wakati zimezalishwa Lupembe au zimezalishwa pale Njombe. Kwa hiyo niombe wajaribu kudhibiti hasa hawa wanaochukua mazao yetu haya wafungashie vifungashio ambavyo vitaandikwa kwamba hilo zao au hiyo bidhaa aliyozalisha imezalishwa sehemu fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo itajwe sehemu ambako bidhaa hiyo imezalishwa, lakini siyo itajwe eneo lingine kwa mfano wanaandika *Made in Kenya* na mwisho wa siku inaonekana Kenya ndiyo inayozalisha hayo mazao kumbe tunazalisha hapa Tanzania, tunazalisha Njombe. Kwa hiyo niombe wajaribu kufuatilia hili na kulidhibiti kwenye upande wa vifungashio ili vioneshe sehemu ambako zao hili limezalishwa na hasa kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niseme juu ya kodi ya mapato hasa kwa wazee wastaafu ambao wamefungua vi biashara vidogo vidogo. Wazee hawa wamekuwa wakipata zile pensheni zao wanafungua biashara ndogo, anakuwa na biashara ya milioni tatu, nne, tano halafu tunakwenda kuwadai kodi. Hebu tuangalie hawa wazee wamefanya kazi miaka mingi sana, wametusaia sana, tuangalie kama biashara ndogo hizi angalau tuwaachie ili waweze kujiwezesha waweze kujikwamua kwenye maisha yao...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hongoli malizia sasa.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru sana, naamini Wizara itayachukulia kimakini haya mambo na niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja hii iliyopo mbele yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ramo Makani, Mheshimiwa Mattar utafuata.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa ajili ya hoja ya Serikali iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, tunajadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/2019, lakini pia tunajadili Mapendekezo ya Serikali Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi. Kwanza niipongeze Serikali kwa kutenga asilimia 37 ya bajeti yote kwa shughuli za maendeleo. Kufanya hivi ni kuendana na mpango wetu wa miaka mitano ambao tulishaupitisha hapo awali wa kwamba tutakuwa katika kila bajeti ya kila mwaka tunatenga fedha kwa ajili ya maendeleo kati ya asilimia 30 na asilimia 40. Kwa hiyo, bajeti hii imeweza kukidhi matakwa hayo ya mpango wa miaka 5 tulionao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kupongeza kwa sababu Serikali imefanya jambo kubwa lifuatalo, pengine wenzangu hawajaliona au wameliona; ni kwamba fedha za ndani ambazo Serikali imeweza kuchangia, kwa mwaka uliopita, mwaka 2017/2018 ambayo ilikuwa ni asilimia 38, kwa fedha za ndani zilikuwa asilimia 75 na fedha za nje zilikuwa asilimia 25. Mwaka huu Serikali imeamua kuongeza mchango wa fedha za ndani na kupunguza mchango wa fedha za nje, kwamba kwa mwaka huu wa fedha mchango wa fedha za ndani ni asilimia 82 wakati mchango wa fedha za nje ni asilimia 18. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii itaweza kwenda kutusaidia kuondoa tatizo kubwa sana ambalo limekuwa likisababisha *budget performance* kuwa siyo nzuri kwa sababu ya kulegalega kwa utoaji wa fedha za nje. kwa mfano, katika mwaka ulioisha wakati utekelezaji kwa upande wa fedha za ndani ulikuwa asilimia 85, fedha za nje zilikuwa asilimia 15 tu peke yake; lakini kwa mwendo huu tunaoenda nao pengine tutafika mahali.

Mheshimiwa Spika, nataka kuishauri Serikali twende hivi, ikiwezekana tufike mahali ambapo fedha zote za maendeleo zitatokana na fedha za ndani na fedha za nje ziwe ni fedha za ziada, tutaweza kwenda kwa kasi na kuweza kutekeleza vizuri zaidi malengo yetu katika miradi ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda labda ningesema jambo moja tu kwamba ingekuwa wadau wa fedha za nje (wachangiaji kutoka nje) nao wangechangia asilimia 85 kama tulivyochangia sisi kwa fedha za ndani, *budget performance* kwa kufikia mwezi Aprili mwaka huu ingekuwa ni asilimia 73. Mahali ambapo hata sisi wenyewe kama tungechangia asilimia 100 na wafadhili wangechangia asilimia 100 kwa mwezi Aprili tungekuwa tumefikisha asilimia 85.4 na kwa hiyo kuwa na mwelekeo wa kuweza kupata matokeo mazuri zaidi ya kibajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya uchumi na mpango wa maendeleo wa Taifa tumefanya vizuri sana, kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na Serikali. tuna mafanikio ya kiuchumi kwa upande wa uchumi wa Taifa kwa vigezo vya uchumi wa Taifa kwa jumla, lakini pia kwa ongezeko la Pato la Taifa na uhibitaji wa mfumuko wa bei. Si tu kwa ndani lakini pia hata katika eneo la Afrika na Kusini mwa Sahara, miongoni mwa nchi za *SADC* na nchi za Afrika Mashariki, takwimu zinajieleza, kwa sababu ya muda siwezi kusoma takwimu hizo, lakini tumefanya vizuri sana kiwango cha kuweza kujipigia Makofi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kufanya vizuri huko kumeelezwa kwenye taarifa hiyo hiyo kwamba kumetokana na jitihada za Serikali katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu, lakini pia kuongezeka kwa uzalishaji wa baadhi ya madini na pia kuimarika kwa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda hapa niwapongeze wachapa kazi wote wa Tanzania, walipa kodi wote, wizara kwa niaba ya Serikali nzima pamoja na uongozi wa juu wa Serikali wakiongozwa na Jemedari Rais Mheshimiwa Dkt.

John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Tanzania akisaidiwa na wasaidizi wake wa karibu kabisa Makamu wa Rais mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pengine tungeweza kuona namna ambavyo tunaweza kufanya vizuri hasa katika ukanda wa Afrika Mashariki. Ili tuweze kufanya vizuri zaidi kipo kitu kimoja ambacho ni nyenzo hatujakitumia sawasawa na hiki siyo fedha, mali wala mtaji mwingine wowote ule isipokuwa tu lugha ya Kiswahili. Pengine wengine wakinisikia nikisema Kiswahili wanaweza wasielewe, lakini watafiti duniani kupitia *The World Economic Forum* wamesema hivi, kwanza wamesema *speaking more than one language can boost economic growth*. Pia wamesema *multi lingualism can fuel exports increase salaries and help innovation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki tuna shida kidogo kwenye mkataba wenyewe wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kiswahili hakipewi umuhimu. Kwenye kifungu cha 137 cha Mkataba wa Afrika Mashariki imeandikwa hivi *Article 137, official language*.

137._ (1) The official language of the community shall be English,

(2) Kiswahili shall be developed as a lingua franca of the community.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu moja kwa moja hapa kupitia Serikali tushauri ili katika uwanja ule wa Afrika Mashariki na Kiswahili kitumika kama *official language*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sababu ya msingi ya kusema hivyo ni kwamba nyaraka muhimu ambazo zinatoa mwelekeo wa kimaendeleo na kuweza kuzungumzia mipango mbalimbali ya Afrika Mashariki kama mkataba wenyewe, lakini *vision* ya

East Africa ya mwaka 2050, pia mipango kama *development strategy, protocols* zote pamoja na *facts and figures* na mambo ya ripoti za kila mwaka zote zipo kwa Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kushindwa kuwafanya Watanzania walio wengi kushiriki katika ushindani huo kwa sababu ya kikwazo cha lugha. Hii inawezekana kwa sababu duniani huko ziko taasisi nyingine zinazounganisha au zinazojumuisha nchi nyingine nyingi zaidi *SADC, European Union, COMESA CARICOM*, ikiwemo na nyingine nyingi. Hata Umoja wa Mataifa wenyewe una lugha sita rasmi, *UN* ina *six official languages* ikiwemo Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kichina, Ki-Russia na Ki-Spanish. Hii inawezesha kwanza ushiriki wa watu wote wanaohusika katika muunganiko huo na kuwawezesha kuweza kuelewa mipango mbalimbali na kuweza kulinganisha mipango ya nchi zao na ile ya nchi hizo za mijumuiko katika hizo *forums*.

Mheshimiwa Spika, nirudi tena upande wa Tanzania, tunao mpango wetu wa muda mrefu unaitwa *The Long Term Perceptive Plan (LTP)* wa mwaka 2011/2012 mpaka mwaka 2025/2026. Kwenye kipengele cha *institutional framework* Serikali ilipangiwa jukumu la kutawanya nyaraka zote za maendeleo kwenda mpaka kwa wananchi. *Vision* yenyewe huo mpango wenyewe wa muda mrefu lakini mipango ya miaka mitano yote huu wa kwanza na huu wa pili na wa tatu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa malizia sasa

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Namalizia kwa kusema kwamba mipango yote hii Serikali iweze kutekeleza kwanza kwa kuitafsiri nayo iwe ya Kiswahili, halafu iweze kuitawanya na kuipeleka kule kwa wananchi ambao ndio watekelezaji wa hii mipango, tutaweza kuona namna ambavyo tunaweza kuongeza kasi ya utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ramo Makani...

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Mheshimiwa Mattar Ali Salum

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Pia nimshukuru sana Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri ambazo anazifanya pamoja na Naibu Waziri wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ambayo inakwenda katika uchumi wa viwanda; na ili tujenge viwanda, viendeleo na viweze kufanya kazi kama nchi nyingine ambazo zimeshaendelea lazima tuimarisha uchumi wa nchi yetu na ni lazima tusimamie kilimo. Viwanda vyetu ili viweze kufanya kazi kwa hali nzuri lazima Serikali yetu iweze kuangalia sekta ya kilimo. Bila kuangalia sekta ya kilimo tutakuwa tunaimba viwanda lakini hatujafika mahali ambapo tunapataka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia sekta ya kilimo bado Serikali yetu haijaweka mkakati rasmi wa kushughulikia tatizo la kilimo. Ukiangalia bajeti ya kilimo bado ni ndogo na vile vile na upelekeaji wa pesa katika sekta ya kilimo bado ni mdogo sana na sisi tunahitaji kwenda katika uchumi wa viwanda kwa nguvu zote. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, jitahidi sana fanya kazi kuhakikisha sekta ya kilimo ndiyo sekta mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo, ikiwa hatujaitizama kwa makini sekta ya kilimo basi hata hili suala la ajira kwa vijana wetu wa Tanzania bado haitofikia mahali pazuri. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aiangalie sekta ya kilimo, ndiyo sekta mama katika nchi yetu, ndiyo sekta ambayo itatutoa

hapa tulipo na kwenda kwenye uchumi wa viwanda. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kusikiliza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tulikuwa Njombe, tulipata tabu sana; kuna kelele sana za wakulima wanakosa mikopo. Sasa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie; wakulima wetu bado wanakosa mikopo katika benki. Sasa wataweza kufanya kazi vipi na mahali pa kupata pesa ili waweze kuimarisha kilimo pasipo na Serikali ni lazima waweze kupata mikopo ndani ya benki zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, benki zimekuwa sugu katika kutoa mikopo kwa wakulima wetu, tumepata kelele nyingi. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kusimamia kwa makini utoaji wa mikopo kwa wakulima wetu. Wakulima wetu ukiwapa mikopo na ukisimamia vizuri ukiwapelekea watalaam vizuri tutatoka hapa tulipo na tutakwenda mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la maji. Hili bado ni tatizo; bajeti ya maji 2017/2018 ilipangwa kuwa takriban bilioni mia sita, zilizotoka ni bilioni mia mbili tu. Tulijadiliana na sisi kama Wabunge tumesema iongezwe Sh.50 kusaidia bajeti hii kuhakikisha wananchi wetu wanapata maji ya kutosha. Kama hatutaongeza Sh.50 tutakuwa hatufiki mahali pale ambapo tuliahidi Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi ni Wabunge ambao tumekuja hapa kwa sababu ya kuwasemea wananchi wetu, tukiishauri Serikali tumwombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kupokea mawazo yetu katika kuongeza Sh.50. Ukiangalia idadi ya bajeti hii, tukienda katika *system* ili tuweze kupata maji safi wananchi wetu wapate maji, tutachelewa kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kulipokea, kuongeza Sh.50 katika lita ya dizeli na petroli ili tuweze kupata maji safi kwa sababu ukiongeza

hakuna tatizo, mimi sijaona tatizo la kukosa kuongeza hili. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kulichukua suala la ongezeko hili la Sh.50 kwenye lita ya petoli na dizeli ili tuweze kufika mahali tunapopataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi wa bahari kuu bado ni tatizo, bado Serikali haijaka katika kulisimamia, kuweka mikakati rasmi ili kuhakikisha uvuvi wa bahari kuu unakwenda kwa kasi sana. Mahali hapa penye uvuvi wa bahari kuu tukipasimamia kikweli kweli kama Serikali, tukiamua kwenda kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu, nchi yetu itaweza kwenda mbele. Uvuvi wa bahari kuu unaweza kuchangia mapato mengi sana na sasa tunakosa mapato makubwa sana kupitia uvuvi wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila tukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha hatujaona kipengele ambacho watasema sasa tutajenga bandari, kununua meli za uvuvi na kufanya tathmini ya samaki ndani ya bahari yetu ambayo tunayo; tuna uwezo gani na tuna samaki kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, tukikaa tukisimamia suala la uvuvi, tukiweza kuwezesha hii sekta ya uvuvi kwa makini, tunaweza kufika mahali ambapo nchi yetu inapataka. Huu uvuvi tukiweza kusimamia kwa makini basi unaweza kuingiza Pato la Taifa kuliko hata hii sekta ya madini. Niiombe Serikali iweze kusimamia kwa makini kuhakikisha suala la uvuvi wa bahari kuu linatazamwa kwa jicho la huruma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao Waheshimiwa Mawaziri wetu wa Wizara ya Uvuvi wako vizuri, wanafanya kazi vizuri na wanashaurika vizuri, basi niombe sana Serikali iweze kuita•izama kuhakikisha kwamba uvuvi huu unakwenda mbio kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanafanya kazi. Uvuvi wa bahari kuu una uwezo wa kutengeneza ajira kubwa sana kutoka kwa wananchi wetu, ni kwa nini tusiweze kusimamia uvuvi wa bahari kuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ndiyo hili la sekta ya uvuvi ambayo tuliiangalia kwa makini, tukiweza kujua tuna kiasi gani cha samaki katika bahari kuu, tukiweza kujua tuna uwezo gani na tukiweza kununua meli yale mapato ambayo tunakosa kutoka katika bahari kuu, tukiweza kuyapata tunaweza kufika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kupatikana kwa ajira kwa vijana, bado ajira kwa vijana upatikanaji wake upo duni sana. Niombe sana, Wizara ya Elimu ipo, tuanze kuwafundisha vijana wetu jinsi ya kujiajiri kutoka shule za msingi ili wakitoka pale wakimaliza chuo kikuu watakuwa wameweza kujiajiri wao wenyewe kuliko kukaa tu kuitegemea Serikali ili iweze kuwaajiri. Suala hili haliwezekani, hakuna Serikali ambayo inaweza kuajiri watu wake wote. Ni lazima kama Serikali tujipange tuhakikishe kwamba vijana wetu tunaanza kuwafundisha mafunzo ambayo hata wakimaliza basi wanaweza kujiajiri wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mattar Ali Salum. Waheshimiwa Wabunge kwa wale ambao mmeleta majina yenu kwa siku ya leo wote mmekuwa *covered*. Kwa hiyo, sasa hapa nina matangazo mawili.

Yupo Mheshimiwa Mbunge ambaye amepoteza funguo za gari aina ya *Toyota Harrier*, kama mtu anazo basi tunaomba azilete kwa Makatibu hapa ili mwenzetu ambaye amepata usumbufu huo aweze kilitumia gari lake vizuri.

Nina tangazo kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Jenista Mhagama, anasema kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inawatangazia uzinduzi wa Kampeni ya Kupima VVU na Kuanza *ARV* mapema itakayofanyika Uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma kesho tarehe 19 Juni, 2018.

Waheshimiwa Wabunge, kesho kutakuwa na uzinduzi wa Kampeni ya Kupima VVU na Kuanza ARV Mapema itakayofanyika Uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma kesho tarehe 19 Juni. Mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wote mnakaribishwa. Ratiba ya shughuli hii inatarajiwa kuanza saa nne asubuhi hadi saa nane mchana. Kwa hiyo, kesho saa nne hadi saa nane, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hebu jaziliza kidogo. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa mujibu wa Kanuni zako za Bunge saa nne Bunge lako litakuwa linaendelea na shughuli na ningeoomba sana kwa ridhaa yako niwahamasishe sana Waheshimiwa Wabunge saa saba baada ya kuahirisha shughuli za Bunge basi waje washirikiane pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu na shughuli zitakazoendelea. Shughuli kubwa na ya muhimu ni ile ya kupima na sisi kama viongozi wawakilishi wa wananchi itakuwa ni vyema sana katika uzinduzi wa kampeni hii ya kitaifa tukajitokeza kesho katika Viwanja vya Jamhuri na kufanya upimaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kampeni hii kwa kweli ni maalum kabisa hasa kwa ajili ya wanaume wote katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, natarajia sana Waheshimiwa Wabunge wanawake tuwasindikize, tukapime na sisi lakini tuwahamasishe zaidi Waheshimiwa Wabunge wanaume ili waweze kwenda kuonesha mfano dhahiri wa kampeni hii wa kutambua afya zetu, kujijali na kuanza kutumia dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nategemea sana Waheshimiwa Wabunge wote tutashiriki na hasa Waheshimiwa Wabunge wanaume kuitikia wito huu wa wanaume kupima UKIMWI kwa hiyari. Hii ni kwa sababu ya taarifa ya matokeo ya utafiti uliofanywa katika nchi yetu ya Tanzania kuelekea 90 90 90 (tisini tatu). Tisini ya kwanza ambayo inawahusu wale wote ambao wanaishi na VVU kujitambua hali zao imeonekana bado kwenye kundi la

wanaume mwikitio bado ni kidogo. Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge twende tukashirikiane kwa pamoja, karibuni sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa msisitizo huo. Natumaini Waheshimiwa tutakumbuka Mheshimiwa Naibu Spika kwenye saa saba uwakumbushe kesho Waheshimiwa Wabunge kujitokeza kwa wingi katika zoezi hilo muhimu sana, tungeomba tujitokeze kwa wingi. Kama kutakuwa na uhitaji baada ya hapo tunaweza tukamwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, vipimo vikawekwa tu hapa mlangoni kwetu kabla ya kuweka dole unapima kwanza hapo halafu unakandamiza hapo ukutani. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa aliyepoteza funguo, funguo yake ni hii hapa tumeipata, kwa hiyo naiacha hapa mezani utaichukua kwa Makatibu, Mheshimiwa Risala. Basi Waheshimiwa Wabunge naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 1.20 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 19 Juni, 2018 Saa Tatu Asubuhi)